# Kielelezo Patanifu cha Katiba ya Kenya

Iliyochapishwa mnamo Novemba 17, 2009 na Kamati ya Wataalam Kuhusu Marekebisho ya Katiba Kulingana na Sehemu 32(1)(a)(i) ya Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya, 2008.

## UTANGULIZI

## SURA YA KWANZA

**UTAWALA WA WATU NA MAMLAKA YA KATIBA**
1. Utawala wa watu
2. Mamlaka ya Katiba
3. Kulinda Katiba

## SURA YA PILI

**JAMHURI**
4. Ikirari ya Jamhuri
5. Eneo
6. Ugatuzi
7. Mji Mkuu wa Kenya
8. Upatianaji Huduma
9. Lugha na Njia za Mawasiliano
10. Nchi na Dini
11. Nembo za Kitaifa
12. Siku za Kitaifa

## SURA YA TATU

**THAMANI ZA KITAIFA, KANUNI NA MALENGO**
13. Thamani za Kitaifa, Kanuni na Malengo

## SURA YA NNE

**URAIA**
14. Kauli za Kijumla
15. Kudumisha kwa Uraia Uliopo
16. Kufuata Uraia
17. Urai kwa Kuzaliwa
18. Uraia na Ndoa
19. Uraia kwa Kujiandikisha
20. Watoto wanaopatikana Kenya na watoto wa kupanga
21. Uraia Mara Mbili
22. Kupokonywa Uraia
23. Makao
24. Majukumu ya Raia
25. Sheria na uraia

## SURA YA TANO

**UTAMADUNI**
26. Kutambua Utamaduni
27. Jukumu la Serikali kuhusiana na utamaduni

## SURA YA SITA

**SHERIA YA HAKI**

**Sehemu ya 1- Vipengele vya jumla kuhusiana na Sheria ya Haki**
28. Haki na uhuru wa kimsingi
29. Utekelezaji wa Sheria ya Haki
30. Utekelezaji wa haki na uhuru wa kimsingi
31. Utekelezaji wa Sheria ya Haki
32. Mamlaka ya mahakama kudumisha na kutekeleza Sheria ya Haki
33. Mipaka ya haki na uhuru wa kimsingi
34. Haki na uhuru unaoweza kuwekewa mipaka

**Sehemu ya 2- Haki na uhuru wa kimsingi**
35. Haki ya kuishi
36. Usawa
37. Uhuru dhidi ya kubaguliwa
38. Jinsia
39. Wazee katika jamii
40. Vijana
41. Watoto
42. Familia
43. Walemavu
44. Makundi Tengwa
45. Hadhi ya kibinadamu
46. Uhuru na usalama wa mtu
47. Utumwa na kazi ya kulazimishwa
48. Usiri
49. Uhuru wa dhamiri, dini, imani na maoni
50. Uhuru wa kujieleza
51. Uhuru wa vyombo vya habari
52. Uwezo wa kuafikia habari
53. Uhuru wa kutangamana
54. Mikutano, maandamano, migomo na malalamishi
55. Haki za kisiasa
56. Uhuru wa kutembea na kuishi
57. Wakimbizi na wanaotafuta hifadhi
58. Uhuru wa biashara, kazi na taaluma
59. Ulinzi wa haki ya kumiliki mali
60. Mahusiano ya kikazi
61. Usalama wa kijamii
62. Afya
63. Elimu
64. Makao
65. Chakula
66. Maji
67. Mazingira
68. Lugha na Utamaduni
69. Haki za Watumiaji
70. Hatua ya Haki za Kiutawala
71. Uwezo wa kupata haki
72. Haki za Mahabusu
73. Haki katika kusikizwa kwa kesi
74. Haki za walio vizuizini
75. Hali ya hatari
76. Tume ya Haki na Maswala ya Kijinsia

## SURA YA SABA

**ARDHI NA MALI**
77. Kanuni za sera ya ardhi
78. Utoaji na uainishaji wa ardhi
79. Ardhi ya umma
80. Ardhi ya jumuia
81. Ardhi ya kibinafsi
82. Umilikaji Ardhi na wasio raia
83. Udhibiti wa matumizi ya ardhi
84. Tume ya Kitaifa kuhusu Ardhi
85. Sheria kuhusu Ardhi
86. Ustawishaji wa makao

## SURA YA NANE

**MAZINGIRA NA MALI ASILI**
87. Kanuni na wajibu kuhusiana na mazingira
88. Utunzaji wa mazingira
89. Hifadhi ya mazingira
90. Utekelezaji wa haki kuhusu mazingira
91. Ustawishaji na maendeleo ya mali asili
92. Makubaliano kuhusiana na mali asili
93. Sheria kuhusu Mazingira

## SURA YA TISA

**UONGOZI NA MAADILI**
94. Majukumu ya uongozi
95. Kiapo cha uamnifu
96. Mienendo ya maofisa wa Serikali
97. Fedha za maofisa wa Serikali
98. Uzuiaji wa shughuli
99. Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi
100. Wajibu wa kuhakikisha uzingatifu
101. Sheria kuhusu uongozi

## SURA YA KUMI

**UWAKILISHAJI WA WATU**

**Sehemu ya 1 – Kanuni za mfumo wa Uchaguzi na Utaratibu wa uchaguzi**

102. Kanuni za jumla
103. Sheria kuhusu uchaguzi
104. Kusajiliwa kama mpigakura
105. Wagombea katika uchaguzi kuzingatia kanuni za upigaji kura
106. Kuzingatia kanuni za uchaguzi
107. Wagombea wa kibinafsi
108. Wagombea wasio na wapinzani
109. Upigaji kura
110. Mizozo ya Uchaguzi
111. Kuwakilishwa kwa watu katika taasisi za Kimataifa

**Sehemu ya 2- Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka na kutodhibitika kwa vitengo vya uchaguzi**

112. Tume Huru ya uchaguzi na Mipaka
113. Kuwekea mipaka sehemu za uchaguzi

**Sehemu ya 3- Vyama vya kisiasa**

114. Kanuni za kimsingi kwa vyama vya kisiasa
115. kikomo cha uanachama katika chama cha kisiasa
116. Kamishna wa vyama vya kisiasa
117. Kudhibiti vyama vya kisiasa
118. Hazina ya Vyama vya Kisiasa
119. Matumizi ya Hazina hiyo
120. Kuwajibika kwa vyama vya kisiasa
121. Vyama vya kisiasa na vyombo vya habari
122. Mipaka ya matumzi ya raslimali za umma

## SURA YA KUMI NA MOJA

**BUNGE**

**Sehemu ya 1 – Muundo na jukumu la Bunge**

123. Kuundwa kwa Bunge
124. Jukumu la Bunge

**Sehemu ya 2 – Muundo na uanachama wa Bunge**

125. Wanachama wa Seneti
126. Uanachama katika Bunge
127. Masharti ya kufaa na kutofaa kuchaguliwa kama mbunge
128. Kukuza uwakilishi wa makundi tengwa
129. Uchaguzi wa wabunge
130. Kutoka ofisini kwa Mbunge
131. Haki ya kumwita na kumkosoa mbunge
132. Kukubalika kwa ubunge

**Sehemu ya 3- Maafisa wa Bunge**

133. Spika na Naibu wa Spika
134. Kuongoza vikao Bungeni
135. Kiongozi Rasmi wa Upinzani Bungeni
136. Karani na wafanyakazi wa Bunge

**Sehemu ya 4 – Kutunga sheria Bungeni**

137. Mamlaka ya kutunga sheria
138. Miswada ya Fedha
139. Maoni ya Bunge jingine
140. Idhini ya Rais
141. Kutekelezeka kwa sheria
142. Haki ya kulalamikia Bunge
143. Idadi ya wabunge katika vikao
144. Lugha rasmi za Bunge
145. Kupiga kura Bungeni
146. Maamuzi ya Seneti
147. Kudhibitiwa kwa utaratibu
148. Uwezo wa kutaka ushahidi
149. Kufikiwa na umma
150. Uwezo, haki na kinga

**Sehemu ya 5 – Ziada**

151. Usajili wa Sheria buniwa
152. Makao ya Bunge
153. Kipindi cha Bunge
154. Tume ya Huduma za Bunge

## SURA YA KUMI NA MBILI

**MAMLAKA YA RAIS**

**Sehemu ya 1- Kanuni na muundo wa mamlaka ya Serikali ya Kitaifa.**

155. Kanuni za mamlaka ya serikali
156. Serikali ya Kitaifa

**Sehemu ya 2- Rais wa Taifa na Naibu Rais**

157. Mamlaka ya Rais wa Taifa
158. Majukumu ya Rais wa Taifa.
159. Majukumu ya Rais katika kutunga sheria
160. Matumizi ya mamlaka ya Rais kwa Rais wa muda
161. Uamuzi wa Rais wa Taifa
162. Uchaguzi wa Rais wa Taifa
163. Sifa za kimsingi za kuchaguliwa na kutochaguliwa kwa Rais wa Taifa
164. Tararatibu katika uchaguzi wa Rais
165. Maswali kuhusu uhalali wa uchaguzi wa Urais
166. Kuchukua hatamu za Urais wa Taifa
167. Masharti ya ofisi ya Rais
168. Kinga dhidi ya kufunguliwa mashtaka.
169. Kuondolewa kwa Rais wa Taifa kwa misingi ya kukosa uwezo.
170. Kumwondoa Rais wa Taifa kupitia kwa kura ya kutokuwa na imani
171. Nafasi katika ofisi ya Rais wa Taifa
172. Mamlaka ya huruma ya Rais
173. Ofisi ya Naibu Rais wa Taifa
174. Nafasi katika ofisi ya Naibu Rais wa Taifa
175. Majukumu ya Naibu Rais wa Taifa
176. Kifo kabla ya kuchukua mamlaka
177. Kuondolewa kwa naibu Rais wa taifa
178. Mshahara na marupurupu ya Rais wa Taifa na Naibu Rais wa Taifa

**Sehemu-3 Waziri Mkuu na Baraza la Mawaziri**

179. Waziri Mkuu
180. Uteuzi wa Waziri Mkuu
181. Masharti ya ofisi
182. Kujiuzulu kwa Waziri Mkuu
183. Mshahara na marupurupu ya Waziri Mkuu
184. Baraza la Mawaziri na Manaibu
185. Kuachishwa kazi kwa Mawaziri na Manaibu wa Mawaziri.
186. Kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu
187. Maamuzi, majukumu na kuwajibika kwa Baraza la Mawaziri
188. Raisi wa Taifa kufahamishwa kwa ukamilifu kuhusu mienendo ya serikali
189. Kugawa majukumu
190. Katibu wa Baraza la Mawaziri
191. Uteuzi na kuachishwa kazi kwa Makatibu Vinara
192. Uteuzi na kuachishwa kazi kwa Makatibu Vinara

**Sehemu ya 4- Ofisi nyingine**

193. Mwanasheria Mkuu
194. Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma
195. Mchunguzi Maalum wa Malalamiko ya Umma
196. Kuondolewa kwa Mchunguzi Maalum wa Mashtaka ya Umma

## SURA YA KUMI NA TATU

**IDARA YA MAHAKAMA**

**Sehemu 1 – Mamlaka ya Idara ya Mahakama na mfumo wa sheria**

197. Mamlaka ya Idara ya Mahakama
198. Uhuru wa Idara ya Mahakama
199. Ofisi na maafisa wa Idara ya Mahakama
200. Mfumo wa Mahakama

Sehemu 2- Mahakama zenye Mamlaka Kuu

201. Mahakama yenye Mamlaka Kuu
202. Mahakama ya Rufani
203. Mahakama ya Katiba
204. Mahakama Kuu
205. Uteuzi wa majaji
206. Kipindi cha kuhudumu ofisini kwa Jaji Mkuu na majaji wengine
207. Kuondolewa kutoka ofisini

Sehemu 3 -Mahakama za chini

208. Mahakama za chini
209. Mahakama za Kadhi
Sehemu 4 – Tume ya Huduma za Mahakama
210. Kubuniwa kwa Tume ya Huduma za Mahakama
211. Majukumu ya Tume ya Huduma za Mahakama
212. Hazina ya Mahakama

## SURA YA KUMI NA NNE

**Sehemu 1- Malengo na kanuni za serikali ya ugatuzi**
213. Malengo ya ugatuzi
214. Kanuni za serikali ya ugatuzi
215. Serikali za maeneo
216. Bunge za maeneo
217. Kamati za mamlaka kuu
218. Uchaguzi wa mkurugenzi wa eneo na nanibu wake
219. Uchaguzi wa meya na naibu wa meya jijini Nairobi
220. Shughuli za kamati kuu za maafisa wa maeneo

**Sehemu ya 3 – Serikali za wilaya**
221. Serikali za wilaya
222. Wanachama wa bunge la wilaya
223. Kamati tendaji za wilaya
224. Uchaguzi wa gavana wa wilaya na naibu wa gavana wa wilaya
225. Shughuli za kamati tendaji ya wilaya

**Sehemu ya 4 – Mamlaka na shughuli za serikali ya ugatuzi**
226. Mamlaka na shughuli zake
227. Kuhamisha mamlaka na majukumu
228. Mamlaka na shughuli zake
229. Kuhamisha mamlaka na majukumu

**Sehemu ya 5 – Mipaka ya serikali zilizogatuliwa**
230. Mipaka ya serikali ya ugatuzi

**Sehemu 6 – Mahusiano ya serikali**
231. Ushirikiano wa serikali katika ngazi tofautitofauti
232. Mikinzano ya sheria

**Sehemu ya 7 – Kuondolewa, kusimamishwa kwa muda, kuvunjiliwa mbali kwa serikali za ugatuzi**
233. Kura ya kutokuwa na imani na kamati kuu ya eneo
234. Kura ya kutokuwa na imani na kamati kuu ya wilaya
235. Kusimamishwa kwa muda kwa serikali ya eneo na wilaya

**Sehemu ya 8 – Kwa ujumla**
236. Sifa za wagombea uanachama wa bunge la eneo au wilaya
237. Kuondoka katika ofisi kama mwanachama wa bunge la eneo au wilaya
238. Uwezo wa kuita mashahidi
239. Ushirikiano na umma, uwezo, nafuu na ulinzi
240. Usawa na tofauti za kijinsia
241. Serikali katika kipindi cha mpwito
242. Kuchapishwa kwa sheria
243. Vipengele vitakavyoundwa na Sheria za Bunge

## SURA YA KUMI NA TANO

**Fedha za umma**

**Sehemu- 1 Usimamizi wa fedha na mapato ya Serikali**
244. Kanuni na malengo ya usimamizi wa fedha na mapato ya umma

**Sehemu 2- Mamlaka ya Ushuru na Kugawa Mapato**
245. Kutoza Ushuru
246. Mamlaka ya Kutoza Ushuru
247. Kiwango cha fedha kwa serikali zilizogatuliwa
248. Sheria

**Sehemu 3- Hazina ya pamoja ya kuhifadhi fedha za umma**
249. Hazina ya pamoja
250. Kutoa pesa kutoka kwa Hazina ya Pamoja
251. Hazina ya Mapato ya serikali zilizogatuliwa
252. Hazina ya Dharura

**Sehemu 4- Kukopa**
253. Ukopaji wa Serikali
254. Mikopo ya serikali zilizogatuliwa
255. Deni la serikali
256. Mikopo iliyodhaminiwa na serikali

**Sehemu 5- Bajeti**
257. Yaliyomo
258. Makadirio ya Taifa ya kila mwaka
259. Miswada ya kugawa mapato na matumizi fedha
260. Bajeti ya kila mwaka ya serikali zilizogatuliwa

**Semu 6- Usimamizi wa fedha**
261. Ununuzi wa bidhaa na huduma za umma
262. Akaunti na ukaguzi wa hesabu za fedha katika mashirika ya umma
263. Udhibiti wa hazina
264. Mdhibiti Bajeti
265. Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

**Sehemu ya 7- Taasisi**
266. Mamlaka ya Kitaifa ya Ushuru
267. Tume ya Ugawanaji Mapato
268. Tume ya Mishahara na Marupurupu
269. Benki Kuu ya Kenya
270. Majukumu ya Benki Kuu
271. Baraza la Kichumi na Kijamii

## SURA YA KUMI NA SITA

**UTUMISHI WA UMMA**

**Sehemu 1 – Utumishi wa Umma**
272. Thamani na kanuni za huduma kwa umma
273. Tume ya Utumishi wa Umma
274. Mamlaka na Majukumu
275. Kuajiri Wafanyakazi wa Serikali zilizogatuliwa
276. Kuwalinda maafisa wa serikali

**Sehemu 2 – Tume ya Kuwaajiri Walimu**
277. Tume ya Kuwaajiri Walimu

**Sehemu 3 – Huduma ya Marekebisho ya Kenya**
278. Kubuniwa na kudhibitiwa
279. Mkurugenzi Mkuu

## SURA YA KUMI NA SABA

**Sehemu 1- Taasisi za Usalama wa Taifa**
280. Kanuni na misimamo
281. Taasisi za usalama wa Taifa
282. Kubuniwa kwa Baraza la Usalama wa Taifa
283. Majukumu ya Baraza la Usalama wa Taifa

**Sehemu 2 - Majeshi ya Ulinzi wa Kenya**
284. Kubuniwa kwa Vikosi vya Ulinzi wa Kenya na Baraza la Ulinzi
285. Uongozi

**Sehemu 3 – Huduma za Taifa za Upelelezi**
286. Kubuniwa kwa Huduma za Taifa za Upelelezi
287. Mkurugenzi –Mkuu wa Huduma
288. Baraza la Kitaifa la Ujasusi .

**Sehemu 4 – Huduma ya Polisi ya Kenya**
289. Kuundwa kwa Huduma ya Polisi ya Kenya
290. Malengo na Majukumu
291. Uteuzi na ufutaji kazi wa Inspekta-Mkuu
292. Majukumu na uhuru wa Inspekta -Mkuu
293. Tume ya Huduma ya Polisi

**Sehemu 5 –Huduma Nyingine za Polisi**
294. Huduma nyingine za polisi

## SURA YA KUMI NA NANE

**TUME NA OFISI HURU**

295. Utekelezezaji wa Sura
296. Malengo ya Tume na ofisi huru
297. Uteuzi na masharti ya ofisi
298. Kuondolewa kutoka ofisini
299. Mamlaka ya jumla
300. Majukumu ya jumla
301. Utendaji wa Tume na ofisi huru
302. Ushirikishwaji
303. Fedha za Tume na ofisi Huru
304. Ripoti za kila mwaka na ripoti nyingine

305. Sheria

## SURA YA KUMI NA TISA

**MAREKEBISHO YA KATIBA**
306. Marekebisho ya Katiba
307. Marekebisho yatakapendekezwa na Bunge
308. Marekebisho yatakayopendekezwa wengi

## SURA YA ISHIRINI

**VIPENGELE VYA KIJUMLA**
309. Utekelezaji wa Vipengee vya Katiba hii
310. Kufasiri Katiba
311. Maelezo

## SURA YA ISHIRINI NA MOJA

**VIPENGELE VYA MUDA NA MATOKEO YA BAADA YA KUANZA KUTUMIKA KWA KATIBA**
312. Sheria zinazohuasiana na Matokeo
313. Tume kuhusiana na kutekelezwa kwa Katiba
314. Wakati wa Mpito
315. Katiba kuanza kutumika
316. Kubatilishwa

## MIPANGILIO

**MPANGILIO WA KWANZA :** Maeneo Na Wilaya

**MPANGILIO WA PILI :** Nembo za Kitaifa

**MPANGILIO WA TATU:** Viapo Vya Kitaifa Na Udhibitisho

**MPANGILIO WA NNE:** Mgao Wa Majukumu Kati Ya Serikali Ya Kitaifa Na Serikali Zilizogatuliwa

**MPANGILIO WA TANO:** Mamlaka Ya Kutoza Ushuru

**MPANGILIO WA SITA:** Mpangilio Wa Sita

# UTANGULIZI

**Sisi Wakenya -**
**TUKITAMBUA** utukufu wa Mungu Muumba wa vyote:
**TUKIWAHESHIMU** mashujaa wetu waliojitoa mhanga kupigania uhuru na haki kwa nchi yetu:
**TUKIJIVUNIA** tofauti zetu za kikabila, kitamaduni na kidini na kuazimia kuishi kwa amani na umoja tukiwa taifa moja dhabiti:
**TUKITHAMINI** mazingira yetu asili ambayo ndiyo urithi wetu na kuazimia kuyadumisha kwa manufaa ya vizazi vijavyo:
**TWAJITOLEA** kukuza na kuhifadhi maslahi ya watu binafsi, familia, jamii na taifa:
**TWATAMBUA** matarajio ya Wakenya wote kwa serikali iliyo na misingi bora ya haki za binadamu, usawa, demokrasia, haki za kijamii na utawala wa kisheria:
**MATUMIZI** ya uhuru wetu, haki yetu ya kuamua aina ya uongozi tuutakao na tukiwa tumeshiriki kikamilifu katika kuiunda katiba hii:
**TUNAKUBALI,** kutekeleza, na kujipa sisi wenyewe na vizazi vijavyo, Katiba hii.

## SURA YA KWANZA

**UTAWALA WA WATU NA MAMLAKA YA KATIBA**

**Utawala wa watu**
**1.** (1) Nguvu zote za kiutawala zinamilikiwa na raia wa Kenya na zinaweza kutumiwa tu kulingana na Katiba hii.
(2) Raia wanaweza kutumia nguvu zao za kiutawala ama moja kwa moja au kupitia kwa wawakilishi wao waliochaguliwa kidemokrasia.
(3)Mamlaka chini ya hii Katiba yamepewa taasisi zifuatazo za Serikali, ambazo zitatekeleza majukumu yao kulingana na hii Katiba –
(a) Bunge na mabaraza ya kutunga sheria katika serikali zilizogatuliwa;
(b)Serikali ya kitaifa na miundo yake katika serikali zilizogatuliwa;
(c) Idara ya mahakama na mojopo mengine huru; na
(d) tume za kikatiba, ofisi huru na ofisi nyingine za Serikali.

**Mamlaka ya Katiba**
**2.** (1) Katiba hii ni sheria kuu ya Jamhuri na inaunganisha asasi zote za nchi katika viwango vyote vya kiserikali na watu wote -
(2) Hakuna mtu anayeweza kudai au kutumia mamlaka ya Nchi bila idhini au kulingana na jinsi ilivyoidhinishwa na Katiba hii.
(3) Uhalali wa katiba hii hauwezi kupingwa na au katika mahakama yoyote au tawi lolote la Serikali.
(4) Sheria yoyote, ikiwemo sheria ya mila na tamaduni, ambayo haiambatani na Katiba hii haitambuliwi kwa kiasi ambacho haiambatani na kitendo chochote ama kutotimiza wajibu kinyume na Katiba hii.
(5) Mtu, au kundi la watu, wanaweza kuchukua hatua katika mahakama inayofaa kulalamika kuhusu sheria yoyote, tendo ama kuachwa nje kwa vipengee fulani vya sheria, ama haiambatani na, Katiba hii.
(6) Iwapo mahakama itafanya uamuzi chini ya ibara (5), inaweza pia kutoa agizo muhimu kutekeleza uamuzi huo.

**Kuilinda Katiba**
**3.** (1) Kila mtu ana jukumu la kuiheshimu , kuitetea na kuilinda katiba hii.
(2) Jaribio lolote la kubuni serikali vingine bila kufuata Katiba hii ni haramu.

## SURA YA PILI

**JAMHURI**

**Ikirari ya Jamhuri**
**4.** (1) Kenya ni Nchi Huru -
(2) Jamhuri ya Kenya imejikita kwenye misingi ya utawala bora kupitia kwa siasa za vyama vingi, utawala shirikishi,uwazi na uwajibikaji, utenganishaji na ugatuzi wa mamlaka, kuheshimu haki za binadamu na uhuru wa kimsingi na utawala wa kisheria.

**Eneo**
**5.** (1) Kenya ina eneo linalotambuliwa chini ya sheria ya kimataifa -
(2) Kenya ina maeneo na mikoa iliyobuniwa kama ilivyo katika Awamu ya Kwanza

**Ugatuzi**
**6.** (1) Mamlaka huru ya watu yatatumiwa katika –
(a) kiwango cha kitaifa;
(b) kiwango cha eneo; na
(c) Kiwango cha wilaya au mkoa.
(2) Serikali katika maeneo mbalimbali ni tofauti na zinategemeana na hutekeleza majukumu yao kwa misingi ya mashauriano na ushirikiano.

**Mji Mkuu wa Kenya**
**7.** Mji mkuu wa Kenya ni Nairobi –

**Upatikanaji huduma**
**8.** Taasisi ya Serikali ya Kitaifa itahakikisha kwamba wananchi wanapata huduma katika maeneo yake yote –

**Lugha na njia za mawasiliano.**
**9.** (1) Lugha ya taifa ni Kiswahili.
(2) Lugha rasmi za Kenya ni Kiswahili na Kiingereza.
(3) Serikali itaheshimu na kukuza maendeleo na matumizi ya lugha za kiasili na lugha ya ishara.
(4) Serikali itaendeleza ukuaji na matumizi ya Breli na njia nyingine za mawasiliano kwa watu wenye ulemavu wa macho na ulemavu wa aina nyingine.

**Nchi na Dini**
**10.** (1) Serikali na dini zitatenganishwa.
(2) Hakutakuwa na dini ya Taifa.
(3) Dini zote zitakuwa sawa nchini.

**Nembo za Kitaifa**
**11.** (1) Nembo za kitaifa za Jamhuri ni –
(a) bendera ya taifa;
(b) wimbo wa taifa;
(c) ngao ya ulinzi; na
(d) muhuri wa serikali
(2) Nembo za kitaifa zimefafanuliwa katika Sehemu ya Pili.

**Siku za Kitaifa**

**12** (1) Siku kuu za kitaifa ni –
(a) Siku kuu ya Madaraka, kuadhimishwa Juni 1;
(b) Siku kuu ya Mashujaa, kuadhimishwa Oktoba 20; na
(c) Siku kuu ya Jamhuri, kuadhimishwa Desemba 12.
(2) Siku ya kitaifa itakuwa ya mapumziko kote nchini.
(3) Bunge linaweza, kupitia kwa sheria kuamua ni siku gani iwe ya kitaifa.

## SURA YA TATU

### THAMANI ZA KITAIFA, KANUNI NA MALENGO

**Thamani za Kitaifa, Kanuni na Malengo**

**13.** (1) Thamani za kitaifa, maadili na malengo yaliyomo katika Sura hii yatafuatwa na taasisi mbalimbali za Serikali, Maafisa wa Serikali na watu wote kila yeyote kati yao –
(a) anatekeleza au anafasiri Katiba hii;
(b) anatumia, anatekeleza au kufasiri sheria yoyote; au
(c) anafanya, anatumia au anatekeleza maamuzi kuhusu sera ya kitaifa.
(2) Thamani za kitaifa,maadili na malengo ni pamoja na –
(a) Kukuza umoja wa kitaifa na kujitolea kwa raia wate kudumisha utaifa na uzalendo;
(b) Kutambua tofauti za watu na kukuza na kuhifadhi tamaduni zao;
(c) Kukuza ushiriki wa watu katika masuala ya kiserikali na ugawanaji na ugatuzi wa mamlaka;
(d) Kuhakikisha kwamba kuna serikali yenye uwazi na uwajibikaji baina ya maafisa wa Serikali, asasi za Serikali na halmashauri nyingine za umma;
(e) Kuchukua hatua zifaazo kuondolea mbali ufisadi wa aina zote;
(f) Kuhakikisha kwamba watu wote wanafaidika na asasi huru za haki sisizopendelea, zenye uwezo na utendakazi bora.

## SURA YA NNE

### URAIA

**Kauli za kijumla**

**14**. Kila raia -
(a) anastahili haki, mapendeleo na faida ya uraia kulingana na mipaka iliyowekwa na Katiba hii;
(b) ana haki ya kupata pasipoti ya Kenya na stakabadhi yoyote ya usajili na utambulisho inayotolewa na Serikali kwa raia wake; na
(c) anatakiwa kutekeleza majukumu ya uraia.

**Kudumisha kwa uraia uliopo**

**15.** Kila mtu ambaye alikuwa raia kabla ya tarehe ya utekelezaji anadumisha uraia wake kuanzia tarehe hiyo.

**Kufuata uraia**

**16**. (1) Uraia unaweza kupatikana kwa kuzaliwa,kujisajili au kujiandikisha .
(2) Kila mtu ambaye hakuwa raia mara moja kabla ya tarehe husika lakini ambaye angelikuwa raia iwapo Katiba hii ingeliidhinishwa ana haki, kwa kutuma maombi, kusajiliwa kama raia.

**Uaraia kwa kuzaliwa**

**17.** (1) Kila mtu anayezaliwa Kenya ni raia iwapo, wakati wa tarehe ya kuzaliwa kwa mtu huyo, ama mama au baba yake ni raia.
(2) Mtu anayezaliwa nje ya Kenya ni raia iwapo, wakati wa tarehe ya kuzaliwa, ama mama yake au baba yake ni raia –
(a) ambaye alizaliwa Kenya; au
(b) kwa usajili au raia wa kuandikishwa.
(3) Iwapo mmoja kati ya wazazi wa mtu alifariki kabla ya mtu huyo kuzaliwa, uraia wa mzazi huyo wakati wa kifo chake unatumika, kwa madhumuni yote ya Sura hii, kama kwamba mzazi huyo alikuwa ameishi hadi kuzaliwa kwa mtu huyo.

**Uraia na ndoa**

**18.** (1) Mtu ambaye ameolewa na raia kwa muda wa angalau miaka saba ana haki, kwa kutuma maombi, kuandikishwa kama raia.
(2) Uraia haupotezwi kupitia kwa ndoa au kuvunjika kwa ndoa

**Uraia kwa kujiandikisha**

**19**. Mtu ambaye amekuwa mkazi halali nchini Kenya kwa muda wa miaka saba mfululizo, na ambaye anatimiza masharti yote ya sheria yaliyoidhinishwa na Bunge, anaweza kutuma maombi ya kujiandikisha kama raia —

**Watoto wanaopatikana Kenya na watoto wa kupanga**

**20.** (1) Mtoto anayepatikana nchini Kenya ambaye anaonekana kuwa na umri wa miaka minane, na ambaye uraia wake na wazazi hawajulikani , anachukuliwa kuwa raia kwa kuzaliwa.
(2) Mtoto ambaye sio raia na ambaye ni wa kupanga na raia ana haki ya kutuma maombi, ya kuwa raia.

**Uraia mara mbili**

**21.** (1) Mtu ambaye ni raia hapotezi uraia wake kwa sababu ya kujipatia uraia wa nchi nyingine —
(2) Mtu ambaye, kwa sababu ya kujipatia uraia wa nchi nyingine na kukoma kuwa raia wa Kenya ana haki, kwa kutuma maombi, kurejeshewa uraia wa Kenya.
(3) Bunge litatunga sheria kuruhusu kuwepo kwa masharti ambapo uraia unaweza kuidhinishwa kwa watu binafsi, isipokuwa watu wanaorejelewa katika ibara (1) na (2), ambao ni raia wa nchi nyingine.

**Kupokonywa uraia**

**22.** Mtu anaweza kupokonywa uraia iwapo mtu huyo alijipatia uraia huo kwa njia ya udanganyifu —

**Makao**

**23.** (1) Watu wafuatao wanaweza kuingia na kukaa nchini Kenya iwapo wanatimiza masharti yaliyowekwa na au chini ya Sheria ya Bunge inayosimamia kuingia na kukaa nchini –
a)raia wa zamani
b) mke wa kigeni au mjane au mume wa kigeni au mjane wa raia; na
c)mtoto wa raia.
(2) Bunge linaweza kuunda sheria inayosimamia kuingia na kukaa nchini Kenya kwa kategoria nyingine za watu na kuruhusu viwango vya makao mengine ya kudumu.

**Majukumu ya Raia**

**24.** (1) Raia wote wana majukumu ya —
(a) Kuelewa kimsingi vipengele muhimu vya Katiba hii na kutetea msingi wake na malengo;
(b) Kuheshimu na kushikilia na kutetea Katiba hii na sheria;
(c) Kukuza demokrasia, uongozi bora na kufuata sheria;
(d) Kupiga kura kwenye chaguzi na kura ya maoni;
(e) Kujaribu kukuza umoja wa kitaifa na kuishi kwa amani na wengine;
(f) Kushirikiana na maajenti wa sheria ili kuhifadhi amani na utangamano;
(g) Lipa ushuru wote anaohitajika kulipa;
(h) asishiriki katika ufisadi;
(i) kufanya kazi kwa maslahi na kuchangia katika maendeleo ya taifa;
(j) kukuza uwezo wao kupitia kwa kujipa mafunzo na kuendelea na mafunzo;
(k)kuchangia kwa maendeleo ya jamii wanapoishi;
(l) endeleza maisha ya jamii na huduma na kutenda mema katika muktadha wa familia;
(m) Kutetea na kulinda mali ya umma kutokana na uharibifu na kutumiwa vibaya;
(n) Kulinda mazingira na kuhifadhi mali asili; na
(o) elewa na kuza nafasi ya Jamhuri katika jamii ya kimataifa.
(2) Majukumu hayo yaliyoelezwa katika kifungu (1) yatatekelezwa kwa usawa, panapohitajika kwa wale wasio raia.

**Sheria na uraia**

**25.** Bunge litaunda sheria —
(a) kueleza taratibu kupitia kwazo mtu anaweza kuwa raia;
(b) kutoa nafasi kwa kukataa uraia kwa kupenda;
(c) kutoa taratibu kwa kunyimwa uraia; na
(d) Kwa jumla , kutoa athari kwa vipengele vya Sura hii.

## SURA YA TANO

### UTAMADUNI

**Kutambua utamaduni**

**26.** Katiba hii inatambua utamaduni kama msingi wa taifa na mkusanyo wa ustaarabu wa watu wa Kenya na jamii na , hasa –
(a) kutilia mkazo thamani na misimamo ya jamii za Kenya, tamaduni zao matamanio yao ya sasa na siku ya siku zijazo;

(b) Inatambua na kulinda thamani za kimsingi na malengo ya utamaduni na inafurahia utamaduni kama msingi wa kukuza fahari ya kitaifa na utambulisho; na
(c) inaakisi na kutilia nguvu upekee wa watu wa Kenya na jamii katika kuchangia, na kushiriki katika utamaduni wa kilimwengu.

**Jukumu la Serikali kuhusiana na utamaduni**

**27.** Serikali –
(a) Itakuza uelewano, uvumiliano na kuonea fahari mseto wa tamaduni;
(b) itaheshimu, kuhifadhi, kulinda , kukuza na kuendeleza turathi za Kenya na hasa, vifaa vyake vya kiutamaduni, kihistoria, kidini, takatifu, kiakiolojia na maeneo mengine muhimu;
(c) Kukuza –
(i) utafiti na sera ya elimu inayokuza utamaduni na thamani za kitamadun na inayowezesha watu kuwa na misingi thabiti ya imani na kimaadili;
(ii) aina zote za kujieleza kitamaduni kote nchini kupitia fasihi, sanaa, sherehe za kitamaduni, sayansi, mawasiliano, habari, vyombo vya habari, machapisho na maktaba na njia nyingine za kitamaduni; na
(iii) utafiti na kurekodi utamaduni wa Kenya ikiwemo historia ya kitaifa na sheria za kiasili;
(d) kutambua, kuunga mkono na kukuza matumizi ya kisasa na ya kitamaduni ya matibabu;
(e) kutambua jukumu la sayansi na teknolojia za kiasili katika maendeleo ya nchi;
(f) kuunga mkono,kukuza na kulinda maarifa ya kiasili na haki miliki za maarifa ya watu wa Kenya;
(g) kupitia kwa sheria, kuhakikisha kwamba jamii zinapewa fidia au mrabaha kwa kutumiwa kwa turathi zao za kitamaduni;
(h) kukuza, pale inapohitajika, matumizi ya mifumo ya kitamaduni ya ukulima, na vyakula na vinyaji vya kiasili; na
(i) kupitia kwa sheria, kutambua na kulinda umiliki wa mbegu na mimea ya kiasili, sifa zao za kimaumbile na matumizi yao na jamii za Kenya.

## SURA YA SITA

### SHERIA YA HAKI

**Sehemu ya 1- Vipengele vya jumla kuhusiana na Sheria ya Haki**

**Haki na uhuru wa kimsingi** –

**28.** (1) Sheria hii ya Haki ni kiungo muhimu katika utawala wa kidemokrasia nchini Kenya na ndiyo msingi wa sera za kijamii, kiuchumi na kitamaduni.
(2) Umuhimu wa kutambua na kulinda haki za kibinadamu na uhuru muhimu ni kulinda heshima ya watu binafsi na jamaa na kukuza haki za kijamii na utambuaji wa uwezo wa binadamu wote.
(3) Haki na uhuru wa kimsingi zinazotajwa katika sura hii-
(a) ni za kila mtu binafsi na wala hazitolewi na serikali;
(b) hazitengi haki na uhuru mwingine wa kimsingi ambao haukutajwa katika Sura hii, lakini zinazotambuliwa na kukubaliwa na sheria, ila endapo ni kwa kiwango ambapo hazikubaliani na sura hii; na
(c) zinazingatia mipaka inayoelezwa katika Katiba hii.

**Utekelezaji wa Sheria ya Haki**

**29.** (1) Sheria ya Haki inahusu sheria zote na inajumlisha mashirika yote ya Serikali na watu wote. –
(2) Kila mtu atafurahia haki na uhuru wa kimsingi uliotajwa katika Sheria ya Haki, kwa kiwango kikubwa kuambatana na hali ya haki au uhuru wa kimsingi.
(3) Katika kutekeleza kipengele Sheria ya Haki, mahakama inapaswa-
(a) kutekeleza sheria kwa kiwango ambacho hakiathiri haki au uhuru wowote wa kimsingi; na
(b) kuegemea fasiri inaendana na utekelezaji wa haki au uhuru wa wa kimsingi.
(4) Katika kufasiri Sheria ya Haki, mahakama, mahakama maalumu, Tume ya Haki za Kibinadamu na maswala ya Kijinsia au mamlaka nyingine zitakuza-
(a) maadili yanayoongoza jamii huru na ya kidemokrasia kulingana na heshima ya ubinadamu, ulinganifu, usawa, na uhuru; na
(b) imani, madhumuni na kusudi la Sheria ya Haki.
(5) Wakati wa utekelezaji wa haki yoyote chini ya Vifungu 61 hadi 66, endapo serikali inadai kuwa haina raslimali za kutekeleza haki hiyo, Shirika la kiserikali,mahakama, mahakama maalumu, Tume ya Haki za Kibinadamu na Maswala ya Kijinsia au mamlaka nyingine yoyote itaongozwa na kanuni zifuatazo –
(a) ni jukumu la serikali kuonyesha kuwa raslimali hazipo;
(b) katika kugawa raslimali, serikali ina jukumu la kuipa kipaumbele uhakikishaji wa uwezekano mkubwa wa kufurahia haki au uhuru wa kimsingi kwa kuzingatia hali halisi, ikiwemo kutengwa kwa baadhi ya makundi au watu binafsi; na
(c Mahakama, mahakama maalumu, Tume ya Haki za Kibinadamu na Maswala ya Kijinsia au mamlaka nyingine haipaswi kuingilia uamuzi wa Asasi ya serikali kuhusu ugavi wa raslimali zilizopo, hasa kwa misingi kuwa utakuwa umefikia uamuzi tofauti.

**Utekelezaji wa haki na uhuru wa kimsingi**

**30.** (1) Ni jukumu la kimsingi la serikali na kila Asasi ya serikali kuzingatia, kuheshimu, kulinda, kukuza na kuhakikisha haki na uhuru wa kimsingi katika Sura hii, ilivyokatika utumizi wa nguvu na majukumu yao.
(2) Serikali itachukua hatua za kisheria, kisera na nyinginezo kuafiki utambuaji wa haki zinazotolewa chini ya vifungu 61 hadi 66
(3) Bunge na Tume ya Haki za Kibinadamu na Maswala ya Kijinsia zitaweka viwango vya upataji haki zilizotajwa katika sura (2)
(4) Serikali itatambua na kurahisisha jukumu la makundi ya raia katika udumishaji na ulinzi wa haki na uhuru wa kimsingi vilivyomo katika Sheria ya Haki.
(5) Mashirika yote ya serikali na maofisa wa serikali wana jukumu la kuelewa, kujitahidi wenyewe kukabiliana na mahitaji ya makundi maalumu katika jamii, wakiwemo wanawake, wazee, walemavu, watoto, vijana na makundi yaliyotengwa, jumuia tengwa na wa jumuia fulani za kikabila, kidini na kitamaduni.
(6) Serikali itaweka na kutekeleza sheria kurahisisha utimizaji wa malengo yake ya kimataifa kwa mujibu wa haki za kibinadamu na uhuru wa kimsingi na itapaswa -
(a) kutoa ripoti kwa wakati unaofaa kwa mashirika ya kimataifa ya haki za kibinadamu kuhusu utekelezaji wa maafikiano kuhusu haki za kibinadamu na vyombo vinginevyo;
(b) kuchapisha ripoti zitakazotolewa na serikali kwa mashirika ya kimataifa ya haki za kibinadamu kwa muda unaostahili na kurahisisha majadiliano na mijadala ya umma na kushiriki kwa mashirika ya kijamii kabla ya kurekebishwa na kuwasilishwa kwa ripoti hizo.
(7) Serikali itasambaza kwa umma Maoni na Mapendekezo ya Jumla ya mashirika ya kimataifa ya haki za kibinadamu kuhusiana na utekelezaji wa malengo yake ya kimataifa
(8) Serikali ya kitaifa inapaswa kutangazia bunge kuhusu endapo na jinsi inavyokusudia kutekeleza mapendekezo hayo.
(9) Serikali itaweka mifumo dhabiti ya kuipa nguvu kamili mielekeo ya Sheria ya Haki

**Utekelezaji wa Sheria ya Haki**

**31.** (1) Mtu anayerejelewa katika sura (2) ana haki ya kutoa malalamiko kwa Tume ya Haki ya Kibinadamu na Maswala ya Kijinsia, na kuanzisha kesi , kudai kuwa haki au uhuru wa kimsingi uliodokezwa katika Sheria ya Haki havijazinga tiwa,zimekiukwa, zimevunjwa au zimetishiwa –
(2) Watu watakaotoa malalamiko kwa Tume au kuanzisha kesi kwa mujibu wa sura ya (1) ni -
(a) mtu anaimiza mslahi yake ya kibinafsi;
(b) mtu anayemwakilisha mtu mwingine asiyeweza kujiwakisha;
(c) mtu mwanachama wa, au kwa hiari ya kundi au tabaka fulani la watu;
(d) mtu aliyejitolea kwa niaba ya umma; na
(e) muungano uliojitolea kwa niaba ya mmoja au kundi miongoni mwa wanachama.
(3) Jaji Mkuu ataweka kanuni zinazoruhusu kesi zilizotajwa katika sura ya (1), hizi zitazingatia vigezo kwamba–
(a) haki za kulalamika zilizotolewa katika Kifungu hiki zinatekelezwa kwa ukamilifu;
(b) Urasmi unaohusiana na kesi hizo , ikiwemo kuanzishwa kwa kesi, unawekwa kwa kiwango cha chini, na hasa kwamba pakiwa na haja, mahakama itakubali kuwepo wa kesi kwa misingi ya rekodi zisizo na lazima ya urasmi;
(c) Hakuna fedha zitakazotozwa kwa kuanzisha kesi chini ya Kifungu hiki;
(d) Mahakama, kwa kuzingatia kanuni za haki za kimsingi haitazuiwa bila sababu na mahitaji madogo madogo; na
(e) Shirika au mtu binafsi mwenye ujuzi maalumu anaweza kwa idhini ya mahakama, kujitokeza kama rafiki ya mahakama.
(4) Kukosekana kwa kanuni zinazoangaziwa katika sura ya (3) hakutamnyima yeyote haki ya kuanzisha lalama chini ya Katiba hii na kusikizwa kwa lalama

hiyo na kushughulikiwa na mahakama.

**Mamlaka ya mahakama kudumisha na kutekeleza Sheria ya Haki**

**32.** (1) Mahakama ya Kikatiba na Mahakama Kuu zina mamlaka kwa mujibu wa Vifungu 203 na 204 kusikiliza maombi ya kusikizwa upya kwa lalama dhidi ya ukiukaji wa haki za kibinadamu au uhuru wa kimsngi uliotajwa katika Sheria ya Haki.

(2) Bunge litatunga sheria kutoa uwezo wa kiasili kwa mahakama za chini katika kusikiza maombi ya kusikizwa upya kwa ukiukaji wa Sheria ya Haki.

(3) Katika kesi yoyote inayoletwa mbele yake chini ya Kifungu 31, mahakama inaweza kutoa usaidizi, ikiwemo-

(a) kukiri haki;
(b) agizo la mahakama;
(c) amri ya uhifadhi;
(d) utangazaji kutotakikana tena kwa sheria yoyote inayotatiza Sheria ya Haki na haikubaliwi kwa misingi ya Kifungu 33;
(e) amri ya kufidiwa dhidi ya Serikali au mtu yeyote anayehusika na uvunjaji wa haki au uhuru wowote wa kimsingi; na
(f) amri ya marekebisho ya kisheria

(4) katika vikao vya mahakama dhidi ya mamlaka ya umma kwa kukiuka Sheria ya Haki, mahakama huenda ikakosa kumtoza mshtaki gharama, au aliyetuma ombi isipokuwa mahakama ikigundua kuwa kesi hiyo haikuwa na maana au haikustahili.

**Mipaka ya haki na uhuru wa kimsingi**

**33.** (1) Hakuna haki au uhuru wowote wa kimsingi unaotajwa katika Sheria ya Haki unaoweza kuwekewa mipaka isipokuwa-

(a) kwa mpaka au ufaafu uliolezwa wazi katika kifungu kinachojumuisha haki hiyo au uhuru huo wa kimsingi au kisheria; na
(b) kwa kiwango kuwa mipaka hiyo haikubaliki katika jamii huru na ya kidemokrasia kwa mujibu wa heshima ya ubinadamu, usawa na uhuru ikizingatiwa vipengele vyote muhimu ikidwemo-
(i) hali ya haki hiyo au uhuru huo wa kimsingi;
(ii) umuhimu wa jukumu la mpaka huo;
(iii) hali na kiwango cha mipaka hiyo;
(iv) haja ya kuhakikisha kuwa ufurahiaji wa haki hizo na uhuru huo wa kibinafsi na mtu yeyote hautatizi haki na uhuru wa kimsingi wa wengine; na
(v) uhusiano uliopo kati ya mpaka na jukumu lake na endapo kuna njia nyingine zisizotatiza sana kuafikia jukumu hilo.

(2) Licha ya ibara ya (1), kifungu cha kisheria kinachowekea mipaka haki au uhuru wa kimsingi-

(a) haikubaliki katika sheria iliyotungwa au kurekebishwa baada ya siku ya kutekeleza katiba hii, isipokuwa sheria hiyo ikidhihirisha nia ya kuzuia haki hiyo au uhuru huo na hali na kiwango cha mipaka hiyo;
(b) haitachukuliwa kama uzuiaji haki au uhuru uliotajwa katika Sheria ya Haki isipokuwa pale ambapo kipengele cha sheria kinaeleza wazi na kwa yakini kuhusu haki au uhuru wa kimsingi unaopaswa kuzuiwa na hali au kiwango cha mipaka hiyo; na
(c) haitazuia haki au uhuru wa kimsingi unaotajwa katika Sheria ya Haki ili kupuuza maswala nyeti na muhimu katika haki hiyo.

(3) Serikali au mtu anayetaka kutosheleza kumnyima haki mtu atapaswa kuthibitishia mahakama, mahakama maalumu au mamlaka nyingine kuwa mahitaji ya Kifungu hiki yamezingatiwa.

(4) Maelezo ya Sura hii kuhusu usawa yatakubaliwa hadi kwa viwango vya utekelezaji wa Sharia ya Kiislamu kwa waumini wa Kiislamu kwa mujibu wa hadhi zao za kibinafsi, hali ya ndoa, talaka na urithi.

**Haki na uhuru unaoweza kuwekewa mipaka**

**34**. Licha ya chochote katika Katiba hii, hakutakuwa na uwekaji mipaka kwa haki na uhuru wa kimsingi ufuatao -

(a) uhuru dhidi ya mateso, unyanyasaji au adhabu zilizokiuka ubinadamu;
(b) uhuru dhidi ya utumwa;
(c) haki ya kusikiziwa mashtaka ; na
(d) haki ya kuitikiwa amri ya kufikishwa mahakamani

**Sehemu ya 2- Haki na uhuru wa kimsingi**

**Haki ya kuishi**

**35.** (1) Kila mtu ana haki ya kuishi.
(2) Mtu hatauwawa kiholela.

**Usawa**

**36.** (1) Kila mtu ni sawa mbele ya sheria na ana haki ya kulindwa na manufaa sawa ya sheria.

(2) Usawa unajumuisha ufurahiaji kwa ukamilifu haki zote na uhuru wote wa kimsingi.

**Uhuru dhidi ya kubaguliwa**

**37.** (1) Serikali haitabagua kwa vyovyote dhidi ya mtu yeyote kwa misingi yoyote ikiwemo asili, jinsia, mimba, hadhi ya kindoa, hali ya kiafya, asili ya kikabila au kijamii, rangi, umri, ulemavu, dini, dhamiri, imani, utamaduni, mavazi, lugha au kuzaliwa.

(2) Mtu hatambagua mwingine kwa ivyovyote dhidi ya mwingine kwa misingi hiyo.

(3) Mtu hatalazimishwa kuonyesha au kueleza kabila au asili ya mtu huyo.

(4) Licha ya ibara ya (1), Serikali itachukua hatua za kisheria na nyinginezo, ikiwemo japo sio lazima mipango ya usawa na sera zilizopangwa kushughulikia upya matatizo yaliyomkumba mtu yeyote au makundi kwa mujibu wa ubaguzi wa mbeleni.

(5) Hatua yoyote inayochukuliwa chini ya (4) itatoa nafasi kwa manufaa kuwa misingi ya haja maalumu.

**Jinsia**

**38.** Wanawake na wanaume wana haki ya kushughulikiwa kwa usawa ikiwemo haki ya kupata nafasi sawa katika shughuli za kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na kijamii.

**Wazee katika jamii**

**39.** (1) Wazee katika jamii wako huru kuendelea kufurahia haki zote na uhuru wa kimsingi uliodokezwa katika Sheria ya Haki.

(2) Serikali itachukua hatua za kisheria na za kisera kuwahakikishia wazee haki za-

(a) kushiriki kwa ukamilifu katika maswala ya jamii;
(b) kufanya shughuli za maendeleo yao;
(c kuwa huru dhidi ya aina zote za ubaguzi na kutumiwa;
(d kuishi katika maadili na heshima;
(e) kuhifadhi hadhi zao kijamii, kiuchumi na kisiasa; na
(f) kupata malezi ya kufaa na usaidizi kutoka kwa familia zao na Serikali.

(3) Bunge litatunga sheria kuweka shirika la kufafanua na kushauri kuhusu sera na mipango ya malezi na ulinzi wa wazee katika jamii.

**Vijana**

**40.** (1) Vijana wanajenga sehemu muhimu ya jamii na wanaruhusiwa kufurahia haki zote na uhuru wa kimsingi uliodokezwa katika Sheria ya Haki, ikizingatiwa haja zao za kipekee.

(2) Serikali itachukua hatua za kisheria na nyinginezo, ikiwemo japo sio lazima sera na mipango ya usawa ili-

(a) kukuza maswala ya vijana;
(b) kuhakikisha kushirikishwa kwa vijana katika siasa; na
(c) kuwalinda vijana dhidi ya tamaduni zinazodhalilisha maadili na hadhi ya maisha yao.

**Watoto**

**41**. (1) Watoto ni sehemu muhimu katika jamii.

(2) Ni jukumu la wazazi, familia, jamii na serikali kuwalea, kuwalinda na kuwasomesha watoto.

(3) Watoto wote, ama waliozaliwa katika ndoa au nje ndoa, wako sawa mbele ya sheria na wana haki sawa chini ya Katiba hii.

(4) Maslahi bora ya mtoto yatakuwa na umuhimu mkubwa katika swala lolote kuhusiana na motto.

(5) Baba na mamaye mtoto, iwe wameoana au hawajaoana, wana jukumu sawa la kumtunza na kumshughulikia mtoto.

(6) Kila mtoto ana haki ya-

(a) jina na uraia kuanzia anapozaliwa na kusajiliwa kwa kuzaliwa kwao;
(b) malezi ya wazazi au yoyote mbadala wakitenganishwa na wazazi;
(c) elimu ya bure na ya lazima;
(d) kulindwa dhidi ya kubaguliwa, tamaduni za kuumiza, kutumiwa vibaya, kutupwa au kunyanyaswa;
(e) kulindwa dhidi ya aina yoyote ya kunyanyaswa na kazi yoyote itakayohatarisha maslahi yao;
(f) chakula cha kutosha, makazi, huduma za malezi ya kiafya na huduma za kijamii;
(g) kutolazimishiwa ghasia au kuadhibiwa katika njia mbovu, zilizokiuka ubinadamu shuleni na katika taasisi nyingine zinazohusika katika malezi ya watoto;
(h) kutoshiriki katika uhasama au kujiunga na mizozo ya kutumia silaha na kulindwa dhidi ya hali hizo;
(i) kutoshikwa au kufungwa isipokuwa endapo hiyo ndio hatua ya

mwisho, na, wakishikwa au kufungwa, washughulikiwe katika njia zinazotukuza maadili ya mtoto na kuzingatia haki zake, ikiwemo japo sio lazima haki za-

(i) kufungwa kwa muda kiasi kidogo tu;
(ii) kutenganishwa na watu wazima katika jela;
(iii) kupewa usaidizi wa kisheria na Serikali; na
(iv) kushughulikiwa katika njia, na kuweka katika hali ambazo zitazingatia ulemavu wa mtoto, endapo upo, jinsia na umri;

(j) kuwa na wakili aliyetolewa na Serikali na kwa gharama ya Serikali katika vikao vya mahakama kumhusu mtoto huyo, kando na yale yanayofikiriwa katika aya ya (k) endapo kutakosekana haki;

(k) kujua maamuzi yanayowahusu, kutoa maoni na maoni hayo kuzingatiwa, kulingana na jinsia na ukomavu wa mtoto huyo na hali ya uamuzi.

(7) Watoto wenye mahitaji maalumu wana haki ya kupewa ulinzi maalum wa Serikali na jamii.

(8) Serikali itachukua hatua za kisheria na nyinginezo kutekeleza maelezo ya Katiba hii na ya nyenzo za viwango vya kimataifa kuhusu haki za mtoto.

**Familia**

**42.** (1) Familia ndio kitengo cha kiasili na kimsingi cha jamii na msingi muhimu katika mpangilio wa jamii.

(2) Kila mtu mzima anayo haki ya kuoa mtu wa jinsi tofauti kutokana na makubaliano yao.

(3) Kila mtu mzima anayo haki ya kuanzisha familia.

(4) Wahusika katika ndoa wana haki sawa wakati wa kuoana, katika ndoa na wakati wa kuvunjwa ndoa yao.

(5) Bunge litatunga sheria inayotambua-

(a) ndoa zilizotekelezwa chini ya utamaduni wowote, au mfumo wowote wa kidini, kibinafsi au sheria ya familia; na

(b) Sheria ya kibinfsi au familia chini ya utamaduni wowote, au inayofuatwa na watu waumini wa dini fulani, kwa kiwango kwamba ndoa au mifumo kama hiyo inazingatia Katiba hii.

**Walemavu**

**43.** (1) Walemavu wana haki ya kufurahia haki zote na uhuru wa kimsingi uliodokezwa katika Sheria ya Haki na kuwa washiriki kwa ukamilifu katika jamii.

(2) Walemavu wana haki ya-

(a) kuheshimiwa na kupewa maadili ya kibinadamu ikiwemo, kushughulikiwa, kuzungumziwa na kurejelewa, katika miktadha rasmi au ya faragha katika njia na maneno yasiyowadunisha au kuwadhalilisha;

(b) kuafikia elimu na taasisi na vifaa vya walemavu vilivyomo katika jamii na kwa jinsi inavyopaswa kutumiwa kwa maslahi yao;

(c) kuafikia ipasavyo sehemu zote zinazofikwa na umma, usafiri wa umma na habari na mawasiliano;

(d) kutumia lugha ya ishara, Breli na njia nyingine mwafaka za mawasiliano;

(e) kushiriki katika maamuzi katika viwango vyote;

(f) kuwa na haki za sawa za kurithi, kuafikia, na kusimamia mali;

(g) kuafikia nyenzo na vifaa vinavyoweza kuwasaidia kuukabili ulemavu huo; na

(h) kushughulikiwa na kupewa nafasi katika anga zote za maisha ambazo ni bora na sawa kwa wenzao wengine katika jamii.

(3) Serikali itachukua hatua za kishheria na nyinginezo, ikiwemo maelezo maalumu kwa wanawake, ili kuhakikisha kuwa walemavu wanafurahia haki zote zinazorejelewa katika ibara ya (2).

**Makundi tengwa**

**44.** (1) Makundi tengwa yana uhuru wa kufurahia haki zote na uhuru wa kimsingi uliodokezwa katika Sheria ya Haki kwa misingi ya usawa, ikizingatiwa asili yao, utamaduni wao, hali na mahitaji yao maalumu.

(2) Serikali itachukua hatua za kisheria na nyinginezo kuweka mipango ya usawa iliopangwa kunufaisha makundi tengwa katika jamii.

(3) Hatua zinazorejelewa katika ibara ya (2) zitajumuisha hatua za kuhakikisha kuwa makundi tengwa-

(a) yanashiriki na kuwakilishwa kwa ukamilifu katika uongozi na katika anga zote za maisha ya kitaifa;

(b) yanapewa nafasi maalumu katoka nyanja za elimu na uchumi;

(c) yanapewa nafasi maalumu ya kuafikia ajira ya kufaidisha;

(d) yanasaidiwa kukuza tamaduni zao, lugha na kaida zao;

(e) yanasaidiwa kufikia maji, huduma za afya na mindo msingo ya usafiri;

(f) yanakuwa na nafasi sawa ya kufikia mahitaji yao ya kimsingi; na

(g) yanaishi maisha yasiyo na kubaguliwa, kunyanyaswa au kutumiwa vibaya.

**Hadhi ya kibinadamu**

**45.** (1) Kila mtu ana hadhi ya kuzaliwa na haki ya kuheshimiwa na kulindwa kwa hadhi hiyo –

(2)Hadhi ya kuzaliwa ya kila mtu-

(a) inajumuisha haki ya kuzika/kuchoma mabaki ya wafu katika njia ya heshima; na

(b) inaendelea hadi wakati wa kuzikwa au kuchomwa kwao.

**Uhuru na usalama wa mtu**

**46.** Kila mtu ana haki ya uhuru na usalama wake, unaojumuisha haki ya-

(a) kutonyimwa uhuru kiholela bila sababu mwafaka;

(b) kutofungwa bila kushtakiwa mahakamani, isipokuwa wakati wa hali ya hatari ambapo kifungo cha sampuli hiyo kinaelezwa katika Kifungu 74;

(c) kuwa huru dhidi ya aina zote za ghasia kutoka kwa umma au watu bianafsi;

(d) kutoteswa katika njia yoyote ile, iwe ya kimwili ay kisaikolojia;

(e) kutopewa adhabu ya kali au kushughulikiwa katika adhabu za kudhalilisha ubinadamu.

**Utumwa na kazi ya kulazimishwa**

**47.** (1) Hakuna mtu atayewekwa katika utumwa.

(2) Mtu hatahitajika kufanya kazi ya kulazimishwa.

**Usiri**

**48.** Kila mtu anayo haki ya usiri wake, inayojumuisha haki ya–

(a) kutosakwa kwao au maboma yao;

(b) mali yao kusakwa;

(c) milki zao kunyakuliwa;

(d) habari kuhusiana na familia zao au mambo yao siri kuulizwa au kufichuliwa kiholela; au

(e) siri za mawasiliano yao kuvunjwa.

**Uhuru wa dhamiri, dini, imani na maoni**

**49.** (1)Kila mtu ana haki ya uhuru wa kuwa na msimamo, dini, mawazo, imani na maoni -

(2) Kila mtu anayo haki, ama kibinafsi au na wengine katika jumuia, kwa wazi au kisiri, kufuata dini au imani yoyote kupitia ibada, maadhimisho, ikiwemo mazingatio ya siku za ibada, matendo na mafunzo.

(3)Kila jumuia ya kidini ina haki ya kuanzisha na kuendesha pahali pa mafunzo kwa gharama yake na kutoa maagizo ya kidini kwa watu wa jumuia hiyo wakati wa utoaji wa mafunzo hayo.

(4) Shughuli na maagizo ya kidini zinaweza kufanyiwa Nchini au katika taasisi za Kitaifa ikiwa-

(a) zinafanywa kwa misingi ya usawa; na

(b) mahudhurio katika shughuli na maagizo hayo ni ya kujitolea; na

(5) Mtu hapaswi kuzuiwa kuafikia taasisi yoyote, ajira au jengo au kufurahia haki yoyote kwa sababu ya imani zao za kidini.

(6) Mtu hatalazimishwa-

(a) kuapa kiapo kinachokwenda kinyume cha dini au imani yake au inayohusisha kuonyesha imani isiyoshikiliwa na mtu huyo;

(b) kuapa katika njia inayokwenda kinyume cha dini au imani ya mtu huyo au inayohusisha kuonyesha imani isiyoshikiliwa na mtu huyo;

(c) kupokea maagizo ya kidini au kushiriki katika au kuhudhuria sherehe au kuzingatia siku ya kupumzika au shughuli nyingine zinazohusiana na dini isiyo ya mtu huyo;

(d) kufanya, kuzingatia au kupitia kaida za kidini;

(e) kufichua imani za au misimamo ya kidini ya mtu huyo; au

(f) kushiriki katika kitndo chochote kisichoambatana na imani au dini ya mtu huyo.

**Uhuru wa kujieleza**

**50.**(1) Kila mtu ana haki ya uhuru wa kujieleza unaojumuisha -

(a) uhuru wa kutafuta, kupokea au kutoa habari au kauli;

(b) uhuru wa kubuni kisanii; na

(c) uhuru wa kiakademia na utafiti wa kisayansi.

(2) Haki inayorejelewa katika ibara ya (1) haifiki kwenye kiwango cha-

(a) propaganda ya vita;

(b) uchochezi wa ghasia

(c) hotuba za chuki; au

(d) utetezi wa chuki-

(i) unaojumuisha uchochezi wa kikabila, matusi yaw engine au uchochezi wa kusababisha maafa; au

(ii) unaotokana na misingi ya ubaguzi iliokataliwa kwa mujibu wa

kifungu 37.

(3) katika kutumia uhuru wa kujieleza, kila mtu ataheshimu haki na hadhi ya wengine.

**Uhuru wa vyombo vya habari**

**51.**(1) Uhuru na kujitegemea kwa vyombo vya matangazo, kuchapisha na vingine vya habari vya aina yoyote unahakikishwa.

(2) Serikali –

(a) haitasimamia au kuingilia mtu yeyote anayehusika na utangazaji, uchapishaji au usambazaji wa chapisho lolote au usambazaji wa habari kwa kutumia chombo chochote; au

(b) haitamwadhibu mtu yeyote kwa maoni au mawazo au maswala ya utangazaji, uchapishaji au usambazaji.

(3) Vyombo vya utangazaji na vyombo vingine vya habari vina uhuru wa kuanzisha chochote, isipokuwa kwa kuongozwa na taratibu za leseni ambazo-

(a) zimeratibiwa kuhakikisha udhibiti wa mawimbi ya hewa na aina nyingine usambazaji wa mawimbi; na

(b) haziingiliwi na serikali, hisia za kisiasa au za kibiashara.

(4)Vyombo vyote vya habari vianvyomilikiwa na serikali-

(a) vitakuwa huru kuweka makala ya kibinafsi ya kitahariri ya matangazo yao au mawasiliano mengine;

(b) havitaegemea upande wowote; na

(c) vitakuwa na nafasi ya kuwasilisha maoni tofauti tofauti na mawazo yanayokinzana.

(5) Bunge litatunga sheria itakayotoa nafasi ya kuanzisha shirika ambalo-

(a) litakuwa huru dhidi ya serikali au mwingilio wa kisiasa;

(b) litamulika maslahi ya sehemu zote za jamii; na

(c) litaweka viwango na kudhibiti na kuchunguza uzingatiaji wa viwango hivyo.

**Uwezo wa kuafikia habari**

**52.** (1) Kila mwananchi anayo haki ya kuafikia-

(a) habari ilizonazo na Serikali; na

(b) habari zozote zilizo na mtu mwingine na zinazohitajika ili kutekeleza au kulinda haki yoyote au uhuru wowote wa kimsingi.

(2) Kila mtu anayo haki ya kutaka kurekebishwa au kubatilishwa kwa habari zozote za uongo au za kupotosha zinazomhusu mtu huyo.

(3) Serikali itachapisha na kutangaza kila habari inayohusu taifa.

**Uhuru wa kutangamana**

**53.** (1) Kila mtu ana haki ya uhuru wa kutangamana -

(2) Haki hiyo inaendelea hadi kwa kutunga, kuendesha na kuendeleza mashirika.

(3) Mtu hatalazimishwa kujiunga na muungano wa aina yoyote.

(4) Serikali itachukua hatua za kisheria na kukubali sera za kutukuza kushiriki kwa mashirika ya kijamii katika maamuzi na katika kusimamia maswala ya umma katika viwango vyote vya serikali.

(5) Sheria yoyote kuhusu usajili wa miungano ya mashirika ya kijamii itahitaji kwamba-

(a) usajili huo hauwezi kuzuia bila sababu maalumu;

(b) usajili utakuwa mikononi mwa shirika litakalokuwa huru dhidi ya kuingiliwa na serikali au aina yoyote nyingine ya ushawishi wa kisiasa;

(c) gharama yoyote itakayotozwa haipaswi kuzidi ile inayohitajika kugharamia utaratibu huo;

(d) kutakuwa na haki ya kusikizwa kwa kesi hiyo kabla kubatilishwa kwa usajili huo;

(e) kunakuwa na rufaa kwa mahakama maalumu ya kujitegemea kubatilisha usajili.

(6) Sheria yoyote inayozingatia viwango vya utendakazi wa miungano ya mashirika ya kijamii, itaundwa kwa kushirikisha miungano husika.

**Mikutano, maandamano, migomo na malalamishi**

**54.** Kila mtu ana haki ya kukutana, kuandamana, kugoma, na kuwasilisha malalamishi yake kwa mamlaka ya umma endapo atafanya hivyo kwa amani, bila silaha na bila haja ya kuomba ruhusa.

**Haki za kisiasa**

**55.** (1) Kila mwananchi yuko huru kuchagua, ikiwemo haki ya –

(a) kuunda, au kushiriki katika uundaji wa chama cha kisiasa;

(b) kushiriki katika shughuli za, au kusajili wanachama kwa niaba ya chama; na

(c) kufanyia kampeni au kusababisha kampeni za chama cha kisiasa.

(2) Kila mwananchi ana haki ya kushiriki uchaguzi huru, wa haki na wa kila mara kwa-

(a) shirika au ofisi yoyote ya umma iliyobuniwa chini ya Katiba hii na inayofanya uchaguzi;

(b) kiongozi wa ofisi yoyote ya chama ambacho mwananchi huyo ni mwanachama.

(3) Kila mtu mzima ana haki ya-

(a) kusajiliwa kama mpigakura na kupiga kura ya siri katika uchaguzi wowote unaorejelewa katika ibara ya (2) na katika kura yoyote ya maoni; na

(b) kugombea wadhifa katika ofisi ya umma, au ofisi katika chama cha kisiasa ambacho wao ni wanachama na endapo atachaguliwa atashika usukani.

**Uhuru wa kutembea na kuishi**

**56.** (1)Kila mtu ana haki ya uhuru wa kutembea.

(2) Kila mtu ana haki ya kuishi nchini Kenya.

(3)Kila mwananchi ana haki ya kuingia, kubaki na kuishi kokote nchini Kenya.

**Wakimbizi na wanaotafuta hifadhi**

**57.**(1)Haki ya kutaka na kupata hifadhi inatambuliwa na itapeanwa kwa mujibu wa sheria na kaida za kimataifa kuhusu wakimbizi.

(2) Bunge litatunga sheria kuambatana na sheria na kaida za kimataifa, kuhusu watu wanaotafuta hifadhi au makao nchini Kenya.

**Uhuru wa biashara, kazi na taaluma**

**58.** (1) Kila mtu ana uhuru wa kuchagua biashara, kazi au taaluma.

(2) Ufanyaji wa biashara, kazi au taaluma utadhibitiwa na sheria.

**Ulinzi wa haki ya kumiliki mali**

**59**.(1)Isipokuwa kwa Kifungu 82, kila mtu ana haki ya kupata na kumiliki mali katika sehemu yoyote ya Kenya, ama kibinafsi au kwa kuungana na wengine.

(2) Bunge halitatunga sheria inayoruhusu Serikali au mtu yeyote –

(a) kumzuia mtu kuwa na mali ya aina yoyote;

(b) kumzuia kuwa na nia au kuwa na haki ya kuwa na mali kama hayo; au

(c) kuwekea mipaka au kuzuia kwa njia yoyote ufurahiaji wa haki yoyote chini ya Kifungu hiki kwa msingi wowote uliodokezwa katika Kifungu 37(1).

(3)Serikali haitamnyima mtu yeyote haki ya kuwa na mali ya aina yoyote, au nia ya kuwa na mali, au haki ya kuwa na mali ya aina yoyote isipokuwa endapo uzuiaji huo –

(a) unatokana na upataji ardhi au nia ya kutaka ardhi au mabadiliko ya nia ya kutaka ardhi, au kumiliki ardhi kwa mujibu wa Sura ya Saba; au

(b) ni kwa matumizi ya umma au ni kwa manufaa ya umma na inatekelezwa kwa mujibu wa Katiba hii au Sheria ya Bunge-

(i) inayotaka malipo kwa ukamilifu ya kumfidia mtu huyo kabla mali hayo kuchukuliwa;

(ii) inayomruhusu mtu yeyote aliye na nia au haki juu ya mali hayo uwezo wa kuafikia mahakama ya kisheria.

(4) Kipengele kinaweza kuundwa cha fidia ya kulipwa wakaazi wa ardhi hiyo kwa nia njema ambao huenda hawana uwezo wa kumiliki ardhi hiyo.

(5) Haki inayotambuliwa na kulindwa chini ya Kifungu hiki haijumlishi mali yoyote ambayo hayajapatikana kisheria.

**Mahusiano ya kikazi**

**60.**(1) Kila mtu ana haki ya kanuni sawa za kikazi.

(2) Kila mfanyakazi ana haki ya-

(a) kulipwa ipasavyo;

(b) masharti ya kufaa ya utendakazi;

(c) kuunda, kujiunga au kushirki katika shughuli na mipango ya vyama vya wafanyakazi; na

(d) kugoma

(3) Kila mwajiri ana haki ya-

(a) kuunda au kujiunga na miungano ya waajiri; na

(b) kushiriki katika shughuli na mipango ya miungano ya waajiri.

(4) Kila chama cha wafanyakazi na miungano ya waajiri ina haki ya-

(a) kuamua usimamizi wake, mipango na shughuli zake;

(b) kupanga; na
(c) kuunda na kujiunga na shirikisho.
(5) Kila chama cha wafanyakazi, muungano wa waajiri na mwajiri wana haki ya kushiriki katika maafikiano ya pamoja.

**Usalama wa kijamii**
**61.**(1) Kila mtu ana haki ya usalama wa kijamii
(2) Serikali itatoa usalama wa kutosha wa kijamii kwa watu wasioweza kujisaidia au wanaoategemea.

**Afya**
**62.** (1) Kila mtu ana haki ya afya inayojumuisha haki ya kupata huduma za malezi ya kiafya ikiwemo malezi ya afya ya uzazi.
(2) Hakuna mtu anayeweza kuzuiwa kupata matibabu ya dharura.

**Elimu**
**63**. (1) Kila mtu ana haki ya kupata elimu.
(2) Serikali itaanzisha mpango wa kutekeleza haki ya kila mtoto kupata elimu ya chekechea na msingi ya bila malipo na ya lazima na katika kufanya hivyo itazingatia watoto
(3) Serikali itachukua hatua kufanya elimu ya shule ya upili na vyuo kuwepo na kuafikika.
(4) Kila mtu ana haki ya kuanzisha na kutunza, kwa gharama yake, taasisi ya kibinafsi ya kutoa elimu inayozingatia mahitaji ya Katiba hii na inayoafiki viwango vilivyowekwa katika sheria.

**Makao**
**64.** Kila mtu ana haki ya kufikia nyumba bora na kwa viwango vya kufaa vya usafi.

**Chakula**
**65.** Kila mtu ana haki ya kuwa huru dhidi ya njaa na kupata chakula cha kutosha kwa ubora wa kukubalika -

**Maji**
**66.** Kila mtu ana haki ya kupata maji safi na salama katika viwango vya kutosha.

**Mazingira**
**67.** (1) Kila mtu ana haki ya –
(a) kupata mazingira safi na salama;
(b) kutunziwa mazingira kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo kupitia hatua za kisheria na nyinginezo ambazo-
(i) zinazuia uchafuzi wa mazingira na uharibifu wa ikolojia;
(ii) zinakuza uhifadhi; na
(iii) kulinda maendeleo yafaayo ya kiikolojia na matumizi ya raslimali asilia; na
(c) Kuafikia habari kuhusu mazingira.

**Lugha na utamaduni**
**68.** (1) Kila mtu ana haki kutumia lugha na kushiriki katika maisha ya kitamaduni ya chaguo lake.
(2) Mtu anayetoka katika jumuia ya utamaduni au lugha fulani hatanyimwa haki, pamoja na wanajumuia hiyo-
(a) kufurahia utamaduni wake na kutumia lugha yake; au
(b) kuunda, kujiunga na kudumisha vyama vya kitamaduni na kilugha na miungano mingine ya raia katika jamii.
(3) Mtu hatamlazimisha mwingine kufanya, kuzingatia au kupitia kaida zozote za kitamaduni.

**Haki za watumiaji**
**69.** (1) Watumiaji wana haki ya-
(a) kupata bidhaa na huduma za ubora wa kukubalika;
(b) habari za kuwafaa kunufaishwa vilivyo na bidhaa na huduma hizo;
(c) kulindwa afya yao, usalama wao, na maslahi yao ya kiuchumi; na
(d) kufidiwa kwa hasara au matatizo yatayotokana na bidhaa au huduma hizo.
(2) Bunge litatunga sheria ya kuhakikisha ulinzi wa watumiaji na wa matangazo huru, kweli na ya kufaa.
(3) kifungu hiki kinaangazia bidhaa na huduma zitakazotolewa na mashirika ya umma au watu binafsi.

**Hatua ya haki za kiutawala**
**70.**(1) Kila mtu ana haki ya kuwajibikiwa na utawala kwa haraka, ipasavyo, kisheria na njia za usawa-
(2) Kila mtu ambaye haki yake au uhuru wake wa kimsingi umeathiriwa au unaweza kutatizwa kabisa na hatua ya kiutawala ana haki ya kupewa sababu katika maandishi ya hatua hiyo.
(3) Bunge litatunga sheria ya kuidhinisha haki zilizotajwa katika ibara na sheria hiyo -
(a) itatoa nafasi ya kurekebishwa kwa hatua hiyo ya kiutawala na mahakama au, ikiwezekana mahakama huru maalumu na isiyoegemea upande wowote; na
(b) kukuza uongozi wa kufaa.

**Uwezo wa kupata haki**
**71.** Serikali itahakikisha uwezekano wa kupa haki kwa watu wote na malipo yoyote yakihitajika, yatakuwa ya kufaa na hayatazuia uwezekano wa kufanyiwa haki.

**Haki za mahabusu**
**72.** (1) Kila mahabusu ana haki ya-
(a) kuarifiwa kwa upole katika lugha anayoelewa kuhusu-
(i) sababu ya kushikwa;
(ii) haki ya kunyamaza; na
(iii) matokeo ya kutonyamaza;
(b) kunyamaza;
(c) kuwasiliana na wakili na watu wengine ambao usaidizi wao unahitajika;
(d)kutolazimishwa kutoa ikirari au ukubalifu ambao unaweza kutumiwa katika ushahidi dhidi yao;
(e) kuwekwa kando na watu wanaohudumia kifungo;
(f) kufikishwa mbele ya mahakama haraka iwezekanavyo, lakini sio zaidi ya saa arobanne na nane baada ya kushikwa au sio baada ya kukamilika kwa siku ya kwanza ya vikao vya mahakama baada ya kumalizika kwa hizo saa arobanne endapo hizo saa arobanne zimekamilika wakati ambapo vikao vya mahakama haviendelei au kwa siku isiyo ya mahakama;
(g) Kufunguliwa mashtaka au kuarifiwa kuhusu sababu ya kukamatwa kwake, au kuachiliwa huru siku yake ya kwanza ya kufikishwa mahakamani; na
(h) kuachiliwa kwa dhamana kwa sababu zinazoeleweka kabla kushtakiwa isipokuwa kukiwa na sababu nyingine za kulazimisha kutendeka kwa kinyume cha dhamana hiyo.
(2) Mtu hatawekwa rumande kwa kosa linaloweza kuadhibiwa kwa kutozwa faini pekee au kufungwa gerezani kwa muda usiozidi miezi sita.

**Haki katika kusikizwa kwa kesi**
**73.** (1) Kila mtu ana haki ya kutaka mzozo wowote unaoweza kusuluhishwa kwa kutumia sheria kuamuliwa katika kikao cha haki mbele ya mbele ya mahakama au, ikiwezekana shirika au mahakama maalumu iliyo huru na isiyoegemea upande wowote.
(2) Kila mshtakiwa ana haki ya kesi yake kusikizwa kwa njia ya haki, ikiwemo haki ya-
(a) kuaminiwa kutokuwa na kosa hadi ithibitishwe kinyume;
(b) kuarifiwa kuhusu mashtaka na taarifa ya kutosha kuyahusu;
(c) kuwa na wakati na vifaa vya kutosha kutayarisha nyenzo za kujitetea;
(d) kushtakiwa mbele ya mbele ya mahakama ya umma iliyowekwa na Katiba hii;
(e) kuanzishiwa na kumaliziwa mashtaka bila kucheleweshwa;
(f) kuwepo wanaposhtakiwa isipokuwa endapo tabia ya mshtakiwa inatatiza vikao vya mashtaka hayo;
(g) kuchagua, na kuwakilishwa na wakili na kuelezwa kuhusu haki hii moja kwa moja;
(h) kuwa na wakili aliyetolewa na Serikali kwa gharama ya Serikali yenyewe, endapo haki ya msingi itakosekana na aarifiwe kuhusu haki hii moja kwa moja;
(i) kunyamaza, na kutotoa ushahidi wakati wa vikao;
(j) kuleta na kupinga ushahidi;
(k) kutolazimishwa kutoa ushahidi wa kuwafunga;
(l) kuwa na usaidizi wa atakayetafsiri bila ya kulipishwa endapo mshtakiwa hawezi kuelewa lugha inayotumiwa katika mashtaka;
(m) kutohukumiwa kwa kitendo, au kosa ambalo wakati wa utendekaji au ukosaji halikuwa-
(i) kosa nchini Kenya; au

Imechapishwa mnamo Novemba 17, 2009 na Kamati ya Wataalam Kuhusu Marekebisho ya Katiba Kulingana na Sehemu 32(1)(a)(i) ya Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya, 2008.

(ii) kosa la jinai chini ya sheria ya kimataifa;
(n) kutoshtakiwa kwa kosa la kulinganishwa na tendo au kosa ambalo mtu huyo ashawahi ama kuachiliwa au kuhukumiwa kwalo;
(o) kunufaika kwa angalau adhabu ndogo kabisa katika adhabu zilizoagizwa endapo adhabu iliyoagizwa kwa kosa lake imebadilishwa kati ya muda wa utendekaji wa tendo hilo na wakati wa kuhukumiwa; na
(p) kukata rufani au kurejelewa kwa kesi hiyo na mahakama ya kiwango cha juu.

(3) Kila mara Kifungu hiki kinataka taarifa kupeanwa, taarifa hiyo itatolewa katika lugha anayoelewa mtu huyo.
(4) Ushahidi unaopatikana katika njia inayokiuka haki yoyote au uhuru wowote wa kimsingi uliodokezwa katika Sheria ya Haki utawachwa endapo utekelezaji wa ushahidi huo utafanya mashtaka kukosa haki au uwe kizuizi katika utoaji haki.
(5) Mshtakiwa anayeshtakiwa kwa kosa fulani, kando na kosa ambalo mahakama inaweza kukamilisha kwa haraka, atakuwa na ruhusa endapo ataomba ya kupata nakala ya rekodi za vikao vya mashtaka.
(6) Mshtakiwa na haki ya kupata nakala ya vikao vya mashtaka kwa wakati unaofaa baada ya kukamilishwa kwa vikao hivyo, kwa malipo fulani inavyoagizwa na sheria.
(7) Mtu anayehukumiwa kwa kosa la jinai na ambaye rufani yake imetupiliwa mbali na mahakama ya ngazi za juu ambapo huyo mtu alikuwa na haki ya kukata rufani, au mtu ambaye hakukata rufaa kwa muda unaoruhusiwa kufanya hivyo, anaweza kulalamikia Mahakama Kuu ili kufanywe mashtaka mapya endapo kutakuwa na ushahidi mpya na wa kukubalika.
(8) Hakuna chochote katika Kifungu hiki kitakachozuia kutengwa kwa wanahabari au raia wengine dhidi ya vikao vyote au vyovyote vya mahakama kwa sababu za kuwalinda mashahidi na wahusika wengine, maadili, amri ya umma au usalama wa kitaifa itakavyohitajika katika jamii huru na ya kidemokrasia.

**Haki za walio vizuizini**

**74.** (1) Mtu yeyote anayezuiliwa chini ya sheria, awe amehukumiwa au la, anazo haki zote na uhuru wa kimsingi uliopo chini ya Katiba hii, isipokuwa endapo ni kwa ikwango kwamba haki au uhuru huo wa kimsingi hauambatani kabisa na sababu yake ya kuwa jela -
(2) Mtu yeyote aliye kizuizini atakuwa na haki ya kufukishwa mahakamani ili isikizwe kesi yake.
(3) Bunge, kupitia sheria, litatoa nafasi ya kushughulikiwa kibinadamu kwa walio kizuizini kwa kuzingatia nyenzo mwafaka za haki za banadamu kimataifa.

**Hali ya hatari**

**75.** (1) Hali ya hatari inaweza kutangazwa tu kwa kuzingatia Kifungu 158(5) na endapo-
(a) Nchi inatishiwa na vita, uvamizi, upinzani mkubwa, vurugu, janga la kitaifa au dharura nyingine zinazohusisha umma; na
(b) endapo utangazaji huo utafaa ili kupata suluhu kwa dharura inayosababisha tangazo hilo.

(2) Tangazo la hali ya hatari, na sheria yoyote itakayotungwa au hatua nyingine itakayochukuliwa kutokana na tangazo hilo, itatekelezeka tu endapo-
(a) kwa matumaini; na
(b) kwa muda usiozidi siku kumi na nne kutoka siku ya kutangazwa hali hiyo ya hatari, isipokuwa endapo Bunge la kitaifa linaamua kuendeleza tangazo hilo.

(3) Bunge la kitaifa linaweza kuendeleza tangazo la hali ya hatari –
(a) kutokana na uamuzi uliochukuliwa-
(i) kufuatia mijadala ya umma Bungeni; na
(ii) na watu wengi inavyodokezwa katika ibara (4); na
(b) kwa muda usiozidi miezi miwili kwa kila mojawapo.

(4) Uongezaji wa kwanza wa muda wa hali ya hatari unataka kura za kuunga mkono za angalau thuluthi-mbili ya wabunge, na utakaofuatia unahitahitaji angalau robo-tatu ya wabunge.
(5) Mahakama ya Kikatiba inaweza kuamua kuhusu ufaafu wa-
(a) tangazo la hali ya hatari;
(b) ongezeko lolote la muda wa tangazo la hali ya hatari; na
(c) sheria yoyote itakayotungwa au hatua yoyote nyingine inayochukuliwa, kwa sababu ya tangazo la hali ya hatari.

(6) Sheria yoyote inayotungwa kwa sababu ya tangazo la hali ya hatari, inaweza kuzuia au kutoka kwa Sheria ya haki endapo tu ni kwa kiwango kwamba-
(a) uzuiaji huo unastahili kutokana na dharura hiyo; na
(b) sheria hiyo inaambatana na majukumu ya Jamhuri chini ya sheria ya kimataifa kuhusiana na hali ya hatari.

(7) Sheria inayorejelewa katika ibara ya (6)-
(a) itachapishwa katika Gazeti rasmi la serikali punde ikiweza kutumika baada ya kutungwa; na
(b) haitatumika hadi itakapochapishwa.

(8) Tangazo la hali ya hatari au sheria inayotungwa au hatua yoyote nyingine inayochukuliwa kwa sababu ya tangazo lolote, haitaruhusu au kuamrisha kufidiwa kwa Serikali au mtu yeyote kwa misingi ya tendo lolote la ukiukaji sheria.

**Tume ya Haki na Maswala ya Kijinsia**

**76.** (1) Kuna Tume buniwa ya Haki za Kibinadamu na Maswala ya Kijinsia.
(2) Tume ya Haki za Kibinadamu na Maswala ya Kijinsia inajumuisha-
(a) Mwenyekiti;
(b) Kamishna wa jinsia;
(c) Mtetezi wa Watu, atakayekuwa na jukumu maalumu la kuhakikisha uongozi wa haki;
(d) Kamishna wa Haki za Wanyonge, atakayekuwa na jukumu maalumu la kuhakikisha wanyonge kutoka makabila na dini fulani na jumuia zilizotengwa; na
(e) makamishna wengine watano watakaoteuliwa kwa kuzingatia Katiba hii.

(3) Kwa makamishna wanaorejelewa katika ibara ya (2)(e)-
(a) mmoja atakuwa na elimu ya kitaaluma na uzoefu wa na jukumu maalumu katika maswala yanayohusu watoto;
(b) mmoja atakuwa mlemavu aliye na elimu na uzoefu wa na jukumu maalumu katika maswala yanayohusu walemavu;
(c) mmoja atakuwa na elimu na uzoefu wa na jukumu maalumu katika maswala yanayohusiana na mahitaji ya kimsingi; na
(d) mmoja atakuwa na elimu na uzoefu wa na jukumu maalumu katika maswala kuhusu haki za wazee.

(4) Kwa kutii kipengele chochote kinachogusia Tume nyingine, majukumu ya Tume hii ni-
(a) kukuza heshima ya haki za kibinadamu na kujenga mazoea ya kuheshimu haki za kibinadamu;
(b) kukuza ulinzi, ujenzi na upatikanaji wa haki za kibinadamu katika taasisi za umma na za kibinafsi;
(c) kukuza viwango vya juu vya haki za kibinadamu katika Jamhuri hii;
(d) kusimamia, kuchunguza na kutoa ripoti kuhusu uzingatiaji wa haki za kibinadamu katika anga zote maisha katika Jamhuri;
(e) kuchunguza tendo au kosa lolote katika uongozi wa umma unaodaiwa kukosa haki au kuwa mbaya;
(f) kuchunguza ukiukaji wa haki za kibinadamu katika vikosi vya usalama wa kitaifa na katika mahusiano yao na umma;
(g) kuchukua hatua za kuhakikisha marejeleo salama ya mazingira ambamo haki za kibinadamu zilikiukwa;
(h) kuhakikisha kwamba taasisi za Serikali yanashughulikia haja za watu, na kutoa suluhu la moja kwa moja endapo wanashindwa;
(i) kupokea malalamishi kuhusu utumizi mbaya wa mamlaka, kutoshughulikia kwa haki kutokana na kubaguliwa kwa misingi ya kijinsia au vinginevyo, kukosekana kwa haki, na ufisadi, ukiukaji sheria, unyanyasaji au mienendo isiyozingatia haki;
(j) kuhusu haki za kibinadamu, itaanzisha yenyewe au kwa misingi ya malalmishi yaliyotolewa, uchunguzi na utafiti na kutoa mapendekezo ya kuimarisha utendakazi wa mashirika ya Serikali;
(k) kuimarisha viwango vya umilisi, uaminifu, uadilifu na uwazi katika kuhudumia umma;
(l) kupendekeza marekebisho ya sheria isiyo na haki au isiyoambatana na Katiba hii;
(m) kupendekeza marekebisho katika shughuli za taasisi za Serikali ambazo zinakiuka haki au haziaambatani na Katiba hii; na
(n) kuwa kama ajenti mkuu wa serikali ya kitaifa katika kuhakikisha udumishaji wa wajibu uliopo chini ya makubaliano kuhusu haki za kibinadamu.

## SURA YA SABA

**ARDHI NA MALI**

**Kanuni za sera ya ardhi**

**77.** (1) Ardhi ndio raslimali ya kimsingi ya Kenya na ndio msingi wa maisha ya watu, na itamilikiwa, kutumiwa na kutunzwa katika njia za kisawa, mwafaka, zalishi na za inayofaa.
(2)Serikali ya taifa itafafanua na kurekebisha panapo haja sera ya kitaifa kuhusu kwa kuhakikisha kanuni zifuatazo-

(a) uwezo sawa wa kuafikia ardhi na raslimali nyingine;
(b) usalama wa haki za ardhi kwa wanaoimiliki, watumizi na wanaoikalia kwa nia njema;
(c) utunzaji mwafaka na zalishi wa raslimali za ardhi;
(d)usimamizi wa ardhi kwa uwazi na kwa gharama ya kufaa;
(e) hifadhi na ulinzi bora wa maeneo nyeti kiikolojia;
(f) uepukaji wa mbaguano wa kijinsia katika sheria, vidhibiti, mila na desturi zinazohusiana na mali yaliyomo katika ardhi hiyo; na
(g) kuhimiza jumuia kutatua mizozo kuhusu ardhi kupitia mifumo ya kiasili inayoambatana na Katiba hii.

**Utoaji na uainishaji wa ardhi**

**78.**(1) Ardhi yote nchini Kenya ni ya Wakenya wote kama taifa, jumuia na kama watu binafsi.
(2) Ardhi yote nchini Kenya inaelezwa kama mali ya umma, jumuia au ya kibinafsi -

**Ardhi ya umma**

**79.** (1) Ardhi ya umma ni -
(a) ardhi ambayo wakati wa kuanza kutumika kwa Katiba hii ni mali ya serikali inavyoelezwa na Sheria iliyopo ya Bunge wakati huo;
(b) ardhi inayomilikiwa, kutumiwa au kukaliwa kisheria na taasisi yoyote ya Serikali, isipokuwa pale ambapo ardhi hiyo inakaliwa chini ya kodi ya kibinafsi;
(c) ardhi iliyokabidhiwa Serikali kwa njia ya kurudishiwa au kusalimishwa;
(d) ardhi ambayo haimilikiwi kisheria na mtu yeyote au jumuia yoyote;
(e) ardhi ambayo mrithi wake hawezi kutambuliwa kivyovyote kisheria;
(f) ardhi yoyote iliyo na madini au mafuta inavyoelezwa kisheria;
(g) misitu ya serikali kando na misitu inayorejelewa katika Kifungu 80 (2)(e), hifadhi ya wanyama, chemichemi za maji, hifadhi za wanyama na sehemu maalumu zilizolindwa;
(h) barabara na mitaa yote iliodokezwa na Sheria ya Bunge;
(i) mito yote, maziwa yote na sehemu nyingine za maji kama inavyoelezwa na Sheria ya Bunge;
(j) mipaka ya maji na chini yake;
(k) ardhi yote kati ya nyanda za juu na za chini za maji;
(l) ardhi yoyote ambayo haijaainishwa kama ya kibinafsi au kijumuia chini ya Katiba hii; na
(m) ardhi yoyote itakayotangazwa kuwa ya umma na Sheria ya Bunge.
(3) Ardhi ya umma, inayoainishwa chini ya ibara (1)(a) hadi (e) itatolewa na kumilikiwa na serikali ya wilaya kwa amana kwa niaba ya wakaazi wa wilaya hiyo na itasimamiwa kwa niaba yao na Tume ya Kitaifa kuhusu Ardhi.
(4) Ardhi ya umma haitatolewa au kutumiwa isipokuwa kwa kuzingatia Sheria ya Bunge inayofafanua hali na masharti ya kutolewa au matumizi hayo.

**Ardhi ya jumuia**

**80.**(1) Ardhi ya jumuia itatolewa na kumilikiwa na jumuia zinazotambuliwa kwa misingi ya kikabila, kitamaduni au maslahi yake.
(2)Kwa mujibu wa ibara ya (1) ardhi ya umma inajumuisha-
(a) ardhi yote inayochukuliwa kisheria na serikali za wilaya kama ya amana;
(b) ardhi iliyosajiliwa kisheria katika jina la wawakilishi wa kundi hilo chini ya vipengele vya sheria yoyote wakati wa utekelezaji wake;
(c) ardhi inayomilikiwa, kusimamiwa au kutumiwa na jumuia maalumu kama misitu ya jamii, malisho ya mifugo au madhabahu;
(d) ardhi yoyote iliyokabidhiwa jamii fulani kupitia njia yoyote ya kisheria;
(e) ardhi zilizorithiwa kutoka kwa wazazi na ardhi ambazo kiasilia zilikaliwa na jumuia za wawindaji; na
(f) ardhi nyingine yoyote itakayotangazwa na Sheria ya Bunge kuwa ya jumuia, lakini haitajumuisha ardhi ya umma ilivyodokezwa katika Kifungu 79.
(3) Ardhi yoyote ya jumuia ambayo haijasajiliwa itashikiliwa kwa amana na serikali za
(4) Ardhi ya jumuia haitatolewa au pengine kutumiwa isipokuwa kwa misingi ya sheria inayofafanua hali na viwango vya haki za kila mwanajumuia hiyo au wanajumuia wote kwa pamoja.
(5) Bunge litatunga sheria kuidhinisha Kifungu hiki.

**Ardhi ya kibinafsi**

**81.** Ardhi ya kibinafsi inajumuisha -
(a) ardhi yoyote iliyosajiliwa na inayomilikiwa na mtu yeyote chini ya umilikaji ardhi bila masharti;
(b) ardhi inayomilikiwa na mtu yeyote kwa kukodi; na
(c) ardhi yoyote nyingine iliyotangazwa na au chini ya Sheria ya Bunge.

**Umilikaji Ardhi na wasio raia**

**82.**(1) Mtu asiye raia anaweza kumiliki au kutumia ardhi kwa misingi ya kukodisha pekee, na mkataba huo hata ukitolewa hautazidi miaka tisini na tisa.
(2) Masikizano, makubaliano au uhawilisho wa aina yoyote unaompa mtu asiye raia wa Kenya uwezo wa kumiliki ardhi kwa zaidi ya miaka tisini na tisa utabatilishwa.
(3) Kwa nia ya Kifungu hiki, kampuni au shirika lolote litakubaliwa tu kuwa sehemu ya nchi endapo wananchi wanamiliki hisa zote au nyingi katika hisa hizo.
(4) Bunge linaweza kutunga sheria kuweka vipengele zaidi vya uendeshaji wa vipengele vya Kifungu hiki.

**Udhibiti wa matumizi ya ardhi**

**83.**(1) Serikali ina mamlaka ya kudhibiti ardhi yoyote au haki yoyote kuhusu ardhi kwa maslahi ya ulinzi, usalama wa umma, mpangilio wa umma, maadili ya umma, afya ya umma, mpango wa matumizi ya ardhi au uendelezaji au utumizi wa mali.
(2) Serikali itahimiza na kuweka mazingira salama ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, na mwongozo wa kisheria ya kuanzisha, kuendeleza na kusimamia mali.
(3) Bunge litatunga sheria kuhakikisha kwamba mawekezo makubwa ya mali yananufaisha jumuia za kiasili na uchumi wao.

**Tume ya Kitaifa kuhusu Ardhi**

**84.** (1)Kuna Tume buniwa ya Taifa kuhusu Ardhi.
(2) Majukumu ya Tume ya Kitaifa kuhusu Ardhi ni-
(a) kutunza ardhi ya umma kwa niaba ya serikali ya kitaifa na iliyogatuliwa;
(b) kupendekezea serikali ya kitaifa sera ya kitaifa kuhusu ardhi;
(c) kushauri serikali ya kitaifa na ile iliyogatuliwa kuhusu utaratibu wa sera kwa maendeleo ya baadhi ya maeneo nchini Kenya, ili kuhakikisha kwamba maendeleo ya ardhi ya jumuia na ya kibinafsi inaafikiana na mpango wa maendeleo kwa maeneo hayo;
(d) kuchunguza mizozo kuhusu umulikaji mali, ukaaji na uwezo wa kufikia ardhi ya umma katika eneo lolote itakavyoelezwa na sheria;
(e) kushauri serikali ya kitaifa kuhusu, na kusaidia katika utekelezaji wa mipango pana ya usajili wa hati za ardhi kokote nchini Kenya;
(f) kufanya utafiti kuhusiana na ardhi na matumizi ya raslimali nyingine za kiasili na kutoa mapendekezo kwa mamlaka mwafaka;
(g) kuanzisha uchunguzi kivyake au kutokana na malalamishi kuhusu ukiuakaji haki uliopo au wa kihistoria kuhusu ardhi na kupendekeza suluhisho mwafaka;
(h) Kurahisisha ushiriki wa jumuia katika uundaji wa sera ya ardhi;
(i) kuhimiza utumizi wa mifumo iliyokubaliwa ya kiasili ya kusuluhisha mizozo kuhusu ardhi;
(j) kukadiria ushuru unaotozwa kwenye ardhi na thamani ya mali katika eneo lolote linalotambuliwa na sheria;
(k) kusimamia na kuwa na jukumu la kuangalia mpango wa ardhi kotekote nchini;
(l) kuimarisha na muda baada ya muda kurekebisha sheria zote zinazohusiana na ardhi; na
(m) kuanzisha marekebisho ya sheria kuhusu matumizi ya ardhi kwa kuzingatia sera ya kitaifa kuhusu ardhi.
(3) Tume ya Kitaifa kuhusu Ardhi itaweka ofisi kotekote nchini Kenya.

**Sheria kuhusu Ardhi**

**85.** (1) Bunge litatunga sheria ya -
(a) kurekebisha, kuunganisha na kusawazisha sheria zilizopo kuhusu ardhi;
(b) kurekebisha sheria za kisekta kuhusu matumizi ya ardhi kwa mujibu wa sera ya kitaifa kuhusu ardhi;
(c) kushauri upana wa ekari za ardhi ya kumilikiwa baada ya kuzingatia ardhi ya kibinafsi;
(d) kudhibiti njia ambapo ardhi yoyote inaweza kubadilishwa kutoka kategoria moja hadi nyingine;

(e) kudhibiti utambuaji na uhifadhi wa mali ya kindoa na hasa boma la kindoa wakati wa ndoa na wakati wa uvunjwaji wa ndoa hiyo;
(f) kuwezesha uthibitishaji wa ardhi inayomilikiwa kwa manufaa ya jumuia na yeyote au shirika, na uhamishaji wa ardhi kama hiyo kwa jumuia zilizo na haki ya kuimiliki;
(g) kulinda, kuhifadhi na kutoa nafasi ya kuafikiwa kwa ardhi yote ya umma;
(h) kuwezesha kuchunguzwa upya kwa nafasi ya ardhi ya umma ili kutambua ustahifu wake;
(i) kutoa nafasi ya kutafutiwa makao kwa wasio na ardhi na maskwota
(ii) ikiwemo kusafishwa kwa makao ya kujianzishia mijini na mashambani;
(j) kuwalinda wanaotegemea wafu wakiwa na haja ya kupata ardhi yoyote
ikiwemo maslahi ya mume na mke wanaoishi katika ardhi;
(k) kuanzisha hifadhi ya ardhi ili kurahisisha uwepo wa ardhi kwa faida ya umma; na
(l) kutoa nafasi kwa swala jingine lolote muhimu la kukuza maelezo ya Sura hii.

(2)Bunge litaweka tarehe ya kukamilishwa kwa marekebisho yanayotakikana katika ibara 1(h).

**Ustawishaji wa makao**

**86.** (1) Serikali itahakikisha –
(a) uanzishaji wa hazina ya ustawishaji wa makao ili kuwawezesha Wakenya kuweza kufikia makao mengi na ya viwango bora; na
(b) uanzishaji na urekebishaji wa sera ya kitaifa kuhusu makao kwa azma ya kuongeza, kudhibiti na kutunza vipimo vya makao ya kitaifa.

(2) Bunge litatunga sheria –
(a) itakayoitaka Serikali na mashirika mengine husika yakiwemo serikali zilizogatuliwa, kuhimiza matumizi ya teknolojia inayokubalika, isiyogharimu pesa nyingi, na ya wastani , vifaa vya ujenzi, ujuzi na mbinu zilizopo katika sekta ya mali almuradi matumizi yao hayaathiri watu na mazingira; na
(b) itakayohakikisha kwamba mawekezo makubwa katika mali yananufaisha jumuia na uchumi wake.

## SURA YA NANE

### MAZINGIRA NA MALI ASILI

**Kanuni na wajibu kuhusiana na mazingira**

**87.** Serikali –
(a) kuheshimu ukamilifu wa michakato ya asilia na jumuia za kiikolojia na kudumisha hifadhi ya mazingira na spishi;
(b) kuhakikisha matumizi yanayofaa , utunzaji na hifadhi ya mazingira na mali asili na ugawanaji sawa wa faida inayotokana na mazingira hayo;
(c) kuhakikisha kwamba desturi za kijamii na kitamaduni zinazotumiwa asilia na jumuia za Kenya kwa utunzaji bora wa mazingira na mali asili zinazingatiwa;
(d) kuiga na kutekeleza makubaliano na mapatano ya kimataifa ambapo Kenya ni mshirika kuhusiana na uhifadhi wa mazingira;
(e) kuhakikisha kwamba mpangilio na utumizi wa mazingira unazingatia maeneo tengwa na wakaazi wake;
(f) kudumisha hifadhi ya kawi na matumizi ya kawi ya kurudiwa upya;
(g) kuzuia uchavuzi wa mazingira na uharibifu wa ikolojia;
(h) kutoa raslimali za kutosha kukomboa maeneo yaliyoharibiwa na maeneo yanayoweza kukumbwa na majanga ili kuyafanya yawe safi na zalishi;
(i) itafanya kazi kufikia na kutunza misitu ili ijenge angalau asili mia kumi ya ardhi nchini Kenya;
(j) Kulinda na kuzidisha ujuzi wa akilini na elimu ya kiasili kuhusu maswala ya viumbe na ya kuzaliwa ya kijumuia; na
(k) kuhimiza kushiriki kwa umma katika utunzaji, ulinzi na hifadhi ya mazingira hayo.

**Utunzaji wa mazingira**

**88.** Kila mtu ana wajibu wa kushirikiana na ofisi za Serikali na watu wengine-
(a) kuhakikisha maendeleo yanayohimilika ya kiikolojia na matumizi ya mali asili;
(b) kuheshimu, kuhifadhi na kulinda misitu;
(c) kuzuia au kukomesha tendo lolote ambalo ni hatari kwa mazingira;
(d) kuchukua hatua za kuzuia au kukomesha tendo au kosa lolote ambalo ni hatari kwa mazingira; na
(e) kudumisha mazingira safi, salama na yenye afya.

**Hifadhi ya mazingira**

**89.** Katika utumizi au utunzaji wa mazingira, Serikali-
(a) italinda raslimali zote za kijenetiki na upana wa kibayalojia;
(b) kuanzisha mifumo ya kutathmini athari ya mazingira, ukaguzi wa mazingira na usimamizi wa mazingira hayo;
(c) kuhimiza kushiriki kwa umma;
(d) kulinda na kuzidisha ujuzi wa kiakili na elimu ya kiasili kuhusu upana na uasilia wa raslimali za jumuia; na
(e) kuhakikisha kwamba viwango vya mazingira vinavyotekezwa katika Jamhuri hii ni vilevinavyokubaliwa kimataifa.

**Utekelezaji wa haki kuhusu mazingira**

**90.** (1) Iwapo mtu anadai kuwa haki ya kupata mazingira safi na ya kiafya inayotambuliwa na kulindwa chini ya Katiba hii imekiukwa, inakiukwa au inaelekea kukiukwa , kwa pamoja na masuluhu mengine ya kisheria yaliyopo kuhusiana na swala hilo, mtu huyo anaweza kuomba mahakama kutoa suluhisho.

(2) Kutokana na ombi la mtu yeyote chini ya ibara (1), mahakama inaweza kutoa amri za sampuli hiyo, au kutoa maelekezo kama hayo iwapo itahisi kwamba yanastahili-
(a) kuzuia au kukomesha tendo au kosa lolote hatari kwa mazingira;
(b) kumshurutisha afisa yeyote wa umma kuchukua hatua ya kuzuia au kukomesha
tendo au kosa lolote hatari kwa mazingira;
(c) kutoa kwa ukiukaji wowote wa haki ya kupata mazingira safi nay a kiafya.

(3) Kwa haja ya Kifungu hiki, haitamlazimu aliyetuma ombi hilo kudhihirisha hasara waliopata.

**Ustawishaji na maendeleo ya mali asili**

**91.** Serikali itahakikisha ulinzi, utunzaji, ukuzaji na maendeleo yanayostahili kuhusu mali asili na –
(a) itafanya utafiti wa kuhakikisha ongezeko la mali asili;
(b) itaondoa ushindani usiofaa katika uzalishaji, uandaaji, usambazaji na uuzaji wake;
(c) itadhibiti mauzo ya nje na ya kuagiziwa kutoka nje;
(d) itadhibiti asili yake, ubora wake, mbinu za uzalishaji wake, uvunaji wake na uandaaji wake;
(e) itaondoa michakato na shughuli ambazo zinaweza kuhatarisha au kuzuia uwepo wake; na
(f) itazitumia kwa manufaa ya Wakenya wote.

**Makubaliano kuhusiana na mali asili**

**92.** (1) Maafikiano yanayohusisha utoaji wa haki au makubaliano na au kwa niaba ya mtu yeyote, ikiwemo serikali ya taifa kwa mtu mwingine, ya kutumia mali asili yoyote ya nchini Kenya, yaliyoafikiwa baada ya siku ya kuanza kutekelezwa kwa katiba hii, yanaweza kuidhinishwa na Bunge.

(2)Bunge, kwa kupitia utungaji wa sheria litatoa viwango vya maafikiano yatakayoidhinishwa chini ya ibara ya (1).

(3) Bunge kwa kupitia njia ya sheria iliyoungwa mkono katika kila Bunge na angalau thuluthi-mbili ya wabunge wote, linaweza kuachilia mbali maafikiano yoyote kutoka kwa ibara ya (1).

**Sheria kuhusu Mazingira**

**93.** (1) Bunge litatunga sheria ya-
(a) kubuni tume ya kitaifa kuhusu mazingira na kuonyesha majukumu yake; na
(b) kuzingatia kwa ukamilifu vipengele vya Sura

## SURA YA TISA

### UONGOZI NA MAADILI

**Majukumu ya uongozi**

**94.** (1) Mamlaka yaliyotolewa kwa ofisa wa Serikali-
(a) ni amana ya umma inayopaswa kutekelezwa katika njia ambayo-
(i) inaambatana na majukumu na makusudi ya Katiba hii;
(ii) inadhihirisha heshima kwa watu;
(iii) inaleta sifa kwa taifa na hadhi kwa ofisi; na
(iv) inakuza imani ya umma katika maadili ya kiofisi; na

(b) yanamwekea afisa huyo wa Serikali jukumu la kuhudumia watu badala ya mamlaka ya kuwaongoza.

(2) Kanuni zinazoongoza uongozi na maadili ni –

(a) uteuzi kwa misingi ya uadilifu, umilisi na ufaafu, au uchaguzi katika uchaguzi huru na wa haki;

(b) kutopendelea katika maamuzi na katika kuhakikisha kwamba maamuzi hayo hayatokani na mapendeleo ya undugu au nia nyingine zozote mbaya;

(c) kutojipendelea kwa misingi ya maslahi ya umma, ikidhihirishwa na –

(i) uaminifu katika utekelezaji wa wajibu wa umma; na

(ii) kutangaza kwa maslahi ya kibinafsi yanayoweza kugongana na wajibu wa umma;

(d) uwajibikiaji wa maamuzi na hatua zinazochukuliwa kwa umma; na

(e) nidhamu na kujitolea katika huduma kwa watu.

**Kiapo cha uaminifu**

**95.** Kabla kuhudumu katika wadhifa wa kiofisi , au kutekeleza majukumu yoyote ya ofisi , kila mtu aliyechaguliwa au kuteuliwa katika ofisi ya Serikali ataapa au kukiri kuwajibikia ofisi hiyo katika njia na hali itakayopendekezwa na Mpangilio wa Tatu, au na Sheria ya Bunge.

**Mienendo yaa maofisa wa Serikali**

**96.** (1) Iwe katika maisha yake ya kuhudumia umma na kiofisi, katika maisha ya kibinafsi, au katika miungano na watu wengine, ofisa wa Serikali atapaswa kudumisha mienendo itayomwepusha na-

(a) mgongano wowote kati ya maslahi ya kibinafsi na wajibu wake wa kuhudumia umma au ofisi;

(b) ukiukaji wa maslahi yoyote ya umma au kiofisi kwa ajili ya maslahi yake ya kibinafsi; au

(c) kudhalilisha ofisi au cheo anachoshikilia ofisa huyo.

(2) Ofisa wa Serikali –

(a) hatatumia ofisi yake kivyovyote kwa faida za kibinafsi;

(b) hatatafuta au kukubali mali, zawadi au manufaa yoyote kama hongo kwa kupendelewa au utekelezaji au utotekelezaji wa jukumu lake rasmi;

(c) hatafuja fedha za umma, au kutumia vibaya au kuharibu mali ya umma bila kufuata sheria;

(d) hatatumia mali au vifaa vya umma kuchangisha michango kutoka kwa raia kwa jukumu lisilo rasmi;

(e) hatatumia uwezo wa ofisi yake kumnyanyasa mtu yeyote kimapenzi, au kujaribu kutaka mapenzi au manufaa mengine yoyote kutoka kwa mtu;

(f) kumshurutisha mtu mwingine-

(i) kufanya chochote kinachokataliwa na Kifungu hiki kwa manufaa huyo ofisa wa Serikali; au

(ii) kufanya tendo lolote linalokiuka sheria.

(3) Iwapo ofisa wa Serikali atapatikana na hatia inayohusiana na lolote katika maswala yanayorejelewa katika Kifungu hiki, ofisa huyo atakoma kushikilia ofisi hiyo.

(4) Mtu anayevunja Sura hii, ataachishwa kazi au kutolewa ofisini kwa mujibu wa taratibu za adhabu inayostahili.

(5) Mtu atakayeachishwa kazi au kutolewa katika ofisi ya Serikali kwa kuvunja Sura hii harusiwi kushikilia ofisi yoyote nyingine ya Serikali.

**Fedha za maofisa wa Serikali**

97. (1) Ofisa wa Serikali atatangaza utajiri wake katika njia ya maandishi na kupitia njia na utaratibu utakaopendekezwa na Tume kwa Tume hiyo ya Maadili na Kupambana na Ufisadi –

(a) punde anapokuwa ofisa wa Serikali; na

(b) angalau kila mwaka akiwa ofisini; na

(c) anapokoma kushikilia ofisi.

(2) Mtu atakapokoma kuwa ofisa wa Serikali, atahitajika kuieleza Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi katika njia na utaratibu utakaopendekezwa na Tume, akitangaza utajiri wake.

(3) Tangazo chini ya Kifungu hiki litajumuisha tangazo la utajiri ambao ofisa huyo huenda anamiliki kwa pamoja na mwenziwe katika ndoa au mtu yeyote mwingine.

(4) Ofisa wa Serikali atakuwa amevunja Sura hii iwapo-

(a) atakosa kutoa tangazo linalohitajika katika Kifungu hiki; au

(b) akitoa taarifa za uongo kimakusudi katika tangazo linalotajwa chini ya Kifungu hiki.

(5) Ofisa wa Serikali –

(a) hatahifadhi akaunti ya benki nje ya Kenya isipokuwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge; au

(b) ataomba au kukubali mkopo au manufaa ya kibinafsi katika hali zinazotatiza uadilifu wake.

(6) Zawadi au mchango wowote kwa ofisa wa Serikali katika sherehe ya umma au rasmi, itakuwa zawadi kwa Jamhuri na itapelekewa Serikali isipokuwa ikiidhinishwa na au chini ya Sheria ya Bunge.

**Uzuiaji wa shughuli**

**98.** (1) Ofisa wa Serikali anayehudumu kwa muda wote hatashiriki katika ajira nyingine yoyote ya kulipia.

(2) Rais wa Taifa, Naibu wa Rais wa Taifa na ofisa yeyote wa Serikali hatashikilia ofisi katika chama cha kisiasa.

(3) Ibara ya (2) haimrejelei Waziri Mkuu, Naibu wa Waziri Mkuu, Waziri au Naibu wa Waziri.

(4) Ofisa aliyestaafu wa Serikali anayepokea pensheni kutoka kwa fedha za umma hatakubali zaidi ya vyeo viwili vya kulipwa mshahara kwa wakati mmoja kama mwenyekiti, mkurugenzi au mwajiriwa wa-

(a) kampuli linalomilikiwa au kudhibitiwa na serikali; na

(b) Taasisi ya Serikali.

(5) Ofisa aliyestaafu wa Serikali hatapokea mshahara kutoka kwa fedha za umma kando na yale yanayorejelewa katika ibara ya (4).

**Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi**

**99.** (1) Kuna Tume buniwa ya Maadili na Kupamabana na Ufisadi itakayojumuisha wanachama tisa.

(2) Majukumu ya Tume hiyo ni-

(a) Kuchunguza swala lolote ambalo kwa maoni ya Tume , linazua shaka kwamba tabia zinazojumuisha ufisadi au uhalifu wa kiuchumi inavyodokezwa katika Sheria ya Bunge imetokea au inaelekea kutukia;

(b) kupokea na kuhifadhi matangazo yanayotakikana na Sura hii;

(c) kuhakikisha uzingatiaji na utekelezaji wa vipengele vya Sura hii;

(d) kupokea na kuchunguza malalamishi kuhusu ukiukaji wa Sura hii na ikiwezekana, kutuma malalamishi hayo kwa mamlaka husika ili hatua mwafaka ichukuliwe; na

(e) kuweka mikakati itakayolenga kuzuia ufisadi, pamoja na kutoa mwongozo kwa taasisi za Serikali.

(3) Bunge linaweza kuitwika Tume jukumu lolote jingine.

(4) Tume haitachunguza swala lolote linalosubiri uamuzi wa mahakama au mahakama maalumu za kisheria.

(5) Tume itabuni na kuhifadhi rekodi ya utajiri wa maofisa wa Serikali utarekodiwa na tume itahakikisha uwepo wa rekodi hizo kwa ukaguzi wa umma.

**Wajibu wa kuhakikisha uzingatifu**

**100.** Kila taasisi ambayo, au ofisa wa Serikali ambaye, ana jukumu la kusimamia maofisa wengine wa Serikali atahakikisha kwamba ofisa huyo anazingatia vipengele vya Sura hii –

**Sheria kuhusu uongozi**

**101.** Sheria ya Bunge –

(a) itaweka mikakati ya kupata usimamizi bora wa Katiba hii;

(b) itapendekeza adhabu kando na zinazodokezwa katika Kifungu 96 ambazo zinaweza kutolewa kwa uvunjaji wa vipengele vya Sura hii;

(c) itaunda kipengele cha utekelezaji wa Sura hii kwa maofisa wa umma; na

(d) itaunda kipengele kingine chochote kitakachohitajika katika kuhakikisha udumishaji wa kanuni za uongozi na maadili yaliyodokezwa katika Sura hii, na utekelezaji wa vipengele vya Sura hii.

## SURA YA KUMI

**UWAKILISHAJI WA WATU**

**Sehemu ya 1 – Kanuni za mfumo wa Uchaguzi na Utaratibu wa uchaguzi**

**Kanuni za jumla**

**102.** Mfumo wa uchaguzi utaafiki kanuni zifuatazo-

(a) uhuru wa wananchi kutekeleza haki zao za kisheria chini ya Kifungu 55;

(b) usawa wa kijinsia katika taasisi zinazoshiriki uchaguzi inavyoelezwa

katika Kifungu 13(2)(j);
(c) uwakilishaji walemavu inavyoelezwa katika 13(2)(k);
(d) uwakilishaji wa watu, ikiwemo jumuia tengwa na vijana;
(e) chaguzi za haki ambazo ni -
(i) za siri;
(ii) huru dhidi ya ghasia, vitisho, uchochezi mbaya, au ufisadi;
(iii) zinasimamiwa na taasisi huru;
(iv) za wazi; na
(v) zinazoongozwa katika njia zisizopendelea upande, sawa, mwafaka na za kuwajibika.

**Sheria kuhusu uchaguzi**

**103.** (1)Bunge litatunga sheria ya kutoa nafasi ya-
(a) kutozuiliwa kwa vitengo vya upigaji kura na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka kwa uchaguzi wa wajumbe wa Bunge na vikao vya Serikali ya wilaya;
(b) uteuzi wa wagombea;
(c) njia ya upigaji kura wakati wa uchaguzi;
(d) usajili wa kuendelea wa wananchi kama wapiga kura katika sehemu zote za nchi ikiwemo muda kati ya kufungwa kwa usajili wa wapiga kura na chaguzi zinazofuata;
(e) taratibu za chaguzi na kura za maoni;
(f) udhibiti na ufaafu wa usimamizi wa uchaguzi na kura za maoni; na
(g) usajili wan a upigaji kura wa raia wanaoishi nje ya Kenya.
(2) Sheria itakayotungwa kwa kuzingatia ibara (1)(c) itahakikisha hasa kwamba upigaji kura katika kila uchaguzi ni-
(a) rahisi;
(b) wa wazi; na
(c) inazingatia mahitaji maalumu ya-
(i) walemavu; na
(ii) wafungwa na wagonjwa hospitali.

**Kusajiliwa kama mpigakura**

**104.** (1) Mwananchi ataweza kusajiliwa kama mpigakura katika uchaguzi au kura ya maoni iwapo wakati wa ombi lake atakuwa –
(a) na angalau umri wa miaka kumi na minane;
(b) ana sifa nyingine inavyohitajika na sheria; na
(c) hafungiwi nje ya usajili kwa msingi unaopendekezwa na sheria.
(2) Mwananchi aliye na sifa za kumwezesha kusajiliwa kama mpigakura atasajiliwa tu katika kituo kimoja cha usajili.
(3) Mipangilio ya usimamizi wa usajili wa wapigakura na zoezi zima la uchaguzi itapangwa ili kurahisisha, na haitamnyima mpigakura yeyote anayestahili haki ya kupiga kura au kugombea katika uchaguzi.

**Wagombea katika uchaguzi kuzingatia kanuni za upigaji kura**

**105.** Wagombea wote katika kila uchaguzi watazingatia kanuni za upigaji kura zitakavyoagizwa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka. Kuzingatia kanuni za uchaguzi

**106.** Katika kila uchaguzi, wagombea wote na vyama vyote vya kisiasa vitazingatia kanuni za upigaji kura zitakazoagizwa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka –

**Wagombea wa kibinafsi**

**107.** Kwa mazingatio ya Kifungu 127 na sifa zitakazopangiwa uchaguzi wa mabaraza ya maeneo na wilaya katika Kifungu 236, mtu anaruhusiwa kuwa mgombea wa kibinafsi ili kuchaguliwa kama mjumbe wa Bunge, baraza la kieneo au baraza la wilaya, iwapo mtu huyo-
(a) ni mwananchi;
(b) si mwanachama wa chama cha kisiasa kilichosajiliwa na hajakuwa mwanachama kwa angalau miezi sita kabla siku ya uchaguzi; na kutoka eneo bunge au wadi ambayo mtu huyo anakusudia kugombea-
(i) katika kiwango cha eneo bunge, wapigakura elfu moja waliosajiliwa; na
(ii) katika kiwango cha wadi ya wilaya, wapigakura mia tano waliosajiliwa.

**Wagombea wasio na wapinzani**

**108.** Endapo mgombea mmoja tu ndiye atakayeteuliwa kufikia mwisho wa uteuzi kabla ya uchaguzi atatangazwa mshindi.

**Upigaji kura**

**109.** Katika kila uchaguzi, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itahakikisha kwamba-
(a) katika mbinu yoyote ya upigaji kura itakayotumiwa, mfumo unakuwa rahisi, sawa, wa kurekebishwa, salama, uwajibikaji na wa wazi;
(b) endapo masanduku ya upigaji kura yatatumika, yenye uwezo wa kuonekana ndani;
(c) kura zinazopigwa zinahesabiwa, kupangwa na matokeo kutangazwa moja kwa moja na msimamizi wa kituo cha upigaji kura hapo kwenye kituo;
(d) matokeo ya kutoka vituo vya upigaji kura yanafunguliwa, kutayarishwa na kutangazwa moja kwa moja na afisa anayesimamia uchaguzi katika eneo hilo la uwakilishi bunge; na
(e) miundo na taratibu mwafaka zimewekwa ili kuondoa uwezekano wa mienendo mibaya ya upigaji kura, ikiwemo kuweka vifaa vya uchaguzi.

**Mizozo ya Uchaguzi**

**110.**(1) Sheria ya Bunge itajenga mifumo ya kusuluhisha mizozo ya uchaguzi.
(2) Malalamishi kuhusu uchaguzi, yanayoripotiwa baada ya utangazaji wa matokeo na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka-
(a) endapo ni katika kura za uRais, yaripotiwe kabla kuisha kwa siku saba; na
(b) katika kesi nyingine yawasilishwe kabla kukamilika kwa siku ishirini na nane.
(3) Malalamishi kuhusu kura za uRais yatachunguzwa kabla kukamilika kwa siku saba baada ya kupiga ripoti na lalama yoyote nyingine itashughulikiwa katika miezi sita baada ya kuripoti.
(4) Huduma ya lalama yoyote inaweza kuwa ya moja kwa moja au kupitia tangazo katika gazeti linalosambazwa katika taifa.

**Kuwakilishwa kwa watu katika taasisi za Kimataifa**

**111.** Kwa kuzingatia mapatano, Bunge litatunga sheria inayoongoza uchaguzi na uteuzi wa wawakilishi wa Jamhuri katika taasisi za kisheria za kimataifa.

**Sehemu ya 2- Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka na kutodhibitika kwa vitengo vya uchaguzi**

**Tume Huru ya uchaguzi na Mipaka**

**112.**(1) Kuna Tume buniwa Huru ya uchaguzi na Mipaka.
(2) Tume hii ina jukumu la kudumisha uchaguzi na kura za maoni zilizo huru na haki na hasa kwa-
(a) usajili wa kila mara wa wananchi kama wapigakura katika sehemu zote za nchi na wale wanaoishi nje ya Kenya kwa kuzingatia kikomo cha usajili huo kabla ya uchaguzi au kura ya maoni;
(b) kurekebishwa mara kwa mara kwa sajili ya wapigakura;
(c) kuweka mipaka ya maeneobunge na wadi;
(d) kudhibiti taratibu za vyama kuteua wagombea wa uchaguzi;
(e) uadilifu na usimamizi mwafaka wa uchaguzi na kura za maoni;
(f) kujenga mifumo ya kisasa ya kukusanya, kutayarisha, kuingiza na kulinganisha data ya uchaguzi;
(g) kusuluhisha mizozo kuhusu uchaguzi ikiwemo mizozo inayohusiana au kutokana na uteuzi japo sio malamishi kuhusu uchaguzi na mizozo inayotokana na kutangaza matokeo ya uchaguzi;
(h) kusajili wagombea wa uchaguzi;
(i) kuimarisha elimu ya mpigakura na utamaduni wa demokrasia;
(j) kuimarisha uchunguzi, usimamizi na tathmini ya uchaguzi;
(k) kudhibiti kiasi cha pesa zitakazotumiwa na au kwa niaba ya mgombea au chama katika uchaguzi wowote;
(l) kujenga kanuni za uchaguzi kwa wagombea na vyama vinavyombea ushindi katika uchaguzi; na
(m) kuchunguza uzingatifu wa matarajio yanayotazamiwa chini ya Kifungu 103(1)(b) kuhusiana na uteuzi wa wagombea wa vyama; na
(n) jukumu jingine lolote linalopendekezwa na Sheria ya Bunge.
(3) Tume ina jukumu la kuendesha-
(a) uchaguzi wa Rais;
(b) uchaguzi wa wajumbe wa Seneti;
(c) uchaguzi wa wabunge wa Bunge la Taifa;
(d) uchaguzi wa wajumbe wa mamlaka za maeneo na kamati kuu za maeneo;

(e) uchaguzi wa wajumbe wa mamlaka za wilaya na magavana wake na manaibu wa magavana hao wa wilaya;

(f) uchaguzi wa meya na naibu wa meya jijini Nairobi;

(g) kura za maoni; na

(h) uchaguzi mwingine wowote utakaopendekezwa na Sheria ya bunge.

(4) Tume itatumia mamlaka yake kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Katiba hii na sheria ya kitaifa iliyotungwa bungeni.

**Kuwekea mipaka sehemu za uchaguzi**

**113.**(1) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itarekebisha idadi, majina na mipaka ya maeneobunge na wadi kila baada ya muda usiopungua miaka minane na usiozidi miaka kumi na miwili lakini kila marekebisho hayo yakamilishwe angalau miezi kumi na minane kabla uchaguzi mkuu.

(2) Na endapo uchaguzi utaitishwa katikati ya miezi kumi na minane ya Tume kukamilisha marekebisho, mipaka mipya haitatekelezeka kwa ajili ya uchaguzi huo.

(3) Katika kuweka mipaka na upeanaji wa majina ya maeneobunge, Tume-

(a) itahitaji kusawazisha idadi ya wakaazi wa eneobunge fulani ikizingatiwa haja ya kuhakikisha uwakilishaji wa kutosha kwa maeneo ya mijini na yale yaliyo na idadi ndogo ya watu; na

(b) itazingatia historia, tofauti na mshikamano wa maeneobunge hayo kwa kuzingatia-

(i) ukubwa wa idadi ya watu, mwelekeo na matarajio;

(ii) maumbile ya kijiografia na maeneo ya miji;

(iii) jumuia lengwana historia, uchumi na mshikamano wake wa kitamaduni; na

(iv) njia za mawasiliano.

(4) Katika kurekebisha mipaka ya maeneobunge na wadi, Tume itashauriana na makundi yoyote husika.

(5) Ikiwezekana, Tume itabadilisha idadi, majina na mipaka ya maeneobunge na wadi.

(6) Kwa kuzingatia ibara (1) na (2), majina na taarifa zaidi ya mipaka ya maeneobunge itakayobuniwa na Tume, zitachapishwa katika Gazeti maalumu la serikali na zitatekelezwa wakato uvunjwaji wa Bunge baada ya kuchapishwa kwake.

(7) Mtu anaweza kuomba Mahakama ya Kikatiba kurekebisha uamuzi wa Tume unaochukuliwa chini ya Kifungu hiki.

(8) Ombi la kurekebishwa kwa uamuzi uliofanywa chini ya Kifungu hiki, litatumwa katika kipindi cha siku thelathini baada ya uchapishaji wa uamuzi ulipo kwenye Gazeti rasmi la serikali na litasikilizwa na kushughulikiwa katika kipindi cha miezi mitatu tangu siku ya kutumwa kwa ombi hilo.

**Sehemu ya 3- Vyama vya kisiasa**

**Kanuni za kimsingi kwa vyama vya kisiasa**

**114.** (1) Kila chama cha kisiasa-

(a) kitadumisha makusudi na kanuni za katiba hii na uongozi wa kisheria;

(b) kitadumisha na kukuza umoja wa kitaifa;

(c) kitakuwa na sifa za kitaifa inavyopendekezwa na Sheria ya Bunge;

(d) kiwe na taasisi ya uongozi iliyochaguliwa kidemokrasia;

(e) kitazingatia kanuni za kidemokrasia za uongozi bora, kudumisha na kuendeleza demokrasia kupitia uchaguzi wa mara kwa mara, haki na huru katika chama, na kudumisha nidhamu katika chama;

(f) kitatekeleza shughuli zake katika njia inayodumisha siasa za kidemokrasia na za amani;

(g) kitaheshimu haki za wengine kushiriki katika harakati za kisiasa, ikiwemo walemavu na wanyonge wengine;

(h) kitaheshimu na kudumisha haki za binadamu na uhuru wa kimsingi, na usawa na ulinganifu wa kijinsia; na

(i) kitazingatia kanuni za uwajibikaji wa vyama vya kisiasa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka.

(2) Chama cha kisiasa –

(a) hakitabuniwa kwa misingi ya kidini, lugha, kiasili, kikabila, kijinsia au kimaeneo au kujihusisha katika kampeni za chuki kuhusu swala lolote katika maswala hayo;

(b) hakitajihusisha au kuhimiza ghasia na, au vitisho kwa wanachama wake, wafuasi, wapinzani au mtu mwingine yeyote;

(c) hakitaanzisha au kutunza vikosi sambamba vya kijeshi, makundi haramu au mengine kama hayo;

(d) hakitashiriki hongo au aina nyingine za ufisadi; au

(e) isipokuwa kwa jinsi ilivyoelezwa katika Sura hii au kwa mujibu wa Sheria ya Bunge, kitakubali au kutumia raslimali ya umma ili kutukuza maslahi yake au wagombea wake katika uchaguzi.

(3) Sheria ya Bunge itatoa nafasi ya kusajili vyama vya kitaifa.

**Kikomo cha uanachama katika chama cha kisiasa**

**115.** (1) Mtu anaweza kujiuzulu kutoka kwenye chama cha siasa kwa kutoa arifa katika maandishi kwa katibu-mkuu msajiliwa wa chama hicho cha kisiasa, na-

(a) iwapo ni Mbunge kwa Spika wa Bunge; na

(b) iwapo ni mjumbe wa serikali ya eneo au wilaya kwa msimamizi wa maswala ya mabaraza hayo.

(2) Mtu hatakuwa mwanachama wa vyama zaidi ya kimoja cha kisiasa kwa wakati mmoja.

(3) Mbunge au mjumbe wa baraza la eneo au wilaya aliyechaguliwa kwa tiketi ya chama fulani cha kisiasa, anakoma kuwa Mbunge au mjumbe wa baraza kwa-

(a) kujiuzulu kutoka kwa chama chake; au

(b) kufukuzwa kutoka kwenye chama kwa kukosa nidhamu baada ya kusikizwa kwa kesi katika kufuata haki kisheria.

(4) Kwa ajili ya ibara (3) , uwepo wa hali zifuatazo pekee hautamwishia mwanachama katika kufukuzwa kutoka kwenye chama-

(a) kujengwa au kuvunjwa kwa muungano ambao chama cha mwanachama huyu ni mshirika;

(b) kuvunjwa kwa chama cha kisiasa ambacho mjumbe huyo ni mwanachama; au

(c) kuunganishwa kwa vyama viwili au zaidi vya kisiasa ambapo mjumbe huyu alikuwa mwanachama katika chama kimojawapo.

(5) Licha ya ibara ya (3), Mbunge au mjumbe wa baraza la maeneo au wilaya hatapoteza uanachama huo isipokuwa endapo katibu-mkuu msajiliwa wa chama husika cha kisiasa ametoa notisi katika maandishi kwa Spika na mwanachama huyo, endapo ibara ya (3) inamhusu mwanachama huyo na-

(a) mwanachama huyo, hajalalamika kwa Mahakama Kuu katika muda wa siku kumi na nne baada ya kupokea notisi, ili itangazwe kwamba ibara hiyo ya (3) haimhusu mwanachama huyo; au

(b) Mahakama Kuu imetupilia mbali malalamishi ya mwanachama kuhusu tangazo kama hilo.

(6) Mahakama Kuu itaamua kuhusu malalamishi yoyote chini ya ibara (5)(b) katika kipindi cha siku tisini.

(7) Mbunge au mjumbe wa baraza la eneo au wilaya aliyechaguliwa kwa tiketi ya chama fulani cha kisiasa atakuwa chini ya sera hizi, wito, falsafa na manifesto ya chama.

(8) Chama cha kisiasa hakitamwadhibu mwanachama wake aliyechaguliwa Bungeni kwa chochote atakachosema mwanachama huyo wakati wa vikao vya Bunge.

(9) Chama cha kisiasa hakitamwadhibu mwanachama yeyote aliyechaguliwa kwa baraza la eneo au wilaya kwa sababu ya chochote atakachosema mwanachama huyo wakati wa vikao vya mabaraza hayo ya maeneo au wilaya.

**Kamishna wa vyama vya kisiasa**

**116.** (1) Kuna ofisi buniwa ya Kamishna wa Vyama vya Kisiasa.

(2) Kamishna huyo ana jukumu katika-

(a) kusajili vyama vya kisiasa na viongozi wake;

(b) kutunza Hazina ya Vyama vya Kisiasa;

(c) kutayarisha na kuchapisha ripoti za kila mwaka kuhusu ripoti za ukaguzi wa fedha wa kila chama cha kisiasa; na

(d) majukumu mengineyo yatakayotolewa kwa Kamishna na Katiba au sheria.

(3) Katika kutekeleza majukumu ya ofisi hii, Kamishna hataongozwa au kudhibitiwa na mtu yeyote au mamlaka yoyote.

**Kudhibiti vyama vya kisiasa**

**117.** (1) Sheria ya Bunge itatoa nafasi ya –

(a) kusajiliwa, kudhibitiwa na kufutiliwa mbali kwa vyama vya kisiasa na maswala mengine kuhusiana na hayo; na

(b) kusuluhisha mizozo kati ya wanachama wa chama fulani cha kisiasa, kati ya vyama ikiwemo vyama vilivyojenga muungano, na kati ya chama na Kamishna wa Vyama vya Kisiasa.

(2) Chama cha kisiasa kinaposajiliwa kitakuwa mshirika.

**Hazina ya Vyama vya Kisiasa**

**118.** (1) Kuna Hazina buniwa ya Vyama vya Kisiasa.

(2) Hazina hii itasimamiwa na Kamishna wa Vyama vya Kisiasa.
(3) Hazina itatoka kwa-
(a) pesa zitakazotolewa na Bunge ambazo hazitazidi asilimia sufuri nukta tatu ya makadirio ya utumiaji wa pesa kabla kukamilika kwa mwaka wa kifedha; na
(b) michango kutoka kwa njia nyingine zinazokubalika kisheria.
(4) Kando na ibara ya (3), Bunge litatunga sheria ya kudhibiti zinakotoka pesa za kutumiwa na Hazina.

**Matumizi ya Hazina hiyo**
**119.** (1) Jukumu la Hazina ya Vyama vya Kisiasa ni kutoa usaidizi wa kifedha kwa vyama vilivyosajiliwa vya kisiasa.
(2) Chama cha kisiasa kilicho na angalau mbunge mmoja Bungeni au katika baraza la wilaya kitaweza kupata usaidizi wa kifedha kutoka kwa Hazina.
(3) Chama hakifaa kupata usaidizi wa kifedha kutoka kjwa Hazina iwapo zaidi ya thuluthi-mbili ya viongozi wake ni wa jinsia moja.
(4)Bunge litatunga sheria ya kuhakikisha usawa katika ugawaji wa fedha kwa vyama vilivyosajiliwa vya kisiasa kwa kuzingatia-
(a) idadi ya kura walizopata katika uchaguzi uliotangulia wa uRais, wa ubunge na wilaya ikiwemo uchaguzi mdogo; na
(b) idadi ya wanawake na makundi tengwa yaliyochaguliwa kupitia kila chama katika uchaguzi huo.
(5) pesa zitakazotengewa chama cha kisiasa kutoka kwenye Hazina hiyo zitatumiwa na chama-
(a) kufidia gharama ya uchaguzi katika chama hicho na usambazaji wa sera zake;
(b) kupanga mafunzo ya raia kuhusu demokrasia, Katiba hii na mazoezi ya uchaguzi; na
(c) kutumia kwa gharama ya usimamizi wa chama ambapo gharama hiyo haitazidi asilimia kumi ya pesa ilizotengewa.
(6) Pesa zinazotolewa kwa chama cha kisiasa hazitatumiwa-
(a) kulipia kivyovyote, mishahara, karo, kuwaridhisha au kumnufaisha mwanachama yeyote au mfuasi wa chama hicho kinyume na ilivyopendekezwa katika ibara ya (5); au
(b)jukumu jingine lolote lisiloambatana na udumishaji wa demokrasia ya vyama vingi.

**Kuwajibika kwa vyama vya kisiasa**
**120.** (1) Chama cha kisiasa kitachapisha wanaokipa fedha kila mara itakavyoelezwa na Kamishna wa Vyama vya Kisiasa.
(2) Katika kipindi cha miezi mitatu ya mwisho wa mwaka wa kifedha kila chama kilichosajiliwa cha kisiasa –
(a) kitachapisha mahali zinakotoka fedha zake;
(b) kitachapisha taarifa za kina kuhusu jinsi kilivyotumia pesa zake;
(c) kuwasilisha ripoti kuhusu matumizi ya fedha kwa Mkaguzi- Mkuu wa hesabu za serikali katika njia itakayopendekezwa na Mkaguzi huyo; na
(d) kuwasilisha kwa Kamishna wa Vyama vya Kisiasa, ripoti za kila mwaka kuhusu shughuli zake katika mwaka mzima wa kifedha.
(3) Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali atakagua rekodi zote za fedha za usajili wa vyama na kutuma ripoti ya ukaguzi wake kwa Kamishna wa Vyama vya Kisiasa na Bunge.
(4) Bunge litatunga sheria –
(a) kufafanua mahali ambako vyama vilivyosajiliwa vya kisiasa havitaruhusiwa kupata michango;
(b) kufafanua mchango mkubwa unaoweza kutolewa na mtu binafssi au taasisi au shirika kwa chama kilichosajiliwa cha kisiasa; na
(c) itakayotoa ruhusa ya kukaguliwa na umma kwa ripoti za kila mwaka, rekodi za kifedha na ripoti za ukaguzi wa vyama vilivyosajiliwa vya kisiasa.
(5) Tume Huru ya Uchaguzi na mipaka itadhibiti kiasi cha pesa zitakazotumiwa na au kwa niaba ya mgombea au chama katika uchaguzi wowote.

**Vyama vya kisiasa na vyombo vya habari**
**121.** Bunge litatunga sheria ambayo-
(a) itakayoweka nafasi sawa ya kutengewa muda katika vyombo vya matangazo vinavyomilikiwa na serikali au aina nyinginezo, kwa vyama vya kisiasa ama wakati wowote au wakati wa kampeni za uchaguzi; na
(b) itakayodhibiti uhuru wa kutangaza ili kuhakikisha kampeni za haki wakati wa uchaguzi.

**122.** Isipokuwa inakavyodokezwa katika Sura hii au Sheria ya Bunge, mtu hatatumia raslimali ya umma kudumisha maslahi ya chama cha kisiasa.

## SURA YA KUMI NA MOJA

**BUNGE**

**Sehemu ya 1 – Kuundwa na jukumu la Bunge**

**Kuundwa kwa Bunge**
**123.** Kuna Bunge buniwa la Kenya litakalojumuisha Seneti na Bunge

**Jukumu la Bunge**
**124**(1) Jukumu la kutunga sheria la Jamhuri hii katika kiwango cha kitaifa ni la Bunge.
(2) Bunge hutokeza tofauti za kitamaduni katika taifa, linawakilisha maoni ya watu na hutekeleza mamlaka yake kwa-
(a) kutunga sheria;
(b) kushauriana kuhusu na kusuluhisha maswala yenye n umuhimu mkubwa kwa raia;
(c) kupima na kupitisha marekebisho ya Katiba hii;
(d) kuidhinisha kugawana kwa mapato miongoni mwa viwango mbalimbali vya serikali na miongoni mwa serikali zenyewe katika kila kiwango na kukadiria hazina ya gharama ya serikali ya kitaifa na taasisi nyingine za Serikali ya kitaifa;
(e) kuhakikisha uwepo wa usawa katika usambazaji wa raslimali za kitaifa na nafasi miongoni mwa sehemu na jumuia zote nchini Kenya;
(f) kuchunguza kwa makini na kusimamia hatua zinazochukuliwa na taasisi za Serikali;
(g) kupima na kuidhinisha mapatano na makubaliano ya kimataifa;
(h) kuidhinisha uteuzi, wakihitajika kufanya hivyo na Katiba hii au sheria ya bunge;
(i) kuchunguza utendakazi wa ofisi ya Rais, Naibu wa Rais na maofisa wa Serikali na ikiwezekana kuanzisha hatua za kuwatoa ofisini; na
(j) kuidhinisha matangazo ya vita na kuendelezwa kwa tangazo la muda wa hali ya hatari.
(3) Jukumu kuu la Seneti ni kuweka taasisi itakayosaidia serikali iliyogatuliwa kugawana na kushiriki katika kukusanya na kutunga sheria ya kitaifa na ku linda maslahi ya serikali hiyo iliyogatuliwa.
(4) Hakuna mtu yeyote au taasisi yoyote, isipokuwa Bunge, itakayokuwa na mam laka kutengeneza kipengele cha kisheria nchini Kenya isipokuwa kwa amri ya Katiba hii au Sheria ya Bunge.
5) Bunge litalinda Katiba hii na kudumisha uongozi wa kidemokrasia kwa Jamhuri hii.

**Sehemu ya 2 – Wanachama wa Bunge**

**Wanachama wa Seneti**
**125.** (1) Seneti itajumuisha-
(a) wanachama waliochaguliwa mmoja kutoka kila wilaya, baraza la wilaya wanaoweza kupiga kura;
(b) wanawake wawili waliochaguliwa na maeneo, na raia wapigakura wa mabaraza ya wilaya katika kila eneo walio na uwezo wa kupiga;
(c) walemavu au walio katika makundi ya vijana, waliochaguliwa mmoja kutoka kila eneo;
(d) Spika atakayekuwa mwanachama wa heshima.
(2) Uchaguzi chini ya ibara ya (1)(c) utafanyika kwa kuzingatia sheria ya bunge.
(3) Baada ya kuchaguliwa, maseneta waliochaguliwa kutoka kila eneo watajenga kundi moja maalumu kwa ajili ya ibara ya 141(2)(a).
(4) Hakuna chochote katika Kifungu hiki kitakachoangaliwa kama kinachowazuia wanawake dhidi ya kugombea nyadhifa katika uchaguzi chini ya (1)(a).

**Uanachama katika Bunge**
**126.** (1) Bunge litajumuisha –
(a) wabunge waliochaguliwa mmoja kutoka kila eneobunge itavyodokezwa na sheria;
(b wanawake waliochaguliwa mmoja kutoka katika kila wilaya, kila wilaya ikitoa mjumbe mmoja kwa kutazamwa kama eneobunge moja;
(c) wanachama saba walemavu na wasiozidi wanne katika jinsi moja;

(d) wanachama saba waliochaguliwa kutoka jumuia, makundi na wafanyakazi tengwa; na

(e) Spika atakayekuwa mwanachama wa heshima.

2) Uchaguzi chini ya ibara ya (1)(c) na (d) utafanywa tu na makundi yanayokub aliwa kupigakura inavyopendekezwa na sheria.

3) Mwanachama anayerejelewa katika ibara ya (1)(c) na (d) atashikilia ofisi hiyo kwa muhula mmoja pekee.

(4) Hakuna chochote katika Kifungu hiki kitakachowazuia wanawake dhidi ya kugomea nyadhifa katika uchaguzi chini ya ibara (1)(a).

(5) Bunge litatunga sheria ya kuidhinisha utekelezaji wa kifungu hiki.

(6) Hata hivyo, pamoja na Kifungu hiki Bunge halitakuwa na wanachama zaidi ya thuluthi-mbili wa jinsia moja.

**Masharti ya kufaa na kutofaa kuchaguliwa kama mbunge**

**127.** (1) Ila tu endapo itakataliwa chini ya ibara ya (2), mtu anafaa kubigiwa kura ubunge iwapo mtu huyo-

(a) ni raia;

(b) amesajiliwa kama mpigakura;

(c) anafikisha kiwango chochote cha kielimu, kimaadili na mahitaji ya maadili ya kikazi itakavyoelezwa na Katiba hii au na Sheria ya Bunge;

(d) ameteuliwa na chama cha kisiasa isipokuwa tu mgombea anayerejelewa chini ya Vifungu 125(1)(c) na 126 (1)(c) na (d);

(e) kwa mujibu wa kuchaguliwa katika Bunge, ni mgombea wa kibinafsi anayeungwa mkono na angalau wapiga kura elfu moja katika eneobunge husika kwa njia itakayopendelewa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka.

(2) Mtu hataruhusiwa kugombea ubunge iwapo mtu huyo-

(a) anashikilia jukumu lolote la serikali au ofisi ya umma kando na kuwa Mbunge;

(b) ni mwanachama wa baraza la kieneo au wilaya;

(c) hana akili timamu;

(d) anakosa pesa za kutosha;

(e) anahudumia hukumu ya kifungo cha zaidi ya miezi sita; au

(f) amepatikana kwa mujibu wa sheria yoyote, akiwa ametumia ofisi ya Serikali au ofisi ya umma vibaya au endapo kwa njia yoyote amekiuka kanuni za Sura ya Tisa.

(3) Mtu hazuiwi kugombea ofisi chini ya ibara ya (2) isipokuwa tu endapo hatua zote za rufani zimekamilishwa, kupuuzwa au kutupiliwa mbali.

**Kukuza uwakilishi wa makundi tengwa**

**128.** Bunge litatunga sheria kudumisha uwakilishwaji Bungeni wa-

(a) wanawake;

(b) walemavu;

(c) vijana;

(d) makabila madogo na wanyonge wengine; na

(e) jumuia tengwa.

**Uchaguzi wa wabunge**

**129.**(1)Kwa kuzingatia Kifungu 180(8), uchaguzi mkuu wa wabunge utafanywa Jumanne ya kabla ya siku ishirini na nane za mwisho wa muhula wa Bunge.

(2) Wanachama wa Seneti wanaorejelewa katika Kifungu 125(1)(a) watachagu liwa kwenye mkutano wa kwanza wa baraza la wilaya baada ya uchaguzi wa baraza hilo la wilaya.

(3) Wanachama wa Seneti wanaorejelewa katika kifungu 125(1)(b) watachaguliwa katika siku ishirini na nane za uchaguzi mkuu wa Bunge.

(4) Endapo kutakuwa na pengo katika ofisi ya mwanachama yeyote wa Seneti ali yechaguliwa chini ya kifungu 125 (1)(a) au (b), Spika atatoa notisi ya maandishi kuhusu pengo hilo katika siku ishirini na moja za utukiaji wa pengo hilo kwa-

(a) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka; na

(b) Baraza la wilaya ambapo mwanachama huyo alikuwa amechaguliwa na baraza husika la kieneo.

(5) Uchaguzi utakaofanywa kwa misingi ya pengo linalorejelewa katika ibara ya (2), utafanywa katika siku ishirini na moja za notisi ya Spika kwa kuzingatia ibara ya (7).

(6) Pengo linapotokea katika nafasi ya Mbunge kando nay a Spika-

(a) Spika husika, atatoa notisi ya maandishi kuhusu pengo hilo katika siku ishirini na moja za utukiaji wake kwa Tume Huru ya Uchaguzi na mipaka; na

(b) uchaguzi mdogo, kuambatana na ibara ya (5) utafanyika katika siku tisini za utukiaji wapengo hilo.

(7) Uchaguzi mdogo hautafanyika katika miezi mitatu kabla ya kufanyika uchaguzi mkuu.

(8) Kwa ajili ya uchaguzi wa Seneti, Eneo la Nairobi litachukuliwa kuwa na wilaya nne na ambazo kila mojawapo itakuwa eneobunge.

**Kutoka ofisini kwa Mbunge**

**130.** Nafasi ya Mbunge itakuwa wazi-

(a) iwapo mbunge huyo anakufa;

(b) iwapo mbunge huyo anajiuzulu katika njia ya maandishi yaliyotumwa kwa Spika husika;

(c) iwapo mbunge huyo anazuiwa kushiriki katika uchaguzi huo chini ya Kifungu 127(2);

(d)iwapo mbunge huyo anakosekana katika vikao vinane mfululizo vya bunge lake wakati ambapo vikao vya bunge vinaendelea, bila ruhusa ya Spika wa bunge lake katika maandishi, na hatoi sababu ya kuridhisha ya kukosekana kwake kwa kamati husika;

(e) iwapo mbunge huyo atatolewa ofisini chini ya sheria ya bunge itakayound wa chini ya Kifungu 101;

(f) iwapo mbunge huyo anajiuzulu au kufukuzwa kutoka chama cha kisiasa kwa mujibu wa Kifungu 115;

(g) iwapo mbunge huyo atajiunga na chama kingine cha kisiasa baada ya kuingia Bungeni kama mgombea wa kibinafsi;

(h) baada ya kukamilika kwa kipindi cha bunge;

(i) endapo ni katika kisa cha Seneta aliyechaguliwa chini ya 125(1)(b), ita kuwa baada ya kukamilika kwa kipindi cha baraza la eneo lililomchagua Seneta huyo; na

(j) endapo ni katika kisa cha Seneta aliyechaguliwa na baraza la wilaya chini ya Kifungu 125(1)(a), itakuwa baada ya kukamilika kwa kipindi cha baraza la wilaya lililomchagua Seneta huyo.

**Haki ya kumwita na kumkosoa mbunge**

**131.** (1) Wapigakura chini ya Vifungu 125 na 126, wana haki ya kumwita na kumkosoa mbunge waliyemchagua kabla ya kukamilika kwa kipindi cha bunge husika.

(2) Bunge litatunga sheria kutoa misingi ya uwezekano wa kuitwa na kukosolewa kwa mbunge huyo na hatua za kufuata.

**Kukubalika kwa ubunge**

**132.** (1) Mahakama Kuu itasikiliza na kuamua iwapo-

(a) mtu amechaguliwa kama mbunge kwa njia sahihi; au

(b) kiti cha mbuge kimetangazwa kuwa wazi.

**Sehemu ya 3- Maafisa wa Bunge**

**Spika na Naibu wa Spika**

**133.** (1) Kutakuwa na-

(a) Spika wa Bunge atakayechaguliwa na Bunge kulingana na Kanuni za Bunge, kutoka miongoni mwa watu walio na sifa zinazohitajika kuchagu liwa kama wabunge na ambao si wabunge; na

(b) Naibu Spika wa Bunge atakayechaguliwa na Bunge kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kutoka miongoni mwa wabunge.

(2) Ofisi ya Spika au Naibu Spika itakuwa wazi-

(a) endapo Bunge linakutana kwa mara ya kwanza baada ya uchaguzi;

(b) iwapo anayeshikilia ofisi anafutiliwa mbali kwa mujibu wa Kifungu 127 (2);

(c) iwapo Bunge husika linaamua kwa wingi wa idadi ya kura zisizopungua thuluthi-mbili ya wabunge;

(d) iwapo anayeshikilia ofisi anakufa; au

(e) iwapo anayeshikilia ofisi hiyo anajiuzulu kwa kuandika barua kwa njia Bunge husika.

**Kuongoza vikao Bungeni**

**134.** Katika kikao chochote cha Bunge-

(a) Spika ataongoza;

(b) Spika asipokuwepo, Naibu Spika ataongoza; na

(c) Spika na Naibu wake wasipokuwepo, mbunge mwingine yeyote atakaye chaguliwa na Bunge ataongoza.

**Kiongozi Rasmi wa Upinzani Bungeni**

**135.**(1) Kutakuwa na Kiongozi Rasmi wa Upinzani.

(2) Wabunge kutoka kwenye chama kilicho na wabunge wengi au wanachama wa vyama vilivyounda muungano bungeni, wanaweza kuchagua mmoja wao kuwa Kiongozi Rasmi wa Upinzani.

(3) Kuhusiana na shughuli za Bunge, Kiongozi rasmi wa Upinzani bungeni-

(a) atakuwa na cheo cha chini ya Rais wa Taifa, Naibu Rais wa Taifa, Waziri Mkuu na Spika;

(b) atakuwa na haki ya kushiriki katika sherehe rasmi za Kitaifa; na

(c) atakuwa na haki ya kutoa hotuba bungeni, punde baada ya Waziri Mkuu atakayetanguliwa na Rais.

(4) Kanuni za bunge zitatoa mazingira bora ya kushiriki kwa Kiongozi Rasmi wa Upinzani bungeni.

**Karani na wafanyakazi wa Bunge**

**136.** (1) Kutakuwa na Karani wa kila bunge atakayeteuliwa na Tume ya Huduma za Bunge kwa idhinisho la Bunge husika.

(2) Ofisi za makarani na ofisi za wahudumu katika ofisi hizo zitakuwa katika ofisi za huduma ya Bunge.

(3) Kwa mujibu wa ibara (4), karani atastaafu baada ya kufikisha miaka sitini na mitano.

(4) Bunge lolote linaweza, kwa zaidi ya thuluthi-mbili ya kura za wabunge linaweza kumfuta Karani.

**Sehemu ya 4 – Kutunga sheria Bungeni**

**Mamlaka ya kutunga sheria**

**137.** (1) Bunge litatumia mamlaka yake ya kutunga sheria kupitia miswada itakayopi ishwa bungeni na kutiwa saini na Rais wa Taifa.

(2) Mbunge yeyote, au kamati ya bunge inaweza kupeleka miswada Bungeni.

(3) Mswada unaweza kutoka katika bunge lolote lakini mswada kuhusu pesa utatoka katika Bunge la kitaifa.

(4) Mswada wowote unaofkishwa bungeni usindikizwe memoranda ya kueleza-

(a) uwezekano wa kukiuka Sheria ya Haki au athari nyingine za Kikatiba;

(b) mchango wowote wa umma katika kutayarisha mswada huo; na

(c) mchango mwingine wowote kutoka kwa umma unaopendekezwa kabla mswada huo kuidhinishwa kuwa sheria; na

(d) endapo pesa za umma zitahitajika katika kutekeleza sheria hiyo inayo pendekezwa kutungwa.

(5) Kamati husika-

(a) tachunguza hali na viwango vya kushiriki kwa umma kwa kila Mswada unaowasilishwa Bungeni; na

(b) kurahisisha kushiriki na kuhakikisha inatekelezwa ipasavyo;

(c) kutambua iwapo pesa za umma zitahitajika katika kutekeleza sheria iliyopendekezwa bungeni.

(6) Bunge litatenga muda wa kutosha kushughulikia Miswada kwa usawa.

**Miswada ya Fedha**

**138.** (1) Mswada wa fedha unaweza kuwasilishwa tu Waziri.

(2) Katika Sura hii, "mswada wa fedha" unamaanisha mswada unaojumuisha vipengele vya kuhusiana na –

(a) kutoza, kupunguza, kubadlisha au kudhibiti ushuru;

(b) kutoza ada fulani kwenye Hazina ya kifedha ya Pamoja au hazina yoyote nyingine ya serikali ya kitaifa au kupunguzwa kwa ada hizo;

(c) kutumia, kupokea, kutunza, kuwekeza au kutoa pesa za umma;

(d) kutolewa kwa pesa kutoka kwenye hazina ya umma na kupewa mtu au mamlaka yoyote au kufutiliwa mbali kwa pesa alizopewa mtu kutoka kwenye hazina ya umma;

(e) kusimamia ukopaji wa pesa au kulipwa kwake; au

(f) maswala mengineyo yanayotokana na maswala hayo.

(3) Katika ibara (2), mitajo ya "ushuru", "pesa za umma", na "mkopo", hayajumui shi ushuru, pesa za umma au mkopo kutoka kwa serikali zilizogatuliwa.

(4) sipokuwa kwa mapendekezo ya serikali ya kitaifa yaliyoidhinishwa na Waziri, hakuna Bunge litakaloendelea na vikao kuhusu mjadala wowote (ikiwemo marekebisho ya mada) na hali ambayo kwa maoni ya Spika inaweza kuingiliana na majukumu ya vipengele vilivyopo katika ibara ya (2).

**Maoni ya Bunge jingine**

**139.** (1) Sheria ikipitishwa na Bunge moja, Spika wa Bunge hilo atautuma kwa m Spika wa Bunge la pili.

(2)Iwapo mabunge yote mawili yanapitisha mswada kwa hali sawa, Spika wa Bunge lililotoa mswada atatuma mswada huo kwa Rais katika siku saba ili aweke saini;

(3)Iwapo Bunge moja litapitisha Mswada na lile jingine liukatae, mswada huo utakuwa umeshindwa isipokuwa ukiwa Mswada wa Fedha.

(4)Endapo mswada fulani kwa maoni ya Spika wa Bunge ni mswada wa pesa, na akautuma katika Seneti Spika huyo atahitajika kuandika idhibati kwamba ni mswada wa kifedha na kuambatisha kwa mswada huo.

(5) Endapo mswada uliotumwa na Bunge kwa Seneti kwa mujibu wa ibara (4), haupitishwi na Seneti katika siku kumi na nne baada ya kutumiwa, mswada huo utapelekewa Rais ili aweke sahihi.

(6) Endapo Bunge moja linapitisha mswada tofauti na, Bunge la pili linapitisha marekebisho yake, Spika wa Bunge la kwanza ataitisha kupigiwa kura upya kwa mswada huo na marekebisho yaliyowekwa na endapo utapitishwa ataupeleka kwa Rais ili aweke saini.

(7) Iwapo mswada unaorejelewa katika ibara ya (6) haupitishwi kwenye Bunge la Kwanza katika hali yake baada ya marekebisho, maspika wa mabunge yote mawili watateua kamati ya upatanishi iliyo na idadi sawa ya wajumbe kupitia machapisho hayo mawili na kujenga moja ambalo ni wakilishi.

(8)Iwapo kamati ya upatanishi itaafikiana kuhusu moja wakilishi, kila bunge linaweza kupiga kura ili kuidhinisha au kukataa mswada huo wakilishi.

(9) Iwapo mabunge yote mawili yataidhinisha mswada huo wakilishi, Spika wa Bunge ulikotoka atampelekea Rais aweke saini katika muda wa siku saba.

(10) Iwapo kamati ya upatanishi inakosa kuelewana katika siku thelathini au mswada huo wakilishi unakataliwa na kila bunge, basi itachukuliwa kwamba mswada huo umeshindwa.

**Idhini ya Rais**

**140.** (1) Katika siku kumi na nne baada ya kupokea mwada uliowasilishwa kwa mujibu wa Kifungu 139, Rais wa Taifa-

(a) ataweka saini; au

(b) atarudisha mswada bungeni ili kuchunguzwa upya na kuchunguza maswala ambayo huenda akawa ameyatilia shaka.

(2) Iwapo Rais ataurudisha mswada bungeni kuchunguzwa upya, Bunge linaweza-

(a) kuurekebisha Mswada huo kwa kuzingatia mapendekezo ya Rais wa Taifa; au

(b) kuupitisha mswada huo kwa mara ya pili bila kufanya marekebisho.

(3) Iwapo Bunge limerekebisha mswada huo , Spika anayehusika atampelekea Rais ili aweke sani.

(4) Iwapo Bunge baada ya kuzingatia mapendekezo ya Rais, itapitisha mswada kwa mara ya pili, kwa angalau nusu ya idadi ya wabunge-

(a) Spika wa Bunge husika atapaswa kumrejeshea Rais wa Taifa aweke saini katika siku saba baada ya kurudishiwa; na

(b) Rais wa Taifa atauweka saini mswada huo katika siku saba.

(5) Iwapo Rais wa Taifa atakosa au kuchelea kuweka saini kwa wakati unaopendekezwa katika ibara (1) au (4)(b), mswada huo utachukuliwa kama ulioanza kutekelezeka siku ya mwisho iliyopaswa kuwekwa saini.

**Kutekelezeka kwa sheria**

**141**. (1) Sheria iliyopitishwa na Bunge na kuidhinishwa na Rais wa Taifa-

(a) itachapishwa katika Gazeti maalumu la serikali katika siku saba za kuidhinishwa; na

(b) inaanza kutumiwa siku ya kumi na nne baada ya kuchapishwa kwake katika Gazeti isipokuwa endapo sheria yenyewe inapendekeza siku ya kuanza kutumiwa kwake.

(2) Sheria inayotetea maslahi ya kifedha ya wabunge haitatekelezeka hadi baada ya uvunjaji wa vikao vya bunge vilivyoidhinishwa kisheria.

(3) Ibara ya (2) haigusii maslahi ya wabunge yanayoambatana na maslahi ya umma kwa jumla.

**Haki ya kulalamikia Bunge**

**142.** (1) Kila mtu ana haki ya kulalamikia Bunge litunge, kurekebisha au kutoa sheria yoyote.

(2) Bunge litaweka vipengele kuhusu utaratibu wa kufurahia haki hii.

**Idadi ya wabunge katika vikao**

**143.** Idadi ya wabunge wanaopaswa kuwepo ili kufanyike kikao ni robo ya wabunge.

**Lugha rasmi za Bunge**

**144.** Lugha rasmi za Bunge zitakuwa Kiswahili, Kiingereza na lugha ya Kiishara na shughuli ya Bunge inaweza kufanywa katika Kiingereza, Kiswahili na lugha ya ishara.

**Kupiga kura Bungeni**

**145.** (1) Swala lolote litakalopendekezwa kutatuliwa Bungeni isipokuwa endapo imependekezwa tofauti na Katiba hii, litaamuliwa kwa wingi wa watu waliopo na kupiga kura katika kila Bunge.

(2)Katika maswala yaliyopendekezwa kuamuliwa katika Bunge lolote-

(a) Spika hatapiga kura; na

(b) kati ya maswala ya kulingana, mshtaki atapoteza.

(3) Kura ya mwanachama anayepiga kura kuhusu mambo yanayomhusu mwenyewe kifedha haitahesabiwa.

**Maamuzi ya Seneti**

**146.** (1) Endapo kwa maoni ya Spika wa Seneti, mswada fulani unahusu maeneo au wilaya utakuwa na idhini ya Spika wa Seneti kwamba ni swala linaloathiri maeneo au wilaya.

(2) Endapo Seneti inapaswa kupiga kura kuhusiana na swala lolote, Spika ataamua iwapo swala hilo linaathiri au haliathiri maeneo au wilaya.

(3) Seneti inapopiga kura kuhusu swala linaloathiri maeneo au wilaya kila seneta atakuwa na kura moja.

(4) Katika Seneti, isipokuwa pale ambapo Katiba hii inasema kinyume-

(a) kila eneo litakuwa na kura moja kwa niaba ya kiongozi wa eneo hilo au, na endapo hakuna kiongozi wa ujumbe huo litaongozwa na mtu mwingine yeyote kwa niaba ya ujumbe huo; na

(b) maswala yote yataamuliwa na thuluthi-mbili ya wingi wa idadi ya ujumbe huo.

(5) Sheria ya kitaifa itakayotungwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa kwa kupitisha Miswada inayoathiri mweneo au wilaya, itatoa mazingira sawa ambapo ujumbe wa Seneti utashauriana kwa ajili ya ibara ya (4)(a).

(6) Mwanachama yeyote wa Baraza la mawaziri au Naibu Waziri anaweza kuhudhuria na kuzungumza katika Seneti, lakini hatashiriki uchaguzi wa swala lolote la Seneti.

**Kudhibitiwa kwa utaratibu**

**147.**(1) Kila Bunge-

(a) litadhibiti taratibu zake lenyewe;

(b) linaweza kuanzisha kamati; na

(c) litatunga Kanuni za Bunge ili kudhibiti vikao vyake ikiwemo vikao vya kamati zake.

(2) Bunge linaweza kuanzisha kamati za pamoja zinazojumuisha wabunge kutoka mabunge yote mawili na kwa pamoja kudhibiti utaratibu wa kamati hizo.

(3) Marejeleo yoyote katika Katiba hii kwa mwanakamati yeyote wa Bunge, yana chukuliwa kama marejeleo ya mwanakamati ya pamoja isipokuwa endapo muktadha unapendekeza tofauti.

(4) Vikao vya kila mojawapo wa mabunge hayo havitazuiwa kuendelea kwa sababu ya-

(a) pengo katika uanachama; au

(b) kuwepo au kushiriki kwa mtu yeyote asiyepaswa kuwepo au kushiriki katika vikao vya bunge hilo.

**Uwezo wa kutaka ushahidi**

**148.** Katika kutekeleza majukumu yake-

(a) bunge lolote na yoyote katika kamati zake, inaweza kumwita mtu yeyote anayesimamia ofisi ya umma au mtu binafssi kutoa ushahidi mbele yake;

(b) kamati ya mojawapo wa bunge inaweza kumteua mbunge yeyote au kumwajiri mtu yeyote wa kusaidia katika kutekeleza majukumu yake; na

(c) bunge lolote linaweza na mojawapo wa kamati zake litakuwa na mamlaka ya Mahakama Kuu katika-

(i) kuhakikisha mahudhurio ya mashahidi na kuwaapisha, au pengine;

(ii) kuwashurutisha kutoa ushahidi wa vibali; na

(iii) kutoa ombi la kuwahoji mashahidi walio katika mataifa ya nje.

**Kufikiwa na umma**

**149.** (1) Bunge-

(a) litafanya shughuli zake kwa njia ya uwazi, na kufanya vikao vyake na vile vya kamati zake mbele ya umma; na

(b) litarahisisha kushiriki kwa umma katika jukumu la Bunge la kutunga sheria na shughuli zake nyingine kamati zake.

(2) Bunge halitatenga umma au chombo chochote cha habari dhidi ya kuhudhuria vikao isipokuwa katika hali mahsusi ambazo Spika ataamua kwamba kuna sababu za kutosha kufanya hivyo.

**Uwezo, haki na kinga**

**150.**(1) Kutakuwa na uhuru wa kujieleza na kujadiliana Bungeni.

(2) Bunge kwa ajili ya kushughulikia majukumu yake kwa mpangilio na ukamilifu linatoa uwezo , haki na kinga kwake, kamati zake na wabunge wake.

**Sehemu ya 5 – Ziada**

**Usajili wa Sheria buniwa**

**151.**(1) Kwa kupitia njia ya sheria Bunge litaanzisha-

(a) Rejista ya Sheria buniwa kwa umma itakayoandikwa katika Kiswahili na Kiingereza kwa njia ya kuona na Breli chini ya Ulinzi wa Spika wa Bunge; na

(b) taratibu nyingine za ziada kuhusu kuchapisha na kusambaza sheria zilizotungwa.

(2) Nakala ya kila sheria buniwa itahifadhiwa katika Rejista ya Sheria buniwa.

(3) Nakala ya kila sheria buniwa iliyohifadhiwa katika Hifadhi iliyokubaliwa kuwa sawa na msajili ni ushahidi wa vipengele vya sheria hiyo buniwa.

(4) Endapo kutakuwa na mgongano kati ya matoleo ya lugha tofauti ya sheria buniwa, toleo litakalokuwa limetiwa saini na Rais wa Taifa litatumika.

(5) Serikali ya kitaifa itahakikisha kwamba sheria zote buniwa-

(a) zinakuwepo katika maktaba zote za umma; na

(b) zinakuwepo katika Breli na vyombo vingine vinavyofaa vipofu na walio na ulemavu mwingine.

**Makao ya Bunge**

**152.** (1) Kuambatana na ibara (2), makao ya Bunge yatakuwa Nairobi.

(2) Vikao vya Bunge lolote vitafanyiwa katika sehemu nyingine, na vitaanza wakati utakaoamuliwa na Bunge.

(3) Kila kutakapochaguliwa Bunge mpya, Rais wa Taifa kwa kupitia notisi ya Gazeti maalumu la serikali, atateua mahali na tarehe, sio siku saba baada ya kukamilika kwa kipindi cha Bunge lililopita katika kikao cha kwanaza cha Bunge.

**Kipindi cha Bunge**

**153.** (1) Kipindi cha kila bunge ni miaka mitano kutoka tarehe ya kikao cha kwanza baada ya uchaguzi isipokuwa katika Bunge kuu linavunjwa mapema kwa mujibu wa Kifungu 180(8).

(2)Wakati wowote Kenya ikiwa katika vita, Bunge linaweza kuamua kwa njia ya kura ya idadi isiyopungua thuluthi-mbili ya wabunge kuongeza kipindi cha Bunge kwa muda usiozidi miezi sita.

(3) Kipindi cha bunge hakitaongezwa chini ya ibara ya (2)-

(a) kwa jumla ya zaidi ya miezi kumi na miwili; au

(b) kabla ya kukamilika kwa kipindi chake baada ya uchaguzi mkuu unaofanyika kulingana na Kifungu 129(1).

**Tume ya Huduma za Bunge**

**154.**(1) Kuna Tume buniwa ya Huduma ya Bunge itakayojumuisha-

(a) mwenyekiti na makamu wake waliochaguliwa na Tume kutoka kwa wana chama walioteuliwa kwa mujibu wa aya (b);

(b) wanachama saba walioteuliwa na Bunge kutoka miongoni mwa wabunge ambapo-

(i) wanne watateuliwa kwa usawa kutoka Mabunge yote mawili na chama au washrika katika muungano unaojenga serikali ya kitaifa na ambao wawili kati yao watakuwa wanawake; na

(ii) watatu watakuwa wamteuliwa na vyama visivyo sehemu ya serikali ya taifa, angalau mmoja wao atateuliwa kutoka kila Bunge na angalau mmoja wao atakuwa mwanamke; na

(c) mwanamume na mwanamke walioteuliwa na Bunge kutoka watu ambao si wabunge lakini wana uzoefu mkubwa kwa maswala yanayohusu umma.

(2) Tume itateua makatibu wake.

(3) Mwanachama wa Tume atatoka ofisini-

(a) iwapo mtu huyo ni Mbunge-

(i) baada ya kukamilika kwa kipindi cha Bunge ambacho mtu huyo alikuwa mbuge;

(ii) mtu huyo anakoma kuwa Mbunge; au

(iii) ikitokea hali kwamba mtu asingalikuwa Mbunge asingaliruhusiwa kuchaguliwa katika wadhifa kama huo; au

(b) iwapo mtu huyo ni mteule, baada ya kufutiliwa mbali kwa uteuzi wake na Bunge.

(4) Kando na ibara ya (3), baada ya kuvunjwa kwa Bunge, mwanachama wa Tume aliyeteuliwa kwa mujibu wa ibara (1)(b) ataendelea kuwa ofisini hadi mwanachama mwingine atakapoteuliwa na Bunge kushika nafasi yake.

(5) Tume ina jukumu la-

(a) kutoa huduma na vifaa ili kuhakikisha utendaji kazi wa Bunge;

(b) kujenga ofisi katika huduma ya Bunge na kuchagua na kusimamia wafanyakazi;

(c) kutayarisha makadirio ya kila mwaka ya matumizi ya pesa katika huduma za Bunge na kudhibiti bejeti yake;

(d) kuanzisha ama kibinafsi au katika mashirika husika, mipango ya kukuza maadili ya demokrasia ya bunge; na

(e) kutekeleza majukumu mengine-

(i) muhimu kwa manufaa ya wabunge na wafanyakazi wa Bunge; au

(ii) yatakayopendekezwa na au kwa mujibu wa sheria.

## SURA YA KUMI NA MBILI

**SERIKALI**

**Sehemu ya 1- Kanuni na muundo wa mamlaka ya Serikali ya Taifa.**

**Kanuni za mamlaka ya serikali**

**155.** (1) Mamlaka ya Serikali hutokana na katiba hii.

(2) Inapaswa kutumika-

(a) kwa njia ambayo inakubaliana na huduma kwa wananchi na jamii za Kenya : na

(b) Kwa hali njema na maslahi yao.

(3) Uhusika wa mamlaka ya Rais ya kitaifa utitilia maananani maeneo na makabila mbali mbali ya Kenya.

**Serikali ya Taifa**

**156.** (1) mamalaka ya Rais wa taifa la Kenya yatafanya kazi kulingana na katiba hii, kwa au ama kwa mamlaka ya taifa ya Rais na Waziri Mkuu pamoja na baraza la Mawaziri.

(2) Rais wa taifa atatekeleza majukumu yake kwa kutumia uwezo wake kwa ushauri wa Baraza la Mawaziri isipokuwa katiba hii iwe inasema vinginevyo.

**Sehemu ya 2 - Rais wa Taifa na Naibu Rais**

**Mamlaka ya Rais wa Taifa**

**157.** (1) Kutakuwa na Rais wa Taifa.

(2) Rais wa Taifa ndiye-

(a) Kiongozi wa Taifa

(b) Amri Jeshi Mkuu wa Majeshi yote ya Kenya; na

(c) Mwenyekiti wa barasa la kitaifa la usalama

(3) Rais ni ishara ya umoja wa kitaifa.

(4) Rais wa Taifa -

(a) ataiheshimu, kuishikilia na kuilinda katiba;

(b) kuulinda uhuru wa taifa la Kenya.

(c) kukuza na kudumisha umoja wa taifa.

(d) Kukuza heshima kwa wingi wa tofauti katika jamii na watu wa Kenya.

(e) kuhakikisha ulinzi wa uhuru na haki za kimsingi za raia na utawala wa sheria .

(5) Rais hatachukua wajibu mwingine wowote simamia ofisi nyingine yoyote ya kitaifa au ya umma.

**Majukumu ya Rais wa Taifa.**

**158.** (1) Rais ata-

(a) toa hotuba katika ufunguzi wa kila bunge jipya teule;

(b) toa hotuba katika kikao maalum cha Bunge mara moja kwa mwaka.

(c) Mara moja kila mwaka-

(i) atoe ripoti, kupitia kwa hotuba kwa taifa, kuhusu hatua ambazo zime chukuliwa na maendeleo ambayo yamepatikana ili kufikia thamana, kanuni na malengo ya kitaifa ambayo yameelezewa katika Sura ya Tatu; na

(ii) chapisha katika gazeti rasmi la serikali, yaliyomo katika hatua na maendeleo yaliyoelezewa katika sehemu ya ibara (i).

(2) Rais wa Taifa kwa mujibu wa Katiba na sheria, atateue na anaweza ku waachiza kazi-

(a) Baraza la Mawaziri ikiwa ni pamoja na, Waziri Mkuu , Manaibu wa Waziri Mkuu na Mawaziri;

(b) Manaibu wa Waziri mkuu;

(c) Majaji wa mahakama zenye mamlaka kuu; na

(d) Ofisa yeyote mwingine wa serikali au wa utumishi wa umma ambaye kikatiba anahitajika kuteuliwa na Rais wa taifa.

(3) Rais anaweza-

(a) Kuwateua mabalozi, na wawakilishi wengine wa nchi kwa idhini ya Bunge; na

(b) Kuwapokea wawakilishi na mabalozi na; na

(c) Kutuza kwa niaba ya wananchi na serikali.

(4) Kwa idhini ya Bunge, Rais wa taifa anaweza kutia saini hati za makubaliano na mikataba ya kimataifa.

(5) Kwa idhini ya baraza la mawaziri, Rais anaweza –

(a) Kwa kutegea Kifungu cha 75; kutangaza hali ya hatari;

(b) kutangaza vita.

(6) Rais wa taifa –

(a) anaweza kuteua tume za uchunguzi; na

(b) Ataifanya ripoti ya tume teule ya uchunguzi kuwasilishwa Bungeni siku ishirini na moja baada ya kupokelewa na Rais wa Taifa.

(7) Rais wa Taifa atashuriana na Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba -

(a) Majukumu ya ya kimataifa Serikali yametekelezwa kupitia kwa majukumu ya Mawaziri Wanaohusika.

(8) Mara moja kila mwaka ,Rais wa Taifa atatoa ripoti kwa Bunge kuhusu maendeleo ambayo yamepatikana katika kutimiza wajibu wa wa kimataifa wa Taifa.

**Majukumu ya Rais katika kutunga sheria**

**159.** (1) Rais wa Taifa anaweza kupendekeza sheria na kuipeleka kwa Braza la Mawaziri kuliomba liikubalishe kupelekwa Bungeni kama msada wa Serikali.

(2) Akikadhiwa Msada ambao umepishwa na Bunge, Rais wa Taifa atatekeleza kwa mujibu wa Kifungu cha 140.

(3) Rais wa Taifa atahakikisha kwamba-

(a) Ushiriki wa wananchi unotakikana kuhusu utekelezaji wa Sheria ambazo zimekubaliwa na Bunge.;na

(b) Waziri Mkuu anatoa majukumu ya utekelezaji na uongizi wa Sheria zote za Bunge.

**Matumizi ya mamlaka ya Rais kwa Rais wa muda**

**160.** (1) Yeyote nanayeshikilia ofisi ya Rais wa Taifa au Yule ambaye anakubaliwa kwa mujibu wa Katiba hii kutumia mamlaka ya Rais wa Taifa-

(a) Wakati wa muda wa kipindi kinachoanzia katika tarehe ya kura ya kwanza katika uchaguzi wa Rais, na kukamilika wakati Rais mpya wa Taifa anapochukua hatamufisi; au

(b) Wakati Rais wa Taifa hayupo au hana uwezo, hawezi kutekeleza mamlaka ya Rais ambayo yanaelezwao katika ibara ya (2).

(2) Mamlaka ambayo yanaelezewa katika ibara (1) ni-

(a) kupendeza na kuteua majaji wa mahakama zenye mamlaka kuu;

(b) kuchukua hatua kutokana na malalamiko yanayopelekea kuondolewa kwa ofisa wa kimahakama.

(c) Mapendekezo au uteuzi wowote wa ofisa wa umma ambaye katiba au sheria hii inamhitaji Rais wa Taifa kuteua;

(d) Kuteua au kumwachisha kazi mabalozi au wawakilishi wa mabalozi na waakilishi wengine;

(e) Msamaha wa Rais;

(f) Mamlaka ya kutuza kwa niaba ya wananchi na Serikali.

**Uamuzi wa Rais wa Taifa**

**161.** Uamuzi wa Rais wa Taifa kulingana na mamlaka ya Katiba hii au kwa sheria nyingine ya Bunge utakuwa kwa maandishi na kuwa na muhuri na saini ya Rais wa Taifa.

**Uchaguzi wa Rais wa Taifa**

**162.** (1) Uchaguzi wa Rais wa Taifa utakuwa kwa njia ya moja kwa moja kwa watu wazima wenye haki ya kupiga kura kwa njia ya siri na utatekelezwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria nyingine yoyote ya Bunge ambayo inaongoza uchaguzi wa Rais.

(2) uchaguzi wa Rais wa Taifa utafanyika-

(a) Siku ya Jumanne punde tu inayotangilia siku ishirini na moja kabla ya kipindi cha Rais wa Taifa kuhudumu kumalizika.

(b) Hali ambazo zinafikiriwa katika Ibara 171.

**Sifa za kimsingi za kuchaguliwa na kutochaguliwa kwa Rais wa Taifa**

**163.** (1) mtu anahitimu kuteuliwa kuwa mgombeaji wa Urais ikiwa mtu huyo-

(a) Ni raia kwa kuzaliwa nchini

(b) amehitimu kugombea uchaguzi kama wa mbunge;

(c) ameteuliwa na wapiga kura wasiopungua laki moja ambao watakuwa hawajapua wapiga kura elfu tano kutoka kwa kila eneo.

(2) mtu hahitimu kuteuliwa kuwa mgombeaji wa uchaguzi wa Urais ikiwa mtu huyo-

(a) anawajibikia taifa la kigeni

(b) ana ofoso au anashikilia ofisi kama ofisa wa Serikali katika utumishi wa umma; au

(c) yeye ni Mbunge.

(3) Ibara(2) (b) haitatumika kwa-

(a) Rais wa Taifa; na

(b) Naibu Rais wa Taifa

**164.** Tarararibu katika uchaguzi wa Rais

(1) ikiwa mgombeaji mmoja wa Rais wa Taifa atateuliwa, mgombeaji huyo atatangazwa kuwa Rais wa Taifa mteule.

(2) iwapo wagombeajiaji Urais wa Taifa watatateuliwa wawili au zaidi, uchaguzi wa Urais utafanyika katika kila eneo Bunge.

(3) Katika uchaguzi wa Urais-

(a) wale wote ambao wamejiandisha kama wapiga kura kwa kusudi la uchaguzi wa Wabunge Wanaruhusiwa kupiga kura.

(b) uchaguzi utakuwa kwa njia ya siri katika siku ambayo imeelezwa

katika Ibara ya 162 wkwa wakati. Huo, katika sehemu hizo na kwa njia ambayo inaweza kuamriwa chini ya Sheria ya Bunge; na

(c) baada ya kuhesabiwa kwa kura katika vituo vya upigaji kura, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itahesabu na kuhakikisha hesabu ya kura na kutangaza matokeo.

(4) Mgombeaji wa uchaguzi wa Urais wa Taifa atayepata-

(a) zaidi ya nusu ya kura Zote zilizopigwa katika uchaguz; na

(b) angalau asilimia ishirini na tano ya kura zilizopigwa katika maeneo mengi;

Atatangazwa kuwa Rais mteule wa Taifa .

(5) Iwapo hakuna mgombeaji amechaguliwa,uchaguzi upya mwingine utaifanyika katika kipindi cha siku thelathini baada ya uchaguzi uliopita na katika uchaguzi huo mpya, wagombeji watakuwa-

(a) mgombeaji au wagombeaji ambao wamepata kura nyingi zaidi; na

(b) mgombeaji au wagombeaji ambao wamepata idadi ya pili ya wingi wa kura.

(6) pale ambapo wagombeaji zaidi ya mmoja wamepata idadi kubwa zaidi ya kura, ibara ya(6)(b) haitatumika na wagombeaji pekee katika uchaguzi mpya watakuwa wale ambao nuiwa na ibara ya (6) (a)

(8) mgombeaji ambaye atapata idadi kubwa, au idadi kubwa zaidi ya kura, katika kutegemea hali hiyo, katika uchaguzi mpya atatangazwa kuwa Rais mteulewa Taifa.

(9) uchaguzi wa Urais utafutiliwa mbali na uchaguzi mwingine kufanyika iwapo-

(a) hakuna mtu ambaye ameteuliwa kama mgombea uchaguzi ambaye ameteuliwa kumalizika kabla ya kipindi kilichowekwa cha kuwasilisha hati za uteuzi;

(b) mgombea uchaguzi ataaga dunia siku ya uchaguzi au siku yoyote kati ya hizo ambapo uchaguzi unafanyika au utafanyika.;au

(c) mgombea uchaguzi ambaye alistahili kutangazwa kuwa Rais Mteule wa Taifa kuaaga dunia baada ya kuanza kushinda uchaguzi lakini kabla ya ya kutangazwa Rais mteule wa Taifa.

(10) uchaguzi mpya wa Urais chini ya kifungum (6) utafayika katika muda siku sitini za tarehe iliyokuwa imewekwa katika uchaguzi uliopita.

(11) Katika siku sba za uchaguzi wa Urais,Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na na Mipaka ita-

(a) kutangaza matokeo ya uchaguzi; na

(b) kupeleka ripoti iliyoandikwa ya matokeo uchaguzi kwa Hakimu Mkuu na Rais aliye mamlakani.

**Maswali kuhusu uhalalali wa uchaguzi wa Urais**

**165.** (1) Mtu anaweza kuwasilisha malalamiko katika Mahakama ya Katiba kupinga uchaguzi wa Rais mteule wa Taifa.

(2) Malalamiko haya yatawasilishwa mahakamani katika muda wa siku saba baada ya tarehe ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa Rais.

(3) Mahaka ya Kikatiba baada ya siku saba za kuwasilisha malalamiko,ita sikiza na kuamua malalamiko na uamuzi huo utakuwa wa mwisho.

(4) Iwapo Mahakama ya kikatiba itaamuwa kuwa uchaguzi wa Rais mteule si halali,uchaguzi mpya utafanyika siku sitini baada ya ya uamuzi huo.

**Kuchukua hatamu za Urais wa Taifa**

**165.** (1) kuapishwa kwa Rais mteule wa Taifa kutakuwa mbele ya jaji Mkuu au iwapo Jaji Mkuu Mkuu hayupo, mbele ya Naibu wa jaji mkuu na mbele ya umma.

(2) Rais mteule wa Taifa ataapishwa Jumanne ya kwanza itakayofuata siku kumi na nne baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa Urais isipokuwa matangazo hayo yawe yamepingwa kulingana na Kifungu 165.

(3) Iwapo matokeo ya uchaguzi wa Urais yamepingwa chini ya Kifungu 165 lakini koti lishikilie matokeo hayo, Rais mteule wa Taifa ataapishwa Jumanne ya kwanza inayofuta siku saba baada ya ya uamuzi wa Mahakama.

(4) Rais mteule anachukua hatamu za Urais kwa kuchukua na kutia saini-

(a) kiapo cha uaminifu; na

(b) kiapo cha kutekeleza majukumu ya Urais kama ilivyoamriwa katika Ratiba ya Tatu.

**Masharti ya ofisi ya Rais**

**167.** (1) Rais wa Taifa atashikilia ofisi kwa kipindi kisichozindisha miaka mitano baada ya kuchukua ofisi.

(2) Kwa ajili ya ibara ya (1), kipindi kile Rais wa Taifa anachohudumu kama Rais wa Taifa baada ya uchaguzi wa Rais mpya wa Taifa na kabla ya kuapishwa kwa Rais mpya wa Taifa, sio sehemu ya masharti ya Rais wa Taifa anayeendelela.

(3) Hakuna mtu atakayekuwa Rais wa Taifa kwa zaidi ya vipindi viwili.

(4) Kwa ajili ya ibara (3), Yule ambaye ahudumu kama Rais wa Taifa kwa muda wa miaka miwili unusu mfululuzizo atachukuliwa kuwa amehudumu kwa kipindi kizima.

**Kinga dhidi ya kufunguliwa mashtaka.**

**168**.(1) mashtaka yoyote ya jinai hayatafunguliwa au kuendelezwa katika mahakama yoyote dhidi ya Rais wa Taifa au yeyote ambaye anashikilia ofisi ya Rais wakati wa hatamu yake kuhusiana na chochote alichokifanya au kutokifanya wakati wa kutekeleza mamlaka yake kwenye Katiba hii.

1) Mashtaka ya kesi za madai hayataanzishwa katika mahakama yoyte dhidi ya Rais wa Taifa au yeyote anayetekeleza majukumu ya ofisi hiyo wakati wa hatamu yake kutokana na chochote anachokifanya au kutofanya katika kutekeleza mamlaka yake yaliyo kwenye katiba hii.

2) Pale ambapo maelezo katika sheria yanaweka mipaka ya wakati ambamo mashtaka haya yanaweza kuwasilishwa dhidi ya mtu huyu, kipindi cha wakati ambapo mtu huyu anashikilia au kutekeleza majukumu ya ofisi ya Rais wa Taifa hakitatiliwa maanani katika kuhesabu wakati ambao unaelezewa na sheria hii.

3) Uhuru wa kutoshtakiwa wa Rais wa Taifa ulio katika Kifungu hiki, hautatumika kwa hatia ambazo Rais wa Taifa anaweza kishtakiwa chini ya mkataba wowote ambao Kenya ni mshiriki na ambao unakataza uhuru kama huu.

**Kuondolewa kwa Rais wa Taifa kwa misingi ya kukosa uwezo.**

**169.**(1) Mbunge akiungwa mkono na robo ya idadi ya Wabunge wote anaweza, katika kikao chochcte cha Bunge kutoa hoja ya kuchunguza uwezo wa kiafya ya akili au mwili wa Rais wa Taifa.

(2) Ikikubaliwa na nusu ya idadi ya Wabunge kwa hali ya uwezo wa kiafya ya akili au mwili wa Rais wa Taifa wa kutekeleza majukumu ya ofisi unahitaji kuchunguzwa, Spika wa Bunge katika kipindi cha siku mbili baada ya uamuzi huu atamjulisha Jaji Mkuu kuhusu uamuzi huu.

(3) Jaji Mkuu katika kipindi cha siku saba, baada ya kupokea notisi ya uamuzi huu kutoka kwa Spika ,atateua tume ya watu tano ambao watakuwa-

(a) Watatu watakuwa wataalamu wa matibabu na ambao wameruhusiwa kisheria.

(b) Mmoja atakuwa wakili wa mahakama kuu; na

(c) mmoja atakuwa Yule ambaye ameteuliiwa na Rais wa Taifa.

(4) Iwapo Rais wa Taifa atashindwa kumteu mtu wa tano, mtu huyu atateuliwa na-

(i) mmoja wa familia ya Rais waTaifa; au

(ii) pale ambapo hakuna mmoja wa jamii anataka kuweza kufanya uteuzi huo, ufanywe na mmoja aliye na uhusiano wa karibu wa kindugu na Rais wa Taifa.

(5) Iwapo Jaji Mkuu hatateua tume katika muda wa kipindi kilichobainishwa katika ibara (3) , Spika wa Bunge atateua tume hii katika muda wa siku saba.

(6) Tume itachunguza suala hili na kuripoti-

(i) kwa Jaji Mkuu katika muda wa siku kumi na nne baada ya kuteuliwa kwa tume hii na Spika wa Bunge.

(7) Spika wa Bunge ataiwasilisha ripoti ya tume Bungeni katika muda wa siku saba baada ya kuipokea.

(8) Pale ambapo Bunge litaamua kwamba suala la uwezo wa kiakili na kimwili wa Rais wa Taifa wa kutekeleza majukumu ya ofisi lichunguzwe, Rais wa Taifa hadi mtu mwingine achukue ofisi ya Rais waTaifa au tume iliyoteuliwa chini ya ibara (3) au tano iripoti kwamba Rais wa Taifa hawezi kutekeleza majukumu yake ya kiofisi, lolote litalotangulia, ataendelea kutekeleza majukumu ya kiofisi.

(9) Ripoti ya tume itakuwa ya mwisho na hautakuwa na rufani na ikiwa tume itaripoti kwamba Rais wa Taifa anawea kutekeleza majukumu yake yake ya ofisi, spika wa atatangaza katika Bunge.

(10)Iwapo tume itatangaza kuwa Rais wa Taifa hawezi kutekeleleza majukumu ya ofisi, Bunge, iwapo litaungwa mkono kwa kura zaidi ya nusu ya Wabunge wote, litaidhinisha uamuzi wa tume na baada ya kuidhinisha Rais wa Taifa ataacha kuwa Rais.

**Kumwondoa Rais wa Taifa kupitia kwa kura ya kutokuwa na imani**

**170.** (1) Mbunge, iwapo ataungwa mkono na thuluthi moja ya Wabunge wote, anaweza, katika kikao chochote cha Bunge, kupendekeza mswada wa kura ya kutokuwa na imani na Rais wa Taifa-

(a) kwa misingi ya ukiukaji mkubwa wa vipengele vya sheria katika katiba na sheria.

(b) kwa kuwa kuna sababu kubwa za kuamini kwamba Rais wa Taifa amefanya hatia iliyo chini ya sheria za kitaifa au kimataifa;au

(c) utovu mkubwa wa nidhamu.

(2) Iwapo theluthi mbili ya Wabunge wote wataidhinisha mswada ulio chini ya ibara (1), spika wa Seneti kwa muda wa siku saba ataitisha mkutano wa Seneti kusikiza mashtaka haya dhidi ya Rais waTaifa.

(3) Baada ya kusikiza mashtaka chini ya ibara (2), Seneti, kwa uamuzi,

litatetea kamati maalum litakalohusisha watu kumi na mmoja kati yao kulichunguza suala hili.
(4) Tume hii maalum itachunguza suala hilo kwa muda wa siku kumi na kuripoti kwa Seneti ikiwa imepata tuhuma halisi dhidi ya Rais wa Taifa zinzoweza kuthibitishwa.
(5) Rais wa Taifa ana haki ya kwenda au kuwakilishwa mbele ya tume hii maalum wakati wa uchunguzi wao.
(6) Iwapo kamati maalum itaripoti kuwa yale yaliyomo katika tuhuma dhidi ya Rais wa Taifa hayajathibitishwa hakuna mashtaka zaidi yatayochukuliwa chini ya Kifungu hiki kutokana na tuhuma hizi.
(7) Iwapo kamati maalum itaripoti kwamba yaliyomo kwenye tuhuma yoyote dhidi ya Rais wa Taifa yamethibitihshwa, Seneti, baada ya kumpa Rais wa Taifa nafasi ya kusikilizwa, itapigia kura mashtaka ya kutokuwa na imani, na Rais wa Taifa ataacha kuwa Rais iwapo theluthi mbili ya Wabunge watapiga kura kuunga mkono mashtaka ya kutokuwa na imani.

**Nafasi katika ofisi ya Rais wa Taifa**

**171.** (1) Ofisi ya Rais wa Taifa itakuwa wazi iwapo mwenya ofisi hiyo-
(a) anaaga dunia;
(b) Anaacha kazi kwa kumwandikia barua S pikawa Bunge; au
(c) Anaondolewa kwa ofisi kulingana na Katiba hii
(2) Pale ambapo ofisi ya Rais wa Taifa, Naibu Rais wa Taifa atachukua ofisa kama Rais wa Taifa-
(a) Pale ambapo nafasi katika ofisi ya Rais wa Taifa imetokea ikiwa kumesalia miaka miwili na nusu kabla ya tarehe ya uchaguzi ujao wa Urais kulingana na Kifungu 162, Naibu Rais wa Kitaifa atachukua uongozi kama Raia wa Taifa kwa wakati unaosalia wa kipindi cha Rais waTaifa.
(b) Pale ambapo nafasi itatokea kukiwa kumesalia zaidi ya miaka miwili na nusu kabla ya tareha ya uchaguzi ujao kulingana Kifungu 162, uchaguzi mpya wa fisi ya Rais wa Taifa utafanyika siku sitini baada ofisi ya Rais wa Taifa kuwa wazi.
(3) Pale ambapo nafasi katika ofisi ya Rais wa Taifa napia katika ofisi ya Naibu Rais wa Taifa itatokea au pale ambapo Naibu Rais waTaifa hawezi kushikilia, Spika wa bunge atashikilia kama Rais wa Taifa, na iwapo kwa sababu yoyote Spika wa Bunge hataweza kushikilia,spika wa seneti atashikilia kama Rais wa Taifa.
(4) Pale ambapo nafasi itatokea kwa hali zinazokusudiwa na ibara (3), uchaguzi Rais wa Taifa utafanyika siku sitini baada ya Spika wa Bunge kuchukua ofisi ya Rais wa Taifa.
(5) Mtu yule ambaye anachukua hatamu za uongozi wa Rais wa Taifa chini ya kifungu hiki, isipokuwa aondolewe kutoka kwa mamlaka na Katiba hii, ataendelea na wadhifa huo mpaka uchaguzi mpya ufanyike na Rais wa Taifa aliyechaguliwa upya kuchukua uongozi.

**Mamlaka ya huruma wa Rais**

**172.** (1) kutakuwa na mamlaka ya msamaha ambao utatekelezwa kwa ombi la Rais wa Taifa kwa mtu yeyeyote kulingana na ushuru wa Kamati ya Ushauri inayorejelewa katika kifungu (2).
(2) Kutakakuapo na Kamati ya Ushauri kuhusu mamalaka ya msama wa Rais, itawahusisha-
(a) Mkuu wa Sheria;
(b) Waziri anaye husika na huduma za urekebishaji; na
(c) Angalau watu wengine watano,na wasiwe watu walio kwenye utumishi wa umma au afisi za serikali,na kama inavyoidhinishwa na sheria za Bunge.
(3) (a) Sheria ya Bunge itatoa muda wa kushika cheo kwa wanakamati wa Kamati ya Ushauri;
b) Taratibu za Kamati ya Ushauri
(c) Kigezo ambacho kitatumiwa na Kamati ya Ushauri katika kueleza ushauri wake.
(4) Kwa kutekeleza mamlaka aliyopewa katika ibara (1), Rais wa Taifa anaweza-
(a) Kumsamehe mtu ambaye amepatikana na hatia, ama huru au kwa masharti;
(b) Kuhairisha ama, kwa muda fulani mahususi au kwa muda usiojulikana, utekelezaji wa adhabu.
(c) Kubadili adhabu ndogo kwa adhabu inayostihili.
(d) Kusamehe semu ya adhabu au adhabu yote.
(5) Kamati ya ushauri itatilia maanani maoni ya wathiriwa wa hatia kutokana nayo, ambapo watapendekeza ya kutekelezwa kwa mamlaka ya msamaha na Rais wa Taifa.

**Ofisi ya Naibu Rais wa Taifa**

**173.** (1) Kutakuwa na Naibu Rais wa Taifa wa Jamhuri.
(2) Kila mgombeaji uchaguzi wa Urais atateua mtu ambaye amehitimu kwa uchaguzi Rais wa Taifa kama mgombeaji wa uchaguziwa Naibu Rais wa Taifa.
(3) tume huru ya uchaguzi na na Mipaka ya maeneo Bunge haitafanya uchaguzi wa kando wa Naibu Rais wa Taifa lakini itatangaza yula ambaye ameteuliwa na aliyechaguliwa Rais wa Taifa kuwa ndiye amechaguliwa kuwa Naibu Rais wa Taifa.
(4) Kuapishwa kwa Naibu Rais wa Taifa kutafanyika mbele ya Hakimu Mkuu au iwapo Hakimu Mkuu hayupo, mbele ya Nibu wa Hakumu Mkuu N wananchi.
(5) Naibu Rais wa Taifa mteule Atachukua mamlaka kwa kula na kutia saini-
a) Kiapo cha uaminifu; na
b) Kiapo cha kutekeleza majukumu ya ofisi kama ilivyoidhinishwa katika Mpangilio wa Tatu.
(6) Mashart ya Ofisi ya Naibi Rais wa Taifa yatanza kutumuka kutoka siku ile Rais wa Taifa atachukua mamlaka na kukoma-
a) Wakati Rais Mpya wa Taifa aliyechaguliwa atachukua mamlaka;
b) Wakati Naibu Rais wa Taifa atachukua mamlaka ya Rais;
c) Aikijuzulu , kuaga dunia au kuachizwa kazi.
(7) Naibu Rais wa Taifa ananweza, kwa wakati wowote, kujiuzulu kwa kumwandikiia notisi Rais wa Taifa na kujiuzulu huku kutaanza kutekelezwa saa na tarehe iliobaishwa katika notisi hiyo, iwapo tare haijabainishwa, adhuhuri ya siku ya kupokelewa kwa notisi hiyo.
(8) Naibu Naibu Rais wa taifa hahudumu kwa zaidi ya vipindi viwili.
(9) Kwa kusudi la ibara (8), mtu Yule ambaye ameendelea kuhudumu kama Naibu Rais waTaifa angalau kwa muda wa miaka miwili na nusu ya kipindi cha Rais wa Taifa, itachukuliwa kuwa ametumikia kipindi kizima.

**Nafasi katika ofisi ya Naibu Rais wa Taifa**

**174.** (1) Iwapo kuna nafasi katika ofisi ya Naibu Rais Wa Taifa, Rais wa Taifa, kwa muda wa siku kumi na nne za ofisi hii kuwa wazi, atamteua mtu ambaye ataidhinishwa na Bunge kujaza nafasi hii.
(2) Bunge litapiga kura ya uamuzi wa uteuzi ndani ya muda siku sitini.

**Majukumu ya Naibu Rais wa Taifa**

**175** (1) Naibu Rais wa Taifa atakuwa Msaidizi Mkuu wa Rais wa Taifa na atamwakilisha Rais katika kutekeleza majukumu ya Kitaifa ya Rais.
(2) Naibu Rais wa Taifa atatekeleza majukumu yaliyotolewa na Katiba au majukumu yoyote ya Rais wa Taifa atakayopewa na Rais.
(3) Wakati Rais hatakuwa na uwezo kwa muda mfupi au hayumo Nchini, Naibu Rais wa Taifa takuwa kaimu Rais wa Tafa.
(4) Naibu Rais wa Taifa hatashikilia ofisi nyingine ya Umma au Sarikali.

**Kifo kabla ya kuchukua mamlaka**

**176.** (1) Iwapo mtu ambaye ametangazwa kuwa Rais mteule wa Taifa anaaga dunia kabla ya kuchukua mamlaka Yule abbaya ameshatangazwa kuwa Naibu Rais wa Taifa atakuwa kaimu Rais na Uchaguzi wa Rais wa Taifa kufanyika chini ya muda wa siku sititini baada ya kifo cha Rais mteule wa Taifa.
(2) Iwapo mtu ambaye ametangazwa kuwa Naibu Rais mteule wa Taifa taaga dunia kabla ya kuchukua mamlaka, ofisi ya Naibu Rais wa Taifa itatangazwa kuwa wazi baada ya Rais mteule kuchukua mamlaka.
(3) Iwapo Rais mteule wa Taifa pamoja na naibu Rais wa taifa wanaaga dunia kabla ya kuchukua maliaka, Spika wa Bunge atakuwa kaimu Rais wa Taifa na uchaguzi mpya kufanyika chini ya siku sitini baada ya kifo cha pili.

**Kuondolewa kwa naibi Rais wa taifa**

**177.**(1) Naibu Rais wa Taifa anaweza kuondolewa mamlakani-
(a) kwa misingi ya kutokuwa na uwezo wa kiakili na kimwili wa kutekeleza majukumu ya kiofisi;
(b) kwa kura ya kutokuwa na imani-
(i) kwa misingi ya ukiukaji mkubwa wa katiba hii au sheria;
(ii) kwa sababu kuna sababu kubwa kuamini kuwa Naibu Rais wa Taifa amefanya uhalifu wa jinai chini ya sheria za taifa na kimataifa
(iii) utovu mkubwa wa nidhamu
(2) Vipengele vya katiba katika Vifingu vya 169 na 170 vinavyohusiana na kutolewa kwa Rais wa Taifa, na kwa marekibisho yanayotakikana, vitatumika katika kumwondoa Naibu Rais wa Taifa.

**Mshahara na marupurupu ya Rais wa Taifa na Naibu Rais wa Taifa**

**178.** (1) mshahara na marupurupu yatakayolipwa Rais wa Taifa na Naibu Rais wa Taifa yatatoka kwa Hazina yapamoja ya Fedha.
(2) malipo na marupurupu na faida za Rais waTaifa na Naibu Rais wa Taifa hayatashushwa wakiwa ofisini na wakiwa wamestaafu.
(3) Malipoya uzeeni yanayopaswa kulipwa Rais mstaafu wa Taifa na Naibu Rais mstaafu wa Taifa pamoja na marupurupu menginine wanayostahili hayatabadilishwa kwenda chini au kuondolewa katika uhai wao.

**SEHEMU-3 WAZIRI MKUUNA NA BARAZA LA MAWAZIRI**

**Waziri Mkuu**

**179.** (1) kutakuwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri, ambaye ndiye atakuwa Kiongozi wa Serikali.

(2) Waziri Mkuu ataelekeza na kuratibu Mawizara na utungaji wa sheria, na anawajibikia Bunge.

(3) Waziziri Mkuu ataongoza mikutano Baraza la Mawaziri.

(4) Iwapo Warizi Mkuu hatakukuwepo, Naibi Waziriri Mkuu atatekeleza majukumu ya Waziri Mkuu.

(5) Naibu Waziri Mkuu, wakati wa kutekeleza majukumu ya Waziri Mkuu chini ya ibara (5), hatatekeleza mamlaka ya yaWaziri Mkuu yanayohusiana na-

(a) Kuteua au kupendekeza kuteuliwa kwa ofisa wa umma; au

(b) Kugawa majukumu au kuhamisha majukumu kutoka kwa Naibu wa Waziri Mkuu, Waziri au Naibu wa Waziri.

**Uteuzi wa Waziri Mkuu**

**180.** 1) Katika siku saba baada ya kuitwa kwa Bunge kuitwa baada ya uchaguzi mkuu,au inapohitajika ili kijaza nafasi katika ofisi ya Waziri Mkuu, isipokuwa tu wakati wa kura ya kutokuwa na imani,Rais atamteua Waziri Mkuu-

(a) Mbunge ambaye ni kiongozi wa chama cha kisisa au muungano wa vyama vya kisia ulio na idadi kubwa zaidi ya Wabunge katika Bunge; au

(b) Iwapo kiongozi wa chama kikubwa cha kisiasa au wa muungano wa vyama vya kisisa ameshindwa kupata imani ya Wabunge, Mbunge ambaye kiogozi wa chama cha kisiasa a muungano wa vyama vya kisiasa ulio na wa pili katika idadi ya Wabunge katika Bunge.

(2) Kila chama cha kisisasa kilichoshiriki katika uchaguzi mkuuwa wa Wabunge kitamteua mtu mmoja kuwa kiongozi wa chama hicho kulingana na Ibara (1).

(3) Pale ambapo hakuna yeyote kwa kuzingatia ibara (1)(a) au (b) ameweza kupata au kudumisha imani ya Bunge Rais wa a Taifa tapendekeza kwa Bunge jina Mbunge ambaye, kwa maoni ya Rais waTaifa, anaweza kupata imani ya Bunge.

(4) Akishapokea pedekezo kutoka kwa Rais wa Taifa, kulingana na ibara (3), Spika wa Bunge atatisha kikao cha Bunge na kuwasilisha pendekezo la Rais.

(5) Katika kipindi cha siku saba baada ya kupokea pendekezo la Rais wa Taifa, ataitisha kupigwa kura katika Bunge ya kuthibitisha uteuzi wa mtu aliyependekezwa na Rais wa Taifa.

(6) Kura kulingana na Ibara (5), itapita tu ikiwa itaungwa mkono na Wabunge zaidi ya ya nusu ya Wabunge wote.

(7) Iwapo Bunge litashinwa kuthibitisha uteuzi wa mtu Yule ambaye amependekezwa na Rais wa Taifa, Bunge kwa kura iliyoungwa mkono na Wabunge wengi waliomo na kumpigia kura Mbunge ili kuteuliwa kama Waziri Mkuu.

(8) Iwapo, katika kipindi cha siku sitini cha Rais wa Taifa kwanza kumteua atakayekuwa Waziri Mkuu, kuwe hakuna yule ambaye amethibitishwa au kuchaguliwa kwa uteuzi, Bunge litavujwa na Tume Huru ya Uchguzi na na Mipaka ya Maeneo Bunge itaitisha uchaguzi mkuu wa wabunge

**Masharti ya ofisi**

**181.** (1) Mtu yule ambaye uteuzi wake kama Waziri Mkuu umathibitishwa,au aliyechguliwa kwa uteiuzi na Bunge,atachukukua mamamlaka kwa kula kiapo cha kutekeleza majukumu ya ya ofisi kama ilivyo katika Mpangilio wa Tatu, mbele ya Spika na Wabunge -

(2) Kipindi mamlaka ya Waziri Mkuu kinaendelea hadi-

(a) Waziri Mkuu aage dunia ajiuzulu,au kuachishwa kazi; au

(b) Mtu mwingine ambaye ameteuliwa kuwa Waziri Mkuu kuchukua mamlaka baada ya uchaguzi.

(3) Hakuna mtu atakayekuwa Waziri Mkuu zaidi ya vipindi Viwili.

(4) Kulingana na ibara (3), mtu Yule ambaye amehudumu mfululizo kwa kwa miaka miwili na nusu itachkuliwa amehudumu kwa kindi kizima.

**Kujiuzulu kwa Waziri Mkuu**

**182.** (1) Waziri Mkuu anaweza kujiuzulu kwa kuandika notisi ya kujiuzulu kwa Rais wa Taifa.

(2) Kujiuzulu kwa Waziri Mkuu kutaanza kutekelezwa-

(a) Siku na wakati uliobainishwa katika notisi; kama upo; au

(b) Adhuhuri ya siku ya kuwasilishwa kwa kwake kwa njia yoyote.

**Mshahara na marupurupu ya Waziri Mkuu**

**183** (1) Mshara na marupupurupu yatakayolipwa Waziri Mkuu yatoka kwa hazina ya pamoja ya fedha.

(2) Mshara mapato na marupurupu ya Waziri Mkuu hayatabadilishwa kumwumiza akiwa ofisini au baada ya kustafu.

(3) Malipo yauzeni yanayopaswa kulipwa, na marupurupu, mapato na faida nyingine anazostahili Waziri Mkuu mstaafu hazitabadilishwa kumwumiza Waziri Mkuu aliyestaafu wakati wa uhai wake

**Baraza la Mawaziri na Manaibu**

**184.** (1) Baraza la Mawaziri litakuwa na-

a) Waziri Mkuu;

b) Naibu wa Waziri Mkuu;

c) Mawaziri wasiopungua kumi na na tano au kuzindisha ishirini;

(2) Waziri Mkuu atawasilisha kwa Rais wa Taifa ili kuteuliwa-

(a) Naibu wa Waziri Mkuu kutoka kwa miongoni mwa Wabunge waliochaguliwa.

(b) Kulingana na ibara (3), mawaziri wasiopungua kumi na watno au kuwa zaidi ya ishirini; na

(c) Manaibu wa Mawaziri wasiopungua kumi na watano na wasiozidi ishirini kutoka kwa miongoni mwa wabunge waliochaguliwa.

(3) Waziri Mkuu anaweza, katika kuwasilisha kwa mawaziri ili wateuliwe kulingana na ibara(2)(b), kuongeza majina ya watu wasiozidi kumi kuto kwa kwa Wabunge waliochaguliwa.

(4) Watu watakaowasilishwa chini ya kifungu (3) watakuwa-

a) Wale ambao wana ujuzi na uwezo uliona uhusiano na wa wizara ambazo wapendekezwa kuteuliwa; na

b) Wale ambao hawakugombea uchaguzi wa Bunge au Seneti katika uchaguzi unaotangulia kuwakilishwa huku.

(5) Katika kuwasilisha watu hawa kwa uteuzi chini ya Kifungu hiki Waziri Mkuu atahahakisha Baraza la Mawaziri linatilia maanani tofauti za watu wa Kenya.

(6) Mtu aliyeteuliwa chni ya kifungu (2) anaweza kuhudhuria na kuzungumza katika Bunge lakini hawezi kupiga kura au kuruhusiwa malipo yoyote au faida yoyote ile kwa sababu ya kuhudhuria.

(7) Mtu atakayechaguliwa kuwa Naibu wa Wziri Mkuu, Waziri au Naibu Waziri-

(a) Atachukua mamlaka kwa kula na kutia saini kiapo kuthibitisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi kama inavyoidhinishwa na Mpangilio wa Tatu, mbele ya Maspika na Wabunge.

(b) Anawea kujiuzulu kwa kumwandikia Rais wa Taifa notisi ya kujiuzulu kupitia kwa Waziri Mkuu;na

(c) Kuendelea kushikilia mamlaka hadi-

i. Mtu huyo aage dunia, ajiuzulu,au aachizwe kazi;

ii. Anayefuta kuteuliwa kuchukua ofisi hiyo, baada ya uchaguzi mkuu wa Bunge kuchukua mamlaka.

(8) Kujiuzulu kunakorejelew katika Ibara ya (7) unaanza kutekelezwa –

(a) Tarehe na wakati uliobainishwa katika notisi; kama upo; na

(b) Adhuhuri katika siku baada ya kuwasilishwa kwa Rais wa, kwa hali nyingine.

(9) Wakati wowote Waziri Mkuu,Naibu wa Waziri Mkuu au waziri mwingine yeyote yule anapokabidhiwa wajibu wa uwaziri, watatoa mwelekeo wwa jumla na uthibiti juu ya wizara hiyo.

**Kuachishwa kazi kwa Mawaziri na Manaibu wa Mawaziri.**

**185.** (1) Rais wa Taifa atamwachisha kazi N aibu Waziri Mkuu Waziri, Naibu Waziri kwa ushauri wa Waziri Mkuu.

(2) Ikiwa Bunge, kwa kuungwa mkono na zaidi ya nusu ya Wabunge wote, kupitisha mwsada wa kutokuwa na imani na waziri, isipokuwa Waziri Mkuu, au Nainu waziri, na waziri huyo akose kujiuzulu kwa muda wa siku tatu baada ya kupitishwa kwa mswada huo,Rais wa Taifa atamwachisha kazi Waziri huyo au Naibu Waziri.

**Kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu**

**186** (1) Mbunge mmoja akiungwa mkonno na thaluthi moja ya wabunge, kwa wakati wowote katika kikao cha Bunge, anaweza kupendekeza mwsada wa kutokuwa na imani na Waziri Mkuu -

(2) Iwapo Bunge, kwa uamuzi ulioungwa mkono kwa kura zaidi ya nusu ya Wabunge wote, watapitisha mswada wa kutokuwa na imani na Waziri Mkuu, Waziri Mkuu atawasilisha kwa Spika wa Bunge notisi ya kujiuzulu kwa Waziri Mkuu na wa Naibu Waziri Mkuu, Braza la Mawaziri na Manaibu wa Mawaziri.

(3) iwapo Waziri Mkuu hatawasilisha notisi kama inavyotakikana katika Ibara (2), kwa muda wa siku saba baada ya kupitishwa kwa mswada huu wa uamuzi, Rais wa Taifa atawaachisha kazi Waziri Mkuu, Baraza la Mawaziri, na Naibu Waziri Mkuu, na vipengele vinavyofaa vya kifungu 180 vitatumika kuhusu uteuzi wa Waziri Mkuu mpya.

(4) Rais wa Taifa hatamwachisha kazi Waziri Mkuu, naibu Waziri Mkuu,Baraza la MawaziriNA Manaibu wa Mawaziri kwa hali zozote isipokuwa zile zinazingatiwa katika Kipengele hiki na Kpengele cha 185.

(5) Licha ya notisi ya kujiuzulu chini ya Ibara (2), au kuachishwa kazi kwa Waziri Mkuu Naibu Waziri Mkuu Mawaziri, na Manaibu wa Mawaziri wchini ya Ibara (3), Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu, Mawaziri, na Manaibu wa Mawaziri wataendelea kuundumu hadi Waziziri Mkuu mpya achukue mamamlaka.

**Maamuzi, majukumu na kuwajibika kwa Baraza la Mawaziri**

**187.** (1) Barasa la Mwaziri litakutana agalau mara moja kwa mwezi.
(2) Idadi inayotakikana kwa Baraza la mawaziri itakuwa nusu ya Baraza lote la Mawaziri.
(3) Uamuzi wa Barasa la Mawaziri utakuwa katika maandishi na utawasilishwa haraka kwa Rais wa Taifa.
(4) Uamuzi wa Baraza la Mawaziri hautakuwa halali na hautatekelezwa isipokuwa uwe umetiwa saini na Waziri Mkuu.
(5) Baraza la Mawaziri linawajibika kwa pamoja na Mawaziri kuwajibikia Bunge kibinafsi-
(a) Kutumia mamlaka yao na utendaji wa majukumu yao; na
(b) Utekelezaji na usimamizi wa sheria zinazowahusu.
(6) Waziri atahudhuria Bunge, kamati za Bunge, anaapohitajika kufanya hivyo,na atajibu maswali yote kuhusu suala lililogawiwa Waziri.
(7) Waziriwa katika Baraza la Mawaziri atato kwa Bunge ripoti kamili na za mara kwa mara kuhusu maswala yaliyo chini ya uthibiti wao.

**Raisi wa Taifa kufahamishwa kwa ukamilifu kuhusu mienendo ya Serikali**

**188.** Waziri Mkuu atakuwa akimfahamisha mara kwa mara na kwa ukamilifu Rais wa Taifa kuhusu jumla ya mienendo ya Serikali na atampasha Rais waTaifa habari zozote ambazo Rais wa Taifa ataomba kutokana na masuala yanayohusu serikali.

**Kugawa majukumu**

**189.** (1) Kwa kiasi cha kutoambatana na Sheria za Bunge , Waziri Mkuu atagawa majukumu ya kutekeleza na kusimsamia Sheria yoyote ya Bunge kwa-
a) Naibu Waziri Mkuu;au
b) Waziri katika Baraza la Mwaziri;
c) Naibu wa Waziri.
(2) kwa kiasi ambacho si cha kutoambatana na Shera za Bunge,Waziri Mkuu anaweza kuhamisha jukumu la kutekeleza na kusimamia Sheria yoyote ya Bunge kutoka kwa mmoja wa Mawaziri katika Baraza la Mawaziri hadi kwa mwingine.
(3) Waziri Mkuu anaweza kugawia Naibu wa Waziri Mkuu, Waziri au Naibu Waziri mamlaka au jukumu la Waziri mwingine katika Baraza la Mawaziri, au Naibu mwingine wa Waziri ambaye hana wajibu au hawezi kutumia kwa muda mfupi mamlaka hayo kutenda jukumu hilo, lakini Waziri Mkuu hatatawagawia Rais na Naibu Rais wa Taifa mamlaka na majukumu.
(4) Uamuzi wa Waziri Mkuu chini ya Ibara(2) na (3) utachapishwa kwenye Gazeti rasmi la serikali.
(5) Waziri Mkuu anaweza kumwalika mti yeyote kwa mkutanao wa Baraza la Mawaziri iwapo kwa maoni yake suala fulani limetokea au lina uwezekano wa kutokea katika mkutanao huo ambalo linahitaji kuhudhuria au kushiriki kwa mtu huyo.
(6) Mtu yeyote ambaye amealikwa katika ibara (5) atafungwa na taratibu na sheria za Baraza la mawaziri lakini hawaruhusuwi kupiga kura kwa suala lolote katika katika mkutano huo.

**Katibu wa Baraza la Mawaziri**

**190** (1). Kuna ofisi teule ya Katibu wa Baraza la Mawaziri
(2) Ofisi ya Katibu wa Baraza la Mawaziri itakuwa ofisi katika utumishi wa umma.
(3) katibu wa Baraza la Mawaziri-
(a) atateuliwa na Rais wa Taifa kwa ushauri wa Waziri Mkuu; na
(b) ataachizwa kazi na Rais wa Taifa kwa ushauri wa Waziri Mkuu.
(4) Katibu katika Baraza la Mawaziri-
(a) Kiongozi wa ofisi ya Baraza la Mwaziri;
(b) Kuwajibika kulingana na maelekezo ya Baraza la Mawaziri, kwa kupanga shughuli za Baraza la Mawaziri na kuweka kumbukumbu ya mikutano ya Baraza la Mawaziri;
(c) Kupeleka uamuzi wa Baraza la Mawaziri kwa watu au mamlaka yanayofaa; na
(d) Awe na majukumu kama ikavyoagizwa na Baraza la Mwaziri.

(5) Katibu wa Baraza la Mawaziri anaweza kujiuzulu kwa kutoa notisi kwa maandishi kwa Rais wa Taifa kupitia kwa Waziri Mkuu, na notisi itaanza kutekelezwa ikipokelewa na Rais wa Taifa.
(6) serikali mpya ikishika mamlaka, yule aliye mamlakani kama Katibu wa Baraza la Mawaziri hatakuwa na mamlaka tena lakini anaweza kuteuliwa kwa mra nyingine.

**Uteuzi na kuachizwa kazi kwa Makatibu Vinara**

**191.** (1) Kuna ofisi ya buniwa ya Katibu Kinara ambayo ni ofisi katika utumishi wa umma.
(2) Kila Wizara itakuwa chini ya usimamizi wa Katibu Kinara.

**Uteuzi na kuachishwa kazi kwa Makatibu Vinara**

**192.** Katibu Kinara-
(a) atapendekezwa na tume ya Utumishi kwa umma na kuteuliwa na Rais waTaifa;
(b) ataachishwa kazi na Rais waTaifa kwa ushauri wa Waziri Mkuu;
(c) Anaweza kustaafu kwa kutoa notisi kwa Rais wa Taifa kupitia kwa Waziri Mkuu.

**SEHEMU YA 4- OFISI NYINGINE**

**Mwanasheria Mkuu**

**193.** (1) Kuna ufisi buniwa ya Mwanasheria Mkuu
(2) Mwanasheria Mkuu atateuliwa na Rais wa Taifa na kuidhinishwa na Bunge.
(3) Sifa za kuteuliwa kama kama Mwanasheria Mkuu ni sawa na za uteuzi kwa ofisi ya Jaji Mkuu.
(4) Mwanasheria Mkuu atakuwa mshauri mkuu wa kisheria kwa Serikali ya taifa na atawajibika kwa –
(a) kuandika, kupitia na kuidhinisha pendekezo (vinginevyo) la kama makubaliano, mikataba na maazimio na hati kwa jina lolote, ambayo serikali ni mshiriki au pale serikali inapendelea kama inavyoelezewa katika Sheria.
(b) kuwakilisha serikali ya taifa mahakamani au au kasi nyingine za kisheria zile ambazo serikali inahusika, isipokuwa kesi za uhalifu; na
(c) kuandika sheria ,ikihusisha, sheri ndogo za serikali ya kitaifa.
(5) Mwanasheria Mkuu atakuwa na mamlaka, kwa ruhusa ya mahakama , kuwa kama rafiki wa mahakama katika kesi za umma zile ambazo serikali si mhusika.
(6) Mwanasheria Mkuu atakuza, kuhifadhi na kufuata sheria, na kulinda maslahi ya Jamhuri.
(7) Mamlaka ya Mwanasheria Mkuu yanaweza kutekelezwa na yeye mwenyewe au na wasaidizi katika ofisi yake akitekeleza kulingana na maagizo maalum ya jumla.
(8) Mwanashera Mkuu hatakuwa chini ya maelekezo au uthibiti wa wa mtu yeyote au mamlaka yoyote katika kutekeleza majukumu ya ofisi ya Mwanasheria Mkuu.
(9) Mwanasheria Mkuu atahudumu kwa kipindi cha miaka sita na hatoweza kuteuliwa tena.

**Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma**

**194.** (1) Kuna ofisi buniwa ya Mkurugenzi wa mashtaka ya umma
(2) Mkurugenzi wa mashtaka ya umma atateuliwa na Rais wa Taifa na kuidhinishwa na Bunge.
(3) Sifa za uteuzi wa Mkurugenzi wa Mashtaka ya umma zitakuwa sawa zile za uteuzi wa Jaji wa Mahakama Kuu.
(4) Mkurugenzi wa mashtaka ya umma atakuwa na mamlaka ya kumwagiza Mkaguzi Mkuu wa Huduma ya Polisi ya Kenya kuchunguza habari yoyote au madai ya vitendo vya uhalifu.
(5) Mkurugenzi wa mashtaka ya umma atatekeleza mamlaka ya Taifa ya kuongoza mashtaka na anaweza-
(a) Kuanzisha na kuendeleza mashtaka ya kesi za uhalifu dhidi ya mtu yeyote katika mahakama yoyote (isipokuwa mahakama za jeshi) kutokana na kosa linalotuhumiwa kuwa limefanywa;
(b) Kuchukua na kuendeleza kesi zozote ya uhalifu zilizoanzishwa katika mahakama yoyote ( isipokuwa katika mahakama za jeshi) zilizoanzishwa na kuendelezwa na mtu mwingine au mamlaka; na
(c) Kwa kutegemea Ibara (8), kukomesha katika hatua yoyote, kabla ya hukumu kutolewa, kesi yoyote ya uhalifu iliyoanzishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka ya umma au kuchukuliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka ya umma kulingana na aya (b)
(6) Pale ambapo kukokomeshwa kwa kesi kunakorejelewa katika ibara (5)(c) kunapotekelezwa baada ya mshitakiwa kukamilisha kutoa utetezi wake , mshitakiwa ataaachiliwa huru.
(7) Bunge linaweza kwa sheria za Bunge kumkabidhi uwezo wa kushitaki mamlaka nyingine isipokuwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya umma.
(8) Mkurugenzi wa mashtaka ya umma hawezi kukomesha kesi bila idhini ya Mahakama.
(9) Mamalaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka yanaweza kutekelezwa na Mkurugenzi bmwenyewe au maofisa wasaidizi wakitekeleza kulingana maagizo maalum au ya jumla.
(10) Mkurugenzi wa Mashtaka ya umma hatahitaji adhini ya mtu au mamalaka yoyote kuanzisha kesi za uhalifu, na kutekeleza mamalaka au majukumu yake

hakutaelekezwa au kudhitiwa na mtu au mamalaka yoyote.
(11) Kwa kutekeleza mamlaka yanayotokana na Kifungu hiki, Mkurugenzi wa mashtaka ya umma atatilia maanani maslahi ya taifa, maslahi ya utendaji haki na haja ya kuzuia na kuepuka matumizi mabaya ya utaratibu wa sheria.
(12) Mkurugenzi wa Mashtaka ya umma atashikilia mamlaka kwa kwa muda wa miaka sita na hatoweza teuliwa upya .

**Mchunguzi Maalum wa Malalamiko ya Umma**

**195.** (1) kuna ofisi buniwa ya ofisa maalum wa kuchunguza malalamiko ya umma
(2) Mchunguzi maalum wa malalamiko ya umma atateuliwa na Rais wa Taifa kwa idhinisho la Benge
(3) Sifa za uteuzi wa mchunguzi wa mashtaka ya umma yatakuwa kama yale ya Jaji wa Mahakama Kuu.
(4) kulingana na ibara (5), Mkurugenzi wa Mashtaka ya umma atatoa ushauri wa kisheria na kutetewa kwa wale ambao hawawezi kugharamia huduma za kisheria.
(5) Bunge kwa sSheria ya Bunge itatoa-
(a) uongozi na usimamamizi wenye ufanisi, wa kufaa na ulio wazi wa ofisi ya mchunguzi maalum wa mashtaka ya umma;
(b) vigezo vya kutoa msaada wa kisheria; na
(c) kuchapishwa habari kuhusu kupatikana kwa msaada wa kisheria.
(6) Mamlaka ya mchunguzi maalum wa mashtaka ya umma yanaweza kutekelezwa na yeye mwenyewe au maofisa wasaidizi wakitekeleza kulingana na maagizo maalum au ya jumla.
(7) Mchunguzi Maalum wa Mashtaka ya umma atakuwa mamlakani kwa kipindi cha miaka sita na hataweza kuteuliwa tena.

**Kuondolewa kwa Mchunguzi Maalum wa Mashtaka ya Umma**

**196.** (1) Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka na mchunguzi maalum wa mashtaka ya umma, wanaweza kuachishwa tu kazi kwa misingi ya-
(a) kutoweza kutekeleza majukumu ya ofisi kukitokana na kukosa uwezo wa kiakili au wa kimwili;
(b) kutozingatia Sura ya Tisa.
(c) kufilisika
(d) mienendo na tabia mbaya katika kutekeleza wajibu wa ofisi au vinginevyo.
(2) Mtu anayetaka Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi wa mashtaka, na Mchunguzi Maalum wa mashtaka ya umma anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa Tume ya Utumishi wa Umma ambayo, licha ya Kifungu 299(2) (b) itakuwa katika maandishi yanayodhihirisha uhakika wa madai yanayounda msingi wa kuondolewa kwa ofisa mhusika.
(3) Tume Ya Utumishi wa Umma itaitaangalia malalamiko haya na, ikiridhika kwamba yanafichua kuwepo kwa msingi chini ya ibara (1), itapeleka malalamiko haya kwa Rais wa Taifa.
(4) Baada ya kuipokea na kuyachunguza malalamiko haya, Rais wa Taifa muda wa siku kumi na nne atamsimamisha kazi ofisa mhusika ikisubiriwa uamuzi wa Rais waTaifa kulingana na (5) na, akitekeleza kulingana na ushauri wa Tume ya Utumishi wa Umma-
(a) kumhusuMwanasheria Mkuu, atateua kamati maalum ikiwa na –
(i) Spika wa Seneti akiwa mwenyekiti;
ii) majaji watatu kutoka kwa mataifa yaliyo na sheria na mamlaka ya sheria inayofanana; na
(iii) watu watatu walio na uzoefu katika masuala ya umma; na
(b)Kumhusu mkurugenzi wa Mashtaka ya umma au Mchunzi wa maalum wa Mashtaka ya Umma, atatua kamati maalum itayohusisha-
(i) wanachama wanne kutoka kwa watu ambao wanashikilia au wamesha kuwa Majaji, wa mahakama zenye mamlaka kuu au waliohitimu kwa uteuzi kama huu;
(ii) wakili ambaye, angalau kwa miaka kumi na mitano amekuwa akiteuliwa na Chama cha Sheria Nchini Kenya; na
(iii) watu wengine wawili walio na uzoefu wa masuala ya umma.
(5) Kamati itachunguza suala hilo na kuripoti kuhusu ukweli na kutoa mapendekezo kwa Rais wa Taifa ambaye atachukua hatua kulingana na mapendekezo ya Kamati.
(6) Mwanasheria Mkuu, Mkurugezi wa Mashtaka ya Umma, Mchunguzi Maaium wa Mashtaka ya Umma, ambao wamesimamishwa kazi kulingana na ibara (4) watapokea nusu mshahara hadi waachishwe kazi au kurudishwa kazini.
(7)Kamati iliteuliwa kulingana na ibara (4) (b) watamchagua mwenyekiti kutoka miongoni mwao.
(8) Kamati zitakazochaguliwa kulingana na ibara (4) (b) kwa njia nyingine zote watakuwa na wajibu wa kuongoza vikao vyao.
(9) Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka, Mchunguzi maalum wa mashtaka ya umma wanaweza kujiuzulu kwa kumwandikia Rais wa Taifa, notisi.

## SURA YA KUMI NA TATU

**IDARA YA MAHAKAMA**

**Sehemu 1 – Mamlaka ya Idara ya Mahakama na mfumo wa sheria**

**197.** (1) Mamlaka ya Idara ya Mahakama
(a) inatokana na watu;
(b) inajikita katika mahakama na mahakama maalum zinazobuniwa kulingana na Katiba hii; na
(c) yatatekelezwa na mahakama pamoja na mahakama nyingine maalum –
(i) kwa mamlaka ya watu na kwa faida ya maslahi yao; na
(ii) kulingana na Katiba hii na sheria;
(2) Katika kutumia mamlaka ya kimahakama, mahakama pamoja na mahakama maalumu zitaongozwa na kanuni zifuatazo –
(a) haki itatendwa kwa kila mtu bila kuzingatia hadhi;
(b) Haki haitacheleweshwa;
(c) njia badalia za kusuluhisha kesi zikiwemo msamaha, mashauriano na maridhaino na njia za kitamaduni za kusuluhisha migogoro zitaimarishwa;
(d) haki itatolewa bila kuzingatia matatizo yaliyopo; na
(e) lengo na kanuni za Katiba hii zitatunzwa na kuendelezwa.
(3) Matumizi ya mbinu za kitamaduni za utatuzi wa migogoro –
(a) haitakiuka Sheria ya Haki;
(b) Haitagongana na haki na maadili au kusababisha matokeo yatakayogongana na haki na maadili;
(c) haitakosa kuambatana na Katiba hii au sheria yoyote iliyoandikwa.
(4) Kila mtu anayetekeleza majukumu ya mahakama na kila mtu anayeshiriki katika utekelezaji wa haki –
(a) atajitahidi kufikia viwango vya juu zaidi vya huduma kwa umma;
(b) atazingatia kanuni zilizofafanuliwa katika Sura ya Tisa; na
(c) ataendelea kujielimisha na kujifahamisha kuhusiana na maendeleo ya sasa katika mfumo wa sheria.
(5) Serikali itatoa raslimali na fursa kwa wafanyakazi wa Mahakama ili kuwawezesha kufikia viwango vya juu kabisa vya kuhudumia umma.

**Uhuru wa Idara ya Mahakama**

**198.** (l) Katika utekelezaji wa mamlaka ya mahakama, Mahakama itazingatia Katiba hii pamoja na sheria na haitadhibitiwa wala kuelekezwa na mtu yeyote mwingine au halmashauri.
(2) ofisi ya jaji wa mahakama yenye mamlaka makuu haitafutuliwa mbali wakati kuna afisa wa cheo cha kuhudumia ofisi hiyo.
(3) Mishahara na marupurupu yanayofaa kulipwa, au kuhusiana na, wafanyakazi katika Idara ya Mahakama, yatatokana na Hazina ya Pamoja.
(4)Mishahara na marupurupu yanayofaa kulipwa, au kuhusiana na majaji hayatabadilishwa kuwanufaisha.
(5) mfanyakazi wa Mahakama hawajibiki katika hatua au kesi kuhusiana na chochote kinachofanywa au kinachokosa kufanywa kwa nia njema katika utendaji kazi kisheria wa jukumu la mahakama.

**Ofisi na maafisa wa Idara ya Mahakama**

**199.** (1) Idara ya Mahakama inahusisha majaji wa mahakama zenye mamlaka makuu na maafisa wa idara za Mahakama.
(2) Kuna ofisi buniwa ya Jaji Mkuu na ofisi ya Naibu Jaji Mkuu.
(3)Jaji Mkuu na Naibu Jaji Mkuu ndio Kiongozi na Naibu Kiongozi wa Idara ya Mahakama mtawalia.
(4) Kuna ofisi buniwa ya Msajili Mkuu wa Idara ya Mahakama ambaye ni msimamizi mkuu na afisa wa uhasibu wa Idara ya Mahakama.
(5) Tume ya Huduma ya Idara ya Mahakama inaweza kubuni afisi nyingine za Msajili patakapokuwa na umuhimu wa kufanya hivyo.

**Mfumo wa mahakama**

**200.** (1) Mahakama zenye mamlaka ni pamoja na Mahakama yenye mamlaka kuu, Mahakama ya Rufani, Mahakama ya Kikatiba na Mahakama Kuu.
(2) Bunge litabuni kwa sheria mahakama zenye hadhi ya Mahakama Kuu kusikiza na kuamua mizozo inayohusu –
(a) ajira; na
(b) Mazingira na utumiaji wa ardhi, na umiliki wa, ardhi.
(3) Bunge litaamua mipaka na majukumu ya mahakama inayofafanuliwa katika ibara (2).

(4) Mahakama saidizi ni mahakama zinazobuniwa chini ya Kifungu 208 au na Bunge kwa masharti ya Kifungu hicho.

**SEHEMU 2- MAHAKAMA ZENYE MAMLAKA KUU**

**Mahakama yenye Mamlaka kuu**

**201.** (1) Kuna Mahakama yenye Mamlaka Kuu buniwa inayojumuisha –
(a) Jaji Mkuu, ambaye atakuwa rais wa mahakama hiyo;
(b) Naibu Jaji Mkuu, ambaye –
(i)atakuwa naibu wa Jaji Mkuu; na
(ii)atakuwa Naibu Rais wa mahakama hiyo; na
(c) sio chini ya majaji watano au zaidi ya majaji saba.
(2) Mahakama yenye Mamlaka ya Kuu itabuniwa vyema kwa minajili ya kesi zake iwapo itakuwa na majaji watano.
(3) Mahakama yenye Mamlaka Kuu itakuwa jijini Nairobi.
(4) Mahakama yenye Mamlaka kuu ina-
(a) Jukumu la kipekee la kusikiza na kuamia mizozo inayotokana na utaratibu wa kura ya kutokuwa na imani na Rais; na
(b) kulingana na ibara (5) na (6), sheria ya rufani ya kusikiza na kuamua rufani kutoka -
(i) Mahakama ya Rufani na Mahakama ya Kikatiba; na
(ii) mahakama yoyote nyingine au mahakama maalum kama inavyoidhinishwa na Sheria ya Bunge.
(5) Hakuna rufani inayoweza kuhamishwa kutoka kwa Mahakama ya Kikatiba hadi Mahakama yenye Mamlaka Kuu kulingana na uamuzi unaohusu kesi ya kupinga kuchaguliwa kwa rais.
(6) Rufani zitahamishwa kutoka kwa Mahakama ya Rufani hadi Mahakama yenye Mamlaka Kuu –
(a) kulingana na haki katika kesi yoyote inayohusisha ufasiri na utekelezaji wa Katiba hii; na
(b) katika kesi nyingine yoyote ambapo Mahakama ya Rufani au Mahakama yenye Mamlaka Kuu inathibitisha kwamba suala muhimu kwa umma linahusika.
(7) Mahakama yenye Mamlaka Kuu haitafungwa na uamuzi wake wa awali iwapo itachukulia kwamba itakuwa kwa maslahi ya haki na maendeleo ya sheria kwa sababu haipaswi kuwekewa mipaka.
(8) Licha ya vifungu vya ibara (2), uamuzi unaotolewa kulingana na ibara (4)(a) na (7) unaweza kutolewa na vikao vya mahakama pekee ambapo majaji wote wa Mahakama yenye Mamlaka Kuu huketi.
(9) Mahakama zote nyingine zitafungwa na uamuzi wa Mahakama yenye Mamlaka Kuu.

**Mahakama ya Rufani**

**202.** (1) Kuna Mahakama ya Rufani buniwa , ambayo –
(a) ina idadi ya majaji wasiokuwa chini ya kumi na wawili kulingana na ufafanuzi wa Sheria ya Bunge; na
(b) inashirikishwa na kusimamiwa kulingana na ufafanuzi wa Sheria ya Bunge.
(2) Kutakuwa na rais wa Mahakama ya Rufani ambaye atateuliwa na Jaji Mkuu kutoka miongoni mwa majaji wa mahakama hiyo.
(3) Mahakama ya Rufani ina mamlaka ya kusikiza rufani kutoka –
(a) Mahakama Kuu; na
(b) mahakama nyingine au mahakama maalum kulingana na ufafanuzi na Sheria ya Bune.

**Mahakama ya Katiba**

**203** (1) Kuna Mahakama ya Kikatiba buniwa ambayo –
(a) Itakuwa mahakama huru;
(b) Itakuwa na majaji wasiopungua watano
(c) Itashirikishwa na kusimamiwa kulingana na ufafanuzi wa Sheria ya Bunge.
(2) Kutakuwa na Jaji Kinara wa Mahakama ya Kikatiba ambaye atateuliwa na Jaji Mkuu kutoka miongoni mwa majaji wa mahakama hiyo.
(3) Mahakama ya Katiba ina mipaka ya kusikiliza swali lolote kuhusu ufasiri wa Katiba hii ikiwemo uamuzi wa –
a) swali iwapo Sheria ya Bunge au sheria nyingine yoyote haiambatani au inakiuka kipengele cha Katiba hii;
b) swali iwapo chcochote kinachosemwa kufanyika chini ya mamlaka ya Katiba hii au sheria nyingine yoyote haiambatani na au inakiuka na kipengele cha Katiba hii;
c) Swali iwapo haki au uhuru wa kimsingi katika Sheria ya Haki imenyimwa, kukiukwa, kuingiliwa au kutishiwa;
d) Kesi ya kupinga uchaguzi wa rais;
e) Suala linalohusiana na mamlaka ya katiba ya Taasisi za Serikali kuhusiana na serikali iliyogatuliwa na suala lolote linalohusu mahusiano ya kikatiba miongoni mwa viwango vya serikali;
f) Suala linalohusu mkinzano wa sheria chini ya Kifungu 232; na
g) Rufani kutokana na uamuzi wa Tume huru ya Uchaguzi na Mipaka;
h) Rufani kutokana na uamuzi wa mahakama maalum iliyoteuliwa chini ya Katiba hii kushughulikia suala la kuondolewa kwa mtu kutoka ofisini.
(4) Mahakama ya Katiba inaweza kutoa maoni ya ushauri kufuatia ombi la serikali ya taifa, taasisi yoyote ya serikali au serikali yoyote iliyogatuliwa kuhusiana na suala lolote linalorejelewa katika aya (3)(e).
(5) Shirika au mtu binafsi aliye na utaalamu mahususi anaweza, kwa idhini ya Mahakama ya Katiba, fika mbele ya mahakama hiyo kama rafiki wa mahakama husika.
(6) iwapo, katika kusuluhisha swali chini ya ibara (1), Mahakama ya Kikatiba itachukulia kwamba, kuna haja ya kutafuta haki tena pamoja na uamuzi wa suala la katiba, mahakama ya katiba inaweza –
(a) toa amri ya kutafuta haki; au
(b) elekeza suala hilo kwa mahakama inayofaa au taasisi ili kuchunguza na kutoa uamuzi sahihi.
(7) Mahakama ya Katiba itakuwa na mamlaka ya kutoa uamuzi wowote unaofaa, ukiwemo agizo la muda, agizo la tamko, tamko la hifadhi, na tamko la ubatilisho na tamko la kuendelea kuwepo kwa tamko la ubatilisho.
(8) Kwa sababu ya ibara (3)(c), Mahakama ya kikatiba itatoa amri kuidhinisha matumizi ya mamlaka yake ya kisheria kuhusiana na mamlaka ya kisheria ya Mahakama Kuu chini ya Kifungu 204(4)(b) na Kifungu 32.
(9) Maamuzi yote ya Mahakama ya Kikatiba katika masuala yanayohusiana na uchaguzi ni ya mwisho.

**Mahakama Kuu**

**204.** (1) Kuna Mahakama Kuu buniwa ambayo -
(a) inajumuisha idadi ya majaji kama inavyoagizwa na Sheria ya Bunge; na
(b) imeshirikishwa na kutekelezwa kama inavyoagizwa na Sheria ya Bunge.
(2) Kutakuwa na Jaji Kinara wa Mahakama Kuu ambaye atateuliwa na Jaji Mkuu kutoka miongoni mwa majaji katika mahakama hiyo.
(3) Kulingana na ibara (4), Mahakama Kuu ina –
(a) mamlaka asilia isiyokuwa na mpaka katika masuala ya uhalifu na raia;
(b) mamlaka ya kubaini swali iwapo haki au uhuru wa kimsingi katika Sheria ya Haki imenyimwa, kukiukwa, kuingiliwa au kutishiwa; au
(c) mamlaka yoyote nyingine, ya awali au ya rufani, inayopewa na au chini ya Sheria ya Bunge;
(4) Mahakama Kuu haina mamlaka kuhusiana na masuala –
(a) yaliyotengewa mamlaka maalum ya Mahakama yenye Mamlaka kuu na Mahakama ya Katiba chini ya Katiba hii; au
(b) ambayo Mahakama ya Katiba imeanza kuyashughulikia chini ya mamlaka yake chini ya Kifungu 203 (2)(2) na (6);
(c) kushindwa chini ya mamlaka ya mahakama zinazotajwa katika Kifungu 200(2).
(5) Mahakama Kuu ina mamlaka ya kusimamia mahakama ndogo na mtu yeyote, asasi au halmashauri, inayotekeleza jukumu la kimahakama au jukumu la mahakama la kubuni, lakini sio mahakama yenye mamlaka kuu.
(6) Kwa malengo ya ibara (5), Mahakama Kuu inaweza kuitisha rekodi za kesi yoyote iliyoko mbele ya mahakama ndogo, au mtu, asasi au halmashauri kama ambavyo imetajwa katika ibara (5) NA inaweza kutoa maagizo yoyote na kutoa maelekezo inayochukulia kuwa yanafaa ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka.

**Uteuzi wa majaji**

**205.** (1) Rais wa Taifa, kwa pendekezo wa Tume ya Huduma ya Mahakama na kwa idhini ya Bunge atamteua Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na majaji wengine.
2) Majaji wa mahakama zenye mamlaka kuu watateuliwa kutoka miongoni mwa watu ambao –
(a) wana shahada ya taaluma ya sheria kutoka chuo kinachotambulika;
(b) wana uzoefu unaohitajika ambao wameupata nchini Kenya na taasisi nyingine ya mataifa yanayotumia mamlaka ya sheria ya Jumuiya ya Madola na zinazorejelewa katika ibara (3),(4),(5) na (6); na
(c) wana mienendo na maadili mema na wasiobagua.
(3) Jaji Mkuu na majaji wa Mahakama yenye Mamlaka Kuu watateuliwa kutoka miongoni mwa watu ambao wana –
(a) uzoefu wa miaka kumi na mitano kama jaji wa Mahakama ya Rufani, Mahakama ya Katiba au Mahakama Kuu;au
(b) uzoefu wa miaka kumi na mitano kama msomi anayeheshimika, afisa katika idara ya mahakama, uanasheria au uzoefu kama huo katika maeneo mengine ya taaluma ya uanasheria; au
(d) kuwa na sifa zinazotajwa katika aya (a) na (b) kwa jumla ya miaka kumi na mitano;
(4) Majaji wa Mahakama ya Rufani watateuliwa kutoka miongoni mwa wato ambao wana –
a) uzoefu wa miaka kumi kama jaji wa Mahakama Kuu; au
(b) uzoefu wa miaka kumi kama msomi anayeheshimika au mwanasheria au uzoefu kama huo katika Nyanja nyingine husika; au
(c) kuwa na sifa zinazobainishwa katika aya (a) na (b) kwa muda wa

jumla ya miaka kumi.

(5) Majaji wa Mahakama za Kikatiba atateuliwa kutoka miongoni mwa watu ambao wana –

(a) uzoefu wa miaka kumi kama jaji wa Mahakama ya Rufani au jaji wa Mahakama Kuu; au

(b) uzoefu wa miaka kumi kama msomi anayeheshimika au mwanasheria au uzoefu kama huo katika Nyanja nyingine husika; au

(c) kuwa na sifa zinazobainishwa katika aya (a) na (b) kwa muda wa jumla ya miaka kumi.

(6) Majaji wa Mahakama Kuu watateuliwa kutoka miongoni mwa watu walio na –

(a) uzoefu wa miaka kumi kama hakimu katika taaluma za uanasheria ;au

(b) uzoefu wa miaka kumi kama msomi anayeheshimika au mwanasheria au uzoefu wa aina hiyo katika Nyanja nyingine husika;

(c) Kuwa na sifa zilizotajwa katika aya (a) na (b) kwa jumla ya muda wa miaka kumi.

(7) Jaji wa Mahakama ya Katiba atakuwa, pamoja na, kuwa mtu –

(a) anayefahamu sheria ya kikatiba na masuala kuhusu katiba.

(b) mwenye idhibati ya kujitolea katika masuala ya thamani za haki za binadamu.

**Kipindi cha kuhudumu ofisini kwa Jaji Mkuu na majaji wengine**

**206.** (1) Jaji atastaafu kutoka ofisini atakapotimiza umri wa miaka sabini.

(2) Jaji Mkuu anahudumu ofisini kwa juma ya miaka kumi au hadi atimize umri wa miaka sabini, yoyote kati ya hizi itakayotokea kwanza.

(3) Licha ya Kifungu 201 (1)(c), ambapo kipindi cha Jaji Mkuu ofisini kinamalizika kabla ya Jaji Mkuu kutimiza umri wa miaka sabini, Jaji Mkuu anaweza kuendelea kuhudumu ofisini kama jaji wa Mahakama yenye Mamlaka Kuu ingawa panaweza kuwepo tayari idadi ya juu zaidi ya Majaji wa Mahakama yenye Mamlaka kuu inayohitajika kuhudumu katika ofisi.

(4) Jaji Mkuu na jaji mwingine yeyote anaweza kujiuzulu kutoka ofisini kwa kutoa arifa kwa Rais wa Taifa.

(5) Iwapo kuna kesi ambazo zilitolewa maoni kabla ya jaji wa mahakama yenye mamlaka kutimiza umri wa kustaafu, jaji anaendelea kuhudumu ofisini kwa muda wa kufikia miezi sita pekee kwa nia ya kutoa hukumu, au kutekeleza jukumu jingine kuhusiana na kesi hizo.

**Kuondolewa kutoka ofisini**

**207.** (1) Jaji wa mahakama yenye mamlaka anaweza kuondolewa tu kutoka ofisini kwa misingi ya –

(a) kushindwa kutekeleza majukumu ya ofisi kwa sababu ya ulemavu wa mwili au akili;

(b) kukiuka kanuzi za utendakazi zilizowekewa majaji wa mahakama kuu na Sheria ya Bunge.

(c) kufilisika;

(d) kushindwa kufanya kazi; au

(e)utovu wa nidhamu, ama katika utekelezaji wa majukumu ya jaji au vinginevyo.

(2) Hatua ya kumwondoa jaji kwenye wadhifa wake kunaweza kuanzishwa Tume ya Huduma za Mahakama itakayochukua hatua hiyo kivyake au kwa sababu ya malalamiko yatakayowasilishwa na kesi mtu yeyote.

(3) Licha ya Kifungu 299 (2) (b) malalamiko yatakayowasilishwa na mtu chini ya ibara (2), yatakuwa katika maandishi , akitaja ushahidi wa madai yake ya kumtaka jaji huyo aondolewe.

(4) Tume ya Huduma za Mahakama itaangalia malalamiko hayo na iwapo itaridhika kwamba inagundua ushahidi chini ya ibara (1),itatuma malamamiko hayo kwa Rais.

(5) Katika muda wa siku kumi na nne baada ya kupokea malalamiko hayo, Rais wa Taifa atamsimamisha kazi jaji huyo, na kwa kuzingatia ushauri wa Tume ya Huduma za Mahakama –

(a) iwapo itakuwa ni Jaji Mkuu, mahakama maalum yenye -

(i) Spika wa Seneti kama mwenyekiti;

(ii) majaji watatu wa mahakama yenye mamlaka kuu kutoka kwa mahakama za zenye kutumia sheria ya kawaida;

(iii) wakili mmoja mwenye uzoefu wa kazi wa miaka kumi na mitano;

(iv) watu wengine wawili wenye uzoefu kuhusu masuala yanayohusu umma; na

(b) iwapo ni jaji tofauti na Jaji Mkuu, atateua mahakama maalum yenye-

(i) watu wanne kutoka miongoni mwa watu ambao wanahudumu au wamewahi kuhudumu kama jaji wa mahakama yenye mamlaka kuu, ambao wana sifa ya kuteuliwa kuhudumu kwenye wadhifa huo, lakini katika kila moja ya hali hizo haijakuwa, katika miaka mitatu inayotangulia, wanachama wa Tume ya Huduma za Mahakama;

(ii) wakili mmoja mwenye uzoefu wa kazi wa miaka kumi na mitano;

(iii) watu wengine wawili wenye uzoefu kuhusu masuala yanayohusu umma.

(6 Mahakama maalum itachunguza suala hilo na kuripoti kuhusu ukweli wake na kutoa mapendekezo kwa Rais wa Jamhuri, ambaye atachukua hatua kulingana na mapendekezo ya mahakama maalum.

(7) Mshahara na marupurupu ya jaji ambaye anasimamishwa kazi chini ya ibara (5) itapunguzwa kwa nusu hadi wakati ambapo jaji huyo ataondolewa au kurudishwa kazini.

(8) Mahakama maalum inayobuniwa chini ya ibara (5)(b), itamchagua mwenyekiti, kutoka miongoni mwa wanachama wake.

(9) Mahakama maalum inayobuniwa chini ya ibara (5) atawajibikia udhibiti vikao vyake.

(10) Jaji ambaye harithiki na uamuzi wa mahakama maalum chini ya kifungu hiki anaweza kukata rufani dhidi ya uamuzi wa Mahakama ya Katiba au iwapo ni jaji wa Mahakama ya Katiba, kwa Mahakama ya Rufani.

**SEHEMU 3 -MAHAKAMA ZA CHINI**

**208. (1) Mahakama za chini ni –**

a) Mahakama za Mahakimu;

b) Mahakama za Kadhi;

c) Mahakama za Kijeshi;na

d) Mahakama yoyote nyingine au mahakama maalum kama inavyoweza kubuniwa kwa Sheria ya Bunge.

(2) Bunge, kwa njia ya sheria litatoa mipaka, mamlaka na majukumu kwa mahakama ambazo zitabuniwa chini ya ibara (1).

**Mahakama za Kadhi**

**209** (1) Kutakuwa na Kadhi Mkuu na idadi kama hiyo, isiwe chini ya tatu, ya kadhi wengine kulingana na itakavyopendekezwa na au chini ya Sheria ya Bunge.

(2) Mtu hatakuwa na sifa za kuteuliwa kushikilia au kuhudumu katika wadhifa wa Kadhi isipokuwa mtu huyo -

(a) anakiri dini ya Uislamu;

(b) ana maarifa ya sheria ya Muislamu inayokubalika na madhehebu ya Waislamu,katika maoni ya Tume ya Huduma za Mahakama, kuongoza vikao vya mahakama ya Kadhi.

(3) Bila kukiuka Kifungu 208, kutakuwa na mahakama za chini zitakazoongozwa na Makadhi kulingana na uamuzi wa Bunge, na kila mahakama ya Kadhi, kwa kuzingatia Katiba hii, itakuwa na mamlaka kulingana na jinsi itakavyoidhinishwa na sheria.

(4) Kadhi Mkuu na Kadhi wengine, au Kadhi Mkuu na Makadhi wengine (wasiopungua watatu) kama inavyoweza kuelezwa na au kuidhinishwa na Sheria ya Bunge, watapewa uwezo kila mmoja kuandaa vikao vya mahakama ya Kadhi yenye mamlaka katika Himaya au katika Himaya ya zamani au katika sehemu ya Himaya ya zamani kulingana na jinsi inavyoweza kuagizwa.

(5) Hakuna sehemu ya Himaya ya zamani ambayo itakuwa nje ya mamlaka ya mahakama ya Kadhi.

(6) Mamlaka ya mahakama ya Kadhi itapanuliwa katika kubainisha maswali ya sheria ya Mwislamu kuhusiana na hadhi ya kibinafsi, ndoa, talaka au urithi katika vikao katika kwayo pande husika zitakiri dini ya Uislamu.

**SEHEMU 4 – TUME YA HUDUMA ZA MAHAKAMA**

**Kubuniwa kwa Tume ya Huduma za Mahakama**

**210.** (1) Kuna Tume ya Huduma za Mahakama buniwa inayohusisha –

(a) jaji mmoja wa Mahakama yenye Mamlaka kuu anayechaguliwa na Majaji wa Mahakama yanye Mamlaka Kuu, ambaye atakuwa mwenyekiti wa Tume;

(b) jaji mmoja wa Mahakama ya Rufani anayechaguliwa na Majaji wa Mahakama ya Rufani;

(c) jaji mmoja wa Mahakama Kuu anayechaguliwa na majaji wa Mahakama Kuu;

(d) Mwanasheria- Mkuu;

(e) mawakili wawili;

(f) mtu mmoja anayechaguliwa na Tume ya Utumishi wa Umma.

(2) Msajili Mkuu wa Idara ya Mahakama atakuwa Katibu wa Tume.

(3 Wanachama wa Tume, isipokuwa Mwanasheria Mkuu atahudumu kwenye ofisi, mradi tu awe na sifa za kufanya hivyo, kwa kipindi cha miaka mitano na ataweza kuteuliwa kuhudumu zaidi kwa kipindi kingine cha miaka mitano na cha mwisho.

**Majukumu ya Tume ya Huduma za Mahakama**

**211.** (1) Tume ya Huduma za Mahakama itahakikisha na kuimarisha uhuru na uwajibikaji wa idara ya Mahakama na kuimarisha uhuru na uwazi wa mahakama na usimamizi bora na wenye uwazi na haki pamoja na –

(a) kupendekeza kwa Rais wa Taifa watu wa kuteuliwa kuwa majaji;

(b) kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masharti ya utendajikazi wa, majaji, mahakimu na maafisa wengine wa mahakama kando na mishahara.

(c) kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu hali na mazingira ya utendajikazi wa wafanyakazi katika idara ya mahakama;

(d) kumshauri Rais wa Taifa, kuhusu uanachama wa mahakama maalum iliyorejelewa katika kifungu 207 (5)(a) na (b);
(e) teua, pokea malalamiko kupinga,kuchunguza na kuwafuta au vinginevyo kuwaadhibu, wasajili,mahakimu na maafisa wengine wa idara ya mahakama, kwa njia ambayo imetolewa na na Sheria ya Bunge.
(f) Kuandaa na kutekeleza mipango ya kuendelea kwa elimu na mafunzo ya majaji, mahakimu,maafisa wengine wa idara ya mahakama na wafanyakazi wengine katika kazi hiyo; na
(g) kuishauri serikali ya taifa kuboresha utendakazi na utekelezaji wa haki na pamoja na kutoa huduma za ushauri wa kisheria.

(2) katika utekelezaji wa majukumu yake, Tume itaongozwa na yafuatayo –
(a) ushindani na utaratibu wenye uwazi katika kuwaajiri maafisa wa idara ya mahakama na wafanyakazi wengine katika idara hiyo.
(b) kukuza usawa wa kijinsia.

**Hazina ya Mahakama**

**212.** (1) Kuna hazina buniwa inayojulikana kama Hazina ya Mahakama ambayo itaongozwa na Msajili Mkuu wa Mahakama.
(2) Hazina hiyo itahifadhi fedha –
(a) fedha zitakazotengwa na Bunge
(b) ruzuku zozote, zawadi, urithi na misaada;na
(3) Hazina hiyo itatumika kugharamia usimamizi wa Mahakama na majukumu mengine kama itakavyokuwa muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Mahakama.
(4) Sheria Sheria itakuwa na kipengele cha udhibiti wa Hazina hiyo.

## SURA YA KUMI NA NNE

**Sehemu ya 1- Malengo na kanuni za serikali ya ugatuzi**

**Malengo ya ugatuzi**

**213**. Malengo ya serikali ya ugatuzi ni:
a) kuhakikisha kuwa kuna mamlaka ya kidemokrasi9a na uwajibikiaji wa serikali huru.
b) kuhimiza umoja wa kitaifa kwa kutambua jamii mbalimbali.
c) kuwapa watu katika kila ngazi mamlaka ya kujitawala na kushiriki katika utumizi wa mamlaka ya Serikali.
d) kutambua haki haki za jamii zote katika kusimamia masuala ya jamii hizona kubuni mtandao na ushirika ili kusaidia katika usimamizi na kuharakisha maendeleo.
e) kulinda na kuhamasisha maslahi na haki za jamii ndogondgo katika ngazi zote nchini..
f) kustawisha miradi ya kijamii na kiuchumi na utoaji wa huduma kwa urahisi na za karibu kote nchini Kenya.
g) kuhakikisha kuna ugawaji sawa wa rasilmali zote za kijamii na za kitaifa kote nchini.
h) kufanikisha ugatuzi wa mamlaka za taasisi za Serikali, uendeshaji wake wa shughuli ama huduma kutoka jijini Nairobi.
i) kuhimiza ushiriki wa watu katika kufikia maamuzi ya masuala yao na
j) kuhakikisha kuna kudhibitiana na kugawana mamlaka kwa njia iliyo sawa.

**Kanuni za serikali ya ugatuzi**

**214.** Serikali zilizogatuliwa kulingana na Katiba hii zinazingatia kanuni zifuatazo:
a) Serikali iliyogatuliwa itazingatia misingi ya kidemokrasia na ugawanaji wa mamlaka.
b) Serikali iliyogatuliwa sharti iwe na njia za kuaminika za ukusanyaji kodi na uhuru wa kutoa hudua kwa njia bora; na
c) siyo zaidi ya theluthi mbili ya wanachama wawakilishi wa taasisi za umma katika serikali ya ugatuzi watakuwa wa jinsia moja.

**Serikali za maeneo**

**215.** (1) Kutakuwa na serikali ya eneo katika eneo, iliyo na bunge na kamati yenyewe mamlaka makuu.
(2) Jukumu kuu la serikali ya eneo ni kuunganisha utekelezaji wa shughuli, katika wilaya zinazounda eneo , Pia mipango ya miradi iliyo katika wilaya mbili ua zaidi za eneo hilo.
(3) Sheria ya Bunge, kulingana na hii Katiba, itatoa mwongozo kuhusu muundo wa utawala na usimamizi wa eneo la Nairobi kama eneo la jiji kuu na mji mkuu wa Kenya.
(4) Licha ya eneo la ya Kifungu cha 228 na Mpangilio wa Nne, Sheria ya Bunge itatoa mamlaka kuhusu utozaji ushuru kwa serikali ya Eneo la Nairobi.

**Mabunge ya maeneo**

**216.** (1) Uwezo wa kutunga sheria wa eneo ni wa bunge la eneo hilo.
(2) Bunge la eneo –
(a) lina wanachama watatu waliochaguliwa na bunge la nchi kutoka katika kila wilaya eneo miongoni mwa wanachama wa bunge la nchi.
(b) linachaguliwa kwa muhula mmoja wa miaka mitano; na
(c) lina uwezo wa kuidhinisha sheria zozote zilizo muhimu ama za kutyokea tu ghafla, uendeshaji na utekelezaji wowote uliokabidhiwa kwao.
(3) Katika kuteua wawakilishi, bunge la nchi litaongozwa na makabila na mambo mengine mengi kama jinsia na uwakilishaji mwingine uliomo wilayani.
(4) Bunge la eneo, huku likizingati ugawanaji wa mamlaka, lina uwezo wa kusimamia kamati yenye mamlaka kuu na taasisi yoyote yenye mamlaka kuu iliyoundwa kisheria na kupitishwa na bunge.

**Kamati za mamlaka kuu**

**217.** (1) Uwezo mkubwa wa mamlaka ya eneo utatumiwa na kamati kuu ya eneo hilo.
(2) Kamati ina watu wafuatao:
(a) mkurugenzi wa eneo, au kama ni Nairobi, meya, aliyechaguliwa kulingana na vifungu vya sheria 218 na 219 mtawalia.
(b) naibu mkurugenzi wa eneo, au kama ni Nairobi naibu wa meya, ambaye amechaguliwa kulingana na vifungu vya sheria 218 na 219 mlawalia.
(c) wanachama wengine wasiozidi watano, ambao si wanachama wa bunge la eneo, walioteuliwa na mkurugenzi wa eneo kwa idhini ya bunge la neo hilo.
(3) mkurugenzi wa eneo na naibu wake watakuwa afisa mkuu na naibu wa afisa mkuu wa eneo lao.
(4) Jijini Nairobi, , meya na naibu wake watakuwa maafisa wakuu mtawalia.
(5) Wanachama wa maafisa wakuu wa eneo watawajibika kwa pamoja na kibinafsi kwa bunge la eneo ili kutekeleza majukumu na mamlaka yao ya kuendesha shughuli za eneo lao.

**Uchaguzi wa mkurugenzi wa eneo na nanibu wake**

**218.** (1) Mkurugenzi wa eneo na naibu wake watachaguliwa na wajumbe ambao ni pamoja na wanachama wa bunge la wilaya la eneo hilo.
(2) Mwanachama wa bunge la wilaya hawezi kuchaguliwa kama mkurugenzi wa eneo ama naibu wa mkurugenzi wa eneo.
(3) Anayewania kiti katika kifungu (1) ambao anapata zaidi ya nusu ya kura katika uchaguzi atatangazwa mshindi.
(4) Kama hakutakuwa na msnhindi, uchaguzi mwingine utafanywa na katika uchaguzi huo watakaogombea viti watakuwa:
(a) mgombea, ama wagombea, waliopata kura nyingi; na
(b) mgombea, au wagombea waliochukua nafasi ya pili kwa wingi wa kura
(5) Mahali ambapo zaidi ya mgombea mmoja amepata kura nyingi sana , kifungu cha (4)(b) hakitafuatwa na wagombea wa pekee katika uchaguzi huo mpya watakuwa wale wanaokubalika kulingana na kifungu cha (4)(a).
( 6) Mgombea anayepa kura nyingi, au nyingi zaidi, itakavyokuwa katika uchaguzi huo mpya, atatangazwa kuwa mshindi.
(7) Kulingana na kifungu cha (8), gavana wa wilaya na nanibu wake, kila mmoja atashikilia wadhifa wake kwa muhula mmoja wa miaka mitano na kila mmoja anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine ambacho kitakuwa cha mwisho.
(8) Kulingana na kifungu cha (7), mtu ambaye amehudumu kwa miaka miwili mfululizo kama gavana wa wilaya ama naibu gavana atachuliwa kuwa alihudumu kwa kipindi kizima.

**Uchaguzi wa meya na naibu wa meya jijini Nairobi**

**219.** (1) Meya na naibu wa meya watachaguliwa na zaidi ya nusu ya kura za wapiga kura ambao watatimiza masharti ya kuwa wakazi wa eneo hili kulingana na Sheria za Bunge.
(2) Uchaguzi wa meya na naibu wake utazingatia upigaji kura wa haki wa kimataifa.
(3) Kwa mujibu wa kifungu cha (1), Sheria za Bunge, zitaelekeza taratibu za kuzingatiwa katika uchaguzi wa meya na naibu wake.

**Shughuli za kamati kuu za maafisa wa maeneo**

**220.** (1) Wanachama wa kamati za maafisa wakuu ya eneo wana jukumu la kutumia mamlaka yao kuliungana na shughuli za mamlaka maalumu na shughuli zinazotolewa kwa eneo hilo.
(2) Mkurugenzi wa eneo anaweza kuwapa majukumu maalumu Wanakamati.

**SEHEMU YA 3 – SERIKALI ZA WILAYA**

**Serikali za wilaya**

**221**. (1) Kila wilaya itakuwa na serikali yake itakayokuwa na bunge na maafisa watendaji.
(2) Kila serikali ya wilaya itagatua shughuli zake na utoa wa huduma ili kuhakikisha kwamba imepata ufanisi wa kutekeleza majukumu yake kadiri iwezekanavyo.
(3) Licha ya kuwepo kwa Sura hii, wilaya zinazounda eneo la Nairobi, kulingana na Kifungu cha129(5) hazitafanya shughuli nyingine yoyote, wala kuwa na mamlaka mengine yoyote ya serikali ya wilaya ila tyu kulingana na Sheria za Bunge kama zinavyorejelewa katika Kifungu cha 215(3).

**Wanachama wa bunge la wilaya**

**222.** (1) Bunge la wilaya lina wanachama wafuatao:
(a) wanachama waliochaguliwa mmoja mmoja kwa kila wadi, aidha moja kwa moja au kwa uwakilishi sawa na mipaka kwa mujibu wa Sheria za Bunge zilizopitishwa baada ya kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka;
(b) idadi ya wanachama wa viti maalumu kulingana na kurawal za vyama vyao vya kisiasa kulingana na kifungu cha (1) (a), kuhakikisha kwamba si zaidi ya theluthi mbili za wanachama ni wa jinsia moja.
(c) idadi ya wanachama kutoka katika makundi yaliyotengwa wakiwemo walemavu, jamii za watu wachache, wazee, vijana kulingana na kura za kila chama cha kisiasa kulingana na kifungu cha (1) (a), kama inavyopendekezwa katika Sheria za Bunge; na
(d) idadi ya wanachama huru kulingaqna na wale waliochaguliwa katika kifungu cha (1) (a).
(2) Kujaza viti maalumu kulingana na kifungu cha (1) (b) kutaamuliwa na baada ya kutangazwa kwa wanachama waliochaguliwa katika kila wadi.
(3) Bunge la wilaya huchaguliwa kwa kipindi cha miaka mitano.

**Kamati tendaji za wilaya**

**223.** (1) Mamlaka kuu ya wilaya hutumiwa na kamati kuu ya wilaya, inayojumuisha:
(a) gavana wa wilaya na naibu wake; na
(b)kulingana na kifungu cha (2) , wanachama wengine huteuliwa na gavana wa wilaya kutoka kwa wanachama wa bunge la wilaya kwa idhini ya bunge hilo.
(2) Idadi ya wanachama walioteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha (1)(b) haitazidi:
(a) theluthi ya wanachama ya wanachama wa bunge la wilaya kama bunge hilo halina zaidi ya wanachama ziaidi ya thelathini; au
(b) kumi; kama bunge lina zaidi ya wanachama thelathini.
(3) gavana wa wilaya na naibu wake, wao mtawalia watakuwa afisa mtendaji na naibu wa afisa mtendaji wa wilaya.
(4) Gavana wa wilaya asipokuwepo, naibu wake ana mamlaka ya kutosha ya kuendesha shughuli zote na majukumu ya gavana wa wilaya.
(5) Wanachama wa kama tendaji ya wanawajibika kwa pamoja na kibinafsi kwa bunge la wilaya katika shughuli zote za utekelezaji wa majukumu yao.

**Uchaguzi wa gavana wa wilaya na naibu wa gavana wa wilaya**

**224.** (1) Gavana wa wilaya na naibu wake watachaguliwa na bunge la wilaya kutoka kwa wanachama wa bunge hilo.
(2) mgombeaji katika uchaguzi kulingana na kifungu (1) anayepata zaidi ya nusu ya kura ziklizopigwa atatangazwa mshindi.
(3) Kama hakutakuwa na mgombe atakayetangazwa mshindi , uchaguzi utafanywa mara ya pili na wagombea watakuwa:
(a) mgombea, au wagombea watakaokuwa wamepata kura nyingi; au
(b) mgombea, au wagombea waliochukua nafasi ya pili kwa wingi wa kura.
(4) Pale inapotukia kuwa zaidi ya mgombea mmoja amepata kura nyingi sana kifungu cha (3) (b) hakitafuatwa na wagombea wa pekee watakuwa kulingana na wanaokubaliwa na kifungu cha (3)(a).
(5) Mgombeaji atakayepata kura nyingi katika uchaguzi, kulingana na mambo yatakavyokuwa, katika uchaguzi huo mpya, atatangazwa mshindi.
(6) Gavana wa wilaya na naibu wake wanashikilia mamlaka ya ofisi zao kwa kipindi cha miaka mitano na wanaweza kugombea tena viti vyo kwa mara ya pili na ya mwisho.
(7) kwa ajili ya kifungu cha (6) , mtu ambaye amehudumu kama gavana wa wilaya ama naibu kwa mfululizo wa miaka miwili unusu au zaidi atachukuliwa kama ambaye amehudumu kwa kipindi chake kizima.

**Shughuli za kamati tendaji ya wilaya**

**225** (1) Kamati tendaji ya wilaya ina majukumu yafuatayo:
(a) Utekelezaji wa sheria za bunge la wilaya;
(b) Utekelezaji, katika wilaya , sheria za eneo na za taifa inavyohitajika kisheria;
(c) Kusimamia shughuli za utawala wa wilaya na idara zake; na
(d) Kushirikisha shughuli za sehemu zote za utawala katika wilaya.
(2) Bila kuzuia mamlaka ya bunge, kamati tendaji ya wilaya inaweza kutayarisha sheria zao wanazopendekeza ili kutekelezwa na bunge.
(3) Kamati tendaji ya wilaya ina uwezo mwingine mkubwa na majukumu kulingana na Katiba au taifa au sheria za eneo.
(4)Kamati tendaji ya wilaya itatoa ripoti kamili za mara kwa mara kwa baraza la wilaya kuhusu masuala chini ya udhibiti wa kamati hiyo.

**Maeneo ya mijini**

**226.** (1) Mamlaka ya Kitaifa itaidhinisha sheria na usimamizi wa maeneo ya mijini.
(2) Sheria inabuniwa chini ya ibara (1) –
(a) Ita –
(i) buni vigezo vya kuweka kimakundi maeneo kama vile ya mijini na miji mikuu;
(ii) buni kanuni za utawala na usimamizi wa maeneo ya mijini;
(iii)ruhusu ushiriki katika utawala wa maeneo ya mijini na miji mikuu; na
(iv) Unda kanuni za uteuzi wa mameya, manaibu wa mameya na wanachama wengine wa kamati tendaji za miji mikuu na maeneo mengine ya miji; na

(b)inaweza-
(i) kuidhinisha utambuaji wa kategoria mbalimbali za maeneo ya mijini; na
(ii) kuunda kipengele cha sheria kuhusu utawala bora wa maeneo ya mijini.

**Katiba au taifa au sheria za eneo.**

**227.** (1) Mamlaka ya kisheria ya wilaya iko katika bunge la wilaya.
(2) Bunge la wilaya, laweza kubuni sheria zozote muhimu, zisizo muhimu sana, utimizaji mzuri wa sheria hizo na shughuli zinazoambatana na majukumu yake.
(3) Bunge la wilaya, likizingatia kanuni ya kugawana mamlaka, lina uwezo wa kusimamia kamati tendaji ya wilaya na vyombo vingine vilivyobuniwa kisheria na kuidhinishwa na bunge.
(4) Bunge la wilaya, laweza kupendekeza kwa bunge la eneo kubuniwa kwa sheria kuhusu jambo lolote lililo katika uwezo wa bunge la eneo.
(5) Bunge la wilaya laweza kupokea na kuidhinisha mipango na sera kwa usimamizi na utambuzi wa rasilmali za taifa, kustawisha na kusimamia miundo msingi na taasisi zao.

**SEHEMU YA 4 – MAMLAKA NA SHUGHULI ZA SERIKALI YA UGATUZI**

**Mamlaka na shughuli zake**

**228.** (1 ) Kinyume na kawaida ya ilivyo katika Katiba, mamlaka na shughuli za serikali ya kitaifa na ile ya ugatuzi yameelezewa katika Mpangilio wa Nne.
(2) Jukumu linalopatikana katika zaidi ya ngazi moja ya serikali ni shughuli iliyo katika eneo zaidi ya moja la utawala la ngazi hizo za serikali.
(3) Shughuli ambayo haijatolewa kwa katiba hii au sheria za eneo au wilaya ni kazi ya serikali ya taifa.
(4) Kando na kifungu cha (1), na kulingana na Katiba hii, serikali ya kitaifa haijatengwa katika kutunga sheria za Jamhuri kuhusu jambo lolote lile.

**Kuhamisha mamlaka na majukumu**

**229.** (1) Mamlaka au majukumu ya serikali katika kiwango kimoja yaweza kuhamishwa hadfi kiwango kingine cha serikali kwa makubaliano kati ya serikali mbili kama:
(a) mamlaka au jukumu hilo litapata uzito zaidi likitekelezwa na serikali hiyo itakayolichukua; na
(b) kuhamishwa kwa mamlaka au majukumu kunaafikiana na sheria ambazo

zinafungamana na utekelezaji wake.

(2) Pale ambapo mamlaka au shughuli imehamishwa kutoka kwa ngazi moja ya serikali hadi kwa serikali ya ngazi nyingine:

(a) mipango itafanywa kuhakikisha kwamba gharama za kutekeleza utekelezaji wa mamlaka au shughuli hiyo iliyohamishwa imefanikishwa; na

(b) uwajibikaji wa kikatiba kwa shughuli au mamlaka itahifadhiwa na serikali iliyopangiwa kulingana na Mpangilio wa Nne.

**Sehemu ya 5 – Mipaka ya serikali zilizogatuliwa**

**Mipaka ya serikali ya ugatuzi**

**230.** (1) Kulingana na Katiba hii, mipaka ya eneo au wilaya itategemea:

(a) wingi wa watu na uongezekaji wao

(b) miundomsingi

(c) historia na misingi ya utamaduni

(d) gharama za usimamizi

(e) maoni ya jamii zinazohusika

(f) makusudi ya ugatuzi wa serikali; na

(g) sifa za kijiografia

(2) Mipaka ya eneo au wilaya yaweza kubadilishwa kwa uamuzi wa angalau theluthi mbili za kila Bunge kufuatia uamuzi wa tume huru iliyoundwa na Bunge kwa sababu hiyo.

**Sehemu 6 – Mahusiano ya serikali**

**Ushirikiano wa serikali katika ngazi tofautitofauti**

**231.** (1) Serikali katika ngazi zote:

(a) itaendesha na kutumia mamlaka yake ikiheshimu utekelezaji na heshima za taasisi nyinginezo za ngazi nyingine za serikali na uwezo wa katiba na taasisi katika ngazi nyingine.

(b) kusaidia, kushirikiana na kushauriana na serikali katika ngazi zote ifaavyo, kutekeleza sheria katika ngazi zote za serikali; na

(c) kushauriana na serikali katika ngazi tofauti tofauti kwa minajili ya kubadfilishana mawazo, kusimamia sera na utawala huku uwezo ukikuzwa.

(2) Serikali katika ngazi tofauti na ngazi sawa, kwa kiasi fulani cha lazima, katika jambo moja, huweza kutumia mamlaka yake, kwa sababu hiyo kuunda muungano wa kamati na mamlaka.

(3) Katika kutofautiana kokote kwa serikali, serikali inayohusika itafanya kila jitihada kutatua mzozo huo ikizingatia taratibu za kisheria kama zilizyo katika Sheria za Bunge.

(4) Sheria ya Bunge inao uwezo wa kutatua mizozo ya serikali kwa mbinu mbadala za kutatu a mizozo zikiwemo kushauriana, kupatanisha na kusuluhisha.

**Mizozo ya kisheria**

**232.** (1) Kifungu hiki kinahusu mizozo ya kisheria inayohusiana na masuala yanayopatikana katika viwango kadhaa vya serikali.

(2) Sheria za taifa hutumika zaidi kuliko za maeneo na wilaya kama:

(a) sheria za taifa zitatumika kwa usawa kote Kenya na masharti mengine yaliyomo katika kifungu cha (3) yametoshelezwa.

(b) sheria za taifa zinalenga kudhibiti maamuzi yasiyo ya busara ya eneo au wilaya ambayo:

(i) yanaweza kuwa na athari mbaya kiuchumi ama maslahi ya kiusalama ya eneo jingine, wilaya au Kenya kwa jumla; au

(ii) zitaepusha kukwamishwa kwa utekelezaji wa sera za uchumi wa taifa.

(3) Hali zinazorejelewa katika kifungu cha (2) (a) ni:

(a) sheria za kitaifa hushughulikia suala ambalo haliwezi kutatuliwa na sheria za maeneo na wilaya pekee.

(b) sheria za kitaifa hushughulikia suala ambalo ili lishughulikiwe kikamilifu linataka sheria ambazo ni sawa katika taifa zima. Hufanya hivi kwa kuwa na:

(i) Kanuni na viwango

(ii) taratibu

(iii) sera za kitaifa na

(c) Sheria za kitaifa ni muhimu kwa:

(i) uhifadhi wa usalama wa kitaifa

(ii) uhifadhi wa umoja wa kiuchumi

(iii) kulinda masoko ya pamoja kulingana na uhamishaji wa bidhaa, huduma na ufanyaji kazi.

(iv) kuhimiza shughuili za kiuchumi miongoni mwa maeneo au mipaka ya wilaya.

(v) kulinda mazingira.

(4) Sheria za maeneo na za wilaya huwa muhimu kuliko za taifa kama mahitaji ya kifungu cha (2) hayajatimizwa.

(5) Sheria za maeneo zina nguvu kuliko za wilaya.

(6) uamuzi wa mahakama kwamba sheria ya ngazi moja ya serikali ni muhimu kuliko ile nyingine. Si kwamba ni kupuuza uwezo wa ngazi hiyo nyingine bali ni kwa manufaa ya kuziimarisha sheria ziwe thabiti zaidi.

(7) Tunapofikiria mzozo kisheria wa ngazi mbili tofauti za serikali , mahakama itapendelea fasiri yoyote inayokubalika ya sheria kuepuka ili kumaliza mzozo wenyewe na kuepuisha mizozo zaidi.

(8) Mahakama inayosikiliza kesi ya mzozo wa kisheria wa kati ya ngazi mbili za serikali itatoa hukumu ila:

(i) kuwepo na umuhimu ama utata na mahakama, kwa hiari yake, inaamua kupeleka katika Mahakama ya Kikatiba; au

(ii) upande wowote ukiomba kwamba kesi yake ipelekwe katika mahakama nyingine.

**Sehemu ya 7 – Kuondolewa, kusimamishwa kwa muda, kuvunjiliwa mbali kwa serikali za ugatuzi**

**Kura ya kutokuwa na imani na kamati kuu ya eneo**

**233.** (1) Mwanachama wa kamati ya eneo anayesimamiwa na wanachama wasiopungua theluthi moja, wakati wowote, bunge linapoendelea anaweza kupendekeza mswada wa kukosa imani na kamati kuu ya eneo.

(2) kama kikao cha muafaka kinaungwa mkono na zaidi ya nusu ya wanachama kikiamua kwamba hakina imani na mkurugenzi wa eneo na naibu wake na kamati yao basi Ikamati kuu ya eneo itaondoka mamlakani na uchaguzi wao utafanyika mara moja kulingana na Kifungu cha 218.

**Kura yako ya kutokuwa na imani na kamati kuu ya eneo**

**234.** (1) Mwanachama wa bunge la wilaya anayeungwa mkono na kiasi cha theluthi moja ya wanachama , anaweza kutoa hoja ya kutokuwa na imani na kamati kuu ya eneo.

(2) kama baraza litaafikiana na uamuzi utakaoungwa mkono na zaidi ya nusu ya wanachama, mkurugenzi wa eneo, naibu wa mkurugenzi wa eneo na wanachama wale wengine wa kamati kuu watatoka mamlakani na uchaguzi mpya kufanyika wa mkurugenzi na naibu wake kulingana na Kifungu cha 218.

**Kusimamishwa kwa muda kwa serikali ya eneo na wilaya**

**235.** (1) Serikali ya eneo au ya wilaya yaweza kusimamishwa kwa muda kutokana na:

(a) katika dharura inayotokana na mizozo ya ndani au vita; au

(b) kama hali za kipekee zinahitaji kuchukuliwa kwa hatua kama hiyo.

(2) serikali ya eneo ama wilaya haitasimamishwa kwa muda kulingana na kifungu cha (1)(b) hadi tume huru ifanye uchunguzi wa mashtaka yaliyowasilishwa dhidi yake, Rais wa taifa aridhike kwamba mashtaka ni ya haki na seneti imeyaidhinisha.

(3) wakati wa kusimamishwa kwa muda katika kifungu hiki, mipango itafnywa ya utekelezaji wa majukumu ya serikali ya eneo au wilaya kulingana na Sheria za Bunge.

(4) Seneti yaweza, wakati wowote, kwa uamuzi unaoungwa mkono na nusu ya wanachama, kufitilia mbali kusimamishwa huko kwa muda.

(5) kusimamishwa kwa muda katika Ibara hii hakuwezi kuwa kwa zaidi ya siku 90.

(6) Muda uliotengwa kulingana na kifungu cha (4) unapoisha, uchaguzi wa serikali mwafaka za maeneo na mikoa itafanyika.

**Sehemu ya 8 – Kwa jumla**

**Sifa za wagombea uanachama wa bunge la eneo au wilaya**

**236.** (1) Labda azuiwe na kifungu cha (2), mtu yeyote anaweza kugombea ubunge wa eneo ama wilaya kama:

(a) ni raia wa Kenya

(b) amesajiliwa kama mpigaji kura

(c) anatimiza sifa zozote za kielimu, tabia nzuri na maadili mema kama inavyotakikana kulingana na Katiba au Sheria za Bunge; na

(d) ameteuliwa na chama cha kisiasa; au

(e) katika uchaguzi wa wilaya, ni mgombea huru, aliyeungwa mkono

na watu 500 waliosajiliwa kama wapiga kura katika wadi husika kama inavyoruhusiwa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka.

(2) Mtu hataruhusiwa kugombea uanachama wa bunge la eneo kama:

(a) ana cheo serikalini au ofisi ya umma, mbali na hiyo ya bunge la eneo ama wilaya anakowania kiti.
(b) hana akili timamu
(c) imetangazwa na kuthibitishwa kuwa amefilisika
(d) anatumikia kifungo gerezani cha miezi sita au zaidi; au
(e) amepatikana , kulingana na sheria yoyote, kwamba ametumia vibaya ofisi ya umma ama kwa njia yoyote kukiuka kanuni za Sura ya Tisa.

(3) Mtu hatazuiwa kulingana na ibara ya (2) ila tu uwezekano wa kukata rufani ama kesi yake kushughulikiwa upya kwa kifungo chake na mbinu zote za kujitetea zimekwisha.

**Kuondoka katika ofisi kama mwanachama wa bunge la eneo au wilaya**

**237.** (1) Ofisi ya mwanachama wa bunge la eneo au wilaya huwa wazi kutokana na:

(a) mwanachama akifa;
(b) mwanachama akijiuzulu na kumwandikia kiongozi wa bunge.
(c) kama mtu huyo akipigwa marufuku kwa mujibu wa Kifungu cha 236(8)
(d) kwisha kwa kipindi chake cha bunge
(e) kama mwanachama atakosa vikao vinane muhimu vya bunge bila idhini ya maandishi kwa kiongozi wa shughuli za bunge.
(f) kama mwanachama ataondolewa ofisini kisheria ilivyowekwa katika Kifungu cha 101;
(g) kama mwanachama atajiuzulu ama kufukuzwa kutoka katika chama cha siasa kulingana na Kifungu cha 115; au
(h) baada ya kuchaguliwa bungeni kama mgombea huru, anajiunga na chama cha kisiasa.

**Uwezo wa kuita mashahidi**

**238.** (1) bunge la eneo au wilaya lina uwezo wa kumwita mtu yeyote mbele yake ama ya kamati yake yoyote ili kutoa ushahidi au habari zinazotakikana.

(2) Kulingana na kifungu cha (1), bunge lina mamlaka ya Mahakama Kuu juu ya:

(a) kuhimiza mahudhurio ya mashahidi na kuwahoji baada ya kula kiapo.
(b) kuwalazimisha mashahidi kutoa nyaraka muhimu mahakamani
(c) kutafuta idhini ya kuwahoji mashahidi ng'ambo

**Ushirikiano na umma, uwezo, nafuu na ulinzi**

**239.** (1) Vifungu 149 na 150 vinarejelea wanachama wa mabaraza ya eneo na ya wilaya kwa idadi sawa na vile walivyokuqwa wakiomba viti vya uanachama wa nbunge.

**Usawa na tofauti za kijinsia**

**240.** (1) Si zaidi ya theluthi mbili ya wanachama wa bunge lililobuniwa kulingana na sura wanafaa kluwa wa jinsia moja.

(2) Kisheria, Bunge litahakikisha kwamba wingi wa masuala ya utamaduni na sheria ya eneo au willaya yanaonyeshwa katika mashirika yenye uwezo mkuu.

(3) Bila kujifunga tu na ibara ya (2), kitengo cha sheria kitalinda maslahi ya jamii zilizotengwa katika wilaya zote.

**Serikali katika kipindi cha mpwito**

**241.** Wakati uchaguzi unapoendelea ili kuunda kikao katika Sura hii, kamati kuu iliyoundwa awali inabakia ilivyokuwa kuendesha shughuli za bunge hadi itakapoundwa upya baada ya uchaguzi.

**Kuchapishwa kwa sheria**

**242.** (1) Sheria ama kanuni nyingine zisizo na mamlaka makubwa na kuundwa na bunge au kamati kuu haiwezi kuchukua hatamu za uongozi hadi itangazwe katika Gazeti rami la Serikali.

(2) Sheria za taifa, wilaya na mikoa zaweza kuwa na mahitaji mengi ya serikali iliyogatuliwa.

(3) ya kila sheria au kanuni nyinginezo zilizoundwa na bunge au kamati kuu ya serikali iliyogatuliwa itawasilishwa kwa Rekodi ya Sheria zilizoundwa.

**Vipengele vitakavyoundwa na Sheria za Bunge**

**243.** (1) Bunge, kulingana na sheria litaunda taratibu kabambe katika masuala yote muhimu au ya lazima kwa mujibu wa Sura hii.

(2) Nafasi yaweza kutolewa ya:

(a) usimamizi wa Nairobikama jiji kuu, miji mingine mikuu na miji mingine
(b) kuhamishwa kwa mamlaka na shughuli kwa ngazi moja ya serikali hadi nyingine, pamoja na kuhamishwa kutoka kwa serikali ya taifa hadi serikali za maeneo ama za wilaya kisheria kulingana na aya zifuatazo za Sheria za Bunge na masharti ya kuhamisha na kurudisha mamlaka yaliyohamishwa.
(c) taratibu za uchaguzi ama uteuzi wa watu, na kuwato mamlakani katika seriklali za ugatuzi, pamoja na uwezo wa wapiga kura na wagombea viti.
(d) taratibu za mabaraza na kamati kuu pamoja na uenyekiti, mfuatano wa mikutano, mahudhurio na upigaji kura; na
(e) kusimamisha kwa muda kwa mabaraza na kamati kuu.

## SURA YA KUMI NA TANO

**FEDHA ZA UMMA**

**Sehemu- 1 Usimamizi wa fedha na mapato ya Serikali**

**Kanuni na malengo ya usimamizi wa fedha na mapato ya umma**

**244.** Malengo ya kimsingi ya mfumo wa usimamizi wa fedha na mapato ya umma ni kuhakikisha-

(a) kuzalisha mapato kwa ufanisi na kunakofaa.
(b) kuzingatia kanuni za uwazi na kuwajibika katika , kuthibiti kunakofaa kwa usimamizi wa-
 (i) mikopo na matumizi ya; na
 (ii) bajeti na taratibu za bajeti
(c) usawa katika kutafuta mapato na kugawa rasilmali ya kitaifa na asilia kote nchini na kujali mahitaji maalum ya jumuia zilizizotengwa;
(d) utekelezaji wa kanuni, usawa wa ushuru, usawa katika kutozwa ushuru kulingana na uwezo wa kiuchumi.
(e) Kutozwa ushuru, kutitilia maanani mzigo wa ushuru wa moja kwa moja kwa serikali zilizogatuliwapamoja na wananchi.
(f) kwamba uzito na faida za ukopaji wa umma umegawa kwa usawa miongoni mwa vizazi vya sasa na vizazi vijavyo.
(g) kwa bajeti na taratibu za bajeti zinakuza uwazi, uwajibibikaji na ufanisi katika usisimamizi wa uchumi wa kifedha, madeni na utumishi wa umma; na
(h) kwamba, hesabu za pesa za serikali zime kaguliwa na kutolewa ripoti mara kwa mara.

**Sehemu 2- Mamlaka ya Ushuru na Kugawa Mapato**

**Kutoza Ushuru**

**245.** (1) hakuna mtu au mamlaka yoyote ambayo-

(a) kutoz, ushuru, ada au malipo kwa niaba ya serikali ya kitaifa au serikali iliyogatuliwa, isipokuwa chini ya mamlaka ya sheria; au
(b) kuvutilia au kubadilisha ushuru, ada au kutoza malipoyaliyo chini ya sheria isipokuwa kamainavyopendekezwa na sheria.

(2) Sheria ambazo zinakubalia kuvutiliwa mbali kwa ushuru wowote ,ada au malipo, zitahakikisha kwamba rekodi ya kuvutiliwa mbali kwa ushuru kama huu na sababu zake zinahifhadhiwa na kupelekewa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali.

(3) hakuna sheria ambayo inaweza kumwingiza au kumwandoa ofisa wa Serikali katika ulipaji wa ushuru kwa sababuza-

(a) mamlaka yanayoshikiliwa na ofisa wa Serikali; au
(b) hali ya kazi ya ofisa wa Serikali.

**Mamlaka ya Kutoza Ushuru**

**246.** (1) Kutoza ushuru na mamlaka megine ya kutafuta mapato ya serikali ya kitaifa na serikali zilizogatuliwa yamo katika Mpangilio wa Tano

(2 Kutoza ushuru na mamlaka mengine ya kutafuta mapato kwa serikali iliyogatuliwa hayatatekelezwa kwa njia ambazo zitaaathiri mapendeleo ya bsre za uchumi wa taifa, kazi za kiuchumi kupita mipaka ya maeneo au usambazaji wa mali na huduma , mtaji au leba.

(3) Pale ambapo serikali mbili au zaidi zitakuwa na utozaji ushuru au mamlaka na majukumu mengine ya kotafuta mapato kwa ajili ya suala lile, kuganywa

kunakofaa kwa mamlaka na majumu haya kutaamuliwa na sheria ya bunge.
(4) Hakuna chochote katika Kipengele hiki kitakachozuia kugawanywa kwa mapato yaliyopatikana chini ya Kifungu hiki kati ya serikali ambazo zina utozaji ushuru huu ua mamlaka na majuku ya kutafuta mapato kuhusu suala hili moja.

**Kiwango cha fedha kwa serikali zilizogatiliwa**

**247.** (1) serikali ya kitaifa itakuza usawa wa kifedha miongoni mwa viwango vyote vya serikali.
(2) Kila serikali iliyogatuliwa-
(a) ina haki ya kiwango sawa cha mapato yaliyopatika na kitaifa; na
(b) inaweza kupata misaada ya usawazishaji au fedha nyingine kutoka kwa mapato ya serikali yakitaifa kwa masharti au bila masharti.
(3) mapato zaidi yanayopatikana na serikali zilizogatuliwa huenda Yasipunguzwe kutoka kwa mgawo wake uliopatika kwa mapato ya kitaifa, au kwa migawo mingine inayopatikana kutoka kwa mapato ya serikali ya kitaifa.
(4) serikali ya kitaifa haina wajibu wa kufidia serikali iliyogatuliwa kwa kosa lake la kutopata mapato ya kiwango sawa na hazina yaka ya fedha na uwezo wake wa kutoza ushuru.
(5) Mgawo wa mapato ya kitaifa kwa serikali zilizogatuluwa utatolewa kwa serikali hiyo kwa haraka na bila kupunguzwa, isipokuwa pale ambapo kutolewa huko kumesimamishwa na Kipengele 263(2).

**Sheria**

**248.** (1) kwa mujibu wa kipengele 246(1) 247, Bunge kwa kuzingatia sheria itathibiti kutozwa ushuru na mamalaka ya kutafuta mapato ya serikali zilizogatuliwa, nakugawa mapato na kutoa misaada kwa serikali zilizogatuliwa.
(2) sheri inayorejelewa katika Ibara (1) na sheria yoyote kuhusu fedha zinazohusu serikaki zilizogatuliwa, zinaweza kutungwa tu baada ya Tume ya Kugawa Mapato , Waziri anayehusika na ugatuzi wa serikali na Mthibiti Bajeti watashauriwa na marekebisho yoa kuwasilishwa kwa Bunge lilofikiwa.
(3) sheria inayorejerewa katika Ibara (1), itatilia maanani –
(a) manufaa ya taifa;
(b) kipengele kingine katika sheria ambacho kinaitajika kulingana na dani na majukumu mengine ya Kitaifa;
(c) mahitaji ya serikali ya kitaifa yaliyobainishwa na malengo na vigezo;
(d) kuhakikisha kwamba kila eneo na wilaya linauwezo wa kutoa huduma muhimu na kutekeleza majukumu waliopewa.
(e) uwezo wa kifedha na ufanisi wa maeneo na wilaya;
(f) maendeleo na mahitaji mengine ya maeneo na wilaya ;
(g) ukosefu wa usawa wa kiuchumi miongoni mwa maeneo na mahitaji ya kuwa na usawa wa kifedha;
(h) mahitaji ya kukubali kuchukua hatua kuhusu sehemu kavu na zile zilizo na ukavu kiasi na sehemu nyingine zilizobaguliwa;
(i) mahitaji ya kukuza mapato kwa kila eneo na wilaya ;
(j) majukumu ya maeneo na wilaya kwa mujibu wa sheria;
(k) mapendeleo ya kuwa na mgawo una uweza kutabilika.
(i) mahitaji ya kuweza kubadilika kukabiliana na dharura na mahitaji mengine ya muda mfupi na vigezo vingine vinavyotokana na malengo sawa na haya.

**Sehemu 3- Hazina ya pamoja ya kuhifadhi fedha za umma**

**Hazina ya pamoja**

**249.** (1) Kuna Hazina ya pamoja buniwa pale amabapo pesa zote zilizotafutwa au pupokelewa kwa niaba ya serikali au kwa imani ya serikali ya kitaifa zitalipwa, isipokuwa fedha amabazo zimeondolewa kwa njia inayofaa kupitia kwa Kipegele cha sheria ya Bunge.
(2) Pesa ambazo zinarejelewa katika Ibara (1) hazihuzishi-
(a) pesa zinazolipwa chini ya Kipengele katika sheria ya Bunge kwa Fedha nyingine za serikali ya kitaifa zilizobuniwa haswa kwa nia hiyo; au
(b) ambazo chini ya sheria ya Bunge, zinaweza kuchukuliwa na taasisi ya serikali katika kiwango cha kitaifa au cha serikali iliyogatuliwa iliyozichukua kwa kusudi la kulipia gharama za matumizi ya shirika la serikali au serikali ilioyogatuliwa.

**Kutoa pesa kutoka kwa Hazina ya Pamoja**

**250.** (1) Pesa hazitaweza kutolewa kutoka kwa Hazina ya Pamoja isipokuwa—
(a) Kusaidia kulipia matumizi kama inavyoelezwa katika Katiba hii ama sheria ya Bunge; ama
(b) wakati kutolewa kwa pesa hizo kumeidhinishwa na sheria ya matozo ama Sheria ya Ziada bungeni.
(2) Pesa haziwezi kutolewa kutoka kwa Hazina yoyote ya serikali ya taifa isipokuwa Hazina ya Pamoja, isipokuwa kama suala la pesa hizo limeidhinishwa na sheria ya Bunge
(3) Pesa haziwezi kutolewa kutka kwa Hazina ya Pamoja au Hazina yoyote ya Umma ya serikali ya taifa isipokuwa Mkurugenzi wa Bajeti ameidhinisha kutolewa kwa pesa hizo kulingana na kifungu 264(4).

**Hazina ya Mapato ya serikali zilizogatuliwa**

**251.** (1) Kutakuwepo na Hazina ya Mapato kwa kila serikali iliyogatuliwa, ambamo kutalipwa pesa ambazo zimelipwa ama zimepokelewa na serikali iliyogatuliwa, isipokuwa pesa ambazo zimetengwa na sheria ya Bunge.
(2) Pesa zinaweza kutolewa kutoka kwa Hazina ya Mapato ya serikali iliyogatuliwa—
(a) Kwa kuonyesha matumizi kwa sheria ya serikali iliyogatuliwa; au
(b) Pesa zinazotolewa moja kwa moja kwa mfuko wa Hazina ya Mapato jambo ambalo limeshughulikiwa na sheria ya Bunge au sheria ya serikali iliyogatuliwa.

**Hazina ya Dharura**

**252.** (1) Kumeundwa Hazina ya Dharura, ambayo itaendeshwa kwa kufuata na sheria ya Bunge.
(2) Bunge litatoa nafasi kwa Waziri, kwa wakati huu, anayehusika na Fedha, akama waziri anatosheka kuwa kumetokea jambo la dharura ambalo halikuwa limepangiwa na hivyo kuhitaji matumizi ya pesa, ambapo hakuna mpango wowote upo, kuelekeza Hazina hiyo ili kukidhi mahitaji hayo.
(3) Ambapo pesa zinatolewa kutoka kwa Hazina ya Dharura, bajeti ndogo ambayo itawasilishwa na sheria ya ziada ya matozo itawasilishwa haraka iwezekanavyo ili kurudisha zile pesa ambazo zilitolewa.

**Sehemu 4- Kukopa**

**Ukopaji wa Serikali**

**253.** (1) Serikali inaweza kukopa kutoka popote .
(2) Serikali ya kitaifa, kwa niaba yake au ya shirika lingine lolote la serikali, mamlaka, au mtu binafsi, haitachukua mkopo, kudhamini mkopo au kupokea msaada, ila tu mashrti na kanuni za shuguli hiyo zimebainishwa kabla , kuidhinishwa kwa uamuzi wa , kila Bunge.
(3) pesa zote ambazo zinapatikana kutokana na shughuli zinazorejelewa katika ibara (2), zitalipwa kwa , na kuwa sehemu moja ya hazina ya pamoja, au hazina nyingine za serikali ambazo zipo au zianzishwe kwa kusudi la shughuli hii.
(4) Katika muda siku saba, baada mojawapo wa Mbunge , kwa uamuzi, itaomba, Waziri wa fedha atawasilisha kwa Bunge zote mbili habari yoyote kuhusu mkopo ambao unastahili kuonyeshwa-
(a) kiasi cha jumla ya deni kwa njia ya mtaji na jumla ya riba;
(b) matumizi ya pesa zilizotokana na mkopo;
(c) mipango ya kulipa mkopo; na
(d) mafanikio katika ulipaji wa mkopo;
(5) kwa kusudi la Kipegele hiki, ' mkopo' unahusisha pesa zilizokopeshwa au kupewa serikali ya kitaifa kwa mashrti ya kurudisha au ya kulipa au aina yoyote nyingine ya kukopa na kukopeshwa kwa kuzingatia ni pesa zipi kutoka kwa hazina ya pamoja au fedha zozote nyingine ambazo zitatumika au kuhitajika kwa matumizi ya kulipa na kulipia madeni .

**Mikopo ya serikali zilizogatuliwa**

**254.** (1) serikali iliyogatuliwa inaweza kuchukua mikopo ya maendeleo ya matumizi ya kawaida iwapo tu ni kulingana na masharti yanayobainishwa na sheria za Bunge.
(2) Serikali iliyogatuliwa haitachukua mkopo bila kwanza kupata idhini kutoka kwa Bunge lake.

**Deni la serikali**

**255.** (1) Kutegemea ibara (2), deni linalodaiwa Jamhuri ni dai kwa Hazina Kuu.
(2) Kipengele cha sheria kinaweza kuundwa kupitia sheria ya Bunge cha Kuruhusu deni lote au sehemu ya deni la umma linalodaiwa Jamhuri kulipwa kwa kutumia hazina nyingine za serikali.
(3) Kwa kusudi la kipengele hiki, deni la serikali linakuwa ni pamoja na fidia ya deni, malipo ya deni hilo, malipo ya gharama na gharama zinazotokea kwa ghafla katika kusimamia deni na udhamini wa serikali uliopo.
(4) Kukopa kwa jumla katika mwaka wowote wa fedha kwa serikali zote mbili, serikali ya kitaifa na serikali iliyogatuliwa kutadhibitiwa na Sheria ya Bunge.

**Mkopo iliyodhaminiwa na serikali**

**256.** (1) Sheria ya Bunge itatoa kanuni na masharti ambayo kila serikali itafuata katika kudhamini mkopo.
(2) Miezi miwili baada ya kumalizika kwa kila mwaka wa fedha, kila serikali itachapisha ripoti kuhusu dhamani ambazo imetoa katika mwaka huo.

**Sehemu 5- Bajeti**

**Yaliyomo**

**257.** Bajeti ya serikali ya taifa na serikali zilizogatuliwa itakuwa na –
(a) makadirio ya mapato na matumizi yakitofautsha kati ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo;
(b) mapendekezo kwa ufadhili wa upungufu unaonuiwa kwa kipindi kinachohusika;
(c) mapendekezo yanayohusu mikopo na na aina zingina za madeni madeni ya kitaifa ambayo yataongeza deni la taifa katika mwaka unaofuatia; na

**Makadirio ya Taifa ya kila mwaka**

**258.** (1) Kwa tare aisio zaidi ya miezi miwili kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha Waziri anayehusika na fedha atawasilisha kwa Bunge-
(a) Makadirio ya mapato na matumizi ya serikali ya kitaifa ya mwaka wa fedha unaofuata; na
(b) Ripoti ya Mpango ulioelezwa kwa undani hazina ya fedha ya kitaifa, masuala ya fedha na maendeleo kwa kipindi cha angalau miaka mitatu (au kwa urefu wa kipindi kama unavyopendekezwa na Sheria za Bunge) uliotayarishwa na Waziri anayehusika na fedha kwa kushirikiana na Wazari anayehusika na mipango na maendeleo ya taifa.

(2) Waziri anayehusika na mambo ya fedha ataweka kwenye makadirio ya kila mwaka kipegele maalum cha bajeti kitakachoruhusu mgao maalum kwa sehumu zilizotengwa, jamii zilizotengwa na makundi yaliyotengwa.
(3) anglau miaka mitatu kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha, kiongozi wa kila idara inayojitathmini, shirika la serikli, tume au mashirika yaliyoanzishwa kulingana na Katiba hii, yatatoa makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya mwaka unaofuta kwa Waziri anayehusika na fedha.
(4) makadiro yaliyotayariswha katika ibara (3) yatawasiliashwa kwa Bunge na Waziri anayahusika na fedha bila kurekebishwa lakini ikiwa na mapendekezo yoyote ambayo Tume ya Kugawa Mapato inaweza kuwa nayo.
(5) wakati wowote kabla ya Bunge kuamua kuhusua makadario ya mapato na matumizi yaliyowasilishwa Bungeni na Waziri mwenyewe au yule aliyemwidhinisha, kamati inayofaa ya Bunge itajadili na kuchunguza makadirio hayo na kutoa mapendekezo yanayofaa kwa Benge.
(6) Kamati inayorejelewa katika ibara (5), katika kujadilina na kuchunguza makadirio, itapata maoni kutoka kwa umma na Baraza la Kiuchumi na Kijamii, na mapendekezo hayo yatatiliwa maanani wakati kamati hii itakapokuwa ikiwasilisha mapendekezo yake kwa Bunge.

**Miswada ya kugawa mapato na matumizi fedha**

**259.** (1) Katika kila mwaka wa fedha, Waziri wa fedha atapeleka Bungeni sehemu ya Mswada wa mapato kutokana na mapendekezo ya Tume ya Kugawa Mapato akigawa mapato kutoka kwa serikali ya taifa miongoni mwa viwango vitatu vya serikali .
(2) Kwa misingi ya mswada wa kugawa mapato uliopitishwa Bungeni kulingana na ibara (1) kila serikali iliyogatuliwa itaandaa na kupitisha Miswada na matumizi yake.
(3) wakati makadirio ya matumizi ya serikali ya kitaifa, tofauti na matumizi yanayotolewa kwa hazina ya fedha ya pamoja na kwa idhini ya Katiba au ya sheria ya Bunge au imekubalishwa na Bunge, yatawekwa kwa mswada , kujulikana kama mswada wa matumizi ambao utawawasilishwa Bungeni kuwakilisha suala kutoka kwa Hazina ya pamoja ya pesa zinazohitajika kwa matumizi hayo na kugawa pesa hizo kwa kusudi linalobainishwa katika mwsada huu.
(4) iwapo, kwa kuzingatia mwaka wa fedha-
(a) kiasi cha pesa kilichotengwa kwa sababu yoyote katika sheria ya matumishi ya fedha hakishi au mahitaji matumizi kutokea kwakusudi ambalo hakuna pesa zilikuwa zimetengwa na sheria ; au
(b) pesa amabazo zimetumiwa kutoka kwa akaunti ya dharura kwa kusudi ambalo halikuwa limtengewa pesa zozote na sheria hiyo, Makadirio ya ziada yakionyesha pea zinazohitajika au zilizotumika yatawasilishwa Bungeni na kukiwa na matumizi zaidi katika miezi mine baada mara ya kwaza ya kutolewa pesa.
(5) idadi ya pesa inayohitajika katika makadirio ya ziada kwa kusudi la kwamba zilizokua zimetolewa hazikutosha haitazidi asilimia kumi ya pesa ambazo zilikuwa zimetolewa awali na Bunge kwa kusudi la mwaka huo wa fedha, lakini Bunge linweza kwa hali maalum, kuidhinisha kutolewa kwa kiwango cha juu.
(6) Pale ambapo, kulingana na mwaka wowote wa fedha ,makadirio ya ziada yameidhinishwa na Bunge, kuambatana na ibara (2), Mswada wa kugawa fedha utawasilishwa Bungeni katika mwaka unaofuta wa fedha ambao unahusiana na makadirio haya yakionyesha idadi ya pesa zlizoidhinishwa kwa sababu zinazobainishwa katika makadilio hayo.
(7) Kivungu 258(5) kinatumika katika makadirio yaliyotengenezwa kulingana na ibara (4).
(8) iwapomswada wa kugawa mapato wa mwaka wa fedha haujaidhinishwa , au hakuna uwezekanao wakuidhinishwa katika mwanzo wa mwaka huo wa fedha, kwa kupiga kura,Bunge linaweza kukubalisha kutolewa kwa pes kutoka kwa hazina ya pamoja.
(9) pesa zinazotolewa kulingana na ibara (8)-
(a) hazitazidi nusu ya idadi iliyo katika makadirio ya matumizi hayo ambayo yamewasilishwa Bungeni;
(b) kwa kusudi la kutimiza matumizi yanayohitajika kutoa huduma za serikali ya kitaifa katika mwaka hua hadi wakati ue mwsada huo wa kugawa umeidhinishwa na Rais ;
(c) ziwekwe chini ya sehemu tofauti za matumizi kwa ajili ya huduma nyingi kulingana kusudi la kuzitoa kwa akaunti hiyo, katika mswada sheria ya kugawa mapato.

**Bajeti ya kila mwaka ya serikali zilizogatuliwa**

**260.** Sheria ya Bunge itaidhinisha-
(a) muundo ya mipango na bajeti ya serikali zo zilizogatiliwa;
(b) yaliyomo katika mipanago na Bajeti ya serikali zote zilizogatiliwa yatahusu asili ya mapato, na vile matumizi yaliyopendekezwa itazingatia mipango na makadario ya kitaifa;
(c) wakati mipango na bajeti za serikali zilizogatiuiwa itawasilishwa;
(d) umbo na namna ya kushauriana kati ya serikali ya kitaifa na serikali zilizogatuliwa katika taratibu za kutayarisha mipango na bajeti.

**Semu 6- Usimamizi wa fedha**

**Ununuzi wa bidhaa na huduma za umma**

**261.** (1) Wakati Shirika la serikali au shirika lolote la umma katika kiwango chochote cha serikali inatoa kadarasi ya bidhaa nahuduma, itafanya hivyo kwa kuzingatia taratibu ambazo ni za haki, usawa uwazi , ushindani na kwa gharama inayofaa.
(2) Sheria ya Bunge itatoa taratibu katika sera zinazohusu ununuzi na uuzaji wa mali utakavyotekelezwa na utahusika kwa zote au mojawapo wa zifuatazo-
(a) aina mbalimbaliza za mapendeleo katika utoaji wa kadarasi;
(b) kuwalinda au kuwapa nafasi watu binafsi au aina ya vikundi vya watu ambao hapo awali waliathiriwa na ushindani usio wa haki au kubaguliwa;

(c) kuwawekea vikwazo walio na kandarasi ambazo hazijafanywa kulingana na makubalianao ya kandarasi, taratibu zinazothibitiwa kitaaluma, au kwa sheria ; na
(d) kuwawekea vikwazo wale ambao wamekosa kutekeleza wajibu wao wa kulipa ushuru au wemapatikana na hatia ya ufisadi au ukiukaji mkubwa wa kanuni na sheria za uajiri.

**Akaunti na ukaguzi wa hesabu za fedha katika mashirika ya umma**

**262.** (1) Katibu mkuu aliye na mamlaka katika wizara na na ofisa ya kuhifadhi akaunti za pesa katika idara au shirika la umma, wana wajibu kwa Bunge kuhusiana na fedha katika Wizara au idara au shirika la umma.
(2) Akaunti zozote za sarikali na taifa zitakaguliwa na Mkurugenzi mkuu wa hesabu za serikali;
(3) Akaunti za ofisi ya Mthibiti Bajeti na za Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali zitakaguliwa na ripoti kutolewa na mhasibu aliyehitimu na aliyechaguiwa na Bunge
(4) Iwapo, akiwa katika ofisi ya umma, ikiwa ni pamoja na ofisi za kisiasa,mtu anaelekeza na kuidhinisha matumizi ya fedha kinyume na sheria kanuni au maagizo,mtu huyo anahusika na kupotea hasara yoyote kutokana na matumizi na anawajibika kulipia hasara hiyo ikiwa ataendelea kuwa ofinisi au la.
(5) Sheria ya Bunge itatoa kanuni za kuhifadhi rekodi za ukaguzi wa akaunti za maendeleo ya Serikali ambazo zimeidhinishwa na kueleza hatua nyingine za kuhifadhi ufanisi, uwazi na usimamizi wa fedha za serikali.

**Udhibiti wa hazina**

**263** (1) Sheria ya bunge itabainisha taasisi ya serikali ya taifa ambayo itajulikana kama hazina na kubuni taratibu za kuhakikisha uwazi na udhibiti wa matumizi katika kila kiwango cha serikali.
(2) kwa kukubaliana na waziri wa fedha, inaweza kusimamisha uhamishaji wa fedha kwa taasisi ya taifa ama shirika lingine la umma kwa kufanya kosa baya, ama kurudia kosa hilo mara kadhaa, katika taratibu zilizowekwa kulingana na ibara cha (1)
(3) Uamuzi wa kusimamisha uhamishaji wa fedha uliochukuliwa kulingana na ibara ya (2) huenda usisimamishe kuhamishwa kwa zaidi ya asilimia hamsini ya fedha zilizotengewa maendeleo yoyote ya serikali.
(4) Uamuzi wa kusimamisha kuhamishwa kwa fedha uliochukuliwa kulingana na ibara ya (2)
a) hakutasimamisha uhamishaji wa fedha kwa zaidi ya siku sitini; na
b) kunaweza kuanza kutekelezwa mara moja, lakini kutasitishwa pole pole, isipokuwa katika siku thelathini baada ya siku ya uamuzi Bunge liidhinishe kwa uamuzi uliopitishwa ba bunge zote mbili.
(5) Bunge linaweza kuanisha tena uamuzi kusimamisha uhamishaji wa fedha kwa muda wa siku zaidi ya siku sitini kwa wakati mmoja.
(6) Kabla ya bunge kuidhinisha kuanisha tena uamuzi wa kusimamisha uhamishaji wa fedha-
a) Mdhibiti wa bajeti atawasilisha ripoti kwa bunge; na
b) serikali gatuliwa inayoathiriwa, taasisi ya serikali au shirika la umma litafahamishwa kuhusu kosa na kupewa nafasi ya kujitetea dhidi ya madai hayo, na kueleza msimamo wake kwa kamati ya bunge inayohusika.

**Mdhibiti Bajeti**

**264.** (1) Kutakuwa na mdhibiti bajeti ambaye atateuliwa na Rais wa taifa kwa idhini ya bunge.
(2) Kuteuliwa kama mdhibiti bajeti mtu atakuwa –
a) mhasibu aliyetaalamika kwa miaka isiyopungua kumi na aliye na tajriba katika usimamizi wa fedha za umma; na
b) mtu mwaminifu na mwadilifu
3) Mdhibiti bajeti atakuwa mamlakani kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena, iwapo atafaulu, kwa kipindi kingine kimoja cha mwisho.
4) Mdhibiti bajeti atasimamia utekelezaji wa bajeti kama ilivyoidhinishwa na viwango vya serikali kwa-
a) Kuhakikisha kwamba pesa zinatumika kulingana mgao ama ikiwa pesa zimetolewa kwa hazina dharura kwa mujibu wa sheria ya bunge kama inavyoelezwa katika kifungu 252;
b) Kutoa mahesabu yenyewe, badala ya bajeti iliyotayarishwa; na
c) Kufanya kazi kwa karibu na hazina, Idara na Wizara.
5) Katika kipindi cha miezi miwili, baada ya kumalizika kwa kila mwaka wa kifedha, mdhibiti bajeti atawasilisha kwa Bunge ripoti kuhusu shughuli za ofisi ya Mdhibiti Bajeti katika mwaka huo wa kifedha.
6) katika kipindi cha miezi mitatu, baada ya kuwasilisha ripoti kulinaga na ibara ya (5) Bunge litajadili na kuitathmini ripoti na kuchukua hatua inayofaa.
7) Katika kutekeleza majukumu ya ofisi, Mdhibiti Bajeti hataelekezwa au kudhibitiwa na mtu au mamlaka yoyote.
8) Mshahara na marupurupu ya Mdhibiti Bajeti yatatolewa kwa Hazina ya Pamoja.

**Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

**265.** (1) Kutakuwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye atateuliwa na Rais wa Taifa na kuidhinishwa na Bunge.
(2) Ili kuteuliwa kama Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mtu atakuwa-
a) mhasibu aliyetaalamika kwa miaka isiyopungua kumi na aliye na tajriba katika usimamizi wa fedha za umma; ukaguzi na usimamizi wa fedha za umma; na
b) mtu mwaminifu na mwadilifu

(3) Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali mamlakani kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena, iwapo atafaulu, kwa kipindi kingine kimoja cha mwisho.
(4) Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali-
a) Atakagua akaunti za serikali ya taifa na serikali iliyogatuliwa na mashirika ya serikali.
b) Kudhibitisha kwamba mgao wa pesa zote uliotolewa na Bunge au zilizotolewa na kiwago chochote cha serikali na kutolewa zimetumiwa kwa lengo lililokusudiwa, na kwamba matumizi yatalingana na mamlaka inayosimamia na kuwa utumiaji pesa ulikuwa wa njia inayofaa na sawa; na
c) Katika kipindi cha miezi sita baada ya kumalizika kwa mwaka wa kifedha kukagua na kuripoti kwa mujibu wa mwaka huo wa fedha kuhusu-
(i) akaunti za umma za kitaifa na za viwango serikali zilizogatuliwa
ii) akaunti zote za hazina na mamlaka za serikali za kitaifa na viwango mbali mbali vya serikali iliyogatuliwa.
iii) Akaunti za mahakama
iv) akaunti za kila tume iliyobuniwa na Katiba hii na kamishna wa vyama vya kisiasa.
v) akaunti za bunge na Seneti
vi) akaunti za vyama vya kisiasa vinavyopata msaada kutoka kwa fedha za umma.
vii) Kaunti za mashirika mengine yanayopata msaada kutoka fedha za umma; na
viii) deni la umma
(5) katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kuwasilishwa kwa ripoti kwa mujibu wa ibara (4) (c) Bunge litajadili, na kutathmini ripoti hizi na kuchukua hatua zinazofaa.
(6) Sheria ya Bunge itatoa mwongozo kuhusu uwekaji wa rekodi na kukagua akaunti za serikali iliyogatuliwa na kueleza hatua nyingine kufikia usimamizi wa fedha ulio wazi na unaofaa.
(7) katika kutekeleza majukumu ya ofisi, mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hataelekezwa au kudhibitiwa na mtu au mamlaka yoyote.
(8) Mshahara na marupurupu ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali utatoka kwa Hazina ya Pamoja.

**Sehemu ya 7- Taasisi**

**Mamlaka ya Kitaifa ya Ushuru**

**266.** (1)Kunaundwa Mamlaka ya Kitaifa ya Ushuru.
(2) Mamlaka yatajumuisha atu wafuatao walioteuliwa na rais wa taifa-
a) mwenyekiti
b) Mteuliwa mmoja kutoka kila baraza la eneo.
c) watu wawili wanaowakilisha serikali za mitaa waliochaguliwa kwa mujibu wa sheria ya Bunge.
d) Watu wawili walioteuliwa na Bunge.

e ) Katibu Mkuu wa Wizara ya; na
f) Mdhibiti Bajeti

3) Jukumu kuu la Tume ni kuamua msingi wa kuwa na mapato kutoka kwa raslimali za kitaifa na kuhakikisha kwamba-
a) Ugawaji huo ni sawa kati ya serikali ya kitaifa na viwango tofauti za serikali iliyogatuliwa.
b) Ugawaji huo ni sawa kati ya viwango tofauti vya serikali iliyogatuliwa katika kiwango chochote; na
c) Panapofaa, misaada inatolea, yenye masharti na isiyo na masharti.
4) Tume-
a) Itaripoti kwa viwango vyote vya serikali mapendekezo yake kuhusu kugawanya mapato ya kitaifa
b) Kila mara kuchunguza upya mapendkezo kama haya ili kuhakikisha yanaambatana na hali zinazobadilika; na
c) Kuingilia katia na kusuluhisha mizozo kuhusiana na mipango ya kifedha kati ya serikali ya kitaifa na serikali iliyogatuliwa.
5) Katika mapendekezo yake, Tume italenga kufafanua na kuwezesha njia za upataji wa mtaji kwa serikali katika viwango vyote ikiwa na lengo la kuhimiza uwajibikaji wa kifedha na kuelekeza serikali zilizogatuliwa kwenye kujisimamia na kutoa mapendekezo kuhusu usaidizi wowote.
6) Katika mapendekezo yake kuhusu kusambaza mapato ya kitaifa, Tume itatilia maanani vigezo viliyoelezwa katika kifungu 248(3)
7) Mapendekezo ya Tume yanaweza kubadilishwa na serikali ya kitaifa kwa kuidhinishwa na Bunge zote mbili iwapo vigezo vilivyowekwa katika ifungu 248 ()3) vitafuatwa.
(8) Sheria ya Bunge itatoa taratibu za utendakazi wa Tume na kufafanua muundo ambamo sera inayorejelewa katika ibara (4) inaweza kutekelezwa.
(9) Tume ina majkumu mengine kama ilivyopewa na sheria ya Bunge.
(10) Katika kutekeleza majukumu yake Tume itazingatia kanuni, vigezo, fomula, hali, misingi yenye kuhakikisha usawa wa ugawanaji na ugawaji wa mapato ya kitaifa na raslimali kama ilivyoelezewa kwenye sheria ya Bunge.
(11) Bila kupitisha tarehe 31 Januari ila mwaka, Tume itatayarisha ripoti kulingana na mahitaji yanayoelezwa na sheria ya Bunge ikieleza mapendekezo kuhusu ugawanaji wa mapato ya kitaifa kwa viwango mbalimbali vya serikali na kuwasilisha ripoti hiyo kwa Bunge kuidhinishwa
(12) Mapendekezo ya Tume kama yalivyo yalivyorekebishwa katika ibara (7) ni ya kimakubaliano kwa serikali zote na itaonyeshwa katika bajeti zao na utozaji ushuru na sera zao za kisheria.

**Tume ya Ugawanaji Mapato**

**267** (1) Kumeundwa Tume ya Ugawanaji Mapato.
(2) Tume itajumuisha watu wafuatao watakaoteuliwa na Rais wa Taifa-
a) Mwenyekiti
b) Mteuliwa mmoja wa kila baraza la eneo
(c)Watu wawili kuwakilisha serikali za wilaya, wateuliwe kulingana na sheria ya Bunge
(d) Wateuliwa wawili wa Bunge;
(e) Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na Fedha; Na
(f) Mkurugenzi wa Bajeti
(3) Wajibu muhimu wa Tume ni kuamua msingi wa kugawana mapato kutoka kwa raslimali za kitaifa na kuhakikisha-
(a)Kugawana ni sawa kati ya serikali ya kitaifa na viwango mbali mbali vya serikali zilizogatuliwa;
b) Kugawana ni sawa kati ya viwango mbali mbali vya serikali zilizogatuliwa katika kila ngazi; na
c) Inapohitajika, kwa masharti au bila masharti, ruzuku zitatolewa.
(4) Tume-
a) Ittoa ripoti kwa viwango vyote vya serikali mapendekezo yake kuhusiana na kugawanywa kwa mapato ya kitaifa.
b) Kupitia mapendekezo hayo kila mara kuhakikisha kuwa yanahusishwa na hali iliyoko.
c) Ingilia kati na kutatua mizozo kuhusiana na mipango ya kifedha kati ya serikali ya kitaifa na serikali zilizogatuliwa.
(5)Katika mapendekezo yake, Kamati italenga kufafanua na kuwezesha vyanzo vya mapato ya serikali katika viwango vyote kwa lengo la kuhimiza matumizi mazuri ya pesa na kuwezesha , kwa muda, serikali zilizogatuliwa kuwa na uhuru wa kifedha na kupendekeza hatua za kuchukuliwa.
(6) Katika mapendekezo yake, kuhusuugawanaji wa mapato, Tume itazingatia vigezo vilivyoelezwa katika Ibara 248 (3)
(7) Mapendekezo ya Tume yanaweza kufanyiwa marekebisho na serikali ya kitaifa kwa makubaliano ya Bunge zote mbili ikiwa kuwa kanuni zilizwekwa katika ibara 248 (3) zinaheshimiwa.
(8) Sheria ya Bunge itatoa taratibu na shughuli za Tume na kueleza mfumo ambamo sera inayorejelewa katika kifungu ( 4) inaweza kutekelezwa.
(9) Tume ina majukumu mengine kama inavyopewa na sheria ya Bunge.
(10) Katika kutekeleza wajibu wake, Tume itaheshimu vipengele , hali, matakwa na vizigatio vingine vyenye kuhakikisha ugawanaji sawa na utoaji wa mapato ya taifa na raslimali kama inavyoelezwa na sheria ya Bunge.
(11) Isipite Januari kila mwaka, Tume itatayarisha ripoti, kulingana na mahitaji ya sheria ya Bunge, ikieleza mapendelezo yake kuhusu ugawanaji wa mapato kwa viwango mbali mbali na kutoa ripoti kwa Bunge ili kuidhinishwa.
(12) Mapendekezo ya Tume, kama ilivyorekebishwa katika kifungu (7) ni mapatano kwa serikali zote, na yataonyeshwa katika bajeti zao na katika utozaji ushuru wao na sera nyingine za sheria.

**Tume ya Mishahara na Marupurupu**

**268.** (1) Kuna Tume buniwa ya Mishahara na Marupurupu.
(2) Tume ya Mishahara na Marupurupu inajumuisha-
a) Mwenyekiti
b) Mwanasheria Mkuu ama mwakilishi wake.
c) Mtu mmoja aliyeteuliwa na Hazina Kuu kutoka kwa idara hiyo.
d) Mtu mmoja aliyeteuliwa na Tume ya Utumishi wa Umma.
e) Mtu moja aliyeteuliwa na Tume ya Huduma za Bunge na asiwe mbunge au mwanachama wa Tume ya Huduma za Bunge
f) Mtu moja aliyeteuliwa na Tume ya Huduma za Mahakama na asiwe mwanachama wa idara ya mahakama au mwanachama wa Tume ya Huduma za Mahakama.
g) Mtu mmoja anayewakilisha mashirika ya kitaaluma
h) Mtu mmoja muungano wa waajiri.
i) Mtu moja kutoka kwa muungano wa vyama vya wafanyikazi; na
j) Watu watano walioteuliwa kwa mujibu wa kifungu 297
3. Majukumu ya Tume ya Mishara na Marupurupu ni-
a) Kuunda na kudurusu mishahara na marupurupu ya wafanyikazi wote wa taifa na maafisa wa umma; na
b) Kusawazisha mishahara na marupurupu wa maafisa wote wa taifa na maafisa wa umma pamoja na maafisa wa serikali zilizogatuliwa na wafanyikazi wa mashirika ya umma.

**Benki Kuu ya Kenya**

**269.** (1) Kuna Benki kuu ya Kenya buniwa.
(2) Benki Kuu ya Kenya ndiyo pekeke iliyo na mamlaka ya kutoa sarafu za Kenya
3) Mamlaka ya Benki kuu ya Kenya yamo kwenye bodi ambayo inajumuisha mwenyekiti, Gavana, NAIBU Gavana na watu wengine wasiozidi wane.
(4) Kwa mujibu wa ibara (6) wanachama wa bodi-
a) watateuliwa na Rais wa taifa na kuidhinishwa na Bunge; na
b) Kuwa mamlakani kwa mipindi kimoja cha miaka mitano na kuweza kuteuliwa tena, ikiwezekana, ikiwa watafaa, kwa kipindi kingine kimoja cha mwisho.
(5) Kuteuliwa kama Gavana ama Naibu Gavana mtu atakuwa elimu pana na ujuzi wa kutosha kuhusu masuala ya uchumi, fedha, na uhasibu na awe mtu mwadilifu na mwenye tabia njema.
(6) Gavana atashikilia mamlaka kwa kipindi cha miaka sita na hatateuliwa tena.
(7) Msingi na taratibu za kumwondoa mwanachama wa Bodi imeelezewa katika kifungu 298.

**Majukumu ya Benki Kuu**

**270** (1) Benki Kuu ya Kenya-
(a)kukuza na kudumisha thamani ya sarafu ya Kenya.
(b) kutoa noti na sarafu mpya
(c) kutekeleza wajibu kama benki na kuwa mshauri wa kifedha
(d) Kutekeleza sera za kifedha za serikali kwa njia thabiti na kwa kuzingatia vipengele vinavyofaa katika sheria kwa manufaa ya uchumi ulio sawa na unaodumisha maendeleo ya Jamhuri.
(e) Kuhimiza na kukuza maendeleo ya kiuchumi na matumizi yanayofaa ya raslimali za Jamhuri, kupitia kwa taratibu za mikopo ya banki na utendaji unaofaa na ulio na ufanisi;na
(f) Kutekeleza majukumu yale yote yale yasiofuatana na Kifungu hiki

kama inavyoalezwa hapa chini.
(2) Banki kuu ya Kenya haitaelekezwa na mtu yeyote au mamlaka yoyote katika kutekeleza mamlaka na majukumu yake.
(3) noti na sarafu zinazotolewa na Benki Kuu la Kenya zinaweza kuwa na michoro inayoonyesha Kenya au hali yake lakini haitakuwa na picha ya mtu binafsi.

**Baraza la Kichumi na Kijamii**

**271.** (1) Kumeundwa Baraza la Kiuchumi na Kijamii ambalo linajumuisha watu tisa wanaoteuliwa katika misingi ya uwezo lakini kwa kuzingatia tofauti kati ya jamii za Kenya, kwa Rais wa Taifa akitekeleza kwa niaba ya Baraza la Mawaziri na kudhibitishwa na Bunge.
(2) Watu wateuliwao kwa Baraza —
(a) wawe wamefuzu na wana ujuzi katika masuala ya kiuchumi na walio na masomo katika uchumi na maendeleo ya kijamii; na
(b) wasiwe na mapendeleo yoyote pindi tu wameteuliwa kwa baraza;.
(3) Majukumu ya Baraza ni —
(a) kushauri serikali ya taifa na Bunge katika masuala ya kiuchumi na kijamii ambayo yana umuhimu kwa taifa;
(b) kushauri serikali ya taifa kuhusu uundaji,usimamiaji, utekelezaji na udurusu wa sera muhimu za kiuchumi na kijamii;
(c) kutathmini na kuripoti kwa Bunge kuhusu athari za miswaada na mapendekezo ya bajeti yaliyowasilishwa Bungeni; na
(d) Kufuatilia maendeleo katika kuboreshwa kwa hali ya maisha ya raia wa Kenya, hasa maisha ya maskini na wanyonge.
(4) Baraza litatekeleza majukumu mengine kama litakavyopewa na sheria ya bunge
(5) Kulingana na bara hii, Bunge litaunda sheria —
(a) Kuratubu jinsi Baraza linavyotekeleza majukumu yake; na
(b) kufafanua kuhusu aina ya ripoti, yaliyomo na jinsi ya kutoa ripoti kwa Baraza.

## SURA YA KUMI NA SITA

**UTUMISHI WA UMMA**

**Sehemu 1 – Utumishi wa Umma**

**Thamani na kanuni za huduma kwa umma**

**272.** (1) Thamani na kanuni za huduma wa umma ni pamoja na –
(a) kudumisha na kukuza viwango vya juu ya maadili ya kitaaluma;
(b) kukuza matumizi bora ya raslimali;
(c) kutoa huduma kwa njia ya haki, usawa na bila mapendeleo;
(d)kuwahimiza watu kushiriki kwenye utaratibu wa kubuni sera;
(e) kuitikia matakwa na mahitaji ya watu haraka na kwa wakati unaofaa;
(f) kujitolea katika utekelezaji wa sera na mipango ya kitaifa;
(g) uwajibikaji katika makosa yanayofanyika katika shughuli za kiusimamizi.
(h) kukuza uwazi katika kutoa habari za kweli na kwa wakati ufaao kwa umma;
(i) kuzingatia aya (k), watu watateuliwa kufanya kazi kwa kuzingatia uwezo, maarifa na ujuzi wao katika kufanya kazi hiyo.
(j) watu binafsi, wake kwa waume pamoja na makundi kutoka jamii mbalimbali kuteuliwa, kupewa mafunzo ya kujiendeleza; na
(k) uwakilishi wa jamii mbalimbali, wake kwa waume, watu wa makabila tofauti na watu na makundi yaliyotengwa,wakiwemo watu wenye ulemavu kwenye huduma kwa umma katika viwango vyote.

(2) Thamani na kanuni za utumishi wa umma zinatumika katika –
(a) kila kiwango cha serikali;
(b) matawi yote ya serikali; na
(c) miradi yote ya serikali
(3) Bunge kwa kutumia sheria litatoa mwongozo wa kanuni za nidhamu kwa maafisa wote wa serilali.

**Tume ya Utumishi wa Umma**

**273.** (1) Kuna Tume buniwa ya Utumishi wa Umma.
(2) Kutakuwa na katibu wa Tume ambaye atakuwa Afisa Mkuu wa Tume.
(3) Katibu wa Tume atakuwa –
(a) atateuliwa na Rais wa Taifa kufuatia pendekezo la Tume ya Utumishi wa Umma na kuidhinishwa na Bunge; na
(b) atahudumu kwa muda wa miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha mwisho cha miaka mitano.

**Mamlaka na Majukumu**

**274.** (1) Mamlaka na majukumu ya Tume ni -
(a) isipokuwa pale ambapo kuna kifungu kinachokiuka Katiba hii au sheria yoyote, kubuni au kuvunjilia mbali ofisi za utumishi wa umma;
(b) isipokuwa pale ambapo kuna kifungu kinachokiuka Katiba hii, au sheria yoyote, kuteua watu kuhudumu au kushikilia ofisi kwa muda katika idara ya utumishi wa umma, kuidhinisha uteuzi na kudhibiti nidhamu na kuwaondoa watu wanaohudumu au kushikilia afisi hizo.
(c) Kukuza thamani na kanuni zilizotajwa katika Kifungu 13 katika idara nzima ya utumishi wa umma;
(d) kudadisi na kuchunguza na kutathmini usimamizi wa shirika na mienendo ya wafanyakazi katika idara ya utumishi wa umma;
(e) kuhakikisha utendajikazi bora katika kuhudumia umma;
(f) kuhakikisha kwamba utaratibu unaohusu uajiri, uhamisho , kupandishwa vyeo na hatua za kinidhamu zinazingatia thamani na kanuni zilizotajwa kwenye Vifungu 13 na 272;
(g) kuchunguza upya mishahara na mazingira ya utendaji kazi, sheria za kazi na hatua za kinidhamu za maafisa wa umma na kukuza nguvu kazi katika idara ya utumishi wa umma na kutoa mapendekezo kuhusu masuala hayo kwa serikali ya kitaifa;
(h) kutoa ripoti kuhusu shughuli na utendakazi wake kulingana na Kifungu 2004;
(i) kutathmini na kuripoti kwa Rais na Bunge kuhusu kiwango ambacho thamani na kanuni zilizofafafuliwa katika Vifungu 13 na 272 vinazingatiwa;
(j) kusikiza na kuamua rufani kuhusu masuala yanayohusiana na huduma kwa umma kutoka kwa serikali zilizogatuliwa; na
(k) kutekeleza majukumu mengine kama inavyoidhinishwa na Katiba hii au Sheria ya Bunge.
(2) Tume inaweza, kulingana na masharti inayoyafafanua, kwa maandishi kugawa yoyote ya mamlaka na majukumu yake chini ya Kifungu hiki kwa mmoja au zaidi ya wanachama wake, au afisa yeyote, taasisi au halmashauri katika idara ya utumishi wa umma.
(3) Ibara (1) haitatekelezwa katika ofisi zozote zifuatazo za utumishi wa umma
(a) ofisi za Serikali;
(b) ofisi ya Balozi au mwakilishi yeyote mkuu wa Serikali katika nchi nyingine;
(c) ofisi ambapo Vifungu 154; 210 (1), 277 au 293 vinarejelea
(d) ofisi katika serikali iliyogatuliwa; na
(e) isipokuwa katika rufaa zinazorejelewa na ibara (1) (g), ofisi yoyote inayohudumu katika serikali iliyogatuliwa.
(4) Mtu atateuliwa chini ya ibara (1) kuhudumu katika ofisi yoyote kama mfanyakazi katika Ofisi ya Rais au rais wa Kitaifa Aliyestaafu, isipokuwa kwa idhini ya Rais wa Kitaifa au Rais wa Kitaifa Aliyestaafu.
(5) Bunge litatunga sheria kuimarisha utendaji kazi wa Tume.

**Kuajiri Wafanyakazi wa Serikali zilizogatuliwa**

**275.** Serikali ya eneo au wilaya inahusika na uajiri, uteuzi, kupandisha madaraka,uhamisho na ufutaji kazi wa wafanyakazi katika utumishi wa umma katika mipaka na utaratibu wake na viwango vinavyofafanuliwa na Sheria ya Bunge.

**Kuwalinda maafisa wa serikali**

**276.** Afisa wa serikali –
(a) Hataonewa au kubaguliwa kwa kutekeleza majukumu ya kiofisi kulingana na Katiba au sheria yoyote nyingine; au
(b)kufutwa au kuondolewa ofisini au kushushwa cheo au kuadhibiwa bila sheria kufuatwa.

**Sehemu 2 – Tume ya Kuwaajiri Walimu**

**Tume ya Kuwaajiri Walimu**

**277.** (1) Kuna Tume buniwa ya Kuwaajiri Walimu
(2) Majukumu ya Tume ya Kuwaajiri Walimu yatakuwa –
(a) kusajili walimu waliopewa mafunzo; na
(b) licha ya Kifungu 275
(i) kuteua na kuajiri walimu waliosajiliwa;

(ii) kuwapa kazi walimu walioajiriwa na Tume kuhudumu katika shule yoyote ya umma na taasisi nyingine.
(iii) kuwapandisha vyeo na kuwahamisha walimu;
(iv) kuwaadhibu na kuwadhibiti walimu;
(v) kuwafuta kazi walimu; na
(vi) kutekeleza majukumu mengine yaliyopewa Tume na Sheria ya Bunge.
(3) Tume itachunguza viwango vya elimu na mafunzo kwa watu wanaojiunga na taaluma ya ualimu na kutoa walimu na itashauri serikali ya kitaifa kuhusu masuala yanayohusiana na taaluma ya ualimu.

**Sehemu 3 – Huduma ya Marekebisho ya Kenya**

**Kubuniwa na kudhibitiwa.**
**278.** (1) Kuna Huduma ya Marekebisho ya Kenya iliyobuniwa katika utumishi wa umma.
(2) Malengo ya Huduma ya Marekebisho ya Kenya ni kuhakikisha –
(a) kwamba wafungwa katika magereza nchini wamehifadhiwa salama na kwamba taasisi hizo zina mazingira yanayofaa binadamu kuishi kulingana na Katiba na sheria;
(b) kuwasimamia wahalifu katika jamii ambao wanahudumu vifungo vya nje au ambao wanachunguzwa; na
(c) kuwarekebisha wahalifu ili kuwaandaa kurudi na kuishi maisha yenye manufaa katika jamii.

(3) Huduma ya Marekebisho ya Kenya itakuwa na muundo na kudhibitiwa ili iweze –
(a) kufikia viwango vya juu vya kitaaluma na nidhamu miongoni mwa wanachama wake na kupitia kwa wanachama hao katika kutekeleza mamlaka yake;
(b) kukuza uwajibikaji na kuzuia ufisadi;
(c ) kuzingatia viwango vya haki za binadamu katika kutekeleza mamlaka yake na utendakazi wa majukumu yake; na
(d) kutoa mafunzo kwa wanachama wake kufikia viwango vya juu vya uwezo wao na kuhusiana na matumizi machache ya mabavu na kuwa na uadilifu na kuheshimu haki za binadamu , uhuru wa kimsingi na heshima ya binadamu.
(4) Huduma ya Marekebisho ya Kenya itaandaliwa kuhusisha muundo wa ugatuzi.
(5) Bunge litatunga sheria -
(a) kubuni miundo ya kutosha kuwezesha utawala unaozingatia uwazi katika Huduma ya Marekebisho ya Kenya;
(b) kuruhusu mpango, usimamizi na utendakazi wa Huduma ya Marekebisho ya Kenya; na
(c) kwa jumla kudhibiti Huduma ya Marekebisho ya Kenya.

**Mkurugenzi Mkuu**
**279.** (1) Kuna ofisi buniwa ya Mkurugenzi –Mkuu wa Huduma ya Marekebisho ya Kenya.
(2) Mkurugenzi – Mkuu atateuliwa na Rais wa Kitaifa, kwa ushauri wa Tume ya Utumishi wa umma na baada ya kuidhinishwa na Bunge.
(3) Mtu atateuliwa kuwa Mkurugenzi- Mkuu iwapo mtu huyo ana sifa zifaazo kitaaluma na –
(a) amehudumu katika Huduma ya Marekebisho ya Kenya kwa angalau miaka kumi; au
(b) ana uzoefu mpana katika usimamizi na utendajikazi kuhusu huduma za marekebisho.
(4) Mkurugenzi-Mkuu atahudumu kwa muhula wa miaka mitano na ataweza kuteuliwa kwa kipindi kingine cha mwisho cha miaka mitano.
(5) Kifungu 297 (3) kuhusiana na sifa za kuajiriwa zinazohitajika na Tume zitazingatiwa katika kumwajiri Mkurugenzi-Mkuu.

## SURA YA KUMI NA SABA

**Sehemu 1- Taasisi za Usalama wa Taifa**

**Kanuni na misimamo**
**280.** (1) Usalama wa Taifa ni ulinzi wa mipaka ya Kenya, watu wake, mali yao,haki na uhuru, na maslahi mengine ya kitaifa dhidi ya vitisho vya ndani na nje.
(2) Usalama wa taifa la Kenya utaimarishwa na kuhakikishwa kulingana na kanuni zifuatazo –
(a) usalama wa taifa unaongozwa na mamlaka ya Katiba hii na Bunge;
(b) Usalama wa taifa utatekelezwa kwa kuzingatia sheria, ikiwemo sheria ya kimataifa, na kwa kuheshimu kikamilifu utawala wa kisheria, demokrasia, haki za binadamu na uhuru wa kimsingi;
(c) taasisi za usalama wa kitaifa zitaheshimu tamaduni mbalimbali za jamii nchini Kenya katika kutekeleza majukumu yake; na
(d) uajiri katika taasisi za usalama wa taifa utaakisi mseto wa watu wa Kenya katika viwango sawa.

**Taasisi za usalama wa taifa**
**281.** (1) Taasisi za usalama wa taifa ni -
(a) Vikosi vya Ulinzi wa Kenya;
(b) Huduma za Taifa za Upelelezi; na
(c) Huduma ya Polisi wa Kenya.
(2) Lengo la kimsingi la taasisi za usalama wa taifa na mfumo wa usalama ni kulinda maslahi ya watu wa Kenya na mali yao na haki na uhuru, na mamlaka , amani, umoja wa kitaifa na mipaka ya Kenya.
(3) Katika utekelezaji wa majukumu yao, taasisi za usalama wa taifa na kila, mwanachama wa taasisi hizo hataruhusiwa -
(a) kuwa na upendeleo kwa njia yoyote,
(b) kuendeleza maslahi ya chama chochote cha kisiasa wala sera zake;
(c) kuhujumu maslahi ya kisiasa au mpango wa kisiasa ambao ni halali chini ya Katiba hii; au
(d) kutii amri yoyote isiyokuwa halali.
(4) Mtu hataruhusiwa kubuni shirika linalohusiana na usalama wa taifa au shirika wa kijeshi isipokuwa inavyoruhusiwa na Katiba hii au Sheria ya Bunge.
(5) Taasisi za uslama wa taifa zitakuwa chini ya mamlaka ya raia.
(6) Bunge litatunga sheria kuruhusu kushughulikia majukumu, utaratibu na usimamizi wa taasisi za usalama wa taifa.

**Kubuniwa kwa Baraza la Usalama wa Taifa**
**282.** (1) Kuna Baraza buniwa la Usalama wa Taifa lenye –
(a) rais wa taifa
(b) Naibu Rais wa taifa;
(c) Waziri Mkuu,
(d) Waziri anayehusika na ulinzi;
(e) Waziri anayehusika na mashauri ya kigeni;
(f) Waziri anayehusika na usalama wa taifa;
(g) Mwanasheria Mkuu
(h) Mkuu wa Majeshi ya Kenya;
(i) Mkurugenzi –Mkuu wa Huduma ya Kitaifa ya Upelelezi; na
(j) Inspekta-Mkuu wa Huduma ya Polisi ya Kenya.

**Majukumu ya Baraza la Usalama wa Taifa**
**283.** (1) Baraza la Usalama wa Taifa –
(a) Litaunganisha sera za humu nchini, za kigeni na za kijeshi kuhusiana na usalama wa kitaifa ili kuwezesha taasisi za usalama wa taifa kushirikiana kikamilifu;
(b) kutathmini na kuchunguza malengo, kujitolea ,na hatari kwa Taifa kuhusiana na usalama wa nchi; na
(c) kuanzisha sera kuhusu masuala ya maslahi ya pamoja ya kiusalama ya taasisi za kiusalama na kudhibiti taasisi hizo.
(2) Baraza la Usalama wa Taifa litatoa ripoti kwa Bunge kila mwaka kuhusiana na hali ya usalama nchini Kenya.
(3) Baraza la Usalama wa Taifa linaweza kwa idhini ya Bunge –
(a)kupeleka wanajeshi nje ya Kenya kwa minajili ya –
(i)kutekeleza majukumu ya Umoja wa Mataifa ya kudumisha amani pamoja na majukumu mengine; au
(ii) kuidhinisha wanajeshi wa kigeni kutumwa Kenya.

**Sehemu 2 - Majeshi ya Ulinzi wa Kenya**

**Kubuniwa kwa Vikosi vya Ulinzi wa Kenya na Baraza la Ulinzi**
**284.** (1) Kuna vikosi buniwa vya Ulinzi wa Kenya vinavyohusisha –
(a) Kenya Army;
(b) Kenya Air Force; na
(c) Kenya Navy.
(2) Mtu hatabuni kikosi cha majeshi au kundi lenye hadhi ya kijeshi isipokuwa inavyoruhusiwa katika Katiba hii.
(3) Kuna Baraza la Ulinzi lililobuniwa linalohusisha –
(a) Waziri anayehusika na ulinzi ambaye atakuwa mwenyekiti;
(b)Naibu Waziri anayehusika na ulinzi ambaye atakuwa naibu mwenyekiti;
(c )Mkuu wa Majeshi ya Kenya;

(d) Kamanda wa Jeshi;
(e) Kamanda wa Air Force;
(f) Kamanda wa Navy; na
(g) Katibu Mkuu katika Wizara inayohusika na ulinzi.
4)Baraza la Ulinzi litamteua Katibu wake.
(5) Baraza la Ulinzi litahusika na sera nzima, kudhibiti, na kusimamia Vikosi vya Ulinzi vya Kenya pamoja na majukumu mengine kulingana na jinsi Bunge litakavyopitisha.

**Uongozi**
**285.** (1) Rais wa Taifa, baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi, atateua Mkuu wa Majeshi, Kamanda wa Majeshi, Kamanda wa Air Force na Kamanda wa Navy.
(2) Uongozi wa Majeshi ya Ulinzi wa Kenya utaakisi tofauti za kimaeneo na za watu wa jamii mbalimbali nchini.
(3) Kuzingatia mamlaka ya uongozi wa Rais wa Taifa kama Kamanda Mkuu, Vikosi vya Ulinzi na makamanda wa huduma watatoa amri kwa vikosi vya Ulinzi wa Kenya na kutekeleza majukumu mengine kisheria kulingana na sheria ya Bunge .

**Sehemu 3 – Huduma za Taifa za Upelelezi**

**Kubuniwa kwa Huduma za Taifa za Upelelezi**
**286.** (1) Kuna taasisi buniwa ya Huduma za Taifa za Upelelezi .
(2) taasisi ya Huduma za Taifa za Upelelezi itahusika na shughuli za kiupelelezi kuhusu usalama ili kuimarisha usalama wa taifa, na kulinda Katiba hii, maslahi ya Taifa na ya watu wa Kenya, na itatekeleza majukumu mengine kulingana na Sheria ya Bunge.
(3) Huduma ya upelelezi, tofauti na Huduma za Taifa za Upelelezi, ambayo ni tawi la Majeshi wa Ulinzi la Kenya au Huduma ya Polisi ya Kenya haitabuniwa isipokuwa kwa njia ya sheria.

**Mkurugenzi –Mkuu wa Huduma**
**287.** (1) Kuna ofisi buniwa ya Baraza la Kitaifa la Upelelezi linalohusisha –
(a) Waziri anayewajibika na masuala yanayohusiana na upepelezi wa kitaifa, ambaye atakuwa mwenyekiti;
(b) Waziri anayehusika na mashauri ya kigeni;
(c) Waziri anayehusika na masuala ya fedha; na
(d) Mwanasheria Mkuu
(2) Mkurugenzi-Mkuu wa Huduma za Taifa za Upelelezi atakuwa katibu wa Baraza la Kitaifa la Upelelezi.
(3) Majukumu ya Baraza la Taifa la Upelelezi yatakuwa ni-
(a) kushauri Huduma Taifa za Upelelezi katika masuala yote yanayohusiana na -
(i) usalama wa kitaifa na sera kuhusu usalama;
(ii) usimamizi wa Huduma; na
(iii) matumizi ya fedha na Huduma; na
(b) kutekeleza majukumu mengine kama yanavyotolewa na Baraza kulingana na sheria.

**Baraza la Kitaifa la Ujasusi .**
**288.** (1) Kumeundwa Baraza la Kitaifa la Ujasusi linalojumuisha —
(a) Waziri anayehusika na masuala yanayohusiana na upelelezi wa taifa, ambaye atakuwa mwenyekiti;
(b)Waziri anayehusika na masuala ya nchi za Kigeni
(c) Waziri wa Fedha; na
(d) Mwanasheria Mkuu.
(2) Mkurugenzi Mkuu wa Huduma ya Upelelezi atakuwa katibu wa Baraza la Kitaifa la Upalalazi.
(3) Majukumu ya Baraza la Kitaifa la Upelelezi—
(a) shauri Huduma ya Kitaifa ya Upelelezi kuhusu mambo yote yanayohusiana na—
(i) Usalama wa kitaifa na sera za upelezi ;
(ii) Usimamizi wa Huduma ; na
(iii) Matumizi ya pesa katika Huduma; na
(b) Tekeleza majukumu mengine kama yatakavyotolewa kwa Baraza na sheria.

**Sehemu 4 – Huduma ya Polisi ya Kenya**

**Kuundwa kwa Huduma ya Polisi ya Kenya**
**289.** (1) Kuna Huduma ya Polisi ya Kenya iliyobuniwa -
(2) Huduma ya Polisi ya Kenya ni huduma ya kitaifa ya polisi, na ugavi wa majukumu yake utafanywa kwa njia itakayozingatia muundo wa serikali ya Kenya iliyogatuliwa.
(3)Bunge litatunga sheria kupitisha Kifungu hiki.

**Malengo na Majukumu**
**290.** (1) Huduma ya Polisi ya Kenya ita-
(a) jitahidi kufikia viwango vya juu vya kitaaluma na nidhamu miongoni mwa wafanyakazi wake; na
(b) zuia ufisadi na kukuza uwazi;
(c) zingatia kanuni zilizotajwa katika Kifungu 280 ( 2);
(d) zingatia viwango vya haki za binadamu;
(e) fundisha wafanyakazi wake kufikia viwango vya juu zaidi ya uwezo na maadili na kuheshimu haki za binadamu na uhuru na heshima za kimsingi;
(f) zingatia kanuni za uwazi na uwajibikaji; na
(g) kimu na kukuza mahusiano na jamii pana.

(2) Huduma ya Polisi ya Kenya itafanya kazi kwa karibu na jamii kuhakikisha –
(a) kudumishwa kwa sheria na mpango;
(b) mazingira salama na yenye amani;
(c) kulindwa kwa haki za binadamu na uhuru wa kimsingi;
(d) usalama kwa watu;
(e) imezuia na kugundua uhalifu;
(f) kuwatunza waathiriwa wa uhalifu na ghasia;
(g) imelinda maisha na mali;
(h) imechunguza uhalifu na makosa; na
(i) imetekeleza sheria ambazo imepewa jukumu la kufanya hiyo;

**Uteuzi na ufutaji kazi wa Inspekta-Mkuu**
**291.** (1) Kuna ofisi buniwa ya Inspekta Mkuu wa Huduma ya Polisi ya Kenya.
(2) Kwa ushauri wa Baraza la Mawaziri, na idhini ya Bunge, Rais wa Taifa atamteua Inspekta-Mkuu wa Huduma ya Polisi ya Kenya.
(3) Inspekta- Mkuu atahudumu wadhifa huo kwa kipindi kimoja cha miaka sita na hatateuliwa tena kwa kipindi cha pili.
(4) Inspekta-Mkuu anaweza kuondolewa mamlakani na Rais wa Taifa pekee kwa –
(a) kushindwa kutekeleza majukumu yake ambayo yanaweza kusababishwa na
ulemavu wa akili au mwili;
(b) utovu wa nidhamu ama akiwa mamlakani au vinginevyo;
(c ) kutojiweza kazini;
(d) sababu nyingine nzuri;
(e) kufilisika;au
(f) kukiuka kanuzi za Sura ya Tisa.
(5) Inspekta-Mkuu hataondolewa kwenye wadhifa huo isipokuwa kupitia kwa pendekezo la jopo litakaloteuliwa na Rais wa Taifa litakalohusisha –
a) jaji wa Mahakama Kuu,ambaye atakuwa mwenyekiti;
b) mwenyekiti wa Tume ya Huduma ya Polisi;na
c) mtu mwingine mmoja mwenye maadili ambaye amewahi kuhudumia umma kwa ufanisi .
(6) Licha ya ibara (5), Rais wa Kitaifa, kwa ushauri wa Baraza la Mawaziri, anaweza kumsimamisha kazi
Inspekta-Mkuu ambaye anaangaziwa katika utaratibu wa ibara (5).
(7)Rais wa Kitaifa, kwa kuzingatia ushauri wa Baraza la Mawaziri anaweza kumteua kaimu Inspekta-Mkuu pale ambapo Inspekta-Mkuu anaachishwa kazi chini ya ibara (6)

**Majukumu na uhuru wa Inspekta -Mkuu**
**292.** (1) Inspekta-Mkuu atatumia mamlaka ya Huduma ya Polisi ya Kenya na kutekeleza majukumu mengine ambayo Bunge linaweza kupendekeza kisheria.
(2) Inspekta- Mkuu atatekeleza majukumu ya kazi yake katika ofisi hiyo kwa njia huru, kulingana na Katiba na sheria na bila woga, upendeleo wala chuki.
(3) Waziri anayehusika na usalama wa taifa anaweza kutoa mwelekeo kisheria kwa Inspekta-Mkuu kuhusu suala lolote la sera kuhusu Huduma ya Polisi ya Kenya; lakini hakuna mtu yeyote anayeweza kutoa maagizo kwa Inspekta-Mkuu kuhusiana na –
(a) uchunguzi wa kosa fulani kosa au makosa fulani mahususi;
(b) kutekeleza sheria dhidi ya mtu au watu fulani mahususi; au
(c) kuajiri, kutoa kazi, kupandisha cheo, kusimamisha au kufuta kazi kwa mfanyakazi yeyote wa Huduma ya Polisi ya Kenya.

(4) Agizo lolote linalotolewa kwa Inspekta-Mkuu na Waziri anayehusika na na usalama wa taifa chini ya ibara (3) itakuwa kwa maandishi na litawasilishwa Bungeni katika muda wa siku thelathini.
(5) Ibara (3) haidunishi mamlaka ya kisheria ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma katika kumwagiza Inspekta Mkuu wa Huduma ya Polisi ya Kenya kuchunguza habari au madai yoyote ya mienendo ya kiuhalifu.

**Tume ya Huduma ya Polisi**

**293.** (1) Kuna Tume ya Huduma ya Polisi buniwa -
(2) Tume ya Huduma ya Polisi itakuwa na –
a) mtu ambaye amehitimu kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu anayeteuliwa na Rais wa Taifa;
b) maafisa wawili wa polisi wa ngazi ya juu waliostaafu watakaoteuliwa na Rais wa Taifa; na
c) watu watatu wenye maadili mema ambao wamewahi kuhudumu serikalini kwa ufanisi mkuu watakaoteuliwa na Rais wa Taifa;na
d) Inspekta-Mkuu wa Huduma ya Polisi ya Kenya.
(3) Rais wa Taifa atamteua mwenyekiti kutoka miongoni mwa wanachama watakaoteuliwa chini ya ibara (2) (a), (b), au (c).
(4) Tume ya Huduma ya Polisi itamteua katibu wake.
(5) Majukumu ya Tume ya Huduma ya Polisi ni, kuhusiana na Huduma ya Polisi, na huduma iliyobuniwa chini ya Ibara 294 ni –
(a) kuajiri na kuteua watu kuhudumu katika ofisi za taasisi hiyo, kuidhinisha uteuzi, kubaini wanaopaswa kupandishwa vyeo na kudhibiti nidhamu na kuwaondoa watu wanaohudumu katika afisa hizo au wanaoshikilia nyadhifa kwa muda katika ofisi hizo.
(b) kushughulikia masuala yote yanayohusiana na viwango au sifa za wafanyakazi wa Huduma zinazohitajika;
(c) Kushughulikia masuala yote yanayohusiana na mishahara, marurpurupu na masharti mengine ya huduma ya wafanyakazi wa Huduma;
(d) kutekeleza majukumu mengine yanayoidhinishwa na Katiba hii au Sheria ya Bunge.
(6) Tume ya Huduma ya Polisi inaweza, kwa maagizo ya kimaandishi na kuambatana na masharti kama yanavyoelezwa na Sheria ya Bunge, kutoa mamlaka yanayotokana na Katiba hii,au Sheria ya Bunge kwa afisa yeyote wa serikali au taasisi ya umma.

**Sehemu 5 –Huduma Nyingine za Polisi**

**Huduma nyingine za polisi**

**294.** (1) Bunge linaweza kubuni huduma nyingine za polisi endapo itakuwa muhimu kufanyahivyo.
(2) Maelezo ya Kifungu 290(1) yanatumika kwa huduma ya polisi inayobuniwa chini ya Ibara hii.

## SURA YA KUMI NA NANE

**TUME NA OFISI HURU**

**Utekelezezaji wa Sura**

**295.** (1) Sura hii inahusu Tume zote zilizotajwa katika ibara (2) na ofisi huru zilizotajwa katika ibara (3) Isipokuwa pale ambapo maelezo mahususi yametajwa kinyume na kwingineko katikaKatiba hii.
(2) Tume hizo ni-
a) Tume ya Ugavi wa Ushuru;
b) Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi;
c) Tume ya Haki za Binadamu na Masuala ya Jinsia;
d) Tume Huru Ya Uchaguzi na na Mipaka ya Maeneobunge;
e) Tume ya Huduma za Mahakama;
f) Tume ya Taifa ya Ardhi;
g) Tume ya Utumishi wa umma;
h) Tume ya Huduma ya Polisi;
i) Tume ya Mishahara;
j) Tume ya Kuwaajiri Walimu; na
k) Tume ya Utekelezaji wa Katiba
(3) Ofisi huru ni pamoja na –
(a) Mkaguzi – Mkuu wa Mahesabu ya Pesa za Serikali
(b) Kamishna wa Vyama Vya Kisiasa; na
(c) Mdhibiti wa Bajeti

**Malengo ya Tume na ofisi huru**

**296.** (1) Malengo ya Tume na ofisi huru ni –
(a) kulinda mamlaka ya watu;
(b) kuhakikisha kwamba matawi yote ya Serikali yanazingatia thamani na kanuni za demokrasia
(c ) kuhakikisha kwamba katiba inadumishwa, kwa kulinda shughuli muhimu za kidemokrasia dhidi ya ushawishi usiofaa, kubadilishwa au kuingiliwa.
(2) Tume na wafanyakazi katika ofisi huru –
(a) watazingatia Katiba hii pekee pamoja na sheria;
(b) wako huru na hawawezi kuelekezwa au kudhibitiwa na mtu yeyote au halmashauri; na
(c) hawatakuwa na upendeleo wowote na watatekeleza majukumu yao bila woga, upendeleo wala chuki.

**Uteuzi na masharti ya ofisi**

**297.** (1) Kila Tume itakuwa na angalau wafanyakazi watatu na sio zaidi ya tisa.
(2) Isipokuwa vinginevyo inavyofafanuliwa katika Katiba hii, mfanyakazi katika ofisi huru na kila mwanachama katika Tume ata-
(a) tambuliwa na kupendekezwa kwa minajili ya kuteuliwa kulingana na utaratibu uliotolewa na Sheria ya Bunge;
(b) idhinishwa na Seneti;
(c) idhinishwa na Rais wa Taifa.
(3) Ili kuteuliwa, mtu atahitaji kuwa na sifa mahususi zinazohitajika kwenye Katiba hii au Sheria ya Bunge.
(4) Kuteuliwa kuhudumu katika Tume na ofisi huru kutazingatia kanuni katika Kifungu 13(2)(i)-(k).
(5) Mwanachama wa Tume anaweza kuwa mfanyakazi wa muda.
(6) Mfanyakazi katika ofisi huru au mwanachama wa tume hatalaumiwa wala kuchukuliwa hatua kwa chochote atakachofanya kwa nia njema katika utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo.
(7) Wanachama wa Tume watamchagua mwenyekiti kutoka miongoni mwao
(a)kwenye kikao cha kwanza cha Tume; na
(b) kila inapokuwa muhimu kujaza pengo.

**Kuondolewa kutoka ofisini**

**298.** (1) Mfanyakazi katika ofisi huru au mwanachama wa Tume anaweza kuondolewa kutoka kwenye wadhifa wao kwa sababu –
(a) ya kushindwa kutekeleza majukumu yao kutokana na ulemavu wa kiakili au kimwili;
(b) ya utovu wa nidhamu ama katika utendajikazi wa mfanyakazi au vinginevyo;
(c) kufilisika;
(d) kutojiweza kazini
(e) kukuika Sura ya Tisa.

(2) Mtu anayeazimia kuondolewa kwa mtu kwa misingi yoyote iliyotajwa katika ibara (1) anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Seneti kwa kuwasilishwa idhibati za madai hayo.
(3) Bunge litachunguza malalamiko hayo na , iwapo litaridhika kwamba yana mashiko chini ya ibara (1), litatuma malalamiko hayo kwa Rais wa Taifa.
(4) Pindi tu baada ya kupokea malalamiko hayo chini ya ibara (3),Rais wa Taifa
(a) anaweza kumsimamisha kazi mtu husika kusubiri matokeo ya uchunguzi wa malalamiko hayo; na
(b) atabuni jopo kulingana na ibara (5).
(5) Jopo hilo litakuwa na –
(a)mtu ambaye anahudumu, au amewahi kuhudumu katika ofisi ya Serikali kama jaji wa mahakama yenye mamlaka kuu, ambaye atakuwa mwenyekiti;
(b) angalau watu wawili ambao wana sifa za kuteuliwa kama majaji wa Mahakama Kuu; na
(c) mwanachama mwingine mmoja ambaye ana uwezo wa kuangalia ushahidi kuhusiana na msingi mahususi wa kumtaka ofisa huyo aondolewe.
(6) Jopo hilo litachunguza suala hilo, na kutoa ripoti ya ukweli na kutoa mapendekezo kwa Rais wa Taifa, ambaye atachukua hatua kulingana na mapendekezo hayo katika kipindi cha siku thelathini.
(7) Mtu atakayesimamishwa kazi chini ya Kifungu hiki ana haki ya kuendelea kupokea mshahara na marurpurupu ya ofisi akiwa amesimamishwa kazi.

**Mamlaka ya jumla**

**299.** (1) Kamishna na mfanyakazi katika ofisi huru –

(a) wanaweza kufanya uchunguzi kwa hiari zao au kufuatia mamalamiko yaliyotolewa na mwananchi;
(b) ana mamalaka ya Mahakama Kuu –
(i) kutoa samansi;
(ii) kuwashinikiza mashahidi kutoa ushahidi au kuwasilisha stakabadhi kwa madhumuni ya uchunguzi wake; na
(iii) kumpeleka mtu katika Mahakama Kuu kwa kukaidi amri ya mahakama;
(c) ana mamlaka muhimu ya kupatanisha ;
(d) kulingana na uhuru uliotolewa na sheria,anaweza kutoza faini au kutaka mtu afidiwe; na
(e) wataajiri wafanya kazi wao.
(2) Malalamiko kwa Tume au mfanyakazi katika ofisi huru yanaweza kuwasilishwa na mtu yayote mwenye haki ya kufanya hivyo chini ya Vifungu 31 (1) na (2) –
(a) katika maandishi, huku misingi ya malalamiko hayo na ushahidi kutolewa;au
(b) kimdomo, ambapo malalamiko hayo yatanakiliwa kimaandishi na kutiwa saini na ofisa wa Tume au ofisi huru.
(3) Tume au afisa katika ofisi huru anaweza, pamoja na majukumu aliyopewa na Katiba hii, kutenda majukumu mengine jinsi Bunge linaweza kuidhinisha kisheria.

**Majukumu ya jumla**
**300.** Tume na ofisi huru zitaelimisha umma kuhusu nia, nafasi na majukumu yao.

**Utendaji wa Tume na ofisi huru**
**301.** (1) Tume inaweza, kulingana na Katiba hii au Sheria ya Bunge, kudhibiti utaratibu wake.
(2) Utendaji wa Tume hautabatilishwa kwa sababu ya pekee ya pengo katika uanachama wake.

**Ushirikishwaji**
**302.** Tume na ofisi huru ni asasi shirikishi na –
(1) ina msusuru wa urithi na mhuri wa pamoja; na
(2) ina uwezo wa kushtaki na kushtakiwa katika jina lake la kiushirika.

**Fedha za Tume na ofisi Huru**
**303.** (1) Fedha za Tume na ofisi huru ni pamoja na –
(a) fedha zinazotengwa na bunge kwa minajili ya utenda kazi wao; na
(b) fedha nyingine zozote zinazopokewa katika utekelezaji wa majukumu yao.
(2) Bunge litatenga fedha za kutosha kuiwezesha kila Tume na ofisi huru kutekeleza majukumu yao na bajeti ya kila Tume na ofisi huru itapigiwa kra kivyake.

**Ripoti za kila mwaka na ripoti nyingine**
**304.** (1) Katika miezi saba baada ya kumalizika kwa kipindi cha fedha, kila Tume na kila kiongozi wa afisi huru atawasilisha ripoti kwa Rais wa Taifa na kwa Bunge.
(2) Kila ripoti itakuwa na –
(a) taarifa za utendajikazi wao katika kutimiza malengo yao;
(b) taarifa za shughuli zao katika mwaka na mipango yao katika shughuli za baadaye; na
(c ) Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Mashesabu ya Serikali.
(3) Rais wa Taifa, Seneti na Bunge anaweza, katika wakati wowote, kuhitaji Tume au mtumishi katika ofisi huru kuwasilisha ripoti kuhusu suala fulani mahususi.
(4) Rais wa Taifa atatoa maoni kwa kuandikia Bunge kuhusu ripoti iliyowasilishwa kwa Rais wa Taifa chini ya ibara (1) na kuhusu ripoti yoyote itakayoitishwa na Rais wa Taifa chini ya ibara (3), na Bunge litajadili ripoti hiyo pamoja na maoni ya Rais wa Taifa.
(5) Kila ripoti itachapishwa na kutangazwa.

**Sheria**
**305.** Bunge linaweza, kwa kutunga sheria inayotoa nafasi kwa utendajikazi wa Tume na ofisi huru zinazorejelewa katika Kifungu 295.

## SURA YA KUMI NA TISA

**MAREKEBISHO YA KATIBA**
**Marekebisho ya Katiba**
**306.** (1) Pendekezo la marekebisho ya katiba hii kulingana na –
(a) mamlaka ya Katiba;
(b) mipaka ya Kenya;
(c) mamlaka ya watu;
(d) thamani za kitaifa, kanuni na malengo yaliyoorodheshwa katika Kifungu 13(2);
(e) Sheria ya Haki;
(f) kipindi cha kuhudumu cha Rais wa Taifa;
(g) uhuru wa Idara ya Mahakama na Tume za kikatiba na ofisi huri zinazorejelewa katika Kifungu 295;
(h) majukumu ya Bunge;
(i) malengo na kanuni na muundo wa kimsingi wa ugatuzi;
(j) maelezo katika Sura hii,
Yatatekelezwa kulingana na Kifungu 307 au 308, na kupitishwa na wananchi wengi wanaopiga kura kwenye kura ya maoni inayofanywa kwa lengo hilo.
(2) Matokeo ya kura ya maoni hayana mashiko kwa malengo ya kuidhinishwa kwa pendekezo la marekebisho linalorejelewa katika ibara (1) isipokuwa angalau asilimia 20 ya wapiga kura waliosajiliwa katika kila maeneo mengi wamepiga kura.
(3) Marekebisho ya Katiba hii ambayo hayajatajwa katika ibara (1) yataidhinishwa ama –
(a) na Bunge, kulingana na Kifungu 307; au
(b) na watu na Bunge, kulingana na Kifungu 108.

**Marekebisho yatakapendekezwa na Bunge**
**307.** (1) Mswada wa kurekebisha Katiba hii –
(a) unaweza kuwasilishwa katika mojawapo ya Bunge;
(b) haupaswi kuangazia suala lolote jingine isipokuwa kutokana na mfuatano wa marekebisho ya sheria yanayotokana na Mswada huo;
(c ) haitaitwa kusomwa kwa mara ya pili katika mojawapo ya Bunge, hadi angalau baada ya siku tisini baada ya tarehe ya kusomwa kwa mara ya kwanza katika Bunge hilo; na
(d) utakuwa umeidhinishwa na Bunge wakati kila Mojawapo ya Bunge limepitisha Mswada huo, katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na tatu, na sio chini ya thuluthi mbili za wabunge katika Bunge hilo.
(2) Bunge litatangaza Mswada wowote wa kurekebisha Katiba hii, na kuandaa majadiliano na umma kuhusiana na Mswada huo.
(3) Wakati Bunge litatangaza Mswada wowote wa kurekebisha Katiba Hii, Spika wa Bunge Mbili watawasilisha kwa pamoja kwa Rais wa Taifa –
(a) Mswada, kutiwa saini na kuchapishwa; na
(b) cheti kwamba Mswada huo umepitishwa na Bunge kulingana na Kifungu hiki.
(4) Katika muda wa siku thelathini baada ya Mswada huo kuidhinishwa na Bunge, Rais wa Taifa atautia saini Mswada huo na kuufanya uchapishwe, kulingana na Ibara (5).
(5) Iwapo Mswada wa kurekebisha Katiba hii unapendekeza marekebisho yanayotajwa katika katika Kifungu 306 (1), Rais wa Taifa –
(a) kabla ya kuutia saini Mswada huo, ataiomba Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka kufanya , katika muda wa siku tisini, kufanya kura ya maoni ya kitaifa kuidhinisha Mswada; na
(b) katika muda wa siku thelathini baada ya mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi na Mipaka kumthibitishia Rais wa Taifa kwamba Mswada huo umepitishwa na raia wengi watakaopiga kura ya maoni, kuutia Mswada na kuusababisha uchapishwe.

**Marekebisho yatakayopendekezwa wengi**
**308.** (1) Marekebisho ya Katiba hii yanaweza kupendekezwa na watu wengi watakaokusanya saini za angalau watu milioni moja waliojiandikisha kupiga kura.
(2) Mkondo huu wa marekebisho ya Katiba unaweza kuwa kwa njia ya pendekezo la kijumla au kwa Mswada kielelezo.
(3) Iwapo mkondo huu wa marekebisho ya katiba ni kwa njia ya pendekezo la kijumla, wadhamini wa njia hiyo wataandaa Mswada kielelezo kutokana na mapendekezo yao.
(4) Wadhamini wa marekebisho yanayopendekezwa na wengi watawasilisha kielelezo cha Mswada na sahihi zilizokusanywa kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka, ambayo itahakikisha kwamba mapendekezo hayo yanaungwa mkono na angalau watu milioni moja waliojiandikisha kupiga kura.
(5) Iwapo Tume huru ya Uchaguzi na Mipaka imeridhika kwamba mapendekezo hayo yanatimiza masharti ya Kifungu hiki, Tume itawasilisha Mswada kielelezo kwa kila baraza la wilaya kwa minajili ya kufikiriwa katika kipindi cha muda usiozidi miezi mitatu baada ya tarehe ya kuwasilishwa na Tume ya Uchaguzi na Mipaka.
(6) Wakati baraza la wilaya limekwisha kuidhinisha Mswada kielelezo, Afisa

Mkuu wa wilaya hiyo atawasilisha nakala ya Mswada kielelezo kwa Maspika wawili wa Bunge zote mbili, pamoja na cheti kwamba baraza la wilaya limeupitisha.

(7) Wakati Mswada Kielelezo umeidhinishwa na wengi katika mabaraza ya wilaya, itauwasilisha Bungeni, ambapo kila Bunge litaushughulikia Mswada huo kulingana na Kifungu 307.

(8) Iwapo Bunge litaidhinisha Mswada, utapelekewa Rais wa Taifa kutiwa saini kulingana na Vifungu 307 (4) na (5).

(9) Iwapo mojawapo ya Bunge litashindwa kuupitisha Mswada, Mswada huo utapalekwa kwa watu kwa kura ya maoni.

(10)Matokeo ya kura ya maoni hayatambuliwi kwa malengo ya kuidhinishwa kwa pendekezo la marekebisho linalorejelewa katika ibara (1) ispokuwa –

(a) angalau asilimia ishirini ya watu waliojiandikisha kupiga kura katika maeneo mengi wamepiga kura; na

(b) wengi wa wapiga kura katika zaidi ya nusu ya maeneo wamepiga kura kuunga mkono.

## SURA YA ISHIRINI

### VIPENGELE VYA KIJUMLA

**Utekelezaji wa Vipengee vya Katiba hii**

**309.** (1) Mtu anayerejelewa katika ibara (2) ana haki ya kuwasilisha kesi katika Mahakama ya Kikatiba, akidai kwamba kipengele chochote cha Katiba hii kimekiukwa, kimevunjwa au kutishiwa.

(2) Watu wanaoweza kuwasilisha kesi mahakamani kulingana na ibara (1) ni –

(a) mtu binafsi anayeshughulikia maslahi yake;

(b) mtu anayechukua hatua kwa niaba ya mwingine ambaye hawezi kufanya hivyo yeye binafsi;

(c ) mtu anayechukua hatua hiyo kama mwanachama wa, au kwa maslahi ya, kundi au makundi ya watu;

(d) mtu anayechukua hatua hiyo kwa maslahi ya umma; na

(e) chama kinachochukua hatua hiyo kwa maslahi ya mmoja au zaidi ya wanachama wake.

**Kufasiri Katiba**

**310.** (1) Katiba hii itafasiriwa kwa namna ambayo –

(a) inakuza malengo, thamani na kanuni;

(b) inaendeleza haki za kibinadamu na uhuru wa kimsingi na utawala wa sheria;

(c) inaruhusu maendeleo ya sheria; na

(d) inachangia utawala bora.

(2) Iwapo kuna mkinzano kati ya matoleo ya lugha tofauti ya Katiba hii, fasiri ya lugha ya Kiingereza ndiyo itakayotawala.

(3) Isipokuwa pale ambapo kuna kipengele kinachoeleza kinyume, mamlaka yatakayotolewa ua jukumu litakalopewa Bunge na Katiba hii kubuni, kuruhusu au kutenda jambo lolote au kitu yatatumika au kutekelezwa na Sheria ya Bunge.

(4) Kila kipengele cha Katiba hii kitafasiriwa kulingana na kanuni za ufasiri kwamba sheria kila mara inazungumza, na hivyo basi, miongoni mwa vitu vingine –

(a) mamlaka iliyotolewa au jukumu linaloidhinishwa na Katiba hii inaweza kutumika au kutekelezwa kulingana na mahitaji ya shughuli hiyo, na mtu anayeshikilia ofisi ambayo imepewa mamlaka hiyo au jukumu hilo.

(b) marejeleo yoyote katika Katiba hii au sheria yoyote nyingine kwa mtu anayeshikilia mamlaka ofisini chini ya Katiba hii inahusu marejeleo kwa mtu anayetekeleza majukumu ya ofisi hiyo kisheria katika wakati wowote husika.

(c) marejeleo ya katiba hii au sheria yoyote nyingine kwa ofisi, taasisi ya Serikali au eneo lililotajwa katika Katiba hii itasomwa pamoja na mabadiliko yoyote rasmi muhimu ili kuifanya iweze kutekelezeka katika hali hiyo; na

(d) marejeleo katika Katiba hii kwa ofisi, taasisi au shirika ni marejeleo kwa ofisi hiyo, taasisi au shirika, au ikiwa ofisi hiyo, taasisi au shirika hazipo tena, kwa mrithi wake au ofisi sawa na hiyo, taasisi au shirika.

(5) Katika katiba hii, isipokuwa muktadha uhihitaji vinginevyo –

(a) iwapo neno au maelezo yamefafanuliwa katika Katiba hii, tofauti zozote za kisarufi au matumizi ya neno linalohusiana na jingine, soma pamoja na mabadiliko yanayohitajika na muktadha; na

(b) neno "ikiwemo" linamaanisha "ikiwemo, lakini pasipokuwa na mpaka", na neno "ikiwemo" linamaanisha "ikiwemo, lakini bila mpaka kwa";

(6) Wakati wa kupiha hesabu ya muda baina ya matukio mawili kwa jukumu lolote chini ya Katiba hii, iwapo muda huo umetajwa –

(a) kama siku, siku ambayo tukio la kwanza linatokea haitahusishwa, na siku ambayo tukio la mwisho linaweza kutokea itahusishwa;

(b) kama miezi, muda ambao kipindi hicho kinamalizika mwanzoni mwa siku katika mwezi husika –

(i) ambayo ina nambari sawa kama tarehe ambapo kipindi hicho kilianza, iwapo mwezi huo una tarehe inayolingana ; au

(ii) hiyo ndiyo siku ya mwisho ya mwezi huo; au

(c) kama miaka, kipindi cha muda huo kinamalizika mwanzoni mwa tarehe ya mwaka husika inayolingana na tarehe ambayo kipindi hicho kilianza.

(7) Iwapo muda uliotengwa katika Katiba hii kwa lengo lolote ni siku sita au chini yake, Jumapili na siku kuu za kitaifa hazitahesabiwa wakati wa kuhesabu muda.

(8) Iwapo, katika tukio fulani mahususi, kipindi cha muda kilichotengwa katika Katiba hii kwa shughuli yoyote kinakamilika Jumapili au siki ya kitaifa ya mapumziko, muda huo unaongezwa hadi siku inayofuatia ambayo sio Jumapili au siku kuu ya kitaifa.

(9) Iwapo hakuna muda maalumu uliotengwa kwa utekelezaji wa shughuli fulani inayohitajika, shughuli hiyo itafanywa bila kucheleweshwa, na hasa kulingana na wakati shughuli hiyo inaibuka.

(10) Iwapo mtu yeyote au taasisi ya Serikali ina mamlaka chini ya Katiba hii kuongeza kipindi cha muda unaoruhusiwa katika Katiba hii, isipokuwa nia tofauti inaangaziwa kwa dharura katika kipengele kinachoidhinisha kuanzishwa kwa halmashauri hiyo, inaweza kutumiwa ama kabla au baada ya kumalizika kwa kipindi hicho.

(11) Isipokuwa pale ambapo kuna kipengele kinyume na Katiba hii, pale ambapo mtu ameondoka kwenye ofisi iliyobuniwa na au chini ya Katiba hii, mtu huyo anaweza, iwapo ana sifa zinazohitajika, kuteuliwa tena au vinginevyo kuchaguliwa kuhudumu katika ofisi hiyo kulingana na Katiba hii.

(12) Pale ambapo, mamlaka au majukumu ya mtu chini ya Katiba hii yanaweza kutumiwa tu baada ya mapendekezo, au kuidhinishwa, au baada ya mashauriano na, mtu mwingine, basi mamlaka hayo, isipokuwa nia kinyume itajitokeza, yatatumima tu baada ya mapendekezo au idhini ya au baada ya mashauriano.

**Maelezo**

**311.** Katika Katiba hii, isipokuwa muktadha unahitaji vinginevyo –

"mtu mzima" ina maana ya mtu ambaye amefikisha umri wa miaka kumi na minane

"hatua ya uthibitisho" inahusisha hatua yoyote inayolenga kuondolea mbali ukosefu wa usawa au kumnyima mtu au kuingilia haki za kimsingi;

"rekebisha" inahusisha kubadilisha, kufuta, kubatilisha, kufutilia mbali, kuongeza kwenye kitu kizima au sehemu yake;

"mtoto" ina maana ya mtu ambaye hajatimiza umri wa miaka kumi na minane;

"raia" ina maana ya raia wa Kenya;

"makundi ya kijamii"ina maana ya watu wa jamii waliounganа pamoja, wanaoongozwa na sheria fulani na ambao ni huru kutokana na Serikali;

"Hazina ya Pamoja" ina maana ya hazina iliyobuniwa na Kifungu 249;

"Tume ya Kikatiba" ina maana ya tume iliyobuniwa na Katiba hii;

"ulemavu" inahusisha ulemavu wowote wa mwili, kiakili, kisaikolojia au ulemavu wa aina nyingine, hali au ugonjwa ambao, au unaochukuliwa na jamuu kuwa na athari za muda mrefu kwa uwezo wa mtu katika utekelezaji wa majukumu ya kawaida ya kila siku;

"stakabadhi" inahusisha chapisho lolote au suala lililoandikwa, kuelezwa kwa njia ya barua, nambari, alama, au zaidi ya njia hizo, ambayo inanuiwa kutumiwa au inayoweza kutumiwa kwa lengo la kurekodi suala hilo.

"tarehe ya kuanza kutumika kwa katiba" ina maana ya tarehe ambapo Katiba hii inaanza kutumika;

"kutunga"ina maana ya kutunga sheria ;

"kipindi cha fedha" ina maana ya kipindi cha miezi kumi na miwili kinachomalizika katika siku ya kumi na tatu ya Juni au siku nyingine kulingana na jinsi Bunge litakavyoamua;

"Gazeti" ina maana ya Gazeti Rasmi la Serikali linalochapishwa na mamlaka ya serikali ya kitaifa, au gazeti jingine linalochapishwa pamoja na Gazeti rasmi la Kenya;

"ofisa wa mahakama" ina maana ya mtu anayehudumu kwenye ofisi, au kaimu katika ofisi ya msajili, naibu msajili, hakimu, Kadhi au afisa msimamizi wa mahakama inayobuniwa chini ya Kifungu 208 (1)(d);

"Kenya" ina maana ya eneo la Jamhuri;

"ardhi" inahusisha

(a) eneo juu ya ardhi au chini ya mwamba;

(b) eneo lolote lenye maji au chini ya ardhi;

(c )maji ya bahari katika eneo kwenye mipaka ya nchi;

(d) raslimali asilia zilizopo juu au chini ya ardhi; na

(e) eneo la anga juu ya ardhi;

"utungaji sheria" ina maana ya Sheria ya Bunge, au sheria iliyobuniwa na mamlaka iliyo chini ya Bunge ikiwemo baraza la serikali iliyogatuliwa;

"jamii iliyotengwa" ina maana –

(a) jamii ambayo, kwa sababu ya uchache wa watu wake, au kwa sababu nyingineyo imekuwa haiwezi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijumla za maisha za kijamii na kiuchumi za Kenya.

(b) jamii ya kitamaduni, ambayo kwa sababu ya mahitaji au azimio la kudumisha utamaduni wake wa kipekee na utambulisho ili usimezwe, imebakia nje ya ujumuisho wa maisha ya kujamii na kiuchumi ya Kenya kwa jumla;

(c) jamii asilia ambayo imebakia na kudumisha maisha na mitindo ya kitamaduni inayojikita kwenye uchumi wa shughuli za usasi na ukusanyaji wa matunda; au

(d) wafugaji au jamii za ufugaji , ikiwa ni pamoja na –

(i) kuhamahama; au

(ii) jamii zinazoishi mahala pamoja ambazo, kwa sababu ya kutengwa kijiografia, hazijashirikishwa kikamilifu katika shughuli za kijumla za kijamii na kiuchumi ya Jamhuri;

"kundi lililotengwa" ina maana ya kundi, ambalo, kutokana na sheria au mazoea kabla au baada ya tarehe ya utekelezwaji wa Katiba hii, walikuwa au wamebaguliwa katika mojawapo au zaidi ya misingi isiyoruhusiwa inayotajwa katika Kifungu 37;

"raslimali asilia" ina maana ya –

(a) jua

(b) maji kwenye na chini ya ardhi;

(c) misitu, raslimali za chembechembe asilia, na

(d) miamba, madini, kisukuku,makaa na nyenzo nyingine za kawi.

"mzee katika jamii" ina maana ya mtu mwenye umri wa zaidi ya miaka sitini;

"mtu" inahusisha kampuni, chama au kundi la watu au shirika;

"chama cha kisiasa" ina maana ya muungano wa watu uliobuniwa kwa madhumuni ambayo yametajwa katika Kifungu 114;

"mamlaka" ni pamoja na heshima, usemi mkubwa au busara;

"mali" ni pamoja na –

(a) ardhi au vitu vingine vya kudumu kwenye ardhi;

(b) bidhaa na mali ya kibinafsi;

(c) mali itokanayo na uwezo wa kufikiri; au

(d) fedha.

"afisa wa serikali" ina maana ya mtu yeyeote anayehudumu au kushikilia ofisi au katika serikali ya taifa au serikali iliyogatuliwa au utumishi wa umma, ambaye mshahara wake hulipwa kutokana na Hazina ya Pamoja au moja kwa moja kutokana na fedha zinazotolewa na Bunge;

"utumishi wa umma" ina maana ya watu wote kwa pamoja isipokuwa maafisa wa Serikali, wanaofanya kazi katika taasisi ya Serikali;

"mshahara na marupurupu" unahusisha mishahara, marupurupu na haki zinazohusisha mishahara ya mtu binafsi, ikiwemo pensheni, malipo ya uzeeni au fedha zozote anazopasa kulipwa mtu anapostaafu;

"jamhuru" ina maana ya Jamhuri ya Kenya;

"Taifa" inapotumiwa kama nomino, ina maana ya mseto wa maafisa, taasisi na asasi nyingine zinazobuni serikali ya Jamhuri chini ya Katiba hii;

"ofisi ya Taifa" ina maana ya yoyote kati ya ofisi zifuatazo –

(a) Rais wa Taifa;

(b) Naibu Rais wa Taifa;

(c) Mwanachama wa Baraza la Mawaziri;

(d) Naibu Waziri

(e) Mbunge;

(f) Mwanachama wa Mahakama;

(g) Mwanachama wa Tume ya kikatiba;

(h) Mwanachama wa bunge au kamati maalumu ya serikali iliyogatuliwa;

(i) Mwanasheria-Mkuu;

(j) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma;

(k) Mchunguzi Maalum wa Malalamiko ya Umma;

(l) Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu;

(m) Msimamizi wa Bajeti;

(n) Katibu wa Baraza la Mawaziri;

(o) Mkuu wa Majeshi;

(p) Kamanda wa Majeshi;

(q) Mkurugenzi-Mkuu wa Huduma za Taifa za Upelelezi; na

(r) Inspekta-Mkuu waHuduma ya Polisi ya Taifa.

(s) Mkurugenzi-Mkuu wa Huduma ya Marekebisho.

"ofisa wa Taifa" ina maana ya mtu anayeshikilia ofisi ya Taifa iliyobuniwa na Katiba hii, au iliyobuniwa na kutambuliwa hivyo na sheria;

"taasisi ya Serikali" ina maana ya Tume, ofisi, shirika au asasi nyingine iliyobuniwa katika Katiba hii na yenye jukumu katika Jamhuri;

"sheria ndogo" ina maana ya sheria, udhibiti,kwa sheria, tangazo au sheria nyingine sawa na hiyo inayobuniwa chini ya mamlaka ya kubuniwa kwa sheria;

"Hazina Kuu" ina maana ya taasisi ya Serikali inayorejelewa katika Kifungu 263(1);

"Maandishi" inahusisha kuchapisha, kupiga picha, kupiga taipu, lithografia, na njia yoyote nyingine inayowakilisha au kuzalisha maneno yanayoweza kuonekana, na Breli; na

"vijana" ina maana ya kijumla ya watu wote katika Jamhuri ambao kila mmoja –

(a) ametimiza umri wa miaka kumi na minane; na

(b) hajatimiza umri wa miaka themanini na mitano.

## SURA YA ISHIRINI NA MOJA

### VIPENGELE VYA MUDA NA MATOKEO YA BAADA YA KUANZA KUTUMIKA KWA KATIBA

**Sheria zinazohuasiana na Matokeo**

**312.** (1) Kwenye Katiba hii ambapo Bunge linahitajika kupitisha sheria kuhusiana na jambo Fulani maalum, Bunge litaunda sheria hiyo katika muda ulioelezwa katika Awamu ya Sita, kuanzia siku ya kuanza kutumika kwa katiba hii.

(2) Licha ya ibara (1), Bunge linaweza, kupitia kwa uamuazi ulioungwa mkono na thuluthi mbili ya Wabunge wote, kuongeza muda uliowekwa kuhusiana na kuhusiana na ibara (1), lakini ingawa muda huo usipite mwaka mmoja, kama Bunge litakavyoamua.

( 3) Uwezo wa Bunge kama ulivyoelezwa katika ibara ( 2) unaweza kutumika- Mara moja tu; na

Katika hali maalum ambayo itaidhinishwa na Spika wa Bunge la Taifa.

(4) Kwa sababu ya ibara (1), Mkuu wa Sheria akishauriana na Tume ya Utekelezaji wa Katiba atatayarisha na kuwasilisha Miswaada Bungeni, kwa muda unaofaa, ili kuwezesha Bunge kupitisha sheria katika muda uliowekwa.

(5) Kwenye Katiba hii ambapo Bunge linahitajika kupitisha sheria kusimamia suala fulani katika muda fulani maalum, lakini likashindwa kufanya hivyo, mtu yeyote anaweza kulalamika kwa Mahakama ya Kikatiba kutoa maelezo kuhusiana na jambo hilo.

(6) Mahakama ya Kikatiba ikitoa uamuzi kuhusu malalamiko kama ilivyo katika kifungu cha (4) inaweza-

(a) Kutoa agizo kuhusu jambo hilo; na

(b) Kutoa agizo ikielekeza Bunge na Mkuu wa Sheria kuchukua hatua kuhakikisha kuwa sheria inayohitajika chini ya ibara (1), inatekelezwa, ndani ya muda uliowekwa katika agizo hilo, na kutoa ripoti kuhusu utekelezaji huo kwa Jaji Mkuu.

(7) Iwapo Bunge litashindwa kuunda sheria kulingana na ibara (1) na (2), Mkuu wa Sheria atamshauri Rais wa Nchi kuvunja Bunge na Rais wa nchi ataivunja Bunge.

(8) Iwapo Bunge limevunjwa chini ya ibara (6), Bunge jipya litaunda sheria inayohitajika kulingana na ibara (1) katika muda uliolezwa katika Awamu ya Nne, kuanzia tarehe ya kuanza kwa kipindi cha Bunge jipya.

(9) Katika hali ambapo Bunge jipya litashindwa kuunda sheria kulingana na ibara (7), maelezo ya ibara (1) hadi (7) yatatekelezwa.

**Tume kuhusiana na kutekelezwa kwa Katiba**

**313.** (1) Inaundwa Tume kuhusu Utekelezaji wa Katiba ambayo utajumuisha—

(a) mwenyekiti; na

(b) wanachama wengine wanane.

(2) Jukumu la Tume ni —

(a) kusimamia, kusaidia na kufuatilia maendeleo ya sheria na taratibu za kiusimamizi kama inavyohitajika kikamilifu ili kutekeleza Katiba hii.

(b) panapohitajika, ianzishe sheria inayohitajika ili kutekeleza Katiba hii;

(c) kuripoti mara mbili kwa mwaka kwa Rais wa nchi na Bunge kuhusu—

(i) hatua za maendeleo za utekelezaji wa Katiba hii; na

(ii) matatizo yoyote kuhusu utekelezaji wa Katiba hii katika muda unaofaa; na

(d) kushirikiana na Tume za kikatiba kuhakikisha kuwa azimio la Katiba hii linaheshimiwa.

(3) Tume itavunjwa wakati Katiba hii itatekelezwa kwa ukamilifu kama itakavyoamuliwa na Bunge.

(4) Maelezo ya Sura ya Kumi na Nane yatatumika kwa Tume.

**Wakati wa Mpito**

**314.** Vifungu kuhusu utekelezaji na matokeo yake

Vipengele vya katiba kuhusu utekelezaji wa muda na matokeo yake vinavyoelezwa katika Mpangilio wa Saba vitatekelezwa siku ya kuanza kutekeleza Katiba hii.

**Katiba kuanza kutumika**
**315.** Katiba hii itaanza kutumika  wakati Rais atafahamisha umma kuhusu kutekelezwa kwa sheria mpya.

**Kubatilishwa**
**316.** Katiba inayotumika kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba hii itaachwa mara moja wakati wa kuanza kutumiwa kwa katiba hii.

## MPANGILIO WA KWANZA

**(Kifungu 5(2))**

**MAENEO NA WILAYA**
**Maeneo ambayo Kenya imegawika—**
1. Eneo la Pwani
2. Eneo la Mashariki
3. Eneo la Kaskazini Mashariki
4. Eneo la Bonde la Ufa
5. Eneo la Nyanza
6. Eeno la Magharibi
7. Eneo la Kati Central
8. Eneo la jiji la Nairobi

**Kenya imegawika katika wilaya—**
**Katika Eneo la Pwani —**
1. Kwale
2. Mombasa
3. Taita Taveta
4. Kilifi
5. Lamu
6. Tana River
7. Malindi

**Katika Eneo la Mashariki —**
1. Makueni
2. Machakos
3. Kitui
4. Mwingi
5. Meru Central
6. Meru South
7. Meru North
8. Tharaka
9. Mbeere
10. Embu
11. Isiolo
12. Marsabit
13. Moyale

**Katika Eneo la Kaskazini Mashariki—**
1. Garissa
2. Ijara
3. Mandera
4. Wajir

**Katika Eneo la Bonde la Ufa —**
1. Kajiado
2. Narok
3. Trans Mara
4. Turkana
5. West Pokot
6. Marakwet
7. Trans Nzoia
8. Keiyo
9. Uasin Gishu
10. Nandi North
11. Nandi South
12. Kericho
13. Bureti
14. Bomet
15. Baringo
16. Koibatek
17. Nakuru
18. Samburu
19. Laikipia

**Katika Eneo la Nyanza—**
1. Bondo
2. Nyando
3. Siaya
4. Suba
5. Kuria
6. Rachuonyo
7. Kisii Central
8. Gucha
9. Nyamira
10. Kisumu
11. Homa Bay
12. Migori

**Katika Eneo la Magharibi—**
1. Busia
2. Bungoma
3. Teso
4. Mt. Elgon
5. Lugari
6. Kakamega
7. Vihiga
8. Butere/Mumias

**Katika Eneo la Kati—**
1. Kiambu
2. Thika
3. Murang'a
4. Maragua
5. Nyandarua
6. Nyeri
7. Kirinyaga


Katika eneo la Jiji la Nairobi
1. Westlands
2. Kasarani
3. Lang'ata
4. Embakasi

## MPANGILIO WA PILI

**(Kifungu 10)**

**NEMBO ZA KITAIFA**

**(a) Bendera ya Taifa**




**Tanbihi:** Vipimo vyote vilivyotolewa haviwakilishi urefu au upana wowote na hivyo ni vinawiana tu.

**Maelezo:**
Mistari mitatu mikubwa yenye upana sawa yenye rangi nyeusi, nyekundu, na kijani kutoka juu hadi chini na kutenganishwa na mistari miembamba mieupe, yenye ngao linganifu na mishale mieupe iliyowekwa juu katikati ya bendera.

**b) Wimbo wa Taifa**

1
Ee Mungu nguvu yetu
Ilete baraka kwetu.
Haki iwe ngao na mlinzi
Natukae na undugu
Amani na uhuru
Raha tupate na ustawi.

2
Amkeni ndugu zetu
Tufanye sote bidii.
Nasi tujitoe kwa nguvu,
Nchi yetu ya Kenya,
Tunayoipenda,
Tuwe tayari kuilinda.

3
Natujenge taifa letu
Ee, ndio wajibu wetu,
Kenya istahili heshima
Tuungane mikono
Pamoja kazini
Kila siku tuwe na shukrani.

**c) Ngao ya Serikali**




**c)Muhuri wa Serikali**




## MPANGILIO WA TATU

**(Kifungu 95)**

**VIAPO VYA KITAIFA NA UDHIBITISHO**
**KIAPO AMA KUKUBALI KUWA NA UAMINIFU KWA RAIS WA TAIFA /KAIMU RAIS NA NAIBU RAIS**

Mimi, ................ , nikifahamu kuwa jukumu muhimu ninalochukua kama Rais wa Taifa/Kaimu Rais wa Taifa wa Jamhuri ya Kenya, naapa /nakiri kwa taadhima kuwa nitakuwa mwaminifu kwa Jamjuri ya Kenya; kwamba nitafuata, kuhifadhi, kutetea, Katiba ya Kenya, kulingana na katiba iliyowekwa, na sheria nyingie zote za Jamhuri, na kwamba nitalinda na kutetea uhuru, uadilifu na hadhi ya watu wa Kenya.( Kama ni kiapo: Ee Mungu nisaidie)

**KIAPO AMA KUKUBALI KUWA RAIS ILI KUTEKELEZA MAMLAKA NA KAZI YA RAIS KWA RAIS WA TAIFA/ KAIMU RAIS WA TAIFA**

Mimi, .................. , naapa/nakubali kwa dhati kuwa nitawatumikia watu wote wa Jamhuri ya Kenya kwa uaminifu katika ofisi ya Rais wa taifa/ Kaimu Rais wa Jamhuri ya Kenya; kwamba nitatekeleza majukumu na wajibu wangu katika ofisi ya Rais wa Taifa/Kaimu Rais wa jamhuri ya Kenya; na nitatekeleza haki kwa wote kwa kufuata Katiba, kulingana na katiba, na sheria za Kenya, bila woga, mapendeleo, ama chuki(Kama ni kiapo: Ee Mungu nisaidie)

**KIAPO AMA KUKUBALI KUWA RAIS ILI KUTEKELEZA KAZI YA NAIBU RAIS WA TAIFA**

Mimi, .................. , naapa ya kwamba/nakubali kwa dhati kwamba kila wakati nitawatumikia watu wa Jamhuri ya na Jamhuri ya Kenya kwa uaminifu na ukweli katika ofisi ya Naibu Rais wa Jamhuri ya Kenya; kwamba nitatekeleza majukumu na wajibu wangu katika ofisi iliyotajwa, kwa uwezo wangu wote; na kwamba wakati wote, nitakapohitajika, nitatoa ushauri wangu kwa ukweli na uaminifu kwa Rais wa Taifa wa Jamhuri ya Kenya; kwamba nitatekeleza haki kwa wote bila woga, mapendeleo, ama chuki; na kwamba kwa njia ya moja kwa moja ama isiyo ya moja kwa moja, sitafichua mambo yoyote ambayo nitayajua kutokana na utendakazi wangu na ninajitolea kuhifadhi siri.(Kama ni kiapo: Ee Mungu nisaidie)

**KIAPO AMA KUKUBALI KUWA Waziri Mkuu ILI KUTEKELEZA Waziri Mkuu WA JAMHURI**

Mimi ,.................... , naapa/nakubali kwa dhati kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Kenya ; kwamba nitaifuata na kuitumikia Katiba ya Kenya na sheria nyingine za Jamhuri ya Kenya; na kwamba nyakati zote nitaitumikia Jamhuri ya Kenya na watu wake kwa ukweli na uaminifu; na kwamba ninajitolea kuchukua ofisi kama Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kenya kwa heshima na hadhi; na kwamba nitakuwa mshauri mkweli na mwaminifu; na kwamba kwa njia ya moja kwa moja ama isiyo ya moja kwa moja, sitafichua mambo yoyote ambayo nitayajua kutokana na utendakazi wangu na ninajitolea kuhifadhi siri isipokuwa itakapohitajika katika wajibu wangu kama Waziri Mkuu na kwamba nitatekeleza majukumu ya ofisi yangu kwa uangalifu na kwa uwezo wangu wote (Kama ni kiapo: Ee Mungu nisaidie).

**KIAPO AMA KUKUBALI KUWA NAIBU WAZIRI MKUU ILI KUTEKELEZA KAZI YA NAIBU WAZIRI MKUU/WAZIRI/NAIBU WAZIRI**

Mimi ,.................... , ninayeteuliwa kama Waziri wa Kenya naapa/nakubali kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Kenya ; kwamba nitaifuata na kuitumikia Katiba ya Kenya na sheria nyingine za Jamhuri ya Kenya; na kwamba nyakati zote nitaitumikia Jamhuri ya Kenya na watu wake kwa ukweli na uaminifu; na kwamba ninajitolea kuwatumikia katika ofisi kama Naibu Waziri Mkuu/Waziri/Naibu Waziri kwa heshima na hadhi; na kwamba nitakuwa mshauri mkweli na mwaminifu kwa Waziri Mkuu ili kufikia usimamizi bora wa masuala ya umma katika Jamhuri ya Kenya; na kwamba kwa njia ya moja kwa moja ama isiyo ya moja kwa moja, sitafichua mambo yoyote ambayo nitayajua kutokana na utendakazi wangu na ninajitolea kuhifadhi siri isipokuwa itakapohitajika katika wajibu wangu kama Naibu Waziri Mkuu/Waziri/Naibu Waziri na kwamba nitatekeleza majukumu ya ofisi yangu kwa uangalifu na kwa uwezo wangu wote (Kama ni kiapo: Ee Mungu nisaidie).

**KIAPO AMA KUKUBALI KUWA KATIBU WA BARAZA LA MAWAZIRI/KATIBU**

**MKUU ILI KUTEKELEZA KAZI YA KATIBU WA BARAZA LA MAWAZIRI / KATIBU MKUU**

Mimi, ......................, nikiwa ninahitajika kuchukua wajibu wa katibu wa Baraza la Mawaziri/ Katibu Mkuu ninaapa ya kwamba/ninakubali kwamba, isipokuwa nikiwa nimepewa na idhini ya Waziri Mkuu, kwa njia ya moja kwa moja ama isiyo ya moja kwa moja, sitafichua majadiliano, kumbukumbu ama nyaraka za baraza la mawaziri ambazo nimezihifadhi, isipokuwa itakavyohitajika katika utendakazi wangu kama Katibu wa Baraza la Mawaziri/Katibu Mkuu. (Kama ni kiapo: Ee Mungu nisaidie)

**VIAPO KWA JAJI MKUU/RAIS WA MAHAKAMA YENYE MAMLAKA KUU, MAJAJI WA MAHAKAMA YENYE MAMLAKA KUU, MAJAJI WA MAHAKAMA YA RUFANI, MAJAJI WA MAHAKAMA YA KIKATIBA, NA MAJAJI WA MAHAKAMA KUU.**

Mimi, ......................, (Jaji Mkuu /Rais wa Mahakama yenye mamlaka Kuu, jaji wa Mahakama yenye Mamlaka Kuu, Jaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji wa Mahakama ya Kikatiba, jaji wa Mahakama Kuu) ninaapa (naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu)/ nakubali kwa dhati kutumikia Wakenya na Jamhuri ya Kenya na kutekeleza haki bila mapendeleo kulingana na Katiba iliyowekwa, na sheria na desturi za Jamhuri, bila woga wowote, mapendeleo, ubaguzi, chuki, ama mapendeleo yoyote ya kisiasa kidini, ama ushawishi wowote. Katika kutekeleza majukumu ya kisheria ambayo nimepewa, wakati wote, kwa uwezo wangu wote, nitatetea, nitahifadhi na kusimamia, na kuhifadhi Katiba kwa minajili ya kulinda hadhi na heshima ya mahakama na mfumo wa mahakama wa Kenya na kukuza haki, uhuru, uwezo wa kisheria na uadilifu ndani yake. (E Mungu nisaidie)

**KIAPO/KUKIRI KUWA MBUNGE (SENETI/BUNGE)**

Mimi,......................, nikiwa nimechaguliwa mwachama wa Seneti/Bunge ninaapa (Kwa jina la Mwenyezi Mungu) (ninadhibitisha ) kwamba nitakuwa mwaminifu na mtiifu kwa raia na Jamhuri ya Kenya; kwamba nitatii heshimu, kutetea, kulinda na kuhifadhi Katiba ya jamhuri ya Kenya; na kwamba nitatekeleza majukumu yangu ya Mbunge kwa uaminifu na makini (Ee Mungu nisaidie).

**KIAPO CHA SPIKA/NAIBU SPIKA WA SENETI/BUNGE**

Mimi ,.................... , nikiwa nimechaguliwa kama Spika/ Naibu Spika wa Seneti/ Bunge ninaapa kwamba(Kwa jina la Mwenyezi Mungu) (nakubali kwa dhati) kwamba nitakuwa mwaminifu kwa raia na Jamhuri ya Kenya; kwamba nitatekeleza majukumu yangu kama Spika/Naibu Spika kwa uaminifu na makini wa Seneti/ Bunge; kwamba nitatii nitaheshimu, nitatea, nitahifadhi nitalinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Kenya; na kwamba nitafanya haki kwa watu wote kulingana na Katiba ya Kenya na sheria na desturi za Bunge bila mapendeleo ama chuki(Ee Mungu nisaidie)

## MPANGILIO WA NNE

**(Kifungu 228(1))**

**MGAO WA MAJUKUMU KATI YA SERIKALI YA KITAIFA NA SERIKALI ZILIZOGATULIWA**

**Sehemu ya 1 – Serikali ya Kitaifa**

1. Mashauri ya kigeni, sera ya kigeni, na Biashara ya Kimataifa
2. Kwa ushauriano na maeneo na wilaya matumizi ya maji ya kimataifa na raslimali za maji.
3. Uhamiaji na uraia.
4. Uhusiano kati ya dini na taifa.
5. Sera ya lugha na ukuzaji wa lugha rasmi na lugha za kiasili.
6. Ulinzi wa kitaifa na matumizi ya huduma za usalama za kitaifa..
7. Usalama wa Kitaifa , pamoja na—
   - (a) Kuweka viwango vya kuandikisha askari wapya, kutoa mafunzo kwa polisi na matumizi ya huduma za polisi;
   - (b) Sheria ya Kiuhalifu; na
   - (c) Huduma za Marekebisho.
8. Mahakama.
9. Sera ya kitaifa ya uchumi na mipango.
10. Sera ya fedha sarafu, benki (pamoja na benki kuu) kuanzishwa na usimamizi wa shughuli za benki, bima na mashirika ya kifedha.
11. Takwimu za kitaifa na data kuhusu idadi ya watu, uchumi na jamii kwa jumla.
12. Haki miliki kuhusu ujuzi wa kiakili
13. Viwango vya Leba.
14. Ulinzi wa watumiaji, pamoja na viwango vya usalama wa kijamii mipango ya pensheni za kitaalamu.
15. Sera ya elimu, viwango, Mitaala, mitihani, na kutoa kwa hati za vyuo vikuu.
16. Vyuo vikuu, taasisi za elimu ya juu na taasisi nyingine za utafiti na elimu ya juu na shule za msingi, elimu maalum kipekee, shule za upili, na taasisi za elimu maalum.
17. Ukuzaji wa michezo na elimu juu ya michezo.
18. Uchukuzi na mawasiliano, pamoja na, hasa—
   - (a) Usafiri wa barabara;
   - (b) Ujenzi na utumikaji wa barabara kuu za kitaifa
   - (c) Viwango vya ujenzi na uhifadhi wa barabara nyingine na maeneo na Wilaya;
   - (d) Reli;
   - (e) Mabomba;
   - (f) Usafiri wa baharini;
   - (g) vyombo vya anga vinavyotumiwa na raia;
   - (h) Usafiri wa angani;
   - (i) Huduma za posta;
   - (j) Mawasiliano ya simu, redio na televisheni, na;
   - (k) matangazo ya redio na televisheni.
19. Ujenzi wa kitaifa.
20. Sera ya nyumba.
21. Kanuni za kijumla za mipango ya ardhi na ushirikishaji wa mipango ya maeneo na wilaya.
22. Uhifadhi wa mazingira na mali asili kwa mpango wa kuanzisha mfumo wa maendeleo ya kudumu, pamoja na, hasa—
   - (a) Uvuvi, usasi na ukusanyaji matunda;
   - (b) Ulinzi wa wanyama na wanyama pori;
   - (c) Uhifadhi wa maji, kuhifadhi maji yanayobaki ya kutosha, taaluma kuhusu maji na usalama wa maji kwenye mabawa; na
   - (d) Sera ya kawi .
23. Nyenzo kuu za kitaifa za kiafya.
24. Usimamizi wa majanga.
25. Minara ya ukumbusho ya zamani na ya kihistoria yenye umuhimu wa kitaifa.
26. Chaguzi za kitaifa.
28. Sera ya Afya.
29. Sera ya Kilimo.
30. sera ya utatibu wa mifugo.
31. Sera ya kawi pamoja na nguvu za umeme na mtandao wa gesi na usimamiaji wa kawi.
32. Uwezeshaji na msaada wa kifundi kwa wilaya.
33. Uwekezaji wa umma.
34. Sera ya utalii na bahati nasibu.

**Sehemu ya 2—Serikali za Kimaeneo**

Isipokuwa ambapo Katiba hii na sheria inapoeleza vinginevyo mamlaka na majukumu ya serikali za kimaeneo katika maeneo yao yote, kwa kushauriana na wilaya katika eneo hilo, yatakuwa—

- (a) Kushirikisha na kusimamia Wilaya katika juhudi zao za kutekeleza sera za kimaeneo na kitaifa na viwango;
- (b) Uundaji wa sera za kimaeneo;
- (c) Uundaji wa viwango vya kimaeneo;
- (d) Mipango ya kimaeneo;
- (e) Usimamizi na tathmini ya utekelezaji;
- (f) Ushirikishi wa, usimamizi na utoaji wa huduma za kimaeneo;
- (g) Kushirikisha shughuli na kutunza miundo msingi na huduma za kimaeneo;
- (h)Kuwezesha na kusawazisha shughuli katika eneo; na
- (i) Uwezeshaji na na msaada wa kifundi kwa wilaya.

**Sehemu ya 3—Serikali za Wilaya**

**Mamlaka na majukumu ya wilaya ni—**

1. Kilimo, pamoja na—
   - (a) Kilimo cha mimea na wanyama;
   - (b) Viwanja vya kuuzia wanyama;
   - (c) Vichinjio vya wilaya;
   - (d) Udhibiti wa magonjwa ya mimea na wanyama; na
   - (e) Uvuvi.
2. Huduma za afya za wilaya, pamoja na, hasa—

(a) Nyenzo za afya za wilaya na maduka ya dawa;
(b) huduma za ambalensi;
(c) Kustawisha afya ya kimsingi;
(d) Kutoa leseni na kusimamia shughulia za kuuza chakula kwa umma;
(e) Huduma za utabibu wa wanyama (isipokuwa usimamiaji wa taaluma);
(f) Makaburi, kumbi za matanga na tunuu za kuchomea maiti; na
(g) Uondoaji taka, maeneo ya kutupa taka na utupaji taka.

3. Kudhibiti uchafuzi wa hewa, uchafuzi wa mazingira kwa kelele, na usumbufu mwingine wa raia na utangazaj wa nje.
4. Shughuli za kitamaduni, burudani za umma na huduma zinazofanya maisha kuwa mazuri, pamoja na—
(a) Kasino na njia nyingine za kamari;
(b) mashindano ya mbio;
(c) Utaoji leseni kwa pombe;
(d) majumba ya Sinema;
(e) maonyesho ya video na kukodisha;
(f) maktaba;
(g) makavazi;
(h) shughuli na nyenzo za michezo na kitamaduni sports ; na
(i) vituo vya wilaya, fuo na neynzo za burudani.
5. Uchukuzi katika wilaya, pamoja na —
(a) barabara za wilaya;
(b) taa za barabarani;
(c) magari na uegeshaji;
(d) usafiri wa umma; na
(e) vivuko, na bandari, isipokuwa usimamizi wa masuala yanayohusiana na shughuli za meli kitaifa na kimataifa.
6. Ustawi na udhibiti wa wanyama, pamoja na;
(a) kutoa leseni kwa mbwa;
(b) Nyenzo za kuhifadhi, kutunza na kuzika wanyama.
7. Ustawishaji wa biashara na usimamizi, pamoja na—
(a) masoko;
(b) leseni za biashara (isipokuwa udhibiti wa taaluma);
(c) usawa katika ushindani wa kibiashara shughuli za kibiashara;
(d) utalii wa humu nchini; na
(e) vyama vya ushirika.
8. Mipango ya wilaya na maendeleo, pamoja na—
(a) takwimu;
(b) usoroveya na uchoraji ramani;
(c) mipaka na uwekaji nyua;
(d) makazi; na
(e) Uunganishaji na udhibitiwa nguvu za umeme na gesi.
9. Elimu katika chekechea, elimu, vyuo vya kifundi vijijini, vituo vya utengenezxaji vinyago, na nyenzo za utunzaji watoto.
10. Kutekelezwa kwa sera za serikali ya kitaifa kuhusu mali asili na uhifadhi wa mazingira, pamoja na—
(a) Uhifadhi na utunzaji wa udongo na maji; na
(b) Uhifadhi wa misitu.
11. Ujenzi na huduma za wilaya, pamoja na —
(a) mfumo wa usimamizi wa maji ya tufani katika nyanda za juu; na
(b) huduma za maji na afya.
12. huduma za kuzima moto, na usimamizi wa majanga
13. udhibiti wa madawa na ponografia.
14. kuhakikisha na kushirikisha ushiriki wa jamii na kata katika usimamizi katika viwango vya chini na kuzisaidia jamii kujenga uwezo wa kuisimamizi ili kuwezesha matumizi ya mamlaka na majukumu na kushiriki katika usimamizi katika viwango vya mashinani.

## MPANGILIO WA TANO

**(Kifungu 246)**

**MAMLAKA YA KUTOZA USHURU**

**Sehemu ya 1 – Mamlaka ya kutoza ushuru ya Serikali ya Kitaifa**

**Bunge la taifa linaweza kukusanya pesa, kwa njia ya ushuru, kodi, ada, na—**
(a) ushuru wa mapato;
(b) ushuru wa dhamana;
(c) ushuru unaotozwa shirika;
(d) ushuru wa forodha na kodi nyingine kwa bidhaa za humu nchini na za kutoka nje;
(e) mapato ya ushuru;
(f) ushuru wa bidhaa zinazouzwa;
(g) ada za stempu za kitaifa;
(h) ushuru kutoka kwa michezo ya bahati nasibu ya kitaifa na taratibu za aina hiyo.
(i) ushuru wa uchukuzi wa barabara, anga, reli, na maji;
(j) kodi za nyumba na mali nyingine inayomilikiwa na serikali ya kitaifa;
(k) ada za leseni zinazotolewa na serikali ya kitaifa;
(l) ada za mahakama, faini na mali twaliwa
(m) risiti za ununuzi wa bidhaa;
(n) ada za kuandikisha magari na ada za leseni za kuendesha magari;
(o) ada za huduma na bidhaa za serikali ya kitaifa; na
(p) kodi nyingine zozote zilizoidhinishwa na sheria za kitaifa.

**Sehemu ya 2 – Mamlaka ya kutoza ushuru ya wilaya**

**Serikali ya wilaya inaweza kukusanya pesa, kwa njia ya ushuru, kodi, ada, na kutoza—**
(a) ushuru wa ziada unaotozwa kiwango sawa cha kima cha ushuru wa ushuru wowote, kinachotozwa kodi, ada, ambao unaotoza kwa sheria za kitaifa isipokuwa ushuru wa kima cha ushuru wa mapato ya makampuni, ushuru wa thamani na ushuru wa forodha na mapato ya ushuru;
(b) ada za matumizi ya ardhi;
(c) ada za kilimo;
(d) ada kwa matumizi ya mali inayomilikiwa na serikali ya wilaya;
(e) ushuru kwa mali na ushuru za ziada kwa huduma zilizotolewa na kwa niaba ya wilaya;
(f) ada za leseni zikiwemo ada za kutoa leseni za pombe, ada za masoko, ada za uchuuzi;
(g) ada za leseni za kufanya biashara;
(h) ushuru wa burudani;
(i) ada za kutunza barabara wilayani;
(j) ushuru wa hoteli na mikahawa wilayani;
(k) ushuru wa mrabaha wa mali asili;
(l) ada za kiingilio kwa mbuga wanyama na za hifadhi za wanyama pori;
(m) ushuru wa uchukuzi;
(n) ada za kuegesha;
(o) kodi nyingine zozote, ada, ushuru wa zaidi, na matazo ambayo wilaya imeruhusiwa kila mara kulingana na sheria za kitaifa kutoza; na
(p) ushuru mwingine wowote , ada, ushuru wa ziada, na matozo ambayo serikali ya kitaifa hajatengewa kutoza .

## MPANGILIO WA SITA

**(Kifungu 312(1))**

## SHERIA ZITAKAZOTUNGWA NA BUNGE

| SURA NA KICHWA CHA KIFUNGU | KIFUNGU | MUDA ULIOWEKWA |
|---|---|---|
| | | |
| **SURA YA NNE:URAIA** | | |
| Uraia wa naturalization | 19 | Miaka miwili |
| Uraia mara mbili | 21(3) | Miaka miwili |
| Makao | 23(2) | Miaka miwili |
| Sheria kuhusu Urai | 25 | Miaka miwili |
| **SURA YA TANO: UTAMADUNI** | | |
| Jukumu la Serikali kuhusiana Utamaduni | 27(i) | Miaka miwili |
| | | Two years |
| **SURA YA SITA:SHERIA YA HAKI** | | |
| Utekelezaji wa sheria ya haki na haki za kimsingi | 30(2),(3) and (6) | Miaka mitatu |
| Uwezo wa Mahakama kutekeleza Sheria ya Haki | 32(2) | Miaka mitatu |
| Uhuru wa kutobaguliwa | 37(4) | Miaka mitatu |
| Wazee katika jamii | 39(2) and (3) | Miaka miwili |
| Vijana | 40(2) | Miaka mitatu |
| Watoto | 41(8) | Mwaka mmoja |
| Familia | 42(5) | Miaka mitatu |
| Walemavu | 43(3) | Miaka mitatu |
| Wanyonge na makundi tengwa | 44(2) | Miaka mitatu |
| Uhuru wa vyombo vya habari | 51(5) | Mwaka mmoja |
| Haki ya kupata habari | 52(4) | Miezi sita |
| Haki ya kutangamana | 53(4) | Mwaka mmoja |
| Haki ya wakimbizi | 57(2) | Mwaka mmoja |
| Elimu | 63(4) | Miaka mitatu |
| Haki za Wateja | 69(3) | Miaka mitatu |

| | | |
|---|---|---|
| Fair administrative action | 70(3) | Miaka mitatu |
| **SURA YA SABA:ARDHI NA MALI** | | |
| Ardhi ya jamii | 80(5) | Miaka miwili |
| Wasio raia kununua ardhi | 82(4) | Miezi sita |
| Sheria kuhusu ardhi | 85 | Miaka miwili |
| **SURA YA NANE:MAZINGIRA NA MALI ASILI** | | |
| Utumiaji na maendeleo ya Mali asili | 91(2) | Miaka miwili |
| Sheria kuhusu uhifadhi wa mazingira | 93 | Miaka miwili |
| **SURA YA TISA:UONGOZI NA UADILIFU** | | |
| Kiapo cha ofisi | 95 | Mwaka mmoja |
| Tume ya Maadili na Kupambana dhidi ya Ufisadi | 99(3) | Mwaka mmoja |
| Sheria kuhusu uongozi | 101 | Mwaka mmoja |
| **SURA YA KUMI : KUWAKILISHA WA WATU** | | |
| Sheria kuhusu Uchaguzi | 103(1) | Mwaka mmoja |
| Kudhibiti vyama vya Kisiasa | 117 | Mwaka mmoja |
| Utekelezaji wa Hazina | 119(4) | Mwaka mmoja |
| **SURA YA KUMI NA MOJA:BUNGE** | | |
| Uanachama wa Seneti | 125(2) | Mwaka mmoja |
| Uanachama wa Bunge | 126(2) | Miaka miwili |
| | | |
| Mamlaka, marupurupu, kinga | 150(2) | Mwaka mmoja |
| Usajili wa sheria buniwa | 151(1) | Mwaka mmoja |
| **SURA YA KUMI NA MBILI:Serikali** | | |
| Utaratibu wa Uchaguzi wa Urais | 164(3)(b) | Mwaka mmoja |
| Mamlaka ya Rais ya msamehe | 172(3) | Mwaka mmoja |
| Mtetezi wa masalahi ya Umma | 195(5) | Miaka miwili |
| **SURA YA KUMI NA TATU: MFUMO WA KISHERIA** | | |
| Mahakama ya Mamlaka Kuu | 201(4)(b)(ii) | Mwaka mmoja |
| Mahakama ya Rufani | 202(2)(b) | Miaka miwili |
| Mahakama Kuu | 204(1)(b) | Miaka miwili |
| Mahakama za kiwango cha Chini | 208(1)(d) | Miaka miwili |
| Mahakama za Kadhi | 209(1) | Miaka miwili |
| Majukumu ya Tume ya Huduma za Mahakama | 211(1)(e) | Miaka miwili |
| **SURA YA KUMI NA NNE: SERIKALI ZILIZOGATULIWA** | | |
| Uchaguzi wa Meya na Naibu Meya wa Nairobi | 219 | Miaka mitatu |
| Maeneo ya miji | 226(1) | Miaka mitatu |
| Ushirikiano kati ya serikali katika viwango mbalimbali | 231 | Miaka mitatu |
| Usawa wa na tofauti za Kijinsia | 240(2) | Mwaka mmoja |
| Kipengele kitakachoundwa na sheria ya Bunge (Kutekeleza Sura) | 243 | Miaka miwili |
| **SURA YA KUMI NA TANO: FEDHA ZA UMMA** | | |
| Utungaji sheria | 248(1) | Mwaka mmoja |
| Hazina ya Pamoja | 249(1) | Mwaka mmoja |
| Hazina ya Mapato kwa serikali zilizogatuliwa | 251(2)(b) | Mwaka mmoja |
| Hazina ya dharura | 252(1) | Mwaka mmoja |
| Kukopa kwa serikali zilizogatuliwa | 254 | Mwaka mmoja |
| Deni la Umma | 255(2) | Mwaka mmoja |
| Bajeti ya kila mwaka ya serikali zilizogatuliwa | 260 | Mwaka mmoja |
| Ununuzi wa Bidhaa na huduma za umma | 261(2) | Mwaka mmoja |
| Akaunti na ukaguzi wa taasisi za umma | 262(5) | Mwaka mmoja |
| Udhibiti wa Hazina Kuu | 263(1) | Mwaka mmoja |
| Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali | 265(6) | Mwaka mmoja |
| Mamlaka ya Ushuru ya Kitaifa | 266(3) | Mwaka mmoja |
| Tume ya Ugawanyaji wa Mapato | 267(8) | Mwaka mmoja |
| Baraza la Kijamii na Kiuchumi | 271(4) | Mwaka mmoja |
| **SURA YA KUMI NA SITA: UTUMISHI WA UMMA** | | |
| Mamlaka na Majukumu | 274(5) | Miaka miwili |
| Wafanyikazi wa serikali zilizogatuliwa | 275 | Miaka miwili |
| Tume ya Kuwaajiri Walimu | 277(4) | |
| Uundwaji wa Huduma ya Urekebishaji ya Kenya | 278(5) | Miaka miwili |
| **SURA YA KUMI NA SABA:USALAMA WA KITAIFA** | | |
| Vikosi vya usalama wa kitaifa | 281(6) | Mwaka mmoja |
| Uundwaji wa huduma ya Polisi ya Kenya | 289(3) | Mwaka mmoja |
| Tume ya Huduma ya Polisi | 293(6) | |
| Huduma nyingine za polisi | 294(1) | |
| **SURA YA KUMI NA NANE: TUME NA OFISI HURU** | | |
| Vikao katika Tume na ofisi Huru | 301(1) | Mwaka mmoja |
| Utungaji sheria | 305 | Mwaka mmoja |
| | | |

## MPANGILIO WA SABA

**(Kifungu 312)**

**VIPENGELE VYA MUDA NA MATOKEO YAKE**

**Haki, majukumu na wajibu wa Taifa**

**1.** Haki zote na majukumu, yanayotokea, kwa serikali ama Jamhuri ambayo yamo kabla tu ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, yataendelea kama haki na majukumu ya Serikali ama Jamhuri chini ya Katiba hii.

**Sheria zilizopo**

**2.** Sheria zote zinazotumika kabla tu ya kuanza kutumika kwa katiba zitaendelea kutumika na zitatumika na mabadiliko hayo, miigo na vikwazo kama inavyowezekana ili kuziweka sambamba na Katiba hii.

**Kanuni za utekelezaji wa Haki na uhuru wa kimsingi**

**3.** Kanunia za utekelezaji wa haki na uhuru wa kimsingi chini ya sehemu ya 84(6) ya Katiba inayotumika kabla tu ya kuanza kutumika kwa mabadiliko mpaka wakati jaji mkuu anaunda kanunia zilizofikiriwa na kifungu 31.

**Bunge**

**4.** Bunge lililopo kabla tu ya kuanza kutumika kwa Katiba litaendelea kama Bunge kwa minajili ya Katiba hii kwa muda ambao linafaa kuendelea.

**Seneti**

**5.** (1) Uchaguzi wa kwanza wa Seneti utafanyika ndani ya siku 14 baada ya uchaguzi mkuu wa kwanza utakaofanywa Katiba hii ikitumika.

(2) Hadi Seneti itakapochaguliwa chini ya Katiba hii, majukumu ya Seneti yatatekelezwa ba Bunge.

(3) Hadi Seneti itakapochaguliwa kulingana na Katiba hii, popote ama jukumu litahitajika kutekelezwa ama kutekelezwa na Bunge na Seneti, kwa pamoja na zikishirikiana, ama moja baada ya nyingine, jukumu ama wajibu utatekelezwa na Bunge.

(4) Jukumu lolote ama wajibu wa Seneti, lita, kama litatetekelezwa ama kufanywa na Bunge kabla ya tarehe inavyotajwa katika sehemu ya kifungu (1) itachukuliwa kama iliyotekelezwa na Seneti kabla ya tarehe hiyo.

**General elections and by-elections**

**6.** Uchauguzi mkuu na chaguzi ndogo zitakazofanywa baada ya kuanza kutumika kwa Katiba zitafanywa kulingana na Katiba hii.

**Mabaraza ya Miji**

**7.** (1) Mabaraza yote ya miji ambayo yameundwa kulingana Sheria ya Mabaraza ya Miji (sehemu ya 265) yaliyopo kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba zitaendelea kuwepo hadi utekelezaji wa muundo mpya kulingana na Sura ya Kuni na Nne kama inavyoelezwa na Sheria ya Bunge

(2) Bunge litaunda sheria inayofafanuliwa na sehemu ya kifungu ya (1) katika kipindi cha miaka miwili ya kuanza kutumika kwa Katiba.

(3) Madiwani wote wa mabaraza ya mji wanaoelezwa katika sehemu ya kifungu (1) wataendelea kuwa madiwani baada ya kuanza kutumika kwa Katiba hadi uchaguzi utakapotangazwa kulingana na sheria inayorejelewa katika sehemu ya kifungu (1)

(4) Siku ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, mipaka ya wilaya ilivyoelezwa katika Mpangilio wa Kwanza jina ambalo linapatana na jina la wilaya tarehe 15, Machi, 2004 ndiyo mipaka ya wilaya hiyo.

**Vyama vya kisiasa**

**8.** (1) Chama cha kisiasa kinachoendeleza shughuli zake kabla tu ya siku ya kutumika kwa Katiba hii, katika kipindi cha miezi kumi na miwili baada ya kutekelezwa kwa sheria inayoidhinisha kusajiliwa kwa vyama vya kisiasa, zinagatia mahitaji ya kusajiliwa kama chama cha kisiasa.

(2) Iwapo baada ya kumalizikwa kwa kipindi cha mienzi sita, chama hakijazingatia mahitaji ya sehemu ya kifungu (1), chama hicho cha kisiasa kitavunjika kisheria na yeyote aliyechaguliwa kwa wadhifa wowote kwa kutumia chama hicho ataendelea kuwa na wadhifa huo, lakini atachukuliwa kuwa mwanachama huru.

**Serikali**

**9.** (1) Watu walio na mamlaka ya Rais na Waziri Mkuu, kabla tu ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, wataendelea na majukumu yao kama Rais na Waziri Mkuu mtawalia, kulingana na Katiba iliyoko kabla ya kuanza kutumikwa kwa

Katiba hii na Sheria na Muafaka wa Kitaifa na Maridhiano iliyopo kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba hii hadi uchaguzi mkuu wa kwanza ufanyika kwa Katiba hii.

(2) Watu walio katika wadhifa wa ofisi za Naibu Rais, Naibu Waziri Mkuu kabla tu ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, watakuwa na mamlaka na wajibu wa Naibu Rais na Naibu Waziri Mkuu katika Katiba inayotumika kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.

(4) Mtu aliye na wadhifa katika Baraza la Mawaziri ama Waziri Msaidizi kabla tu ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, ataendelea kushikilia wadhifa huo katika Katiba hii kulingana na Katiba iliyoko kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.

(5) Mtu ambaye kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba hii ametumikia kipindi cha muhula mmoja ama zaidi kama Rais hataruhusiwa kugombea Urais kuanzia siku ya kuanza kutumika kwa Katiba

**Utawala wa Mikoa**

**10.** (1) Baada ya kufanyika kwa uchaguzi unaorejelewa katika sehemu ya 7, mfumo wa usimamizi unaojulikana Utawala wa Mikoa utavunjwa na serikali ya kitaifa itaunda mfumo wake wa kiusimamizi kufuata na kuheshimu serikali iliyogatuliwa uliobuniwa katika Katiba hii.

(2) Kulingana na sehemu ya kifungu (1), maafisa wa serikali waliokuwa wakifanya kazi chini ya mfumo unaojulikana kama Utawala wa Mikoa wataripoti kwa Tume ya Utumishi wa Umma ili kupewa kazi upya.

(3) Ingawa sehemu ya kifungu (1), machifu, manaibu wa machifu na wazee wa vijiji wataendelea kufanya kazi vivyo hivyo chini ya serikali za wilaya kama itakavyoamuliwa na na kila serikali ya wilaya.

(4) Kuanzia siku ya kuanza kutumika kwa Katiba, mali yote iliyokuwa ikishikiliwa na serikali ya taifa na ambayo inapatikana katika mikoa, wilaya na tarafa na kata, itaendelea kuwa mali ya umma.

(5) Hadi wakati ambapo serikali za wilaya na serikali za kimaeneo zitakapoundwa, mali yote inayohifadhiwa na serikali za wilaya kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba hii itahifadhiwa na serikali za wilaya na haitahamishwa ama kuuzwa kwa njia yoyote bila idhini kwa maandishi ya serikali ya kitaifa na kuhamishwa kokote bila idhini hakutatambuliwa.

**Ofisi zilizoko**

**11.** (1) Mtu ambaye kabla tu ya kuanza kutumika kwa Katiba hii alikuwa afisa ama anashikilia ofisi kwa muda iliyobuniwa na Katiba iliyotumiwa kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba, ataendelea kushikilia ofisi ama kuishikilia kwa muda kulingana na Katiba kwa kipindi kilichobaki, kama kipo, ya kipindi chake kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.

(2) Mtu ambaye kabla tu ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, alikuwa anashikilia wadhifa fulani ama akishikilia wadhifa kwa muda ofisi ambayo inabuniwa na Katiba iliyoko kabla tu ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, kama anahitajika kufanya hivyo kulingana na Sura ya Tisa, anaweza katika siku thelathini za kuteuliwa kwa Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi, atawasilisha nyaraka na ushahidi unaohitajika.

(3) Mtu ambaye kabla tu ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, alikuwa anashikilia wadhifa fulani ama akishikilia wadhifa kwa muda katika ofisi ya umma inayobuniwa na sheria yoyote iliyoandikwa, kwa sasa inayoambatana na Katiba hii, ataendelea kushikilia wadhifa huo ama kuushikilia kwa muda kama kwamba ameteuliwa kwa ofisi hiyo katika Katiba hii, na kama anahitajika ambayo inabuniwa na Katiba iliyoko kabla tu ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, kama anahitajika kufanya hivyo kulingana na Sura ya Tisa, anaweza katika siku thelathini za kuteuliwa kwa Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi, atawasilisha nyaraka na ushahidi unaohitajika.

(4) Vipengele vya sehemu hii havitaathiri mamlaka yaliyopewa mtu yeyote ama uwezo wa kisheria katika Katiba hii kuvunja ofisi ama kuwandoa watu kutoka ofisi hizi.

(5) Utaratibu wa kuajiriwa na watu kujaza nafasi zinazotokana na kutekeleza kwa Katiba hii kutaanza siku ya kuanza kutekeleza kwa katiba hii na kumalizika katika mwaka mmoja kulingana na vipengele vya Katiba hii..

(6) Katika hali ambapo mtu ameacha ofisi ambayo alikuwa akiishikilia kabla ya siku ya kuanza kutekeleza Katiba hii, na ofisi hiyo inabaki katika Katiba hii, mtu huyo anaweza, kama anahitimu, anateuliwa, kuchaguliwa, ama kupewa wadhifa huo kulingana na vipengele vya Katiba hii, katika siku thelathini za kuteuliwa kwa Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi atawasilisha nyaraka na ushahidi unaohitajika kulingana na Sura ya Tisa.

(7) Majukumu ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma yatatekelezwa na Mwanasheria Mkuu hadi Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atakapoteuliwa kulingana na Katiba hii.

(8) Majukumu ya Mkurugenzi wa Bajeti yatatekelezwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hadi Mkurugenzi wa Bajeti ateuliwe kulingana na Katiba hii. Katiba hii, Licha ya sehemu ya (1), na labda awe ameondolewa mapema kwa Katiba hii, Mwanasheria Mkuu na Mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali wataendelea kuwa ofisini kwa kipindi cha miezi sita kuanza siku ya kuanza ya kutekelezwa Katiba na watu wapya watateuliwa kwa ofisi hizo kulingana na Katiba hii.

**Kiapo cha uaminifu kwa Katiba**

**12.** Katika siku ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, Rais na afisa yeyote ama mtu yeyote ambaye kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, alikuwa ameapa ama amekubali kama ilivyo katika kiapo kinachohitajika, ama anayehitajika kuchukua kiapo cha uaminifu ili kuchukua ofisi katika Katiba hii, ataapa inavyohitajika katika Katiba hii.

**Urithi wa taasisi, ofisi, mali na madeni**

**13**. (1) ofisi ambayo imebiuniwa na Katiba ndiyo mrithi wa kisheria wa ofisi kama hiyo ama taasisi iliyobuniwa na sheria ya bunge iliyokuwa ikifanya kazi kabla ya siku ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii, hata ikiwa inatambuliwa kwa jina lile lile au ikiwa imepewa jina jipya.

(2) Madeni yote, mali na na raslimali nyingine ambazo kabla ya siku ya kuanza kutumika kwa Katiba hii zilikuwa za Serikali au Jamhuri, vyovyote vile, itaendelea kuwa hivyo hata baada ya siku ya kuanza kutumika kwa Katiba.

(3) Kwa lengo la sehemu hii, Mamlaka ya Ukusanyaji Ushuru ambayo ilikuwepo kabla tu ya Katiba hii inaendelea kama Mamlaka ya Kitaifa ya Ukusanyaji Ushuru inayorejelewa katika kifungu namba 266.

**Pensheni, bahashishi, na manufaa mengine**

**14**. Sheria inayohusu pensheni, bahashishi na mshahara kwa walio na nyadhifa za kikatiba itakuwa sheria ambayo ilitumiwa wakati manufaa hayo yalipotolewa, na sheria yoyote nyingine ambayo itatumika baadaye ambayo haimfaidi mtu huyo

**Idara ya Mahakama**

**15.** (1) Katika kipindi cha siku thelathini za kuanza kutumika kwa Katiba hii, Rais na Waziri Mkuu,wakifanya kazi kwa pamoja katika misingi ya mkataba wa kitaifa wa maridhiano

Waliokubaliana katika Katiba iliyopo kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, watajadiliana wataunda Tume ya muda ya Huduma za Mahakama ambayo, kulingana na sehemu hii, itawakagua majaji kabla ya siku ya kuanza kutekeleza katiba mpya.

2) Tiume ya Huduma za Kimahakama ya muda itajumuisha—

(a) Majaji wawili wasio Wakenya walio majaji ama waliostaafu kila mmoja wao akiwa amefanya kazi katika nchi ya jumuiya ya Madola kama jaji ama jaji mkuu na ambaye mmoja wao atateuliwa kuwa mwenyekiti.

(b) Majaji wawili wa mahakama kuu ya Kenya ama mahakama ya rufani ambao watakuwa Wakenya; na

(c) Wakili ambaye ana ujuzi wa miaka kumi na mitano kama msomi mashuhuri, afisa wa mahakama, ama wakili ama mwenye ujuzi katika nyanya nyingine yoyote ya kisheria, aliyeteuliwa na Chama cha Mawakili wa Kenya.

(3) Jaji ambaye alikuwa kazini kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba mpya, anaweza, katika siku sitini, ya kuanza kutumika Katiba mpya kuamua kustaafu na baada ya kustaafu anaweza kupata kiinua mgongo chake kulingana na Katiba.

(4) Jaji Mkuu aliye ofisini kabla tu ya siku ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii, katika siku sitini za kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii, ataacha kazi na anaweza kuamua—

(a) Kustaafu kutoka idara ya mahakama; au

(b) kutegemea utaratibu wa kuchuja katika sehemu hii, aendelee kuhudumu katika mahakama ya rufani.

(5) (a) Tume ya muda ya Huduma za Mahakama inaweza kuchunguza, kwa kuzingatia jaji—

(i) Kesi yoyote ya jinai ambayo haijakamilishwa ama ambayo imekamilishwa.

(ii) Mapendekezo yoyote kwa minajili ya mashtaka yaliyoletwa na Mwanasheria Mkuu, Tume ya Kupambana na Ufisadi, ama taasisi yoyote inayofaa;

(iii) Kufaa kwa uteuzi kama jaji katika misingi iliyowekwa kwenye Katiba;

(iv) uhodari na bidii; na

(v)Jambo lingine lolote lenye umuhimu.

(b) Katika utendakazi wake katika sehemu hii, Tume ya muda ya Huduma za Mahakama itaheshimu na itaongozwa na vigezo na viwango vya

kimataifa kuhusiana na uhuru wa idara ya mahakama.

(6)Katika kushughulikia kila jaji, Tume ya Muda ya Huduma za Mahakama itazingatia malalamiko yoyote ambayo hayajashughulikiwa kuhusiana na jaji yeyote katika siku ya kuanza kutekeleza Katiba hii kabla ya mambo yafuatayo—

(a) Tume ya Kupambana na Ufisadi;
(b) Tume kuhusu Malalamiko ya Mawakili ama Kamati ya Nidhamu ya Mawakili
(c) Tume ya kudumu kuhusu Malalamiko ya Umma;
(d) Tume ya Huduma za Mahakama; na
(e) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

(7) Tume ya Muda ya Huduma za Mahakama itashughulikia kesi zifuatazo kulingana na uzito wake—

(a) Majaji wa mahakama ya rufani kulingana na cheo ;
(b) Majaji kumi wa Mahakama Kuu kila mara, kulingana na cheo.

(8) Kila mara, baada ya mwanzoni kumsikiliza kila jaji Tume ya Muda ya Huduma za Mahakama itakuwa na maoni kuwa kuna sababu za kuamini kuwa jaji huyo ni anaweza kuwa asiyefaa kuhudumu kama jaji, Tume ya muda ya Huduma za Mahakama itamhitaji jaji anayehusika kwenda kwa likizo akiwa analipwa mshahara wake kama kawaida huku akisubiri kukamilishwa kwa uchuguzi kuhusiana na kesi yake

(9) Wakati ambapo malalamiko ama jambo fulani kumhusu jaji limeshughulikiwa na kumamilishwa na kufikiwa uamuzi kuwa mtu anayehusika hafai kuwa jaji, Tume ya Muda ya Huduma za Mahakama itaweza kumjulisha jaji huyo kwa kumwandikia na kumweleza hivyo na kutoka siku ya barua hiyo, jaji huyo atachukuliwa kuwa ameachishwa kazi.

(10) Katika wakati wowote wa kuchunguza majaji, ikiwa Tume ya Muda ya Huduma za Mahakama itamfikiria jaji kufaa kuendelea na kazi, itatangaza hivyo na jaji huyo ataendelea na majukumu ya ofisi kama kwamba ameteuliwa katika Katiba hii.

(11) Nafasi zitakazoachwa kutokana na shughuli hii na zile zinazotokana na utekelezaji wa vipengele vya Sura ya Kumi na Tatu zitajazwa baada ya Tume mpya ya Huduma za Mahakama imeteuliwa kama inavyofafanuliwa katika Katiba hii.

(12) Isipokuwa muhula wake uongezwe kwa kauli ya Bunge, Tume ya Muda ya Huduma za Mahakama itavujwa baada ya mwaka mmoja kuanzia siku ilipoanza kazi.

(13) Kuunda na kuteuliwa kwa majaji kwa mahakama yenye Mamlaka Kuu na Mahakama ya Kikatiba kutashughulikiwa katika mwaka mmoja kuanzia siku ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.

**Vikao vya mahakama na masuala ambayo hayajakamilishwa**

**16**. Isipokuwa kama imeelezwa katika Katiba hii, vikao vyote vya mahakama ambavyo havijakamilishwa mahakamani vitaendelea kusikizwa na kuamuliwa na mahakama hiyo hiyo ama mahakama nyingine kama hiyo iliyobuniwa na Katiba hii ama kama ilivyoelekezwa na Jaji Mkuu ama Msajili wa Mahakama Kuu.

Kuwachunguza maafisa wa Mahakama

**17.** (1) Tume ya Huduma za Mahakama itatekeleza uchunguzi wa kwa maafisa wote wa mahakama.

(2) Katika kuwachunguza maafisa wote wa mahakama kulingana na sehemu ndogo (1) sehemu 15 itatekelezwa pamoja na mabadiliko yanayofaa.

**Tume za Kikatiba**

**18.** (1) Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi na Tume kuhusu Utekelezaji wa Katiba itaundwa kati ya siku tisini kuanzia siku ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii.

(2) Katika miezi tisa ya kuteuliwa kwa Tume ya Maadili na Uadilifu na Tume kuhusu Utekelezaji wa Katiba, Tume zifuatazo zitateuliwa kulingana na umuhimu wake—

(a) tume ya Huduma za Mahakama;
(b) tume ya Ugawaji wa Mapato ;
(c) tume ya Huduma za Polisi;
(d) tume ya Utumishi wa Umma;
(e) tume ya Haki za Kibinadamu na Jinsia;
(f) tume ya Mishahara;
(g) tume ya Kitaifa kuhusu Ardhi;
(h) Tume ya Kuwaajiri Walimu.

**Tume ya Huduma za Mahakama**

**19.** Kuundwa kwa Tume ya Huduma za Mahakama kutafanywa katika siku sitini tangu siku ya utekelezaji wa Katiba hii na Tume itachukuliwa kuwa iliyoundwa sawa kulingana na Katiba hii ingawa kunaweza kuwa na nafasi katika uanachama wake kwa sababu huenda uteuzi usiwe umefanywa na majaji wa mahakama yenye Mamlaka Kuu ama Mahakama ya Kikatiba

**Tume ya Haki za Kibinadamu na Jinsia**

**20.** (1) Makamishna wa Tume ya Haki za Kibinadamu na Jinsia wakiteuliwa chini ya sheria ya Tume ya Haki za Kibinadamu na Jinsia, inaanza siku ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hiii na makamishna wa Tume ya Kitaifa kuhusu Jinsia na Maendeleo watakuwa makamishna wa Tume ya Haki za Kibinadamu na Jinsia kwa wakati muda wao wa kuhudumu hautakuwa umeisha lakini kila kamishana atahifadhi masharti ya kazi kuanzia siku ya kuanzia kutekelezwa kwa Katiba hii.

(2) Mwenyekiti wa Tume ya Kitaifa kuhusu Haki za Kibinadamu na Jinsia atakuwa mwenyekiti wa Tume ya Haki za Kibinadamu na Jinsia kwa muda wake wa kuhudumu uliosalia.

**Tume Huru ya Muda ya Uchaguzi na Mipaka**

**21.** Tume Huru ya Muda ya Uchaguzi na Mipaka ikibuniwa katika Katiba iliyoko kabla ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii itaendelea kwa kipindi cha miezi ishirini na minne tangu siku ya kuteuliwa kwa makamishna wao katika Katiba iliyoko kuanzia siku ya kutekelezwa kwa Katiba hii, isipokuwa kipindi hicho kiongezwe na Bunge, na Tume Huru ya Muda ya Uchaguzi na Mipaka itateuliwa kwa Katiba hii kabla ya kuisha kwa kpindi hicho

**Tume ya Uadilifu na Kupambana dhidi ya Ufisadi**

**22.** Mkurugenzi wa Tume ya Kupambana na Ufisadi yuko ofisini kulingana na sheria ya Tume ya Kupambana na Ufisadi na Makosa ya Kiuchumi kuanzia siku ya kuanza kutumika kwa Katiba hii ataendelea na wajibu wake kwa kipindi chake ambacho kimebaki.

**Ukiukaji wa haki za kibinadamu wa siku za nyuma**

**23.** Bunge linaweza, katika miezi sita ya kutekelezwa kwa Katiba hii kwa sheria itawezesha Tume ya Haki za Kibinadamu na Jinsia ama taasisi yoyote nyingine iliyobuniwa na Bunge—

(a) Kuchunguza aina zote za ukiukaji wa haki za kibinadamu kulikofanywa na yeyote ama kundi kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.
(b) Kuchunguza chanzo cha migogoro kati ya raia pamoja na mauaji ya halaiki, mapigano ya kikabila na mauaji ya kisiasa na kuwatambua waliohusika; na
(c) Toa mapendekezo kuhusu –
  (i) Kushtakiwa kwa wale wanaohusika;
  (ii) Kuwalipa fidia waathiriwa;
  (iii) Maridhiano; na
  (iv) kulipa fidia.

**Umiliki wa Ardhi**

**24.** (1) Siku ya kuanza kutumika Katiba hii, yeyote anayetaka ardhi yenye mkataba wa kupangisha ulio zaidi ya miaka tisini na tisa, ikiwa itatolewa na yeyote yule likiwa limemilikiwa na mtu asiye raia utarudishwa na kuwa wenye miaka tisini na tisa, isipokuwa ibatilishwe vinginevyo.

(2) Hadi jamii zitakapotambuliwa na hati zao kuandikishwa, mashamba ya kijamii yatahifadhiwa na Tume ya Kitaifa kuhusu Ardhi kwa niaba ya jamii mbali mbali.

(3) Katika hali ambapo wakati wa kuanza kutumika Katiba hii, mtu yeyote ambaye si raia wa Kenya alimliki ardhi isiyo na masharti nchini Kenya, haki hiyo yake itarejeshwa kwa Jamhuri ya Kenya ili kuhifadhi kwa niaba ya raia wa Kenya na taifa litampa mtu huyo haki baadala ya kiwango cha chini na kulipa kodi kwa mkataba wa kupangisha usiozidi miaka tisini na tisa.

**Mafunzo ya Umma**

**25.**Kuanzia siku ya utekelezaji wa Katiba hii, Serikali kupitia kwa taasisi husika, itatekeleza mafunzo kwa umma kuhusu Katiba hii kwa raia wa Kenya katika lugha za taifa na lugha za kiasili.

**Fedha**

**26.** Hakuna chochote katiba mpya.

Kamati ya Wataalam wa Marekebisho ya Katiba
Delta House, Chiromo Road, Westlands, Nairobi
P.O. Box 8703 - 00200, Tel:+ 254 020 4443214 - 16
info@coekenya.go.ke, www.coekenya.go.ke